# TANZANIA ELECTION MONITORING COMMITTEE
# (TEMCO)

## RIPOTI YA UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA WA MWAKA 2010

**Machi, 2011**

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| AFP | - | Alliance for Tanzania Farmers Party |
| AG | - | Attorney General/ Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| APPT-Mandeleo | - | African Progressive Party |
| ARO | - | Assistant Registration Officer/ Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi |
| BAWACHA | - | Baraza la Wanawake wa CHADEMA |
| CBO | - | Community Based Organization |
| CCJ | - | Chama Cha Jamii |
| CCM | - | Chama Cha Mapinduzi |
| CEDAW | - | Convention on the Elimination of All Forms of Discrimination Against Women |
| CHADEMA | - | Chama Cha Demokrasia na Maendeleo |
| CHAUSTA | - | Chama cha Ustawi na Demokrasia |
| CSO | - | Civil Society Organization |
| CUF | - | Civic United Front/ Chama cha Wananchi |
| DED | - | District Executive Director |
| DKWK | - | Daftari la Kudumu la Wapiga Kura |
| EEA | - | Election Expenses Act/ Sheria ya Gharama za Uchaguzi |
| EMB | - | Election Management Body |
| ESP | - | Election Support Programme |
| FBO | - | Faith Based Organization |
| FEM ACT | - | Feminist Activist Coalition |
| FIA | - | Freedom of Information Act |
| FOS | - | Friends of Dr. Slaa/ Marafiki wa Dk. Slaa |
| HoR | - | House of Representatives/ Baraza la Wawakilishi |
| ID | - | Identity Card/ Kitambulisho |
| IEMS | - | Integrated Election Management System |
| IFJ | - | International Federation of Journalists |
| IT | - | Information Technology/ Teknohama |
| LHRC | - | Legal and Human Rights Centre |
| LTO | - | Long Term Observer |
| MDG | - | Millenniun Development Goals/ Malengo ya Maendeleo ya Milenia |
| NCCR-Mageuzi | - | National Convention for Construction and Reform |
| NEC | - | National Electoral Commission/ Tume ya Taifa ya Uchaguzi |
| NGO | - | Non-Governmental Organization |
| NLD | - | National League for Democracy |
| NRA | - | National Reconstruction Alliance |
| PNVR | - | Permanent National Voters' Register/ Daftari la Kudumu la Wapiga Kura |
| RO | - | Returning Officer/ Msimamizi wa Uchaguzi |
| RPP | - | Registrar of Political Parties/ Msajili wa Vyama vya Siasa |
| SAU | - | Sauti ya Umma |
| TADEA | - | Tanzania Democratic Alliance |

| | | |
|---|---|---|
| TAKUKURU | - | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TAMWA | - | Tanzania Media Women Association |
| TAWLA | - | Tanzania Women Lawyers Association |
| TBC | - | Tanzania Broadcasting Corporation |
| TCA | - | Tanzania Communication Authority |
| TCD | - | Tanzania Centre for Democracy |
| TEMCO | - | Tanzania Election Monitoring Committee |
| TGNP | - | Tanzania Gender Networking Programme |
| TLP | - | Tanzania Labour Party |
| TV | - | Televisheni |
| UDP | - | United Democratic Party |
| UMD | - | Union for Multiparty Democracy |
| UNDP | - | United Nations Development Programme |
| UNIFEM | - | United Nations Development Fund for Women |
| UPDP | - | United Peoples' Democratic Party |
| UWT | - | Umoja wa Wanawake Tanzania |
| VIS | - | Voters Interaction System |
| WEO | - | Ward Executive Officer |
| ZEC | - | Zanzibar Electoral Commission/ Tume ya Uchaguzi Zanzibar |

## YALIYOMO


**ORODHA YA VIFUPISHO .................................................. I**

**1. MBINU NA NJIA ZA UANGALIZI WA UCHAGUZI WA MWAKA 2010 .................. 1**

1.0 UTANGULIZI .................. 1
2.0 NJIA NA MBINU ZA UKUSANYAJI WA DATA .................. 1
3.0 UMUHIMU WA KUANGALIA UCHAGUZI WA MWAKA 2010 .................. 2
4.0 MALENGO YA UANGALIZI WA UCHAGUZI .................. 2
5.0 MPANGO WA UANGALIZI .................. 4
6.0 VIGEZO VYA UJUMLA VYA TATHMINI YA UCHAGUZI .................. 4
7.0 MUHTASARI WA RIPOTI .................. 5
8.0 SHUKRANI .................. 7

**2. USAJILI WA WAPIGA KURA .................. 9**

1.0 UTANGULIZI .................. 9
2.0 DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA NCHINI TANZANIA .................. 9
3.0 MCHAKATO WA KUANDIKISHA WAPIGA KURA TANZANIA .................. 10
4.0 MCHAKATO WA USAJILI WA 2010 .................. 14
5.0 MATATIZO KATIKA MCHAKATO WA USAJILI WA WAPIGA KURA .................. 17
6.0 NEC NA USIMAMIZI WA MCHAKATO WA USAJILI .................. 20
7.0. KITENDAWILI CHA USAJILI MKUBWA WA WAPIGA KURA NA UCHACHE WA WATU WALIOJITOKEZA SIKU YA KUPIGA KURA .................. 21
8.0. HITIMISHO .................. 22

**3. UTEUZI WA WAGOMBEA .................. 23**

1.0 UTANGULIZI .................. 23
2.0 MUKTADHA WA KISHERIA NA TARATIBU ZA VYAMA .................. 23
3.0 UTEUZI WA WAGOMBEA NDANI YA VYAMA VYA SIASA .................. 27
4.0 UTEUZI WA TUME YA UCHAGUZI NA MATOKEO YAKE .................. 32
5.0 MGOMBEA BINAFSI .................. 34
6.0 HEKAYA ZA KUPITA BILA KUPINGWA .................. 36
7.0 TATHMINI YA TEMCO YA MCHAKATO WA UTEUZI .................. 38
8.0 HITIMISHO .................. 39

**4. USIMAMIZI WA CHAGUZI ZA MUUNGANO 2010 .................. 40**

1.0 UTANGULIZI .................. 40
2.0 SHERIA NA MISINGI YA KIASASI ILIYOONGOZA CHAGUZI ZA 2010 .................. 40
3.0 USIMAMIZI WA CHAGUZI .................. 42
4.0 MAJUKUMU YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI .................. 43
5.0 UHURU WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI .................. 43
6.0 FEDHA ZA KUGHARAMIA UCHAGUZI .................. 46
7.0 UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA .................. 46
8.0 UBORESHAJI WA MIFUMO YA KUSIMAMIA CHAGUZI .................. 47
9.0 ELIMU YA MPIGA KURA .................. 50

9.0 HITIMISHO ..... 51

**5. MWENENDO WA KAMPENI ..... 52**

1.0 UTANGULIZI ..... 52
2.0 MUKTADHA NA MAJUMUISHO ..... 52
3.0 TARATIBU NA MAADILI YA KAMPENI ..... 54
4.0 MLOLONGO, TARATIBU NA MBINU ZA KAMPENI ..... 55
5.0 MASUALA NA AJENDA ZA KAMPENI ..... 60
6.0 MASUALA YA KIUSALAMA ..... 62
7.0 GHARAMA ZA KAMPENI ..... 63
8.0 FAIDA ZA KUWA MGOMBEA/CHAMA KILICHOPO MADARAKANI ..... 64
9.0 MATATIZO NA MIGONGANO ..... 65
10.0 TATHMINI YA JUMLA ..... 70
11. HITIMISHO ..... 71

**6. VYOMBO VYA HABARI KATIKA MCHAKATO WA UCHAGUZI ..... 72**

1.0 UTANGULIZI ..... 72
2.0 WAJIBU WA VYOMBO VYA HABARI KATIKA MCHAKATO WA UCHAGUZI ..... 72
3.0 VYOMBO VYA HABARI VILIVYOTANGAZA MCHAKATO WA UCHAGUZI WA 2010 ..... 76
4.0 UTANGAZAJI WA VYOMBO VYA SERIKALI ..... 78
5.0 UTENDAJI WA VYOMBO VYA HABARI VYA BINAFSI ..... 81
6.0 UHURU WA KUJIELEZA WAKATI WA MCHAKATO WA UCHAGUZI ..... 83
7.0 KUCHUNGUZA NA KUIBUA MAOVU ..... 84
8.0 UWEZO NA UDHAIFU WA VYOMBO VYA HABARI NCHINI TANZANIA ..... 85
9.0 UZINGATIAJI WA MAADILI YA KITAALUMA ..... 87
10.0 HITIMISHO ..... 88

**7. USHIRIKI WA WANAWAKE KATIKA UCHAGUZI ..... 89**

1.0 UTANGULIZI ..... 89
2.0 NYENZO ZA KITAIFA NA KIMATAIFA ..... 89
3.0 USHIRIKI WA WANAWAKE KAMA WAPIGA KURA ..... 89
4.0 USHIRIKI YA WANAWAKE KAMA WAGOMBEA ..... 90
5.0 UTEUZI WA VITI MAALUM KATIKA VYAMA ..... 91
6.0 USHIRIKI WA WANAWAKE KATIKA KAMPENI ..... 92
7.0 ELIMU YA KURA KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE ..... 93
8.0 UUNGAJI MKONO WAGOMBEA WANAWAKE ..... 94
9.0 MATOKEO YA UCHAGUZI KWA WANAWAKE: WASHINDI NA WALIOSHINDWA ..... 95
10.0 HITIMISHO ..... 97

**8. KUPIGA KURA, KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO ..... 98**

1.0 UTANGULIZI ..... 98
2.0 MCHAKATO WA KUPIGA KURA ..... 99
3.0 MCHAKATO WA KUHESABU KURA ..... 102

4.0 KUTANGAZA MATOKEO ........ 104
5.0 MWITIKIO WA WAPIGA KURA ........ 106
6.0 MALALAMIKO BAADA YA KUPIGA KURA ........ 107
7.0 HITIMISHO ........ 108

**9. UCHAGUZI MKUU TANZANIA 2010: KWA KIASI GANI ULIKUWA HURU NA WA HAKI? ........ 109**

1.0 UTANGULIZI ........ 109
2.0 MASUALA YATOKANAYO NA UANDIKISHAJI WAPIGA KURA ........ 110
3.0 MASUALA YATOKANAYO NA UTEUZI WA WAGOMBEA ........ 111
4.0 MASUALA YATOKANAYO NA KAMPENI ........ 112
5.0 KUPIGA KURA, KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO ........ 115
6.0 TAMKO LA TEMCO KUHUSU UCHAGUZI WA 2010 ........ 116
7.0 MAPENDEKEZO ........ 117

**REJEA ........ 120**

**VIAMBATISHO ........ 125**

# SURA YA KWANZA

## MBINU NA NJIA ZA UANGALIZI WA UCHAGUZI WA MWAKA 2010

### 1.0 UTANGULIZI

TEMCO (Tanzania Election Monitoring Committee) ni mkusanyiko wa asasi za kiraia ulioundwa mwaka 1994 na asasi ishirini na nne ili kuangalia uchaguzi wa Tanzania. TEMCO imeangalia chaguzi zote za Tanzania tangu mwaka 1995, 2000, chaguzi ndogo za mwaka 2003 na 2005. Kwa sasa asasi wanachama wa TEMCO zimeongezeka hadi kufikia 152. Kama ilivyokuwa kwa chaguzi zilizopita, TEMCO iliangalia uchaguzi wa mwaka 2010 uliofanyika tarehe 30 Oktoba. TEMCO inaongozwa na Kamati Tendaji ambayo hufanya maamuzi yote muhimu yakiwemo mtazamo kuhusiana na namna uchaguzi ulivyoendeshwa. Kamati Tendaji hufanya kazi kwa usaidizi wa Timu ya Menejimenti inayoongozwa na Mwenyekiti, ambaye ndiye Mkuu wa Sekretariati. Ripoti hii inamulika uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Jamhuri ya Muungano. Chaguzi za Zanzibar zitakuwa katika ripoti tofauti.

Kutokana na uziefu wake mkubwa katika kuangalia uchaguzi Tanzania, TEMCO ilishinda tenda ya kuangalia uchaguzi wa mwaka 2010, iliyotangazwa na UNDP (United Nations Development Programme). TEMCO iliweka waangalizi wa muda mrefu katika majimbo yote isipokuwa yale tu ambayo wagombea wake walipita bila kupingwa. TEMCO pia iliajiri waangalizi 7,000 wa muda mfupi kwa ajili ya kushuhudia zoezi la kupiga na kuhesabu kura. TEMCO iliandaa programu mahsusi ya kufundishia waangalizi wa uchaguzi wa muda mrefu na muda mfupi. Ilitengeneza seti ya vitendea kazi vya kuwaongozea waangalizi wawapo kazini na kurahisisha mtiririko wa habari kutoka majimboni hadi makao makuu. Data na takwimu zilikusanywa na kufanyiwa tathmini na wataalamu waliobobea katika taaluma ya siasa na takwimu.

TEMCO iliamua kuangalia uchaguzi wa mwaka 2010 kutokana na imani kuwa kufanyika kwa chaguzi huru na haki ni muhimu katika kuimarisha demokrasia. Shughuli zake zilihusisha mchakato mzima wa uchaguzi ikiwamo uandikishaji wa wapiga kura, uteuzi wa wagombea, kampeni, na upigaji na uhesabuji wa kura pamoja na kutangaza matokeo. Kila moja ya hatua hizi inachambuliwa katika sura mahsusi katika ripoti hii. Mara tu baada ya matokeo kutangazwa, TEMCO ilitoa tathmini ya awali ya mchakato wa uchaguzi. Katika kuangalia ikiwa uchaguzi ni huru na wa haki, vigezo vinne hutumika:

(i) Namna sheria zinavyofahamika na kufuatwa na wahusika wakuu;
(ii) Uhuru na uwezo wa wasimamizi wa uchaguzi (NEC and ZEC);
(iii) Ukaribu wa Tume ya Uchaguzi kwa wapiga kura, wagombea na vyama; na,
(iv) Uhalali na kuaminika kwa matokeo.

### 2.0 NJIA NA MBINU ZA UKUSANYAJI WA DATA

Ili kufanikisha majukumu ambayo yameelezwa, TEMCO iliandaa “mbinu chotara” kukusanya data na takwimu kutoka kwa wadau mbalimbali ikiwamo madodoso. Majibu ya maswali elekezi yalipatikana kutoka vyanzo tofautitofauti kwa kutumia njia mbalimbali zikiwemo zifuatazo:

### (i) Ushuhuda

Njia ya ushuhuda ni nyenzo muhimu katika utafiti huu. Mathalani, mgombea akidai kwamba alitumia shilingi x na mtafiti "akashuhudia" kuwa timu yake ya kampeni ilikuwa na zaidi ya mgari 50 ya kifahari kwa ajili ya kuwazungusha, inawezekana mtafiti huyu akalazimika kutathmini gharama za kampeni kama 10x. "Kuona ni kuamini". Waangalizi wa uchaguzi walipewa mafunzo na maelekezo maalum ili wawe makini katika kufuatilia kwa undani na kurekodi kila wanachokiona. Katika mchakato huu, TEMCO iliongozwa na "Mwongozo kwa Waangalizi wa Uchaguzi" uliotolewa na Tume ya Uchaguzi. Baadhi ya vyama vya siasa vilitoa mwaliko rasmi kwa TEMCO kushuhudia zoezi la uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vyao.

### (ii) Usaili

Usaili wa kina ulifanywa kwa watu mbalimbali majimboni ili kukusanya data na habari juu ya maswali yaliyokuwa kwenye dodoso. Watu hawa walijumuisha viongozi na watendaji wa vyama vya siasa, wagombea, wajumbe wa kamati na timu za kampeni, viongozi wa asasi za kiraia zilizokuwa mstari wa mbele katika kutoa elimu ya mpiga kura, na baadhi ya wapiga kura. Katika ngazi ya kitaifa, usaili ulifanywa kwa viongozi wa kitaifa wa vyama vya siasa, maafisa na wajumbe wa NEC, maafisa wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa pamoja na maafisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

### (iii) Usawiri wa Nyaraka

Waangalizi wa uchaguzi walisawiri nyaraka muhimu walizopata kutoka kwa wadau mbalimbali wa uchaguzi. Walitumia sehemu ya taarifa katika nyaraka hizi kujaza dodoso na kuandaa ripoti za kina mwisho wa zoezi la uangalizi wa uchaguzi.

## 3.0 UMUHIMU WA KUANGALIA UCHAGUZI WA MWAKA 2010

Kama ilivyogusiwa awali, hamu ya TEMCO kuangalia uchaguzi wa mwaka 2010 ilisukumwa na ufahamu kuwa uchaguzi ni uti wa mgongo wa demokrasia. Inafahamika dhahiri kuwa mpito kuelekea kwenye demokrasia bado mbichi na unahitaji kulelewa ili kufikia ukomavu. Waama, TEMCO ilikwishaangalia chaguzi nyingine za vyama vingi zilizotangualia na ilikuwa katika nafasi ya kuleta uzoefu wake katika uchaguzi huu.

Kutokana na rekodi yake thabiti katika kuangalia chaguzi zilizotangulia, TEMCO imejenga uaminifu miongoni mwa wadau muhimu wa uchaguzi ambao wanaikubali kuwa inaaminika, ni mahiri na haipendelei upande wowote. Wadau hawa walitarajia TEMCO iendeleze kazi yake ya kuangalia uchaguzi wa mwaka 2010, ili kuchangia katika kuboresha ufanisi na haki katika mchakato wa uchaguzi.

## 4.0 MALENGO YA UANGALIZI WA UCHAGUZI

Kama ilivyokuwa kwa chaguzi zilizotangulia, lengo kuu la kuangalia uchaguzi wa mwaka 2010 lilikuwa ni kufuatilia kwa umakini machakato mzima wa uchaguzi, ili kubainisha kama

ulikuwa huru na wa haki au la. Malengo mahsusi yalijumuisha haya yafuatayo:

(a) Kuangalia mchakato mzima wa uchaguzi, ikiwamo kutenga majimbo ya uchaguzi, kuandikisha wapiga kura, kuteua wagombea, kampeni za uchaguzi, kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo;
(b) Kuangalia na kutathmini utendaji haki katika usimamizi wa zoezi zima la uchaguzi, na hasa uongofu wa miundombinu ya kisheria (sheria za uchaguzi, kanuni na taratibu), vyombo vya usimamizi (NEC na Tume ya Uchaguzi Zanzibar), vyombo vya dola, na vyombo vya ulinzi na usalama;
(c) Kutathmini uongofu katika kugawanya na kutumia rasilimali za taifa baina ya vyama vya siasa, hasa ruzuku ya serikali, na vyombo vya habari vya umma (redio, televisheni na magazeti);
(d) Kutathmini utekelezaji baina ya washindani wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sheria Namba 6 ya mwaka 2010, iliyopitishwa ili kudhibiti matumizi ya pesa katika chaguzi;
(e) Kutathmini kiwango ambacho, mambo yote yakizingatiwa, uchaguzi ungeweza kusemwa kuwa ni huru na wa haki; na,
(f) Kuchukua mizania ya masomo muhimu kutokana na uchaguzi kwa lengo la kurekebisha kasoro zilizojitokeza katika chaguzi zitakazofuata.

Ili kufanikisha malengo haya, TEMCO ilijiwekea vigezo vya kuongoza uangalizi wa uhaguzi wa mwaka 2010 na kusaidia katika kutoa tathmini ya uhuru na uhaki wa uchaguzi. Vigezo hivi vilijumuisha: (i) kupima uongofu (impartiality) wa vyombo vya dola; (ii) kuangalia kama kulikuwa na usawa katika kuwafikia wapiga kura; (iii) kutathmini uwezo na uongofu wa Tume ya Uchaguzi na mfumo mzima wa uangalizi; (iv) kutafuta ushahidi wa vikwazo vyovyote vya ushindani wa kisiasa; (v) kuona kama kulikuwa na usawa katika kufikia rasilimali za umma, au uwanja wa ushindani haukuwa sawa; (vi) kutathmini uwezo/udhaifu wa vyama vya upinzani; na (vii) kutafuta ushahidi wa athari za masalia ya urithi wa chama kimoja. Vigezo hivi na vinginevyo, vilitoa mwongozo kwa waangalizi wa TEMCO katika kutathmini mwenendo wa uchaguzi wa 2010 na kutoa cheti cha ubora.

Katika kuangalia uchaguzi wa mwaka 2010, ilikuwa ni muhimu sana kuangalia muktadha wa kisiasa na kiuchumi ambamo uchaguzi ulifanyika. Mojawapo ya mambo yaliyovutia yalihusiana na suala la mgombea binafsi. Mahakama Kuu ilitoa hukumu awali ikiruhusu mgombea binafsi katika ngazi zote za uchaguzi ikisisitiza kuwa kuzuia wagombea binafsi ni kinyume cha katiba. Hata hivyo, serikali ilikata rufaa dhidi ya uamuzi huo. Uamuzi wa Mahakama ya Rufaa uliacha nyuma mjadala mkali lakini siyo utatuzi wa suala lenyewe. Mahakama ilitoa hukumu kuwa ni kazi ya Bunge – siyo mahakama – kubadilisha vipengele vya Katiba. Wachambuzi wengi wanaamini kuwa mjadala wa mgombea binafsi umechangia sana katika kuchochea madai ya sasa ya katiba mpya. Bila shaka yoyote, matakwa ya kuwa mtu awe mwanachama ili agombee, ni mazonge ya chama kimoja.

Kuelekea katika uchaguzi mkuu wa 2010, ulizuka mwenendo wa kutia shaka kufuatia ghasia na vurumai katika chaguzi ndogo zilizofanyika. Dalili za vurugu hizi zilionekana katika chaguzi ndogo zilizofanyika kuziba nafasi zilizoachwa wazi katika baadhi ya majimbo yakiwemo: Kiteto, Mbeya, Tarime, na Busanda Tanzania Bara na Magogoni, Zanzibar. Mbali ya vurugu na ghasia, viongozi waandamizi wa CCM na serikali walizomewa na misafara yao

kushambuliwa nyakati za kampeni. TEMCO ilitaka kujua kama mwenendo huu ungeendelea wakati wa uchaguzi mkuu.

## 5.0 MPANGO WA UANGALIZI

Programu za uangalizi wa uchaguzi zilijumuisha kufuatilia mchakato mzima wa uchaguzi katika majimbo yote yaliyokuwa na ushindani. Kwa minajili ya uangalizi wa uchaguzi, kila mkoa uliunda Kamati ya Uangalizi ya Mkoa (REMCO). REMCO ziliundwa na asasi tano ambazo ni wanachama wa TEMCO katika mkoa husika. Pamoja na asasi hizi, waangalizi wa uchaguzi katika mkoa walikuwa sehemu ya REMCO. REMCO zilifanya mikutano kila baada ya wiki mbili. Kazi yao kubwa ilikuwa ni kuhakikisha kuwa ripoti za waangalizi wa uchaguzi kweli ziliakisi kile kilichokuwa kinatokea. REMCO pia zilihakiki majina ya waangalizi wa muda wa uchaguzi walioteuliwa na asasi wanachama.

Tovuti ya TEMCO www.temco.udsm.ac.tz ilianzishwa mahsusi kwa ajili ya kutoa habari motomoto za uangalizi wa uchaguzi.

## 6.0 VIGEZO VYA UJUMLA VYA TATHMINI YA UCHAGUZI

Imekuwa desturi kwa TEMCO kutoa "cheti" ambacho kinaendana na "uhuru na uhaki wa uchaguzi". Vyeti vya TEMCO vinatofautiana kuanzia cheti cha *uchaguzi huru na wa haki* mpaka *Uchaguzi uliovia.* Yafuatayo ni maelezo mafupi ya vyeti hivi.

*Cheti cha Uchaguzi Huru na wa Haki* kinaonyesha kuwa uchaguzi ulikwenda vizuri na hakukuwa na kitu chochote tofauti ambacho kingesababisha uingie dosari. Kama kulikuwa na upungufu wowote, usingeweza kubadilisha matokeo kwani ulikuwa mdogo na wa kawaida tu.

*Cheti cha Uchaguzi Huru na wa Haki Wenye Walakini* huashiria uchaguzi ulikuwa kwa ujumla huru na wa haki, lakini kulikuwa na kasoro ambazo ziliwaathiri vibaya baadhi ya washiriki.

*Cheti cha Uchaguzi Huru Lakini siyo wa Haki* kinaonyesha kushamiri kwa vitendo vya kuvunja sheria za uchaguzi, na hasa zikichukua sura ya kubarikiwa na vyombo vya dola au Tume ya Uchaguzi, ambavyo vilizuia ushiriki sawa wa baadhi ya vyama, wagombea au wapiga kura.

*Cheti cha Uchaguzi Usio Huru Wala wa Haki* hutolewa pale ambapo kuna upendeleo dhahiri katika mchakato wa uchaguzi au kuna vitisho vingi kwa wagombea na vyama.

*Cheti cha Uchaguzi Uliovurugwa* hutolewa pale ambapo kuna uthibitisho wa wasimamizi wa uchaguzi kushindwa kuendesha uchaguzi kwa sababu za ukosefu wa umahiri, au mipango mibovu kiasi ambacho inakuwa vigumu hata kufanya tathmini.

*Cheti cha Uchaguzi Uliovia* hurejea uvunjaji mkubwa na wa makusudi wa sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi na kusababisha idadi kubwa ya wagombea, vyama na wapiga kura kujitoa katika mchakato wa uchaguzi, na hivyo kushindikana kufika tamati ya uchaguzi kisheria.

## 7.0 MUHTASARI WA RIPOTI

Ripoti hii ina sura tisa. Baada ya utangulizi huu, sura inayofuata imejikita katika kuangalia uandikishaji wa wapiga kura. Sura ya Tatu inaangalia uteuzi wa wagombea ndani ya vyama na katika Tume za Uchaguzi. Hii inafuatiwa na tathmini ya usimamizi wa uchaguzi katika sura ya nne. Sura ya Tano inaangalia kampeni.Dhima ya vyombo vya habari inapimwa katika sura ya sita. Sura ya Saba inatupia jicho la udadisi katika ushiriki wa wanawake katika uchaguzi. Sura ya Nane inatathmini upigaji kura, kuhesabu kura na kutangazwa matokeo. Sura ya Tisa inatoa hitmisho la TEMCO kuhusiana na uangalizi wa zoezi zima la uchaguzi. Yafuatayo ni maelezo mafupi ya kila sura.

Sura ya Pili inachunguza uandikishaji wa wapiga kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura (DKWK). Lengo kuu lilikuwa ni kuona ni kwa kiasi gani kuanzishwa kwa DKWK kumepunguza upungufu uliojitokeza nyuma kabla ya kuanzishwa kwake. Mojawapo ya matatizo yaliyokuwa yakijitokeza mara nyingi ilikuwa ni uwezekano wa kujiandikisha mara mbili na ununuzi wa shahada. Kwa kuwa shahada hazikuwa na picha ya mpiga kura, iliwezekana kwa baadhi ya watu kupiga kura zaidi ya mara moja kwa kutumia shahada za watu wengine. Wakati mwingine shahada zilizonunuliwa ziliharibiwa katika jitihada za kupunguza kura hasimu. Kilichoonekana mara baada ya kuanzishwa kwa DKWK kuelekea uchaguzi wa mwaka 2005 ni kuwa, watu wengi walivutiwa kuandikishwa kwani wa walitaka kupata kitu cha kuwatambulisha kwa kuwa Watanzania hawana vitambulisho vya utaifa. Vitambulisho vya NEC na ZEC vimekuwa muhimu sana katika kufanikisha mambo mengine yasiyohusiana na uchaguzi, kama vile, kuomba mikopo benki au kupokea pesa zinazotumwa kwa njia ya elektroniki. Hii inaweza kueleza kitendawili cha watu wengi kujitokeza kujiandikisha na siyo kupiga kura.

Kumekuwa na matatizo mengi kuhusiana na kadi zinazotolewa na Tume ya Uchaguzi, ikiwamo idadi kubwa ya wapiga kura kupoteza kadi zao na hivyo kushindwa kupiga kura. Inaonekana kuna tatizo kubwa katika kuhifadhi nyaraka miongoni mwa wapiga kura wengi, na pengine wengine hawana hata sehemu nzuri za kuzihifadhia. Tatizo hili lilikuwa kubwa kwa kuwa NEC hawana ofisi inayohusika na maendeleo ya wapiga kura, ambapo wale waliopoteza kadi zao wangeweza kwenda kupata nyingine. Isitoshe pamoja na kuboresha mfumo wa ufatiliaji wa wapiga kura, bado ilishindikana kupata majina ya baadhi yao na hivyo kuwakosesha wengi haki ya msingi ya kuchagua. Tatizo hili liliripotiwa katika majimbo mengi, ikiwemo Dar es Salaam. Ili kukabiliana na upungufu uliojitokeza, inapendekezwa kuwa mchakato wa uandikishaji wa wapiga kura uboreshwe kwa kuongeza matumizi ya teknolojia yatakayowezesha uandikishaji kufanyika kupitia mtandao.

Uteuzi wa wagombea unachunguzwa katika sura ya tatu. Mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama na katika Tume za Uchaguzi ulikuwa wa kuvutia. Kutokana na manufaa ya kuwa madarakani pamoja na imani kuwa tiketi ya chama tawala ingetosha kuhakikisha ushindi, ushindani ndani ya CCM ulikuwa mkali na mara nyingi ulihusisha rafu za kisiasa. Hakika Sheria ya Gharama za Uchaguzi ilipitishwa ili kudhibiti matumizi hasi ya pesa wakati wa uchaguzi. TAKUKURU walifanya kazi kubwa kufuatilia na kuziba mianya ya rushwa. Katika jitihada hizi, baadhi ya wagombea walinaswa na kutuhumiwa kutoa rushwa, na hatimaye kufunguliwa mashtaka mahakamani. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa pesa zilikuwa

“zikiwafuata” wapiga kura kiasi kwamba mbinu mpya za usambazaji wa pesa na kuwakwepa TAKUKURU zilibuniwa.

Suala la mgombea binafsi liliibua mswali mengi kuhusiana na sheria, taratibu na miongozo ya uchaguzi iliyopo. Pamoja na kuwa kulikuwa na mifano ya wagombea waliopita bila kupingwa, wengi wao pia “walipalilia njia”. Hali hii ya pili ilileta wasiwasi miongoni mwa wanataaluma na hasa kwa kuwa ilihusisha matumizi ya hila na ujanjaujanja kuwavunja nguvu waliojitokeza kuwapinga, ama ndani ya vyama au katika Tume. Sura hii inamulika sarakasi nyuma ya wagombea wanaopita bila kupingwa na inatoa angalizo kuwa, wagombea wanaokosa wapinzani kwa sababu yoyote ile, angalau wapigiwe kura ili kupima kiwango chao cha kukubalika na wapiga kura. Mkazo kuwa ili kugombea ni lazima mtu awe mwanachama unajadiliwa kama moja ya mapengo ambayo yanahitaji kushughulikiwa haraka ili kuondoa harufu za chama kimoja wakati wa mfumo wa vyama vingi.

Usimamizi wa uchaguzi ni mada ya sura ya nne. Kama jukumu la msingi la Tume ya Uchaguzi, namna uchaguzi unavyosimamiwa hutoa ishara ya uchaguzi huru na wa haki. Sura hii inaonyesha maeneo ambayo Tume ya Uchaguzi ilifanya vizuri. Uamuzi wa Tume kupitisha rufani zilizowekwa dhidi ya mawaziri waandamizi wa serikali uliongeza imani ya Tume machoni mwa jamii. Ilikuwa dhahiri kuwa baadhi ya Wasimamizi wa Uchaguzi walikuwa katika nafasi tete ilipofikia kutoa uamuzi dhidi ya mawaziri. Baadhi ya wanasiasa hawa wana ushawishi mkubwa na wana mizizi mirefu ndani ya serikali na chama tawala. Wengi wao ni mabosi wa wasimamizi wa uchaguzi nje ya uchaguzi.

Sura ya Sita imejikita katika kampeni za uchaguzi. Kampeni ni muhimu sana kwani ndizo kiungo baina ya wagombea na wapiga kura. Wapiga kura hukipa kura chama ambacho kitawashawishi kuwa kitaboresha maisha yao kikipewa ridhaa ya kushika mamlaka ya dola. Kampeni pia hutumika kuonyesha umashuhuri na uwezo wa vyama. Vyama mashuhuri na vyenye uwezo hufanya kampeni za kuvutia na zenye mafanikio ukilinganisha na vyama visivyokuwa na iwezo na umashuhuri. Uvumbuzi wa hivi karibuni wa mbinu za kapeni unajadiliwa ndani ya sura hii. Sura inaangazia baadhi ya kampeni “zilizopitiliza” mipaka zilizofanywa na vyama vyenye pesa. Vyama visivyokuwa na uwezo havikuwa na uhuru mkubwa wa kuchagua katika *menu* ya mbinu za kampeni. Moja ya mambo ya jumla yanayoibuliwa ndani ya sura hii ni pamoja na vurugu na matumizi yaliyopitiliza ya manufaa ya utawala (incumbency adavantage).

Kama vyama vinataka kufanya kampeni zitakazofana, na kama wadau wote katika uchaguzi watataka kuwasiliana, basi vyombo vya habari vinatoa jukwaa hilo. Sura ya Sita inawasilisha tathmini ya utendaji wa vyombo vya habari katika kufikia lengo hili kuu. Tathmini imetilia maanani umiliki wa vyombao vya habari kama moja ya nguzo kuu za ufanisi wa vyombo husika. Sura inahitimisha kuwa pamoja na kuwa Tanzania inajivunia wingi wa vyombo vya habari, vyombo hivyo bado vinadhibitiwa sana. Katika hali hii, ufanisi wa vyombo vya habari wakati wa uchaguzi huathirika sana.

Imetolewa hoja kuwa demokrasia inayoacha nyuma nusu ya watu wake ni butu na batili. Hivyo basi, ushiriki wa wanawake katika uchaguzi ni moja ya mihimili ya uchaguzi huru na wa haki. Nadharia ni kuwa kwa kadri ambavyo mchakato wa uchaguzi unafikika zaidi, ndivyo ambavyo wanawake wengi zaidi watajitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi. Swali la kujiuliza ni kama idadi ya wagombea wanawake imeongezeka, imepungua au imebaki bila kubadilika. Sura ya Saba inatoa mwanga juu ya maswali haya kwa kuangalia uchaguzi wa mwaka 2010. Juhudi za kimataifa katika kuboresha ushiriki wa wanawake, ikiwamo suala linaloleta ubishani la nafasi maalum, zinajadiliwa. Mojawapo ya maangalizo makuu ni kuwa wanawake bado wanakabiliana na changamoto nyingi kushiriki katika uchaguzi kama wagombea. Hata hivyo cha kufurahisha ni kuwa wanawake walijishughulisha kikamilifu na kuwa kiungo muhimu katika michakato mingine ya uchaguzi, ikiwemo kufanya kampeni.

Sura ya Nane inaelezea mchakato wa kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo. Inaelezea pia matukio ya baada ya uchaguzi na mwitikio wa wananchi wa matokeo ya uchaguzi. Moja ya mambo makubwa yaliyojitokeza ni kusimamishwa kwa zoezi la uchaguzi katika majimbo saba na kata 28. Tatizo la orodha za wapiga kura zisizokamilika liliukumba uchaguzi wa mwaka 2010. Baadhi ya wapiga kura hawakuona majina yao katika vituo vya kupigia kura kwa hiyo walishindwa kupiga kura. Wengine wanaunganisha mwitikio hafifu wa wapiga kura na matatizo kama haya. Jingine ni vurugu zilizosabishwa na kuchelewa kutolewa kwa matokeo katika baadhi ya majimbo. Ingawa maelezo rasmi yalikuwa ni ugeni wa teknolojia iliyotumika kuingizia matokeo, kuchelewa kwa matokeo katika majimbo yenye ushindani mkali kulileta hisia za “mchezo mchafu”.

Imekuwa desturi sasa kwa TEMCO kutoa tamko kuhusu mwenendo wa uchaguzi kwa kutoa mojawapo ya vyeti vilivyoelezewa hapo juu. Tamko la TEMCO liko katika Sura ya Tisa. Kabla ya kutoa tamko hili, TEMCO ilichunguza kwa makini kila hatua katika mchakato wa uchaguzi. Hivyo, tamko linatoa wastani wa tathmini ya hatua zote.

## 8.0 SHUKRANI

Ripoti hii ni kilele cha juhudi za pamoja za asasi na watu binafsi. TEMCO inatoa shukrani zake za dhati kwa wadau wote ambao kwa namna mbalimbali walifanikisha zoezi la uangalizi wa uchaguzi wa Tanzania wa mwaka 2010.

Fedha zilitolewa na *Mradi wa Kuwezesha Uchaguzi* (Election Support Project - ESP). Mradi huu unahusisha nchi mbalimbali zikiwemo Canada, Denmark, Kamisheni ya Ulaya (The European Commission), Finland, the Netherlands, Norway, Sweden, Switzerland, UNDP na Uingereza. ESP inaendeshwa chini ya Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) Tanzania. Tunawashukuru sana kwa mchango wao wa pesa, uliowezesha TEMCO kuajiri Sekretariati na kumudu gharama za uangalizi wa uchaguzi.

Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unastahiki shukrani za pekee kwa kutoa msingi, uhalali na msaada kama ambavyo umekuwa ukifanya huko nyuma. Kazi ya TEMCO ilifaidika sana kutokana na upana wa taaluma ambazo Chuo kinatoa.

Tunatoa shukrani za dhati kwa wanachama 152 wa TEMCO kwa moyo wao wa kujitolea. Tulichagua Waangalizi wa Muda Mrefu na Waangalizi wa Muda Mfupi kutoka kwa wanachama wa TEMCO. Shukrani nyingi ziwaendee Waangalizi wa Muda Mrefu (Waratibu wa Mikoa na Waangalizi wa Majimbo) waliojitolea muda wao karibu miezi miwili kufanya kazi majimboni mbali na makaazi yao. Waangalizi wa Muda Mfupi walifanya kazi iliyotukuka ya kufuatilia matukio siku ya kupiga na kuhesabu kura.

Ni dhahiri kuwa bila ushirikiano wa NEC na Tume ya Uchaguzi Zanzibar, kazi ya TEMCO isingewezekana. TEMCO inazishukuru Tume zote za uchaguzi kwa kutoa vibali vya kuangalia uchaguzi kwa wakati, kwani bila hivyo isingewezekana kuendelea na zoezi. Huko majimboni pia Wasimamizi wa Uchaguzi walitoa ushirikiano mkubwa kwa Waangalizi wa TEMCO na wengi wao hawakusita kutoa ushirikiano pale walipoombwa kufanya hivyo na Waangalizi.

Katika uandaaji wa muswada wa ripoti hii, tunawashukuru wafuatao: Prof. Samuel Mushi, Prof. Rwekaza Mukandala, Prof. Amon Chaligha, Dk. Yusufu Lawi, Dk. Ambrose Kessy, Dk. Deogratius Rugaimukamu, Bi. Annmarie Mavenjina, Bw. Lawrence Kilimwiko na Bw. Lupa Ramadhani. Aidha tunatoa shukrani kwa Timu ya Menejimenti ya TEMCO, chini ya uongozi wa Prof. Rwekaza Mukandala (Mwenyekiti), Dk. Benson Bana (Meneja Mradi), Dk. Yusufu Lawi (Mchambuzi wa Siasa), Bw. Lupa Ramadhani (Afisa Utawala wa Mradi), Bw. Dunia Nassoro (Mhasibu wa Mradi) pamoja na Sekretariati ya REDET kwa kazi nzito waliyoifanya ili kuhakikisha utendaji mzuri wa kazi za kila siku za TEMCO. Juhudi na michango ya baadhi ya wanataaluma katika Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala, ambao walijitolea kufanya kazi ya kuandaa Muswada wa Mradi (Project Proposal) zinastahili pongezi za dhati.

Ieleweke kuwa ni TEMCO pekee ndiyo yenye dhamana ya ripoti hii yakiwemo maoni, makosa, na upungufu wowote uliomo. Ripoti hii haiakisi mawazo au misimamo ya watu binafsi na asasi zilizotajwa.

Kwa hiyo basi, ripoti hii ni mchango wetu kwa wapiga kura wa Tanzania, vyama vya siasa, Tume ya Uchaguzi Tanzania na Tume ya Uchaguzi Zanzibar, asasi mbalimbali za serikali zinazohusika na uchaguzi, jamii kwa ujumla na wadau wote wa siasa za Tanzania, wa ndani na wa nje ya nchi. Tuna matumaini kuwa ripoti hii itachangia katika kuboresha chaguzi, ili hatimaye ziwe huru na za haki.

## SURA YA PILI

## USAJILI WA WAPIGA KURA

### 1.0 UTANGULIZI

Usajili wa wapiga kura bado ni jambo muhimu sana kwa wanadharia na watendaji wa demokrasia. Licha ya kwamba usajili wa wapiga kura unatazamwa kama kigezo cha wananchi kushiriki katika chaguzi, au kama kipimo cha ubora wa maisha ya kisiasa na kiraia, watafiti wa ushiriki wanautazama usajili wa wapiga kura kama sehemu muhimu ya mchakato wa kidemokrasia. Hii ni kwa sababu, ili kuweza kupiga kura lazima wananchi wajisajili kwanza. Hata hivyo, lazima kuwe na mazingira mazuri na tulivu ya kuwavutia wapiga kura wengi ili wajisajili kwa mfano: kurahisisha mfumo wa usajili, uelewa na ufahamu mzuri wa wananchi juu ya jambo lenyewe, . Iwapo mambo haya yatatimizwa, basi wananchi wanaweza kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi. Uzoefu umeonyesha kwamba kukamilika kwa hatua hii ya kwanza ni tatizo kubwa, lakini kukiwa na idadi kubwa ya wanachi waliosajiliwa inachingia sana wananchi kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura[1].

Sura hii inazungumzia juu ya usajili wa wapiga kura wa mara ya kwanza na uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura (DKWK) wakati wa uchaguzi mkuu Tanzania, 2010. Sura hii imegawanywa katika sehemu kuu saba. Sehemu ya kwanza inatoa mwongozo wa kisheria kwa ajili ya usajili wa wapiga kura nchini Tanzania. Sehemu ya pili inajadili mwongozo wa kisheria wa DKWK nchini Tanzania. Sehemu ya tatu inaelezea mchakato wa usajili katika uchaguzi mkuu wa 2010. Sehemu ya nne inatazama michakato ya usajili na uboreshaji wa DKWK. Sehemu ya tano inajadili baadhi ya matatizo/changamoto za mchakato wa usajili kama zilivyoainishwa na Kamati ya Kusimamia Uchaguzi Tanzania (TEMCO). Sehemu ya sita inatathmini uwezo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) katika kuhodhi na kusimamia zoezi zima la uandikishaji wa wapiga kura pamoja na kuboresha DKWK katika uchaguzi mkuu wa 2010. Sehemu ya saba inahitimisha mjadala kuhusu usajili wa wapiga kura Tanzania Bara.

### 2.0 DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA NCHINI TANZANIA

Katika jitihada za kuwavuta wapiga kura zaidi, na wakati huohuo kukwepa baadhi ya matatizo yaliyojitokeza katika chaguzi zilizopita, Ibara ya 5(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ibara ya 12 ya Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 zilirekebishwa January, 2000 (TEMCO, 2005). Marekebisho hayo yalifungua njia ya kuanzishwa kwa DKWK nchini Tanzania. NEC iliweza kuanzisha mfumo huu mpya wa uandikishaji wa wapiga kura kwenye DKWK kwa msaada mkubwa kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP) kupitia programu yake ya uwezeshaji wa chaguzi, yaani *"Elections Support Programme"*. Lengo hasa la DKWK ni kuwapata na kuwasajili wapiga kura wapya na kuboresha kumbukumbu za waliopo. Mfumo huu mpya wa kusimamia kumbukumbu za wapiga kura kwa kuanzisha orodha ya kudumu una lengo la kuwezesha upatikanaji wa haraka wa taarifa za mpiga kura lakini pia unasaidia kuondoa upungufu unaohusiana na

[1] Hata hivyo, kama tutakavyoona katika sehemu zinazofuata, hii haikuwa sababu katika chaguzi zilizopita hivi karibuni Tanzania Bara, ambapo ni wapiga kura wachache sana walijitokeza (chini ya 40%).

usajili, kama vile usajili mara mbili. Ingawa Sheria ya Uchaguzi inaruhusu uanzishaji wa DKWK nchini Tanzania, mifumo miwili tofauti ilianzishwa na NEC na ZEC.

Hata hivyo kuanzisha DKWK nchini Tanzania, halikuwa jambo rahisi. Mahitaji ya kuwa na DKWK yalizua mjadala mzito kwa miaka kadhaa kutokana na matatizo mengi yaliyojitokeza kuhusu uandikishaji wa wapiga kura katika chaguzi zilizopita. Ni muhimu kukumbuka kwamba Tanzania ilikuwa ikitumia usajili maalumu wa wapiga kura, ambao ulitumika katika chaguzi zote zikiwemo chaguzi za 1995 na 2000. Katika chaguzi hizi, NEC, ilikuwa ikiandikisha wapiga kura upya katika kila uchaguzi, na hii ilisababisha matatizo mengi kama vile mpiga kura kuandikishwa mara mbili, upungufu katika usahihi wa kumbukumbu za mpiga kura, na kuandikishwa kwa watu ambao hawajafikia umri wa kupiga kura. Kwa hiyo hitaji la kuwa na DKWK lilipoanza baada ya uchaguzi wa 1995, lilipokelewa kwa shauku kubwa na wadau wote, ikiwa ni pamoja na vyama vya upinzani, asasi za kiraia na watafiti. Hata hivyo, kulikuwa na mashaka juu ya uadilifu na utendaji haki wa chombo ambacho kingekuwa na wajibu wa kutunza kumbukumbu hizo. Wakati DKWK lilipoanzishwa hatimaye mwaka 2004, lilionekana kuwa nafuu kubwa kwa wapiga kura wengi, hasa wale wa vyama vya upinzani ambao waliliona kama mfumo ambao ungepunguza matatizo ya uandikishaji wa wapiga kura na kuweka kumbukumbu zao mahali salama na pa kudumu.

Ikumbukwe kwamba, kwa kuanzisha DKWK, haina maana kwamba uandikishaji wa wapiga kura utakuwa wa mara moja na kukoma. Kwa maneno mengine DKWK litapitwa na wakati haraka sana. Hii ni kwa sababu wapiga kura wanatazamiwa kuendelea kubadili maeneo yao ya makazi (kuhama) na anwani zao, hivyo kutakuwa na haja ya kurekebisha au kuboresha daftari mara kwa mara. Zaidi ya hayo kutakuwa na wapiga kura wapya wenye sifa za kupiga kura kila mwaka, kwa mfano vijana wanaofikia umri unaostahili kupiga kura (miaka 18) na wengine ambao watapata uraia. Katika mazingira kama haya, kumbukumbu za wapiga kura zilizohifadhiwa katika DKWK zitatakiwa ziboreshwe kabla uchaguzi mwingine haujafanyika ili kuhakikisha kwamba wale watakaopiga kura wanastahili.

## 3.0 MCHAKATO WA KUANDIKISHA WAPIGA KURA TANZANIA

Baada ya maandalizi ya DKWK, NEC ilianza kuandikisha wapiga kura kwenye daftari hilo kuanzia tarehe 7 Oktoba mwaka 2004. Zoezi hilo lilimalizika tarehe 10 Mei, 2005. Tofauti na chaguzi nyingine ambapo utaratibu wa daftari haukuwepo, chaguzi za 2005 na 2010 DKWK lilitumika. Ili kuhakikisha usajili unaenda vizuri, NEC iliunda kanda ambazo zilisaidia kuendesha mchakato wa usajili wa wapiga kura wapya katika DKWK kwa nchi nzima (Tazama Jedwali Na.2.1).

**Jedwali Na. 2.1: Usajili wa Wapiga Kura kwa Kanda za Kiutawala Mwaka 2005**

| KANDA | MIKOA | TAREHE |
|---|---|---|
| **Kusini** | Mtwara, Lindi | *07/10/2004 – 03/11/2004 |
| **Kusini** | Mbeya, Iringa, Ruvuma, Rukwa | 28/10/2004 – 17/11/2004 |
| **Nyanda za Juu** | | |
| **Kati** | Dodoma, Singida, Tabora, Kigoma | 05/12/2005 – 25/12/2004 |
| **Ziwa** | Kagera, Mwanza, Mara, Shinyanga | 12/01/2005 – 01/02/2005 |
| **Kaskazini** | Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Manyara | 19/02/2005 – 11/03/2005 |
| **Pwani** | Dar es Salaam, Pwani, Morogoro | 29/03/2005 – 18/04/2005 |
| **Zanzibar** | Kaskazini Pemba, Kusini Pemba, Kaskazini Unguja, Kusini Unguja na Mjini Magharibi | ** 27/04/2005 -10/04/2005 |

*Katika kanda ya kusini, usajili wa wapiga kura uliongezwa muda kwa siku saba.
**Usajili Zanzibar ulifanyika kwa siku 14.
**Chanzo:** Grant Masterson (2009)

Kufuatia maboresho ya DKWK, idadi kamili ya wanachi walioandikishwa kupiga kura mwaka 2010 katika Tanzania Bara ilikuwa 20,137,303 (Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola, 2010). Daftari jipya la wapiga kura lina picha ya mpiga kura na utambulisho mwingine kama ilivyoainishwa katika sheria ya uchaguzi ya mwaka 1985 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2010). Baada ya mchakato wa usajili, mpiga kura anapewa kitambulisho cha kupigia kura chenye picha yake mwenyewe. Huko nyuma picha haikuwa ya rangi lakini baada ya kubadili kuwa ya rangi, iliwavuta wapiga kura wengi kwa sababu vitambulisho hivyo vipya vilionekana kuwa ni vizuri zaidi kuliko vile vya zamani, pia vilirahisisha utambulisho (Tazama sehemu ya 4.2).

### 3.1 Mwongozo wa Kisheria

Mwongozo wa kisheria unaosimamia usajili wa wapiga kura Tanzania Bara unapatikana katika Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 Sura ya 342 kama ilivyorekebishwa na sheria za chaguzi (mbalimbali) za 2010. Sheria hizi zinatoa vigezo vya uandikishwaji wa wapiga kura na uanzishaji wa DKWK. Sehemu muhimu kuliko zote ya sheria hii ni ya 12 ambayo inaruhusu uanzishwaji wa DKWK katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zaidi ya hilo, sehemu ya 15(1) inataja kwamba Tume itakuwa na jukumu la kuweka muda wa kupitia usajili wa wapiga kura katika kila wilaya na katika kila jimbo la uchaguzi.

### 3.2 Sifa za Kuandikishwa Kupiga Kura

Sehemu ya 10 (1) ya Sheria ya Uchaguzi inaweka bayana masharti na vigezo vya mtu anayestahili kuandikishwa kupiga kura. Sehemu hiyo inataja kwamba, kila raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 na zaidi, ana haki ya kujiandikisha kama mpiga kura na kupiga kura katika uchaguzi wowote wa Umma nchini Tanzania. Kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi, mpiga kura anayejiandikisha katika wilaya fulani ya uchaguzi na akawa mkazi katika wilaya nyingine katika Tanzania Bara, basi anaweza kuomba kuhamishia usajili wake kule anakoishi. Hii, hata hivyo, ilikua tofauti huko Zanzibar ambapo mpiga kura alitakiwa awe ameishi mfululizo katika Shehia hiyohiyo kwa miezi isiyopungua 36, kabla ya kusajiliwa. Kwa maana nyingine, wapiga kura katika Tanzania Bara na Zanzibar wanawajibika kwa mifumo na taratibu tofauti za usajili wa wapiga kura.

**3.3 Kukataliwa Kujiandikisha na Kigezo cha Ombi la Kuandikishwa Kupiga Kura**

Sheria ya Uchaguzi iko wazi kuhusu masharti na vigezo ambavyo kama havitatimizwa basi vinaweza kumzuia mwombaji kupata usajili. Kwa mfano, sehemu ya 11(1) inaeleza kwamba: "hakuna mtu atakayeandikishwa kama mpiga kura chini ya sheria hii kama:

- Atakuwa ametangaza kuwa raia mtiifu wa taifa jingine zaidi ya Tanzania
- Atakuwa amehukumiwa na sheria inayotumika Tanzania, kuwa hana akili timamu, au kuwekwa kizuizini.
- Atakuwa amehukumiwa kifo na mahakama yoyote Tanzania au kifungo kinachozidi miezi sita na mahakama au na mamlaka nyingine iliyopewa nguvu kisheria.
- Atakuwa amezuiwa kusajiliwa kama mpiga kura chini ya vifungu vya sheria hii au sheria yoyote inayotumika kuhusiana na makosa yanayohusu uchaguzi wowote".

Kwa hiyo kama mwombaji hana sifa za kuandikishwa, sheria inampa nguvu Msajili Mwandamizi kukataa kumwandikisha. Kama mwombaji hataridhishwa na uamuzi wa Msajili Mwandamizi, basi Msajili Mwandamizi atajaza Fomu Namba 3 na kumwelekeza kukata rufaa kwa Afisa Msajili. Mwombaji yeyote ambaye hataridhishwa na uamuzi ya Afisa Msajili basi anaweza kukata rufaa kupinga uamuzi huo katika Mahakama ya Wilaya kwa muda usiozidi siku 14. Mahakama ya Wilaya itatakiwa kutoa uamuzi juu ya rufaa hiyo ndani ya siku 14 tangu rufaa hiyo ilipoletwa na kupeleka uamuzi wake kwa Afisa Msajili. Rufaa itakapoamuliwa, Mahakama ya Wilaya itatakiwa kupeleka tamko kuhusu jina la mtu linalotakiwa kuandikwa au kufutwa kwenye daftari la wapiga kura.[2] Ufuatao ni utaratibu wa kutoa pingamizi dhidi ya wapiga kura walioandikishwa tayari.

a) Mpiga kura aliyeandikishwa anaweza kutoa pingamizi dhidi ya jina lake mwenyewe au jina la mtu mwingine kubaki katika DKWK kwa sababu mtu huyo hana sifa au hana sifa tena ya kuandikishwa kama mpiga kura, au kwamba mtu huyo amefariki. Afisa Msajili anatakiwa kutoa tangazo la pingamizi kwa watu ambao orodha yao katika daftari la wapiga kura imetolewa pingamizi kwa muda usiozidi siku saba baada ya kupokea pingamizi hilo na kuwataka walalamikiwa kutoa maelezo kwa maandishi.
b) Afisa Msajili anatakiwa kutoa tangazo la muda wa siku saba kwa wahusika wote akitaja muda, tarehe na mahali ambapo pingamizi litasikilizwa.
c) Afisa Msajili anatakiwa kufanya uchunguzi kwa umma kuhusu mapingamizi yote yaliyotolewa ndani ya siku saba.
d) Afisa Msajili anatakiwa kutoa uamuzi juu ya pingamizi kwa muda usiozidi siku saba tangu siku ya mwisho ya kutoa tangazo la uchunguzi.

Mtu yeyote ambaye hataridhishwa na uamuzi wa Afisa Msajili anaweza kukata rufaa katika mahakama ya Wilaya kwa muda usiozidi siku 14 tangu uamuzi huo utolewe. Mahakama ya Wilaya lazima isikilize na kuamua rufaa hiyo kwa uwazi katika muda usiozidi siku 14 tangu siku rufaa hiyo ilipowasilishwa. Uamuzi wa Mahakama ya Wilaya utakuwa wa mwisho[3]. Hivyo malalamiko na mapingamizi dhidi ya mpiga kura aliyesajiliwa yanaweza kufanywa kutokana na matatizo kama uingizaji wa taarifa za mpiga kura kimakosa, kuondolewa kwa taarifa za mpiga kura kimakosa au uvunjifu wa vifungu vya Sheria ya Uchaguzi.

[2] Tazama taarifa zaidi kuhusu michakato ya usajili wa wapiga kura kwenye tovuti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (http://www.nec.go.tz/votersregistration) 4/12/2010.
[3] ibid

### 3.4. Uzoefu wa Usajili wa Wapiga Kura Katika Siku Zilizopita: Baadhi ya Takwimu

Kwa ujumla, usajili wa wapiga kura Tanzania umekuwa wa mafanikio katika chaguzi zilizopita, hasa uchaguzi wa 2005 ambapo asilimia 96 ya wapiga kura waliojiandikisha walijitokeza kupiga kura (Tazama Jedwali Na. 2.2).

**Jedwali Na. 2.2: Mchanganuo wa Idadi ya Wapiga Kura Waliokusudiwa Kuandikishwa na Idadi Kamili ya Wapiga Kura Walioandikishwa Katika kila Mkoa**

| Na | MKOA | WALIOKUSUDIWA | WALIOANDIKISHWA | ASILIMIA (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mtwara | 635,114 | 572,027 | 90.1 |
| 2. | Lindi | 432,563 | 395,730 | 91.5 |
| 3. | Iringa | 744,322 | 670,547 | 90.0 |
| 4. | Mbeya | 1,046,971 | 942,053 | 90.0 |
| 5. | Rukwa | 471,787 | 437,833 | 92.9 |
| 6. | Ruvuma | 576,730 | 505,512 | 87.0 |
| 7. | Kigoma | 658,418 | 595,074 | 90.38 |
| 8. | Singida | 524,838 | 474,603 | 90.43 |
| 9. | Dodoma | 847,259 | 748,629 | 88.36 |
| 10. | Tabora | 816,868 | 722,435 | 88.44 |
| 11. | Mara | 636,463 | 681,981 | 108 |
| 12. | Kagera | 910,087 | 912,256 | 100.2 |
| 13. | Shinyanga | 1,288,164 | 1,243,157 | 97 |
| 14. | Mwanza | 1,407,357 | 1,404,211 | 97.36 |
| 15. | Arusha | 650,755 | 656,398 | 101 |
| 16. | Tanga | 823,961 | 791,668 | 96 |
| 17. | Kilimanjaro | 705,549 | 659,514 | 93 |
| 18. | Manyara | 501,516 | 483,083 | 96 |
| 19. | Morogoro | 921,217 | 897,347 | 97 |
| 20 | Pwani | 466,797 | 456,781 | 98.0 |
| 21 | Dar es Salaam | 1,503,494 | 1,691,983 | 113.0 |
| | **TOTAL** | **16,570,230** | **15,942,824** | **96.0** |

Chanzo: NEC, 2005

Takwimu za maboresho ya DKWK kati ya mwaka 2007 na 2008 zinaonyesha kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa la wapiga kura wapya walioasajiliwa (Tazama jedwali na.3) Takwimu hizi zinaonyesha kuwa Watanzania wanathamini chaguzi na ndiyo maana wengi wamejitokeza kusajiliwa. Hata hivyo, usahihi wa idadi ya wapiga kura bado ni kitendawili. Hii ni kwa sababu NEC ilitegemea sana sensa ya mwaka 202 kufanya makadirio ya wapiga kura wanaotegemewa kujiandikisha, wakati sensa hii ilifanyika takriban miaka minane iliyopita. Hii ina maana kwamba, makadirio haya yanaweza kuwa si sahihi wakati wa uchaguzi kutokana na tabia ya mabadiliko ya idadi ya watu. Kuna watu wengi wanaoshindwa kujiandikisha, kinyume na kuliko takwimu za idadi ya waliojiandikisha zinavyoonyesha. Baadhi ya wananchi wenye sifa za kupiga kura wanaweza kuwa hawamo katika DKWK.

**Jedwali Na. 2.3: Maboresho ya DKWK (2007 - 2008)**

| Na | Mkoa | Walioandikishwa | Maboresho | Masahihisho | Waliofariki |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ARUSHA | 723,874 | 73,629 | 27,798 | 1,109 |
| 2 | DAR ES SALAAM | 1,912,662 | 231,547 | 97,869 | 1,476 |
| 3 | DODOMA | 849,561 | 90,122 | 32,617 | 2,910 |
| 4 | IRINGA | 758,262 | 84,201 | 31,670 | 10,183 |
| 5 | KAGERA | 1,048,294 | 133,700 | 56,244 | 10,502 |
| 6 | KIGOMA | 666,114 | 65,136 | 21,604 | 1,383 |
| 7 | KILIMANJARO | 739,529 | 78,129 | 32,874 | 3,803 |
| 8 | LINDI | 450,620 | 61,965 | 28,574 | 2,476 |
| 9 | MANYARA | 533,894 | 49,602 | 18,357 | 905 |
| 10 | MARA | 752,906 | 88,967 | 33,738 | 2,049 |
| 11 | MBEYA | 1,056,126 | 104,272 | 34,460 | 5,566 |
| 12 | MOROGORO | 988,113 | 92,516 | 36,878 | 2,761 |
| 13 | MTWARA | 658,220 | 85,532 | 39,164 | 3,130 |
| 14 | MWANZA | 1,586,919 | 188,679 | 79,938 | 3,795 |
| 15 | PWANI | 518,841 | 48,582 | 22,686 | 1,744 |
| 16 | RUKWA | 489,289 | 61,204 | 20,067 | 1,867 |
| 17 | RUVUMA | 607,920 | 103,120 | 30,761 | 2,775 |
| 18 | SHINYANGA | 1,380,953 | 151,642 | 53,279 | 2,306 |
| 19 | SINGIDA | 545,074 | 62,445 | 22,753 | 1,640 |
| 20 | TABORA | 840,014 | 116,510 | 39,828 | 2,262 |
| 21 | TANGA | 891,942 | 102,562 | 45,011 | 4,519 |
| 22 | *ZANZIBAR | 15,540 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | | **18,014,667** | **2,074,065** | **806,170** | **69,161** |

**Chanzo:** Tovuti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (http://www.nec.go.tz/?modules=registration&sub) 7/12/2010.

### 4.0 MCHAKATO WA USAJILI WA 2010

Hatua ya kwanza ya usajili wa wapiga kura ilikuwa ni kuwapata na kuwaelimisha maafisa watakaofanya kazi ya usajili na kuanzisha vituo vya usajili. Sehemu ya 8 ya Sheria ya Maafisa Wasajili na 13 ya 2004, inataja kwamba, "…kila Mkurugenzi wa Jiji, Manispaa, Mji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya atakuwa Afisa Msajili kwa lengo la kusajili wapiga kura katika kila Jimbo la Uchaguzi, na Msajili huyo anaweza kuwa kwa ajili ya Jimbo moja au zaidi ya jimbo moja la Uchaguzi". Baada ya kumalizika kwa zoezi la usajili, Maafisa Wasajili walipeleka fomu zote kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi ambaye aliidhinisha maandalizi ya daftari la muda la wapiga kura. Baada ya daftari la muda la wapiga kura kuandaliwa, lilipelekwa kwa maafisa wasajili kwa ajili ya uhakiki katika ngazi ya kata. Hii iliwawezesha wapiga kura kuangalia kama majina na sifa zao zimeingizwa kwa usahihi katika daftari la wapiga kura na hivyo kuweza kutoa pingamizi kwa wale walioandikishwa bila kuwa na sifa za kutosha. Maafisa wasajili walitoa maamuzi juu ya mapingamizi yaliyotolewa na kufanya masahihisho ya lazima na kupeleka marekebisho hayo kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi.

### 4.1 Ajira na Mafunzo kwa Watumishi wa Usajili

Ajira na mafunzo kwa watumishi wa usajili ilikuwa ni shughuli nyingine muhimu katika maandalizi ya daftari la wapiga kura 2010. Mchakato huu ulifanana sana na ule wa 2005; kwa mfano, makarani wa usajili na wapiga picha, pamoja na mafunzo yalifanyika katika ngazi ya

jimbo kupitia Maafisa wa Usajili (ROs) na wasaidizi wao (AROs). Hii ilifanyika kwa majimbo yote ya uchaguzi ya Tanzania Bara. Kila jimbo lilitafuta watumishi kwa ajili ya kazi hii ndani ya jimbo hilohilo. Wengi waliochaguliwa walikuwa ni waalimu wa shule za msingi na sekondari. Nafasi hizi zilitangazwa katika magazeti ya ndani, mbao za matangazo, na redio. Kama ilivyoanishwa na TEMCO, 2005 waombaji wa nafasi hizi walitakiwa kuwa watu waadilifu, waaminifu na wenye nia thabiti ya kufanya kazi na walitakiwa pia kutokuwa na ushabiki wa vyama vya siasa (yaani wasiwe na nafasi ya uongozi katika chama chochote cha siasa). Walitakiwa pia kuwa wakazi wa jimbo lilelile la uchaguzi. Wapiga picha walitakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu wa kupiga picha. Waliochaguliwa walikula kiapo cha usiri, utii na uaminifu kwa NEC. Makarani wa usajili na wapiga kura wote kwa pamoja walihudhuria semina elekezi kwa siku mbili.

**4.2 Maboresho ya DKWK**

Kila mchakato wa uchaguzi huanza kwa kutambua idadi ya wenye sifa za kupiga kura katika eneo ambapo uchaguzi utafanyika. Hii hufanyika kwa kuandikisha wapiga kura wapya, au kuboresha kumbukumbu za wapiga kura ambao tayari wamesajiliwa katika DKWK. Maboresho haya yanasaidia watu wenye sifa ya kupiga kura kuweza kupiga kura siku ya uchaguzi. Vivyo hivyo uboreshaji unasaidia kuhakiki usahihi wa wapiga kura walioandikishwa kwa kuondoa majina ya wapiga kura ambao wanakosa sifa za kupiga kura, kwa mfano waliofariki na waliohamia katika makazi mapya na kusajili wapiga kura wapya. Lazima ifahamike kwamba, wachunguzi wa TEMCO hawakuangalia muda wa usajili ambao ulikuwa ni kati ya mwezi Julai na Agosti 2010. Hata hivyo, wachunguzi wa TEMCO waliombwa kutengeneza upya taarifa za usajili kama zilivyopatikana katika vyanzo vya habari mwishoni mwa mwezi Agosti, 2010.

Kwa kawaida, Uchaguzi Mkuu nchini Tanzania hufanyika kila baada ya miaka mitano, lakini ili mtu aweze kupiga kura katika uchaguzi wowote, iwe ni wa Rais, Wabunge au Madiwani, lazima aandikishwe kwanza. Kama ilivyojadiliwa katika chaguzi zilizopita, DKWK lazima liboreshwe mara zote na NEC. Baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2005, NEC imeshaboresha DKWK mara mbili; katika mwaka 2007/2008 na 2009/2010. Wapiga kura huwa wanakumbushwa kuhakiki au kurekebisha kumbukumbu zao kama vile kubadilika kwa makazi yao, kupoteza sifa za kupiga kura wakati uchaguzi mkuu au uchaguzi mdogo unakapokaribia. Kwa mfano katika uchaguzi mkuu uliopita hivi karibuni, marekebisho ya mwisho ya daftari la wapiga kura yalianza mwezi Aprili hadi Julai, 2010. Wapiga kura walipata nafasi ya kurekebisha kumbukumbu zao katika DKWK. Maboresho hayo yalijumuisha kuandikisha wapiga kura wapya ambao walikuwa wametimiza umri wa kupiga kura, kuhamisha taarifa kwa wale waliokuwa wamehamia katika makazi mengine, kuwafuta katika daftari wale waliopoteza sifa za kupiga kura ikiwa ni pamoja na waliofariki. Kwa mujibu wa TEMCO (2010), marekebisho ya kwanza ya daftari la wapiga kura, yalisababisha ongezeko la wapiga kura kutoka takriban milioni kumi na sita (15,935,493) mwaka 2005, hadi milioni kumi na tisa (19,685,239) mwaka 2010 (Tanzania Bara). Ikumbukwe kwamba Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) pia ilisajili watu wenye sifa za kupiga kura kwa ajili ya mgombea urais wa Muungano na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano. Kwa muktadha huo, Tume ya Uchaguzi Zanzibar ilisajili wapiga kura 407,658 katika Uchaguzi Mkuu wa 2010 na hivyo kufanya jumla kuu ya wapiga kura walioandikishwa Tanzania Bara na Visiwani kufikia 20,137,303. Hili ni ongezeko la takriban 20% la wapiga kura wapya ukilinganisha na takwimu za usajili za mwaka 2005. Kwa kulinganisha, karibu wapiga kura 8,929,969 na

10,112,365 waliandikishwa katika chaguzi za 1995 na 2000 kwa mtiririko huo (TEMCO, 2000).

Taarifa ya Majimbo ya Uchaguzi ya TEMCO inaonyesha kulikuwa na mwamko mkubwa wa wapiga kura wapya waliojiandikisha, lakini pia ni wapiga kura wachache waliojitokeza kukagua taarifa zao katika DKWK. Hii inatokana na sababu mbalimbali, kwa mfano, watu wengi walijitokeza kuandikishwa ili wapate vitambulisho ambavyo wangeweza kuvitumia kwa shughuli mbalimbali kama vile benki na katika usajili wa simu zao. Ijulikane kwamba Tanzania haitoi vitambulisho vya uraia kwa raia wake. Ikizingatiwa kwamba watu wengi hawana vitambulisho rasmi kama vile pasipoti, na leseni za udereva, basi waliona vitambulisho vya kupigia kura kama vitambulisho mbadala. Hata hivyo, baada ya usajili, wengine hawakwenda kuhakiki taarifa zao siku ya uchaguzi.

Kwa ujumla, kulikuwa na upungufu mwingi ulioripotiwa kwa TEMCO kuhusiana na jinsi zoezi zima lilivyoendeshwa. Kwa mfano, baadhi ya ripoti zinaonyesha wazi kuwa watendaji wa mitaa wanaohusika na usajili hawakuwa na nia thabiti ya kusimamia kikamilifu zoezi hilo. Hii ilionekana katika mkoa wa Dar es Salaam ambapo halikuonekana tangazo hata moja katikati ya jiji lililohamasisha watu kwenda kuhakiki na kuboresha taarifa zao katika DKWK. Zaidi ya hayo, hakukuwa na jitihada za makusudi zilizofanywa na uongozi wa mkoa na serikali za mitaa kuwajulisha wapiga kura umuhimu wa kuhakiki na kurekebisha taarifa zao katika DKWK. Katika mikoa mingine pia mwamko wa watu kwenda kuhakiki na kuboresha taarifa zao ulikuwa mdogo. Kwa mfano baadhi ya ripoti kutoka katika mkoa wa Kilimanjaro zilionyesha watu hawakuhudhuria katika vituo vya maboresho kwa sababu mbalimbali: Kwanza ni mtu mmoja tu katika familia aliyekagua daftari kwa niaba ya wenzake; pili wapiga kura walitumia vitambulisho vyao vya kupigia kura kwa nyingine na hivyo kupiga kura kulipewa uzito mdogo. Hii ina maana kwamba, ni wapiga kura wachache tu waliojitokeza kwenda kuhakiki taarifa zao baada ya kupewa vitambulisho vya kupigia kura. Mwisho, wapiga kura wengi walijitokeza kuhakiki DKWK katika siku za mwisho, licha za jitihada za maafisa wasajili kuwahamasisha watu kupitia vikundi vya sanaa, matangazo kupitia vipaaza sauti vilivyokuwa vimefungwa kwenye magari, na kupeleka DKWK katika kila kata ili kurahisisha zoezi la uhakiki. Kutokana na hilo, ilikuwa vigumu kushughulikia matatizo ya watu ambao majina yao hayakuwemo katika DKWP kwa wakati muafaka, kabla ya siku ya uchaguzi (Ripoti ya Uangalizi ya Jimbo la Temeke ya TEMCO, 2010).

Taarifa ya upotevu wa vitambulisho vya kupigia kura katika majimbo mengi ya uchaguzi ilionyesha kuwa upotevu ulikuwa mdogo. Ripoti nyingi za TEMCO kwa ujumla zinaonyesha kwamba idadi ya watu waliotoa taarifa ya kupotea au kuharibika kwa vitambulisho vyao vya kupigia kura ilikuwa ndogo. Kwa upande mmoja kuna wale waliotoa taarifa ya kupotea au kuharibika kwa vitambulisho vyao vya kupigia kura, kwa sababu walitambua kuwa kupiga kura ni haki yao ya msingi. Kwa upande mwingine, kuna wale waliotoa taarifa kwa sababu kadi zao za kupigia kura zilikuwa kama nyezo kwao kwa kuwa walizitumia kama vitambulisho vya kawaida (Ripoti ya Jimbo la Uchaguzi, Njombe, 2010). Katika majimbo mengine ya uchaguzi, kulikuwa na ongezeko la waliojitokeza kuhakiki kwa sababu safari hii picha katika kitambulisho cha mpiga kura zilikuwa ni za rangi tofauti na ilivyokuwa zamani. Baadhi ya Maafisa Wasajili waliohojiwa na wachunguzi wa TEMCO walidai kwamba watu wengi walioelewa umuhimu wa kadi zao za kupigia kura walitoa taarifa mapema baada ya kupotea au kuharibika kwa kadi hizo kwa sababu hizohizo tulizokwisha zitaja. Hii inatiwa

nguvu na ripoti kutoka Jimbo la Uchaguzi la Lindi Mjini ambayo inaonyesha kwamba idadi ya watu waliojitokeza kuhakiki DKWK ilikuwa ndogo sana. Mwangalizi anasema kwamba, wale ambao hawakutilia maanani kuhakikiki DKWK hawakuweza kupiga kura siku ya uchaguzi. Ni wazi kwamba wale ambao hawakuweza kupiga kura walileta malalamiko yao dhidi ya Maafisa Wasajili ambao walituhumiwa kufuta majina ya watu katika DKWK kwa maslahi binafsi. Baadhi ya sababu kwa nini watu hawakutaka kutoa taarifa ya kupotea au kuharibika kwa vitambulisho vyao vya kupigia kura ni pamoja na muda na urasimu mkubwa katika kupata kitambulisho kipya, ikiwemo kutoa hati ya polisi kuonyesha upotevu huo. Baadhi ya wapiga kura walitoa taarifa kuhusu matatizo yao kwa maafisa watendaji wa kata siku chache kabla ya uchaguzi wakitarajia kuruhusiwa kupiga kura. Hata hivyo maafisa hawa hawakuruhusiwa kutoa vitambulisho vipya nje ya utaratibu uliowekwa.

## 5.0 MATATIZO KATIKA MCHAKATO WA USAJILI WA WAPIGA KURA

### 5.1. Elimu kwa Wapiga Kura na Mwitikio

Uzoefu uliopatikana kutokana na uangalizi wa uchaguzi uliofanyika hivi karibuni Tanzania uliofanywa na TEMCO unaashiria kwamba elimu kwa wapiga kura ilitolewa kikamilifu. Kwa upande mmoja, baadhi ya Wasimamizi Waandamizi wa Uchaguzi walisema kwamba elimu kwa wapiga kura ilikuwa ni changamoto kubwa ambayo iliathiri zoezi zima la uboreshaji wa DKWK. Kwa upande mwingine, kulikuwa na jitihada zilizofanywa na maafisa wa NEC kutoa elimu kwa wapiga kura. Kwa mfano, Mwangalizi wa TEMCO katika Jimbo la Bukoba Mjini anaripoti kwamba taarifa kuhusu uboreshaji wa DKWK zilisambazwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari, ikiwa ni pamoja na vituo vya redio vilivyopo jimboni humo kama vile Redio Kasibante FM na Redio Vision FM. Baadhi ya matangazo, vipeperushi na matamasha ya muziki yalitumika kuhamasisha watu kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kurekebisha taarifa zao katika DKWK. Licha ya jitihada hizi, ni watu wachache tu waliojitokeza kurekebisha kumbukumbu za taarifa zao kwenye Daftari la Wapiga Kura. Kutoka Njombe, mtazamaji wa TEMCO anaarifu kwamba uhamasishaji uliofanywa na vyama vya siasa hasa vya upinzani ulisaidia kukuza uelewa na umuhimu wa kujiandikisha na kuhakiki taarifa zilizopo katika DKWK. Baadhi ya vyama vya upinzani vilifanya kampeni ya nyumba kwa nyumba kuhamasisha watu kujiandikisha. Kulikuwa na mashirika mengine yakisaidiwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) ambayo nayo yalikuwa yakitoa elimu kwa wapiga kura, lakini ni mapema mno kutoa tathmini ya mchango wao katika zoezi la usajili wa wapiga kura.

### 5.2 Kujiandikisha Mara Mbili

Katika majimbo mengi ya uchaguzi, kulikuwa na kata mpya zilizoanzishwa karibu na siku ya uchaguzi, na baadhi ya watu ilibidi waambiwe wakajisajili katika hizi kata mpya. Kutokana na uwezo mdogo wa baadhi ya maafisa wasajili katika kuhakiki taarifa zilizotolewa na wapiga kura, baadhi ya wapiga kura ambao walikuwa wamepoteza vitambulisho vyao vya kupigia kura au walioambiwa wajiandikishe tena walijikuta wanajiandikisha mara mbili katika kata tofauti.

Kwa ujumla, kulikuwa na hisia nzito kati ya watu wa kawaida na maafisa wa usajili kwamba ulikuwepo upungufu mkubwa katika zoezi la usajili, ikiwemo kujisajili mara mbili. Katika baadhi ya majimbo hii ilisababisha shutuma kadhaa kutokana na tuhuma za kununua na kuuza kadi za kupigia kura. Japo ni vigumu kutolea ushahidi tuhuma hizi, kuna dalili kwamba rushwa imejikita katika zoezi zima la usajili wa wapiga kura. Japo katika baadhi ya majimbo wapiga kura hawakuhitajika kutoa ripoti ya polisi au barua kutoka kwa Afisa

Mtendaji wa Kata kama ushahidi kwamba wamepoteza kadi zao za kupigia kura, wapiga kura wasio waaminifu walitumia udhaifu huo na kutumia vibaya nafasi hiyo kwa kujiandikisha mara mbili (Ripoti ya Jimbo la Lindi, 2010).

**5.3 Majina Kutokuwepo katika DKWK**

Ripoti ya TEMCO inaonyesha kwamba kulikuwa na baadhi ya majina ambayo yalikosekana katika DKWK. Baadhi ya majina katika daftari hayakwenda sambammba na orodha halisi ya wapiga kura iliyohakikiwa. Kwa mfano, Mwangalizi wa Uchaguzi katika Jimbo la Ilala aligundua kuwa baadhi ya watu walishindwa kupiga kura katika kituo cha kupigia kura cha Hospitali ya Amana kwa sababu majina yao hayakuwemo katika daftari la wapiga kura. Ingawa baadhi ya majina hayakuwepo bila kutoa sababu yoyote, kulikuwa na mengine ambayo yaliwekewa alama kuwa hayajathibitishwa au hayana sifa. Kuna wengine ambao walikuwa wameshakamilisha taratibu zote za usajili na kusajiliwa lakini majina yao hayakuwemo katika orodha ya wapiga kura, kama ilivyoonekana siku ya uchaguzi. Tatizo kama hili liliripotiwa pia katika mkoa wa Mara. Kwa mfano, Mwangalizi wa TEMCO jimbo la Mwibara anaarifu kwamba baadhi ya wapiga kura hawakuonekana katika DKWK, na majina yao hayakubandikwa katika mbao za matangazo katika vituo husika kwa hiyo hawakuweza kupiga kura. Tatizo hili lilikuwa limesambaa sana katika mkoa wa Mara. Baadhi ya majina ya wapiga kura yalikosewa kuandikwa, wengine taarifa zao hazikuwa sambamba na taarifa katika vitambulisho vyao vya kupigia kura. Ilishangaza kuona baadhi ya wapiga kura walikuwa wameondolewa sifa za kupiga kura katika daftari bila stahili. Mfano ni pale ambapo mpiga kura mmoja aliyewekewa alama kuwa amefariki lakini akajitokeza katika kituo cha usajili. Tukio hili la kusikitisha liliripotiwa na mwangalizi wa TEMCO wa mkoa wa Mara, Jimbo la Musoma Mjini katika kituo cha kupigia kura cha Maktaba ya Mkoa[4].

Katika majimbo mengine, kulikuwa na makosa mengi sana ya uchapaji wa majina ya wapiga kura. Katika baadhi ya maeneo, tatizo hili lilitatuliwa kwa kutumia kifaa maalumu cha kuhakiki usahihi wa jina la mpiga kura na matatizo mengine katika siku ile ya uchaguzi. Katika baadhi ya vituo vya kupigia kura ambapo mashine hii haikuwepo, basi wapiga kura walikwenda kwenye vituo vingine vya jirani.

Kimsingi matatizo haya yaliyoripotiwa ni ya mtu mmojammoja na siyo ya kitaasisi au kikundi. NEC ilitoa muda wa kutosha kwa watu kujiandikisha na kuhakiki taarifa zao katika DKWK. Katika maeneo mengine kama Dar es Salaam, muda wa usajili na uhakiki uliongezwa pia. Ripoti za TEMCO zinaonyesha kwamba baadhi ya wapiga kura hawakujitokeza kwa wakati kuhakiki taarifa zao katika daftari na hivyo ilikuwa vigumu kutatua matatizo yao siku ya uchaguzi kwa sababu tayari walikuwa wameshachelewa mno, ndiyo sababu waliambiwa waangalie majina yao katika vituo vya kupigia kura vilivyokuwa jirani. Kwa upande mwingine, tabia ya kutunza na kuboresha DKWK, haikupewa hamasa stahili na NEC. Hii ilionekana katika baadhi ya majimbo ambapo hakukuwa na matangazo kuhusu umuhimu wa wapiga kura kujiandikisha na kuhakiki taarifa zao katika DKWK. Ilibainika pia kuwa baadhi ya serikali za mitaa hazikuwa na utaratibu mzuri wa kuweka kumbukumbu kama za idadi ya vifo, wanaohama kutoka jimbo moja kwenda jingine, na idadi ya watu waliotimiza umri wa kupiga kura (Ripoti ya Mkoa wa Dar es Salaam, 2010). Kwa mfano ilikuwa vigumu kupata takwimu sahihi za watu waliofariki au waliohamia katika majimbo mengine, ambao tayari walikuwa wameandikishwa katika baadhi ya majimbo mkoani Kilimanjaro (Ripoti ya Jimbo la Vunjo, 2010). Kama NEC haitafanya jitihada za

[4] Mpiga kura aliyetajwa kuwa 'amefariki' ni mwenye jina la Rehema Ayoub Kagire, Kitambulisho na. 47370683. Kwa maelezo zaidi, soma Ripoti ya Mkoa wa Mara.

mukusudi kuingilia kati uboreshaji wa daftari katika ngazi za chini, basi DKWK la Taifa litabaki kuwa na taarifa zisizo sahihi na zilizopitwa na wakati. Hata hivyo, wakati daftari la wapiga kura lilipelekwa hadi ngazi ya kata mwaka 2005, katika uchaguzi wa 2010, lilipelekwa hadi kwenye vituo vya usajili. Kwa namna hii, wapiga kura walikuwa na muda wa kutosha kulifikia daftari na kuhakiki taarifa zao kama vile namba za usajili na usahihi wa majina yao. Inashangaza kwamba ni watu wachache sana waliojitokeza kuhakiki taarifa zao katika daftari kama ilivyojadiliwa katika sehemu ya 4.2. Zaidi ya hayo, Mfumo wa Mawasiliano ya Wapiga Kura (VIS) uliowawezesha wapiga kura kuangalia taarifa zao katika orodha ya NEC kupitia ujumbe mfupi wa simu ulianzishwa na NEC katika Uchaguzi Mkuu wa 2010. Kulikuwa na mkataba maalumu kati Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCA) na NEC ambapo nambari 15455 ilitolewa ili kuwawezesha wapiga kura kujua vituo vyao vya kupigia kura na hivyo kurahisisha zoezi la kupiga kura siku ya uchaguzi. Ni wazi kwamba ni watu wachache sana walioifahamu huduma hii kwani ilicheleweshwa sana kutolewa. Baadhi ya watoa huduma za simu kama Zain (sasa Airtel) hawakumudu sana kusaidia utaratibu huu mpya[5].

**5.4 Taarifa za Usajili wa Mpiga Kura**

Ukiondoa takwimu za sensa iliyopita, hakukuwa na taarifa nyingine ambayo ingeweza kutegemewa kama msingi wa kufanya makadirio ya idadi ya watu wenye sifa za kupiga kura katika kila jimbo. Kwa maana hii, Wasimamizi wa Uchaguzi walionekana kutumia mbinu tofauti ambazo baadhi yake zilitofautiana na takwimu za NEC. Kwa mfano, idadi ya wapiga kura iliyotolewa na Afisa Msajili wa Singida Mjini ya 63,235, ilikuwa chini ya idadi iliyotolewa na Afisa wa Uchaguzi wa Wilaya baada ya kuhesabu kura za Rais katika jimbo hilo ambayo ni 64,525; ambayo ilibadilika tena kuwa 65,515 wakati wa kuhesabu kura za wabunge (Ripoti ya Jimbo la Singida Mjini, 2010). Maafisa wengi wa Usajili walitumia kanuni iliyotolewa na NEC lakini kanuni hii ilisaidia kuwafahamu wale tu waliotegemewa kujiandikisha na siyo wapiga kura wenye sifa za kupiga kura. Mfano mzuri ni kutoka Jimbo la Tandahimba ambapo kulikuwa na tatizo la wapiga kura ambao taarifa zao hazikuwepo baada ya kata mpya kuanzishwa. Jumla ya wapiga kura walioandikishwa ilikuwa ni 124,832, baada ya marekebisho ya mara ya mwisho ya DKWK. Mwezi Julai, 2010, kata nane mpya zilianzishwa katika Jimbo la Tandahimba na hivyo kufanya jumla ya kata zilizopo katika jimbo hilo kufikia 30. Inashangaza kuona kwamba, kata mpya zilisababisha ongezeko la wapiga kura walioandikishwa kutoka 124,832 hadi 125,6743 kutoka katika vituo 368 vya kupigia kura katika jimbo hilo. Kutokana na taarifa ya Mtazamaji wa TEMCO, hakukua na maelezo yoyote yaliyotokana na tofauti hii. Kutokana na mifano kutoka majimbo haya mawili, ni wazi kwamba kulikuwa na tatizo kubwa la kukadiria idadi kamili ya watu walioandikishwa na wenye sifa za kupiga kura katika baadhi ya majimbo ya uchaguzi.

Zaidi ya hayo, changamoto kubwa katika kuboresha DKWK ilikuwa ni kupata takwimu sahihi na za uhakika kuhusu watu walioandikishwa, wale ambao walikwisha fariki au kuondoka katika jimbo lile. Iligundulika kwamba wapiga kura waliokuwa wakiondoka na kuingia katika jimbo hawakuwa wakitoa taarifa, na hivyo kuwa vigumu kupata takwimu sahihi.Vivyo hivyo taarifa za wapiga kura waliofariki katika jimbo hazikuwa zikiripotiwa. Kwa mfano Msimamizi Mwandamizi wa Uchaguzi katika Jimbo la Bukoba Mjini alieleza bayana kwamba kulikuwa na wapiga kura 63 katika DKWK waliokwisha fariki lakini taarifa zao hazikuwemo, kwa hiyo ilikuwa vigumu kutoa takwimu sahihi. Katika sehemu hii, tunaweza kuhitimisha kwa kusema kwamba japo ngazi za chini zilifanya kazi kubwa sana ya kusajili wapiga kura, NEC (katika ngazi ya Taifa) ilionekana kudhibiti mchakato mzima wa

[5] Kwa maelezo zaidi, tazama Sura ya Nne katika Ripoti hii juu ya "Usimamizi wa Chaguzi".

usajili. Katika baadhi ya maeneo, ngazi hizi za chini hazikupata taarifa madhubuti kuhusu DKWK na wengine walipata taarifa hizo siku chache tu kabla ya siku ya uchaguzi.

### 5.5 Mawakala wa Vyama vya Siasa

Katika kuboresha DKWK, vyama vya siasa vilitakiwa kuwa na mawakala wao katika kila kituo cha usajili kama ilivyoelezwa na sehemu ya 15A(1): "chama cha siasa kinaweza kumteua mtu mmoja kuwa wakala wa usajili katika kila kutuo cha usajili katika jimbo la uchaguzi kwa lengo la: (a) kuhakiki watu wenye sifa za kusajiliwa na (b) kumsaidia Msajili Mwandamizi katika kufuata sheria na taratibu zilizowekwa kuhusu usajili wa wapiga kura." Wakati Chama Cha Mapinduzi (CCM) kiliweza kuweka mawakala karibu katika vituo vyote vya usajili, vyama vingi vya upinzani havikuweza kufanya hivyo. Baadhi ya vyama vya upinzani, vilidai kwamba havikuwa na uwezo wa kuwalipa mawakala wote na hivyo viliweka mawakala katika zile kata za usajili ambazo wagombea wao walikuwa na nguvu na hivyo kuwa na uwezakano mkubwa wa kushinda. Kitendo cha vyama vya siasa kushindwa kuweka mawakala katika baadhi ya vituo vya usajili kinaweza kutafsiriwa kama mojawapo ya udhaifu wa mfumo wa uchaguzi wa Tanzania. Tangu sheria ilipobadilishwa baada ya uchaguzi mkuu wa 1995, kuondoa ruzuku kwa vyama vya siasa wakati wa chaguzi, mambo yamezidi kuwa magumu, hasa kwa vyama vya upinzani visivyo na nguvu kubwa ya kiuchumi.

## 6.0 NEC NA USIMAMIZI WA MCHAKATO WA USAJILI

Kwa ujumla, NEC ilionyesha uwezo mkubwa wa kitaasisi katika mchakato wa usajili. Ukiacha matatizo machache yaliyojitokeza, vifaa vyote vya usajili vilitolewa vya kutosha na kwa wakati muafaka. Maafisa wa NEC walitembelea vituo vya usajili mara kwa mara na walitoa ufumbuzi kwa matatizo yaliyoripotiwa ikiwa ni pamoja na kuharibika kwa kamera mara kwa mara. Isitoshe, vituo vya usajili vilikuwa na wafanyakazi wa kutosha, vilifunguliwa kwa wakati muafaka kwa ajili ya wapiga kura kujiandikisha na kuhakiki taarifa zao katika daftari. NEC pia ilibandika daftari la muda la wapiga kura katika ngazi ya kata kwa muda mrefu wa kutosha. Katika baadhi ya majimbo muda wa usajili uliongezwa ili kuwaruhusu wapiga kura zaidi kujiandikisha na kuhakiki taarifa zao katika DKWK. Hii ilitoa fursa pia kwa wale walioandikishwa kuangalia orodha ya walioandikishwa kutoa pingamizi kwa watu ambao hawakuwa na sifa za kusajiliwa. Ripoti za TEMCO zinaonyesha kwamba, kulikuwa na malalamiko mengi kuhusu baadhi ya wapiga kura kuandikishwa zaidi ya mara moja. Mkurugenzi wa Uchaguzi baadaye alikiri NEC kugundua matatizo ya takriban wapiga kura 2000 kusajili mara mbili nchi nzima. Ulinzi katika vituo vya usajili ulikuwa wa kutosha isipokuwa vituo vichache havikuwa na walinzi. Licha ya upungufu huu, hakukuwa na matukio makubwa ya kiusalama yaliyoripotiwa.

Kwa ujumla, wadau mbalimbali na waangalizi wa zoezi la usajili, wakiwemo waangalizi wa TEMCO, wameipongeza sana NEC kwa jinsi ilivyosimamia vizuri zoezi la kuandikisha wapiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa 2010. Kwa jumla, usajili ulifanyika vizuri karibu katika majimbo yote ambayo waangalizi wa TEMCO walikuwemo japo kulikuwa na matatizo madogomadogo yaliyoonekana. NEC pia inapongezwa kwa kuanzisha Mfumo Shirikishi wa Udhibiti wa Uchaguzi (IEMS) ambao ulisaidia upatikanaji wa haraka wa taarifa za usajili katika Tanzania Bara. Kwa mfano NEC iliweza kuchapisha majina ya wapiga kura waliosajiliwa katika kila kituo kutoka makao makuu na kuyabandika ndani ya siku chache

katika vituo hivyo ili wapiga kura waone taarifa zao. Haya ni mafanikio makubwa ukilinganisha na usajili wa mwaka 2005[6].

## 7.0. KITENDAWILI CHA USAJILI MKUBWA WA WAPIGA KURA NA UCHACHE WA WATU WALIOJITOKEZA SIKU YA KUPIGA KURA

Kitendo cha wapiga kura wachache (takriban 42%) kujitokeza siku ya kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa 2010 nchini Tanzania kinathibitisha kwamba DKWK halikuwa na mchango mkubwa kwa wapiga kura kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi, ijapokuwa kulikuwa na ongezeko la mamilioni ya wananchi walioandkishwa. Katika chaguzi zilizopita, hamasa ya wapiga kura kujiandikisha na kujitokeaza kupiga kura ilikuwa juu. Kwa mfano mwaka 2000 na 2005 wapiga kura walijitokeza kupiga kura kwa 84.4% na 72.28 kwa mtiririko huo (EISA, 2006). Kinadharia, wapiga kura wengi wakijitokeza siku ya kuandikishwa inatoa picha kwamba watajitokeza vilvile kwa wingi siku ya kupiga kura; lakini sivyo ilivyokuwa kwa Tanzania. Hii inaibua maswali mengi: Kwa nini wapiga kura hawakujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi wakati Tanzania Bara imekuwa na rekodi nzuri ya wapiga kura kujitokeza kwa wingi katika chaguzi zilizopita? Ni mambo gani yalisababisha wapiga kura kujitokeza kwa wingi kujiandikisha na siyo kupiga kura? Kunaweza kuwa na maelezo tofauti kwa maswali haya. Sehemu ya maelezo inaweza kuwa kulikuwa na jitihada kidogo katika kuwaelimisha wapiga kura juu ya haki yao ya kidemokrasia katika dhana nzima ya uchaguzi; lakini vilevile juu ya matumizi ya vitambulisho vyao vya kupigia kura kama vitambulisho vya kawaida. Ripoti za Waangalizi wa TEMCO majimboni zinaonyesha kwamba kitu kilichowasukuma watu kujiandikisha kwa wingi katika uchaguzi wa 2010 ilikuwa ni kupata kadi za kupigia kura ambazo ziliweza kutumika pia kama vitambulisho vya kawaida. Hata hivyo, hii siyo sababu ya kutosha kwa sababu mwaka 2005 wapiga kura wengi sana (96%) walijitokeza kujiandikisha licha ya elimu ndogo kuhusu upigaji kura. Vilevile wakati huo hakukuwa na suala la vitambulisho lakini bado watu walijitokeza kwa wingi kupiga kura, kwa takriban asilimia 72. Hii inahitaji sababu zaidi. Sababu ya pili inayoweza kuwafanya wapiga kura wajitokeze kwa wingi ni vyama vya siasa au wagombea wanaopendwa na wapiga kura wengi. Katika uchaguzi wa 2010 wapiga kura walionekana kuwa katika njia panda na kukosa maamuzi wachague chama gani. Hapana shaka kwamba uchaguzi uliopita ulikuwa na ushindani mkubwa hasa baada ya mgombea wa urais kupitia CHADEMA, Dk. Wilbroad Slaa, kuingia katika kinyang’anyiro hicho. Tofauti na 2005 ambapo watu wengi walijiandikisha na kujitokeza kwa wingi kupiga kura kwa sababu ya kuteuliwa kwa Jakaya Kikwete kugombea urais kupitia CCM, katika uchaguzi wa 2010 wapiga kura wengi walionekana kuchoshwa na siasa kutokana na utendaji usioridhisha wa serikali ya CCM, hasa kwa namna inavyoshughulikia matatizo makubwa ya rushwa na ubadhrifu wa mali ya umma.

Ukizingatia mijadala mikubwa iliyozuka Bungeni katika kipindi cha 2005-2010 ambayo ilisababisha kushtakiwa kwa watendaji wakuu wa serikali kwa tuhuma za rushwa, wapiga kura wengi walipoteza imani ya kukipigia tena kura Chama Cha Mapinduzi. Matokeo yake ni kwamba wapiga kura walikuwa na fursa mbili: Kwa upande mmoja, kuna wale ambao matarajio yao hayakutimizwa na wagombea wa CCM kwa hiyo wakapigia kura vyama vya upinzani. Hii inaweza kuthibitishwa na ukweli kwamba upinzani ulipata zaidi ya robo (26%) ya kura zote zilizopigwa. Kwa upande mwingine, kuna wale ambao hawakuona sababu ya kupiga kura baada ya kukatishwa tamaa na utendaji kazi wa mgombea wa CCM. Sababu

[6] Tazama Sura ya nne kwa mjadala zaidi kuhusu mfumo huu.

nyingine inaweza kuwa ni matokeo ya uteuzi wa wagombea wa CCM katika kura za maoni. Kwa jumla kura za maoni zilifanana sana na uchaguzi wenyewe kwani wagombea walipambana sana ili kushinda chaguzi za ndani ya vyama. Baada ya mchakato wa kura za maoni, baadhi ya wapiga kura walifikiri ndio mwisho wa shughuli na kujiridhisha kwamba wagombea wao wangeshinda tu uchaguzi kwa namna yoyote ile. Matokeo yake ni kwamba baadhi ya wapiga kura hawakujitokeza tena siku ya uchaguzi wenyewe. Mwisho inawezakana kulikuwa na tofauti ya idadi ya wapiga kura walioandikishwa iliyotokana na NEC. Kama ilivyojadiliwa katika sura hii, NEC ilitegemea sana sensa ya makazi katika kufanya makadirio ya wapiga kura tarajali. Wakati mwingine takwimu hizo hazikufanana na zile zilizotolewa na wasimamizi wa uchaguzi na waandamizi wao.

## 8.0 HITIMISHO

Mtazamo wa jumla ambao waangalizi wote wa TEMCO majimboni na mikoani wanakubaliana nao ni kwamba, mchakato wa usajili wa wapiga kura Tanzania Bara uliendeshwa na kusimamiwa vizuri ukilinganishwa na chaguzi zilizopita. NEC ilifanikiwa kuongoza, kusimamia na kudhibiti mchakato huo vizuri. Pamoja na matatizo ya watu wachache kujitokeza kuhakiki taarifa zao katika zoezi la uboreshaji na baadhi ya majina kukosekana katika DKWK, bado NEC iliongoza mchakato wote kitaalamu, na baadhi ya mafanikio yaliweza kuonekana. Kwa mfano wapiga kura wapya wengi sana waliandikishwa. Kusajiliwa kwa wapiga kura wengi wenye sifa za kupiga kura ni mkakati na rasilimali muhimu ambazo vyama vya upinzani, hasa vile vinavyochipukia haviwezi kudharau. Hii ni kwa sababu wapiga kura wenye sifa za kupiga kura tayari wanaweza kutegemewa sana na vyama hivi katika kuvipigia kura. Kutokana na uzoefu uliopatikana, suala la kujiandikisha kupiga kura nchini Tanzania linaonekana kuwa ni jukumu binafsi la mpiga kura. Hata hivyo, serikali inaweza kuufanya usajili uwe rahisi au mgumu na hivyo kusababisha kujitokeza au kutojitokeza kwa wapiga kura siku ya uchaguzi. Kwa sasa usajili wa wapiga kura hauonekani kama ni tatizo kubwa, ila uboreshaji wa DKWK ulikuwa duni. Ingawa zoezi la usajili halikuwa la gharama kubwa kifedha, suala la muda linaweza kuwa kikwazo kikubwa katika usajili na uboreshaji wa daftari siku za mbele. Kwa ujumla, usajili wa wapiga kura ni wa gharama katika uchaguzi wowote katika nchi yoyote duniani. Wananchi nchini Marekani wamekuwa wakilipia gharama hizi wao wenyewe (Highton, 2004:58). Hivyo hakuna mtu anayeweza kusema kwamba usajili nchini Tanzania hauna gharama kwa wapiga kura. Wapiga kura wanatembea umbali mrefu kwenda kujiandikisha, wanatumia muda wao mwingi katika vituo vya kujiandikishia ili kuhakikisha taarifa zao zimerekodiwa vizuri, na wanajitolea muda wao ambao wangeutumia kujipatia kipato ili kushiriki shughuli hii ya kidemokrasia. Licha ya gharama zote hizi, watu wamekuwa na utamaduni wa kujitokeza kwa wingi na kujiandikisha. Hata hivyo watu lazima wapime muda watakaoutumia katika zoezi la usajili na kutimiza majukumu mengine pia. Kwa ujumla, ikiwa wananchi hawaoni matokeo ya haraka ya ushiriki wao huwa wanajitenga na siasa. Hivyo kitendo cha wananchi wengi kuendelea kutopiga kura, kama ilivyoonekana katika uchaguzi wa 2010, kinaashiria kwamba kupiga kura ni jambo ambalo halina maslahi kwa wapiga kura wengi, na halitoi fidia ya kutosha kwa muda waliotumia.

## SURA YA TATU

## UTEUZI WA WAGOMBEA

### 1.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tutachambua mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama na pia uteuzi wa NEC (NEC). Sura imeganywa katika sehemu saba. Sehemu ya pili inaelezea muktadha wa kisheria na taratibu za vyama. Inaonyesha kuwa pamoja na kuwa kuanzishwa kwa Sheria ya Gharama za Uchaguzi 2010 ilikuwa ni hatua kubwa, utekelezaji ulikumbwa na kigugumizi. Sehemu ya tatu inatathmini uteuzi ndani ya vyama kwa kuangalia mitindo iliyotumika. Vyama vingi vilijitahidi kuwa na mchakato wa wazi na shirikishi kwa kadri ilivyowezekana. Lakini uhalisia ulikuwa na tofauti kubwa sana kwa kulinganisha na viwango vya nadharia ya demokrasia. Mjadala wa kujitoa kwenye chama kimoja na kujiunga na kingine utafuatia. Sehemu ya nne imejikita katika mchakato wa uteuzi ndani ya Tume. Uteuzi wa Tume ni muhimu sana kwani ni wa mwisho na hauwezi kupingwa mahakamani. Suala la mgombea binafsi ni somo la sehemu ya tano. Sehemu hii inatilia shaka hekima ya kuwalazimisha watu kupata uteuzi wa vyama ili kugombea nyakati hizi za siasa huria. Hoja yetu ni kuwa kung'ang'ania lazima ya kupata uteuzi wa vyama, ni kuishi enzi za utawala wa chama kimoja na siasa za kidikteta. Sehemu ya sita inawasilisha *majojo* ya wagombea wanaopita bila kupingwa. Ingawa kuna wagombea waliopita bila kupingwa katika uchaguzi wa mwaka 2010, tunaona ipo haja ya kupitia upya sheria ya uchaguzi ili kuwafanya walau wagombea wa aina hii kupigiwa kura. Sehemu ya saba inawakilisha tathmmini ya mchakato wa uteuzi kama ilivyotolewa na Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO. Mwisho kabisa tutamaliza kwa hitimisho la makala nzima.

### 2.0 MUKTADHA WA KISHERIA NA TARATIBU ZA VYAMA

Muktadha wa kisheria haukubadilika sana ukilinganisha na chaguzi zilizopita. Uteuzi wa wagombea ulifanywa kwa kuzingatia matakwa ya kisheria, chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977, Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985, kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1979 (NEC, 2001; TEMCO, 2006).

Mbali ya kutimiza matakwa ya vyama husika, wagombea walitakiwa kutimiza matakwa ya Katiba na Sheria ya Uchaguzi. Wagombea wa Urais walitakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

- Wawe na miaka 40 na pia wawe Watanzania kwa kuzaliwa;
- Wawe wanachama wa chama kilichosajiliwa na wateuliwe na vyama kugombea nafasi hii;
- Watimize masharti yote ya kuwa mbunge;
- Wajaze fomu za uteuzi zitolewazo na Tume ya Uchaguzi, zikiambatana na wadhamini wasiopungua 200 kutoka mikoa 10 ya Tanzania, na kati ya hiyo walau miwili kutoka Zanzibar; na
- Waweke dhamana ya Shilingi 1,000,000 (TEMCO, 2006).

Wagombea ubunge walitakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

- Wawe na umri wa miaka 21 na kuendelea;

- Waweze kusoma na kuandika kwa Kiswahili au Kiingereza;
- Wasiwe wametiwa hatiani na mahakama yoyote kwa kosa la jinai au kukwepa kulipa kodi ndani ya kipindi cha miaka mitano kabla ya uchaguzi;
- Wawe wanachama na wateule wa vyama husika;
- Wapate udhamini wa watu wasiopungua 25 waliojiandikisha kupiga kura katika eneo husika;
- Wajaze fomu mahsusi; na
- Kuweka dhamana ya Shilingi 50,000.

Matakwa ya umri na kodi kwa wagombea udiwani ni sawa na yale ya wabunge. Zaidi ya hapo, wagombea wanatakiwa kudhaminiwa na walau wakaazi 10 katika kata ambao wamejiandikisha kupiga kura. Dhamana inayotakiwa ni Shilingi 10,000. Dhamana zote za ngazi za ubunge na urais huchukuliwa iwapo mtu atajitoa au atapata pungufu ya asilimia 10 ya kura zilizopigwa (TEMCO, 2006).

Matakwa haya ya kisheria yameendelea kuwepo tangu uchaguzi wa mwaka 1995. Kupitishwa kwa Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 kulileta msisimko hasa kwa kuwa mgombea urais wa CCM alikwishaazimia kushughulikia suala la matumizi ya pesa katika chaguzi. Kimsingi Sheria ya Gharama za Uchaguzi 2010 imelenga kudhibiti matumizi ya pesa nykati za uchaguzi ili kutokomeza vitendo vya rushwa. TEMCO ilifuatilia kwa karibu sana utekelezaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi na matokeo yake yatatolewa katika ripoti nyingine. Kuhusiana na hili vilevile TEMCO ilikuwa ikotoa Vijarida ikiwemo Kijaria cha Utekelezaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi (Election Expenses Act Series No. 1 of September 2010). Ni vizuri tukarejea kwa kirefu yaliyomo katika kijarida hiki.

Kitu cha kwanza kilichoonekana ni kuwa matukio ya rushwa yaliongezeka zaidi katika uchaguzi wa mwAka 2010 ikilinganishwa na chaguzi zilizopita licha ya kupitishwa kwa sheria ya kuzuia vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi. Pili, tofauti na huko nyuma, wagombea wanne wa ubunge na udiwani kupitia CCM walifikishwa mahakamani kwa makosa yanayohusiana na rushwa wakati wa uchaguzi. Mkoa wa Iringa pekee ulikuwa na wagombea watatu waliofikishwa mahakamani: Joseph Mungai aliyekuwa akigombea jimbo la Mufindi Kaskazini (The Guardian, 12 Agosti 2010), Fredrick Mwakalebela aliyegombea Iringa Mjini (*Tanzania Daima*, 18 Agosti 2010) na Fadhili Ngajiro aliyegombea Iringa Mjini pia (*Nipashe* 13 Agosti 2010). Wa nne ni Esther Mambali aliyegombea kupitia viti maalum Umoja wa Vijana wa CCM (*Mwananchi*, 19[t] Agosti 2010).

Baadhi ya wanachama wa CCM walikiri kuwa ni chama chao ndicho kimelea vitendo vya rushwa kwa kuruhusu kuwepo kwa takrima huko nyuma. Walibainisha kuwa pamoja na kuwa katika uchaguzi wa 2010 takrima ilipigwa marufuku, watu wasingekwenda kwenye mikutano ya kampeni ya CCM kama wasingeletewa magari ya kuwabeba pamoja na kuhakikishiwa burudani kutoka kwenye vikundi mbalimbali. Hali hii haikuwakumba wagombea wa vyama vya upinzani kwani wananchi wanafahamu kuwa vyama vyao havina pesa.

Cha pili kilichojitokeza ni kuwa kulikuwa na pesa nyingi zikufukuza wapiga kura kiasi kwamba mbinu mpya zilibuniwa kuwakwepa maafisa wa TAKUKURU. Mbinu zilizoripotiwa na magazeti zilihusisha ugawaji wa moja kwa moja wa pesa uliofanywa na wagombea au mawakala wao, kutumia huduma za kutuma pesa za simu za mkononi, au kutoa zawadi za vitu kama vile simu za mkononi, chakula, vinywaji, na pikipiki. Katika maeneo mengi, wagombea waligawa pikipiki ili kurahisisha ugawaji wa pesa katika majimbo

yaliyokuwa na miundombinu migumu. Wabunge wengi pia waligawa pesa au kutoa zawadi kwa kisingizio cha kutimiza ahadi walizotoa awali.

Cha tatu na pengine cha muhimu zaidi ni kuwa kulikuwa na ama uwezo mdogo, kukosekana utashi au vyote katika kutekeleza Sheria ya Gharama za Uchaguzi, 2010 ndani ya vyombo husika vya serikali. Ripoti za TEMCO na taarifa za kwenye vyombo vya habari zilionyesha kuwa vyama vyote vileivyoendesha zoezi la kura za maoini havikuzingatia kutekeleza Sheria ya Gharama za Uchaguzi 2010, havikuweza kudhibiti rushwa na wala havikuweka msisitizo kwa wananchama wao kufuata maadili. (TEMCO Newsletter, Septemba 2010). Kwa kipindi chote cha mchakato wa uteuzi ndani ya CCM, tarehe 18 Julai mpaka 1 Agosti 2010, neno rushwa lilikuwa masikioni mwa Watanzania kila siku. Kulikuwa na taarifa nyingi za vyombo vya habari kuanzia wagombea waliotiwa mbaroni wakati wakiotoa mlungula mpaka wale waliovunjika miguu wakiruka kuta pale walipovamiwa na maafisa wa TAKUKURU wakati wakigawana pesa za rushwa.  Kwa hakika CCM ililemewa na mzigo na ilitegemea makali ya TAKUKURU kuiokoa.

Kwa upande mwingine, taratibu za uteuzi ndai ya baadhi ya vyama zilibadilika. CCM iliamua kuwa wanachama wote watawapigia kura wagombea wote watakaotaka kupitishwa na chama kugombea nafasi mbalimbali. Wagombea walitakiwa kuzunguka pamoja katika gari moja na kwenda kwenye mikutano pamoja wakati wa kuomba kura. Hata hivyo jitihada hizi hazikuzaa matunda yaliyotarajiwa kwani wagombea walibunimbinu mpya za hila. Mbinu kubwa iliyotumika ilikuwa ni kununua kadi za chama kwa wingi na kuzigawa kwa wananchama “wapya” ili wawapigie kura za maoni. “tofauti na ilivyotarajiwa, utaratibu mpya ulichochea zaidi kuliko kuzuia vitendo vya rushwa, kiasi ambacho ununuzi wa kura uliojitokeza haujawahi kushuhudiwa katika muongo uliopita” (TEMCO Newsletter, 2010). Ilidhaniwa kuwa kwa kupanua wigo wa wapiga kura, ingekuwa kinga kwa watoa rushwa kwani wasingeweza kuhonga wanachama wote. Lakini wagombea watoa rushwa walitafuta njia mpya za kuwafikia wapiga kura kama kununua kwa wingi na kugawa kadi za CCM kwa minajili ya kuongeza idadi ya wapiga kura wao.

CHADEMA ilitaka kuongeza demokrasia katika uteuzi wa wagombea katika nafasi za viti maalum kama walivyofanya CCM kwa kutoa fursa kwa wanachama wote kuanzia ngazi za chini kupiga kura. Hata hivyo, mwishowe zoezi hili liligubikwa na rushwa na ukiukwaji wa taratibu kiasi kwamba chama kiliachana kabisa na utaratibu huu. Hatimaye kamati ya washauri ilipewa jukumu la kufanya uteuzi wa wagombea wa viti maalum.

CUF pia walibadilisha utaratibu wa uteuzi. Katika uchaguzi wa 1995 wanachama wote wa CUF walishiriki katika uteuzi wa madiwani, wawakilishi na wabunge. Mwaka 2000 na 2005 CUF waliachana na utaratibu huu badala yake kura za maoni zilipigwa na wajumbe katika ngazi ya jimbo na baadaye kuthibitishwa naBaraza Kuu. Utaratibu wa mwaka 1995 ulirejewa katika uchaguzi wa mwaka 2010 kwa kile ambacho chama kilieleza kama ni “kupeleka demokrasia katika ngazi za chini” (TEMCO, 2010b). Utaratibu huu hata hivyo ulitekelezwa kikamilifu Zanzibar ambako ni ngome ya kisiasa ya CUF. Matokeo yake baadhi ya vigogo na wabunge na wawakilishi wa muda mrefu waliangushwa na vijana waliojitokeza kwa wingi. Kulikuwa na malalamiko ya rushwa ingawa siyo kwa kiwango kilichoshuhudiwa Tanzania Bara. Hii pengine ni kwa sababu Sheria ya Gharama za Uchaguzi 2010 haitumiki Zanzibar. CUF pia ilipandisha ada za uteuzi kimyakimya. Matahalani, Kifungu cha Pili cha taratibu za uchaguzi za CUF kinaonyesha kuwa ada ya kuchukulia fomu ya urais ni Shilingi 500,000; shilingi 50,000 kwa wagombea ubunge na uwakillishi na shilingi 10,000 kwa wagombea udiwani (TEMCO, 2010b).

Kwa ujumla wake, mchakato wa uteuzi wa wagombea kwa uchaguzi wa mwaka 2010 ulikumbwa na kiwango kikubwa cha rushwa kuwahi kushuhudiwa. Pengine tuongeze mapema hapa kuwa kwa kusema hivi hatumaanishi kuwa kupitisha kwa Sheria ya Gharama za Uchaguzi ilikuwa ni *Danganya Toto.* Hii ilikuwa ni hatua kubwa kuelekea kwenye chaguzi huru na za haki isipokuwa tu kama tulivyogusia bado kuna changamoto nyingi sana katika utekelezaji wa Sheria hii.

Kuna mambo mengi yalichangia katika ufanisi mdogo katika utekelezaji wa Seria ya Gharama za Uchaguzi. Kwa kurahisisha uchambuzi tumezigawanya sababu hizi mafungu mawili: sababu za kimfumo na sababu za utendaji. Mambo ya kimfumo yanahusisha sababu ambazo ziko ndani ya sheria yenyewe ambazo zinakuwa kikwazo kwa utekelezaji. Sababu za kiutendaji ni zile ambazo zinahusiana na utaratibu mbaya wa kitaasisi. Tutaanza na sababu za kiutendaji.

Sababu mojawapo wa kiutendaji ni uwezo mdogo au kukosa utashi kwa vyama vya siasa. Kwa harakaharaka inaonekana kuwa vyama havikuwa na ari ya kutekeleza Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Sheria yenyewe kwa hakika imeweka imani kubwa kwa vyama vya siasa. Maana yake ni kuwa ilidhaniwa kuwa vyama vya siasa vitakuwa na rasilimali watu, vitendea kazi na nia ya kutekeleza Sheria ya Gharama za Uchaguzi 2010. Katika uhalisia wake hii iliongeza mkanganyiko kuliko kurahisisha utekelezaji kwani viongozi wa vyama ambao walitakiwa kusimamia utekelezaji wa sheria hii ama walikuwa wagombea – hivyo kuhitaji nao usimamizi – au watoto wao, wake zao na ndugu na rafiki wa karibu walikuwa wagombea. Ilikuwa vigumu kwao kujichunga wenyewe.

Matahalani, Katibu wa Mipango na Fedha wa CCM ambaye alitakiwa kusimamia nidhamu ya matumizi ya pesa ndani ya chama, Bw. Amos Makala alikuwa akigombea jimbo la Mvomero. Hata kabla ya mchakato rasmi wa uteuzi kuanza, tayari kulishazuka tuhuma na malalamiko kuwa Bw. Makala alikuwa akiwahonga wapiga kura kwa kugawa pesa isipokuwa TAKUKURU walishindwa kumkamata (*Mwananchi*, 18 Julai 2010). Pamoja na kuongezeka kwa malalamiko hayo, CCM hawakuwahi kumuonya Bw. Makala, pengine kwa kukosa ushahidi. Naibu Makatibu wakuu wote wawili wa Bara na Visiwani walikuwa wakigombea pia. Ingawa hawakukumbwa na tuhuma zozote za rushwa hali ingekuwa tete kama wangehusiswa na rushwa.

Pia, Bw. January Makamba, mtoto wa Katibu Mkuu wa CCM, Yusufu Makamba, alikuwa akigombea ubunge katika jimbo la Bumbuli. Chama hakikuchukua hatua yoyote zilipozuka tuhuma kuwa January aliwakaribisha wazee kutoka kata ya Mgwashi na kuwapa takrima ikiwemo vinywaji, chakula na pesa (*Raia Mwema*, 2- 8 Juni 2010). Mtoto wa Waziri Mkuu alikuwa akigombea ubunge kupitia viti maalum, ingawa hakuteuliwa na hakutuhumiwa kwa rushwa. Lakini habari ambayo ilitawala vyombo vya habari ni ile iliyomhusisha mke wa aliyekuwa Spika wa Bunge na waziri, Magreth Sitta. Bi. Sitta akigombea kupitia viti maalum mkoa wa Tabora, alishikiliwa na kuhojiwa na PCCB kwa kilichodaiwa kuwa ni tuhuma za rushwa. Siku chache baadaye Bw. Sitta alitoa tamko lililokuwa na onyo kuwa atawatia adabu TAKUKURU kwa kumdhalilisha mke wake na kumshushia hadhi yake (*HabariLeo*, 31 Julai 2010). Alikuwa na matarajio makubwa ya kuchaguliwa kwa kipindi kingine cha uspika. Wakati yakiwepo mapendekezo ya Kamati Maalum ya Bunge ambayo hayajatekelezwa na mengine yakitaka Mkurugenzi wa TAKUKURU aachie ngazi siyo vigumu kufahama Bw. Sitta alimaanisha nini kwa kuwatia adabu TAKUKURU.

Sababu za kimfumo zinahusisha muundo wa Sheria yenyewe. Kukosekana kwa tafsiri dhabiti ya Sheria kulichangia katika kushusha ufanisi wakati wa utekelezaji wa sheria. Kukosekana kwa maelezo yanayojitosheleza kuhusu mwisho wa kutoa ahadi au kutekeleza ahadi kuliwafanya baadhi ya wabunge kuendelea kusingizia kuwa wanatekeleza ahadi hadi wakati wa uchaguzi. Ilishindani kuchukua hatua kwani sheria haisemi wazi kama mbunge anatakiwa kusimamisha misaada yote ikifika kipindi Fulani. Mathalani, waziri wa zamani Dk. Juma Ngasongwa aliyekuwa akigombea katika jimbo la Unga Magharibi alikiri kutoa mabati na simenti kwa viongozi wa Manda Chini, Lugala na Madubila akisema kuwa alikuwa akitekeleza ahadi alizotoa awali (*Mtanzania*, 19 Julai 2010). Malalamiko kama haya yalikuwa magumu kufuatilia kwa sababu ya pengo katika sheria.

## 3.0 UTEUZI WA WAGOMBEA NDANI YA VYAMA VYA SIASA

Kama ilivyokuwa kwa chaguzi zilizopita, uteuzi wa wagombea nafasi ya urais, na ubunge uliendelea kufuata Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977. Ibara ya 39 (1) (c) na 67 (1) (b) zinataka wagombea urais na wagombea ubunge kuteuliwa na vyama vya siasa. Kwa wagombea wa udiwani, vipengele mahsusi vipo katika Ibara ya 39 (2) (f) ya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1979 (NEC, 2001). Uteuzi wa wagombea ulikuwa ni kipimo cha umaarufu, ukubwa, uwepo, rasilimali na hakika demokrasia ndani ya chama. Wakati vyama vingine vilikuwa na utaratibu unaofanana, na unaoeleweka ambao ulitumika kwa ngazi zote, vyama vingine havikuwa na taratibu zinazoeleweka.

Uteuzi kwa mwaka 2010 uliendelea kuonyesha tarakibu (models) tatu za uteuzi: (i) ushirikishwaji kamili, (ii) tarakibu ya ushikishwaji nusunusu na (iii) "kunyofoa" (hand-picking model). Mpaka sasa ni CCM na CUF ndio waliweza kutumia tarakibu ya ushirikishwaji kamili. Tarakibu hii iliboreshwa zaidi kwa kuwaruhusu wananchama wote kuwapigia kura wagomnea wote waliojitokeza. Wagombea walipigiwa kura za maoni na vikao vya vyama katika ngazi husika vilipitisha majina. Utaratibu huu ulikuwa wazi kiasi kwakmba TAKUKURU waliweza kufuatilia vitendo vya rushwa wakati wa kura za maoni. Hata hivyo nguvu ya TAKUKURU ilipunguzwa kasi baadaye kwa sababu ambazo haziko wazi.

Taratibu ya ushirikishwaji nusunusu inajitokeza pale ambapo wajumbe (na siyo wanachama wote) wanapopiga kura ya maoni kuonyesha chaguo lao. Tarakibu hii hutumika na vyama vya upinzani vilivyoimarika kama vile CHADEMA na NCCR-Mageuzi.

Utaratibu wa "unyakuaji" ni utaratibu hafifu kabisa kidemokrasia na hutumika na vyama ambavyo havijajiimarisha. Ni utaratibu wa maamuzi kutoka juu ambapo wakubwa huamua nani asimame katika uchaguzi. Katika uhalisia katika vyama hivi kila aliyeweza kugharamia kampeni aliweza kusimama kwa tiketi ya chama kwani hakukuwa na ushindani mkubwa ndani ya chama. Misuguano ilikuwa mikubwa ndani ya vyama vikubwa hasa CCM. Misuaguano na michuano hii ilisababisha baadhi wa wagombea waliokosa uteuzi kuhama vyama.

### 3.1 Uteuzi wa Madiwani na Wabunge

Ushahidi kutoka majimboni ulionyesha kuwa CCM, CUF na CHADEMA, kwa viwango tofauti, walikuwa na mfumo unaoeleweka wa kuteua wagombea katika nafasi mbalimbali, ingawa ni CCM pekee ndio waliweza kufuata taratibu hizi katika ngazi ya madiwani na wabunge lakini siyo urais.

CCM ilikuwa na utaratibu mzuri zaidi wa kufanya uteuzi. Hakika, tunakubaliana na mwangalizi wa Uchaguzi wa Tanga aliyebainisha kuwa CCM ilikuwa na muundo, rasilimali watu na fedha za kutosha kuendesha zoezi la uteuzi lilikuwa wazi na shirikishi. Kinadharia utaratibu wa CCM ulikuwa ni wa kidemokrasia kuliko ndani ya vyama vingine. Katika uhalisia, utaratibu huu uliingia dosari hasa kwa kuwa wagombea walifanya hila kucheza na mfumo. Pesa na zawadi nyingine zilitumika sana na wakati huohuo wagombea wakinunua kadi na kugawa kwa wanachama wapya ili waongeze idadi ya kura (LTO Iringa Report, 2010). Mratibu wa TEMCO mkoa wa Mara anabainisha matukio kama haya pia ambapo kura za maoni ziligubikwa na vikwazo vingi ikiwemo rushwa, matumizi ya kadi bandia za CCM, matumizi ya orodha bandia za wanachama na kwa ujumla ushawishi mkubwa wa watu wenye pesa (LTO Mara Report, 2010). Iringa Mjini mathalani, matukio kama haya yalitokea katika uteuzi wa wabuge na madiwani. Uteuzi wa mbunge ulikuwa habari ya kitaifa. Mgombea aliyeongoza kura za maoni alituhumiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa ingawa hakukamatwa papo kwa hapo, wale waliodhaniwa kupewa pesa ndio waliokamatwa. Mgombea huyu hata hivyo alipeekewa mahakamani na jina lake halikurudishwa na vikao vya juu vya kitaifa. Katika jimbo hilihili kulikuwa na tuhuma kuwa wagombea udiwani walikuwa wakishawishiwa na mgombea ambaye alitaka kugombea umeya. Mgombea huyu inasemekeana aliwadhamini baadhi ya wananchama wa CCM na kuwapa msaada wa pesa baadhi ya wagombea wa udiwani.

Huko Njombe Magharibi mgombea wa CCM aliyeongoza kura za maoni jina lake lilikatwa na vikao vya kitaifa vya CCM. Mgombea aliyekuwa nafasi ya tatu ndiye aliyeteuliwa. Matokeo yake ni kuwa aliyeongoza kura za maoni alihamia CHADEMA. Katibu Mwenenzi wa CCM alinukuliwa na vyombo vya habari baadaye akisema kuwa mgombea huyu alisimamishwa kugombea nafasi yoyote ndani ya chama kwa sababu ya rekodi yake mbaya ya nidhamu (*The Citizen*, 16 Agosti 2010). Mgombea aliyeshinda huko Njombe Kaskazini ndiye pia mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Iringa aliyeibuka mshindi baada ya kumshinda mbunge wa siku nyingi wa jimbo hilo. Hata hivyo alionekana kama mgombea dhaifu kwani elimu yake ilionekana kuwa ndogo na pia kwa sababu ya upendeleo wa kikabila. Alioneka kama mtu wa nje kutoka eneo lingine. Hata hivyo alikuwa ni tajiri aliyeungwa mkono na matajiri wenzake kutoka eneo moja. Huko Mlalo vikao vya juu vya CCM viliamua kumchukua mshindi wa tatu Bw. Hassan Ngwilizi ambaye alikuwa anatetea nafasi yake ya ubunge, kitu kilichosababisha maandamano na kujitoa kwa Bw. Charles Kagonji na kujiunga na CHADEMA. Huko Kilindi mgombea wa CCM ambaye aliachwa kwenye kura za maonji likwenda mpaka mahakama kuu kushitaki kuwa mgombea liyekuwa akitetea kiti chake “aliiba” matokeo ya kura za maoni (LTO Tanga Regional Report, 2010). Huko Muhambwe, CCM ilikuwa na wakati mgumu kufuatia maamuzi ya ngazi za juu ya kurudisha jina la mgombea aliyekuwa hatakiwi. Wagombea walikataa kusaini fomu za matokeo ya kura za maoni wakilaumu kuwa taratibu za CCM hazikufuatwa (LTO Kigoma Regional Report, 2010). Vikao vya juu vya CCM vilirudisha jina lake licha ya tuhuma kuwa alikuwa akijihusisha katika ujambazi na biashara zilizotia shaka. Katibu wa CCM Mkoa wa Kigoma ambaye inasemekana alipinga uteuzi wake, alipewa barua ya uhamisho kwenda Dodoma usiku wa manane.

Kwa ujumla hata hivyo, CCM iliheshimu kura za maoni baada ya kujifunza madhara ya kuacha wagombea wanoapendwa na wananchi. Katika kufanya maamuzi ya mwisho CCM iliangalia matokeo ya kura za maoni, utendaji wa mgombea mtarajiwa, na uwezo wa wagombea kujieleza. Kwa hivyo mbali na wagombea wane, CCM ilifuata maoni ya wanachama katika kufanya uteuzi wa mwisho. Wale walioachwa walikuwemo: Bw. Fredrick

Mwakalebela (Iringa Mjini), Bw. Athuman Ralome (Moshi Mjini), Bw. Hussein Bashe (Nzega) na Bw. Thomas Nyimbo (Njombe Magharibi).

Katika jimbo la Moshi Mjini, CCM ilichukua mshindi wa tatu ikikariri kuwa mshindi wa kwanza asingeweza kukabili vishindo na kumshinda mgombea wa CHADEMA ambaye ameshikilia jimbo hilo kwa muda mrefu. Kwa sababu hizo hizo vikao vya juu vya CCM viliamua kumchukkua mshindi wa tatu katika jimbo la Nzega huku wakimuacha Bashe ambaye ilisemekana hakuwa na uraia wa Tanzania. CCM ilimchukua mshindi wa tatu bdala yake, Dk. Kigwangala wakisema kuwa alikuwa anakubalika zaidi kuliko mshindi wa pili. Kuangushwa kwa Selelii kunatokana na vita dhidi ya ufisadi ambayo inasemekana alikuwa mmoja wa wapiganaji wake. Tukio la kumsimamisha Bashe lilichukua sura ya kitaifa. Baadaye waziri wa mambo ya ndani alikaririwa akisema kuwa uraia wa Bashe haukuwa na shaka. Ni vile tu waziri hakutuambia ni upande upi wa shaka aliokuwa akiuongelea.

CCM iliwapitisha mawaziri wa zamani, Basil Mramba (Rombo) na Andrew Chenge (Bariadi Magharibi), wote wakikabiliwa na kesi za jinai mahakamani. Haikuwapitisha wagombea wengine waliokuwa na kesi kama hizo za jinai akiwemo mgombea wa jimbo la Iringa Mjini ikisema kuwa mgombea huyu alihusishwa katika tuhuma za rushwa wakati wa uteuzi (the Citizen, 16 Agosti 2010).

Uteuzi katika vyama vingine haukuwa na mivutano mikubwa. Tarakibu zilizotumika katika vyama hivi zilikuwa za kidemokrasia na nyingine za unyakuaji. Katika majimbo mengi ambayo TEMCO ilikuwa na waangalizi wake, wagombea hawakuwa na upinzani ndani ya vyama. Wachache waliojitokeza walijadiliwa na kupendekezwa na ngazi za kata na jimbo katika majimbo husika. Hata chama kama CHADEMA ambacho kilionekana kutoa ushindani mkali sana baadaye, katika majimbo mengi kilikuwa dhaifu na hakikiwa kikijulikana kabla ya uteuzi wa CCM. “Mvuto wa Slaa” na makosa ndani ya CCM hakika viliinufaisha CHADEMA. Umaarufu wa CHADEMA uliongezeka maradufu mara baada ya Dk. Slaa kuteuliwa kuwa mgombea urais kwa tiketi ya CHADEMA.

Kama ilivyobainishwa na Mwangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO Mkoa wa Mara, vyama vingine havikuwa na msingi mzuri na vilitumia njia za uteuzi wa ushirikishwaji nusu au unyakuaji. Vyama kama UDP, DP, UPDP, Demokrasia Makini na Jahazi Asilia kwa kiasi kikubwa vilitumia njia za unyakuaji. Tanga mathalani, mwanagalizi wa TEMCO aligundua kuwa CUF haikuwa na ofisi ya mkoa na badala yake shughuli zote za kichama za mkoa zilikuwa zikifanyika kutokea katika ofisi ya wilaya.

CHADEMA iliigawanya nchi katika majimbo kwa kutumia kanuni ya rangi. Kwa kuzingatria kanuni hii majimbo yaligawanywa kwa kutumia rangi kama vile nyekundu, kijani, nyeupi, na vumbi. Rangi nyekundu iliwakilisha majimbo ambayo yalionekana kuwa CHADEMA ilikuwa na uwezekano mkubwa wa kushinda. Rangi ya kijani ilionyesha majimbo ambayo majimbo ambayo juhudi zaidi zilitakiwa ili kushinda. Rangi nyeupe iliashiria majimbo ambayo katika mtazamo wa viongozi wa CHADEMA kulikuwa na uwezekano wa kupata kura kiasi. Kundi la mwisho la majimbo ni yake ya rangi ya vumbi. Haya ni yale ambayo CHADEMA ilidhani ilikuwa ni kupoteza muda kugombea kwani uwezekano wa kushinda ulikuwa mdogo (LTO Report Dar es Salaam, 2010). Sababu za msingi za kuja na mkakati huu haziko wazi ikitiliwa maanani kampeni kubwa iliyofanywa na CHADEMA kukijenga nchi nzima. Kampeni hii ilipewa jina la Oparesheni Sangara na ilifuatia vuguvugu lililojitokeza mara baada ya CHADEMA kuibuka mshindi katika uchaguzi mdogo jimbo la Tarime. Viongozi wa CHADEMA walizunguka nchi nzima wakikusanya wanachama wapya.

Kwamba CHADEMA imejitahidi sana kupata wabunge katika maeneo mengi zaidi ya nchi ambako haikuwa ikijulina vya kutosha, ni dalili ya mafanikio ya operesheni Sangara.

Mwitikio wa vyama kuvutia wagombea ulitofautiana. Kama ambavyo uteuzi wa madiwani kwa jiji la Dar es Salaam unajionyesha, ni CCM, CUF na CHADEMA pekee ndio waliweza kusimamisha wagombea katika ngazi zote na kata zote. Vyama vingine vilisimamisha wagombea katika baadhi ya kata tu. Mathalani *Alliance for Tanzania Farmers Party* (AFP) kilibainisha kuwa kilipata usajili wa kudumu mwezi Novemba 2009 na hivyo hakikuwa na muda wa kutosha kujiandaa na uchaguzi. Pamoja na hayo, ukata ulizlazimisha wagombea kujitegemea wenyewe kuendesha kampeni.

NCCR-Mageuzi, chama kilichotamba wakati wa uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi mwaka 1995, kikapotea mwaka 2000, kilirudi kwa nguvu kiasi baada ya kushinda viti vine vyote mkaoani Kigoma. Ndani ya NCCR Mageuzi, wagombea wote walijadiliwa katika ngazi ya jimbo. Mapendekezo ya jimbo hupelekwa makao makuu kwa uthibitisho.

### 3.2 Uteuzi wa Wagombea Urais

Taratibu za uteuzi wa wagombea urais zilitofautiana ndani ya vyama. Uteuzi wa Dk. Wilbrod Slaa kama mgombea urais kwa tiketi ya CHADEMA uliwashangaza wachambuzi na watazamaji wengi wa siasa za Tanzania. Mgombea urais kupitia CHADEMA mwaka 2005 na mwenyeketi wake, Bw. Freeman Mbowe alikwishatangaza mapema kuwa atagombea ubunge katika jimbo la kwao Hai. Dk. Slaa pia alikwishatangaza kuwa ataendelea kugombea ubunge katika jimbo la Karatu. Hata hivyo CHADEMA hatimaye ilimteua Dk. Slaa kuwa mgombea urais katika dakika za mwisho. Itoshe kusema kuwa uteuzi wa mgombea urais ndani ya CHADEMA ulitokana na majadiliano ya siri, na hivyo mchakato wake ulikosa uwazi na ufasaha wa utaratibu.

Uteuzi wa mgombea urais ndani ya CCM ulitabirika kwa kiasi kikubwa kwa kuwa rais aliyepo anamaliza kipindi chake cha kwanza na alikuwa na sifa za kuendelea kugombea. Ingawa katiba ya CCM haiwakatazi wananchama kushindana na rais aliyeko madarakani, kumekuwa na utamaduni wa kumwachia rais aliyepo madarakani kupita bila kupingwa katika kipindi cha pili. Kwa mantiki hii, mgombea mmoja aliyejitokeza kutangaza nia ya kugombea urais kwa tiketi ya CCM alikejeliwa na kukatishwa tamaa. Hata hivyo utamaduni huu unaonekana kupata upinzani kadri siku zinavyokwenda. Nia ya John Shibuda kumkabili rais aliyeko madarakani ni mfano mmoja wa hili. Hivyo, mkutano wake mkuu wa Dodoma ulikuwa zaidi shamrashamra. Siku zote mbili za mkutano zilionyeshwa moja kwa moja na vituo vya televisheni na redio na vikundi mashuhuri vya sanaa na burudani vilialikwa. Rais Kikwete alipata kura 1,893 za NDIO sawa na asilimia 99.16 wakati kura 16 tu za HAPANA (asilimia 0.84). Bahati mbaya waangalizi wa TEMCO hawakushuhudia zoezi la kuhesabu kura ingawa walikubaliwa kuangalia mchakato wa kutangaza matokeo.

Wagombea wa CUF hawakubadilika kwani ni walewale waliokuwa wakigombea chaguzi zote toka kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi ndio walioteuliwa. Kwa kiasi kikubwa mchakato wa uteuzi ulikuwa wa wazi kwa maana kuwa kila mgombea aliulizwa wastani wa maswali kumi na wajumbe. Pia waangalizi wa TEMCO waliruhusiwa kuangalia mchakato mzima ikiwemo upigaji kura na kuhesabu kura. Prof. Ibrahm Lipumba alipitishwa kugombea urais wa Jamhuri kwa kupata kura 671 (asilimia 99). Kura mbili tu ndio zilimkataa. Mgombea urais wa Zanzibar Maalim Seif Sharif Hamad alipata kura 667 (asilimia 96.4) za NDIO kati ya kura 675. Kura tano zilikuwa za HAPANA wakati tatu ziliharibika.

TEMCO ilialikwa kupeleka waangalizi katika mikutano ya CCM na CUF. Tofauti kati ya mkutano wa CCM na ule wa CUF ni kuwa katika mkutano wa CCM hakukuwa na maswali yaliyoruhusiwa kutoka kwa wajumbe. Katika mkutano wa CUF kila mjumbe aliyetaka kuuliza swali alipewa nafasi na mgombea aliweza kuulizwa maswali kumi.

Kilichovutia katika utezuiz wa CCM ni uteuzi wa nfasi ya rais wa Zanzibar. Kwa kuwa rais Karume alikuwa anamaliza muda wake ushindani ulifunguliwa ambapo wanachama 11 walijitokeza kuwania urais, baadhi yao vigogo serikalini. Wagombea wengi walikuwa mawaziri au naibu mawaziri katika serikali iliyotangulia aidha Bara au Zanzibar. Ushindani mkali ulitarajiwa kati ya wagombea wanne: Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Dk. Ali Mohamed Shein, Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mh. Shamsi Vuai Nahodha, Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari na Utamaduni Mh. Ali Juma Shamhuna na Waziri Kiongozi mstaafu Dk. Gharib Ali Bilal. Tofauti na mwaka 2000 ambapo kura za maoni za Zanzibar zilifahamika, safari hii wajumbe walipiga kura lakini matokeo yake hayakuwekwa wazi. Baada ya tetesi za muda mrefu katika vyombo vya habari, uteuzi wa Dk. Ali Mohamed uliwashangaza wengi. Ilisemekana kuwa Dk. Gharib Bilal aliyekuwa na ushawishi mkubwa katika siasa za Zanzibar alikwashaazimia kuwa asingekubali kurudi Zanzibar bila urais wa Zanzibar. Hatimaye aliteuliwa kuwa mgombea mwenza wa rais Jakaya Kikwete katika uchaguzi wa muungano. Shamsi Vuai Nahodha aliteuliwa kuwa mbunge na rais na kisha kuteuliwa kuwa waziri wa mambo ya ndani ya nchi.

### 3.3 Uteuzi wa Vyama na Kuhama Vyama

Imeanza kuwa sehemu ya utamaduni wa kisiasa Tanzania kwa wagombea kuhama vyama pale wanaposhindwa kupata uteuzi katika vyama vyao. Wakati mwingine wale wanaohama hulalamikia ukiukwaji wa taratibu za uteuzi ndani ya vyama na hudai kuwa wao nmi maarufu na wanaweza kuchaguliwa bila kujali chama watakachoingia. Kwa ujumla CCM wanaonekana kuwa wahanga wakati CHADEMA wamefaidika na wimbi la kuhama vyama. Kama Jedwali 3.1 hapa chini linavyooneysha, wagombea wane waliohama vyama walishinda katika uchaguzi mkuu. Hii ilikuwa taofuti kabisa na uchaguzi wa mwaka 2005 kwani waliohama kutaoka CCM kwenda vyama vya upinzani wote walianguka kwenye uchaguzi mkuu.

Uteuzi ndani ya vyama haikuwa sababu pekee ya wagombea kuhama vyama vyao. Huko Hanang wagombea sita wa udiwani kwa tiketi ya CHADEMA na CUF waliamua kuhama vyama vyao wakati wa ziara ya mgombea urais wa CCM rais Jakaya Kikwete hivyo kuleta pigo kubwa kwa vyama vya upinzani huku wakiwaacha wagombea wa CCM wakipita bila kupingwa katika kata husika (LTO Report Manyara, 2010).

**Jedwali Na. 3.1: Waliojitoa na Kujiunga na Vyama Vingine Kabla na Baada ya Uteuzi**

| Jina la Mgombea | Jimbo | Chama cha Awali | Chama alichokwenda | Matokeo ya Uchaguzi | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Shinda | Shindwa |
| John Shibuda | Maswa West | CCM | CHADEMA | √ | |
| Sylevester M. Kasulumbayi | Maswa East | CHAUSTA | CHADEMA | √ | |
| Thomas Nyimbo | Njombe West | CCM | CHADEMA | | √ |
| Charles Mwera | Tarime | CHADEMA | NCCR-Mageuzi | | √ |
| David Kafulila[7] | Kigoma South | CHADEMA | NCCR-Mageuzi | √ | |
| Fred Mpendazoe[8] | Kishapu | CCM | CCJ, CHADEMA | | √ |
| Alcardo Ntagazwa | Muhambwe | CCM | CHADEMA | | √ |
| Prof. Kulikoyela Kahigi | Bukombe | CCM | CHADEMA | √ | |
| Rose Kamili | Hanang | CCM | CHADEMA | | √ |
| Charles Kagonji | Mlalo | CCM | CHADEMA | | √ |

Chanzo: TEMCO na Ripoti za Vyombo vya habari

## 4.0 UTEUZI WA TUME YA UCHAGUZI NA MATOKEO YAKE

Uteuzi rasmi wa Tume ya Uchaguzi haukuwa na matatizo. Wagombea urais wawili waliachwa kwa kushindwa kujaza fomu zao ipasavyo. Baadaye SAU walipinga uamuzi wa Tume mahakamani wakidai kuwa walijaza fomu zao pamoja na kupata saini za wadhamini isipokuwa maafisa wa Tume hawakuzipitia vizuri kwa muda muafaka. Waliongeza kuwa maafisa wa Tume walishindwa kujitokeza wakati wa kuhakiki majina ya wadhamini. Mahakama ilifutilia mbali shitaka hili. Mgombea mwingine, Christopher Mtikila, aliyeenguliwa kwa sababu zinazofanana na hizi aliamua kutokwenda mahakamani. Hata hivyo baadaye matokeo ya kura yalipotangazwa alijisifu kuwa wapiga kura wote ambao hawakujitokeza kwenda kupiga kura wangempigia yeye kama angeruhusiwa kugombea.

Kesi hizi za kuenguliwa kwa wagombea, hata kama hazikuhusisha vyama vyenye nguvu, vinatilia mkazo udhaifu uliopo katika utaratibu wa uteuzi wa Tume. Uteuzi rasmi hufanywa ndani ya siku moja tu. Kama kuna kosa katika kujaza fomu au kosa linguine, hakuna muda wa kurekebisha. Manufaa ya mchezo huu wa *paka na panya* yanatia shaka. Huko iringa ilitokea tukio la kushangaza ambapo mgombea alipoteza mkoba ukliokuwa na fimu za uteuzi pamoja na nyaraka nyingine na hakukuwa na muda wa kujaza upya fomu hizo. Iringa Mjini mgombea ubunge wa CUF na diwani mmoja walienguliwa kufuatia pingamizi la NCCR Mageuzi kuwa namba za shahada za wadhamini wao zilikosewa na hazikuwemo kwenye DKWK (LTO Report Iringa, 2010).

Mwenyekiti wa Wilaya wa CUF baadaye alikiri kufanya makosa katika kujaza fomu za wadhamini. Msimamizi wa uchaguzi alisisitiza kuwa CUF haikutumia ipasavyo siku tatu walizopewa kuhakiki majina ya wadhamini wao. Hata hivyo hatari ya kupanga siku moja tu kwa ajili ya uteuzi inabakia palepale. Nyakati hizi ambazo wagombea hutumia kila aina y

[7] David Kafulila alihama kabla ya mchakato rasmi wa uteuzi ndani ya vyama kufuatia siasa za kupanga safu za uongozi ndani ya CHADEMA kuelekea uchaguzi mkuu.

[8] Fred Mpendazoe Mbunge wa Kishapu, aliamua kujiuzulu ubunge na kujiunga na CCJ chama ambacho kilikuwa hakijasajiliwa na baadaye alijiunga na CHADEMA iliposhindikana kusajili CCJ AKAJIUNGA NA CHADEMA. Aligombea jimbo la Segerea lakini akaangushwa na Makongoro Mahanga wa CCM

ahila kutengua uteuzi wa washindani wao, ni hatari kuwa na siku moja tu ya uteuzi. Kwa hakika, wagombea wengi walipita bila kupingwa katika uchaguzi wa mwaka 2010 walitumia hila hizi.

### 4.1 Pingamizi, Malalamiko na Ushughulikiaji wa Rufaa

Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2010 zinaeleza taratibu za kufuatwa iwapo mgombwea anataka kuweka pingamizi. Mkurugenzi wa Uchaguzi, Msajili wa Vyama vya Siasa na Mgombea ubunge ndio wanaoweza kuweka pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea yeyote wa ubunge. Pingamizi la mgombea dhidi ya mwingine hutakiwa kujazwa katika fomu Namba 9B na hutakiwa kuwa na vifuatavyo, habari binafsi za muweka pingamizi, na sababu za pingamizi. Mwelekeo dhahiri katika uchaguzi wa 2010 ilikuwa kwamba mapingamizi mengi yaliwekwa kwa sababu ya kutaka kutoa mwanya kwa wagombea kupita bila kupingwa.
Mgombea akifanikiwa kumuengua mshindani wake sit u anakuwa amepata njia ya mkato ya kushinda, bali pia natakuwa amekwepa machungu na gharama zinazohusiana na kampeni za uchaguzi.

Baada ya kupokea pingamizi, Msimamizi wa Uchaguzi humuarifu kwa maandishi mgombea aliyewekewa pingamizi na kumpa fursa ya kujieleza. Msimamzizi wa Uchaguzi ana waibu wa kuwasilisha kwa maandishi maamuzi yake kwa pande zote. Msimamizi wa Uchaguzi akikubaliana na pingamizi humfuta katika orodha ya wagombea, mgombea aliyewekewa pingamizi. Ripoti za TEMCO zinatilia shaka iwapo utaratibu huu ulifuatwa. Hakika katika baadhi ya majimbo, waliowekewa pingamizi hawakupata nafasi ya kusikilizwa.

Ikitokea mgeombea hakuridhika na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi, kuna nafasi ya kukata rufaa Makao Makuu NEC. Taratibu za kukata rufaa zinapatikanan katika Kanuni za Uchaguzi 2010 kipengele cha 31 (vipengele vidogo 1-6). Mtu yeyote ambaye hakuridhishwa na uamuzi wa msimamizi wa uchaguzi hanma budi kukata rufaa kwa NEC ndani ya saa ishirini na nne tangu wakati uamuzi ulipotolewa. Mtego ni kuwa fomu za rufaa (Fomu Namba 12) ni lazima zipatikane kwa msimamizi wa uchaguzi (ambaye anakuwa mlalamikiwa katika shauri hili). Ilivyotokea huko Nyamagana inaeleza mtego huu unavyofanya kazi. Kwanza msimamizi wa uchaguzi alikataa kutoa fomu za rufaa kwa mgombea wa CHADEMA aliyetaka kukata rufaa. Mgombea huyu hakuwa na njia nyingine isipokuwa kupanda ndege kuwahi makao makuu ya Tume kupata fomu za rufaa. Alizijaza na kulazimika kuzipeleka tena kwa Msimamizi wa uchaguzi kwa ajili ya kupitishwa pamoja na kupata ushahidi ikiwamo fomu Na. 8b na 9b kabla ya kuwasilishwa tena Dar es Salaam.

Rufani zote hushughulikiwa kwa mujibu wa kipengele cha 35 cha Kanuni za Uchaguzi. Tume ina mamlaka ya kumwita mtu yeyote kutoa ushahidi au ufafanuzi kuhusiana na rufaa iliyo mbele yake. Baada ya hapo Tume inawajibika kumtaarifu mrufani kwa maandishi uamuzi wake. Kanuni hapa ziko wazi lakini TEMCO ilishuhudia matatizo yanayoweza kujitokeza. Kwa kesi ya Mtama, ambayo pia ilimhusisha waziri katika serikali iliyokuwa inamaliza kuda wake, Tume ilituma uamuzi wake, lakini kupitia kwa msimamizi wa uchaguzi wa Mtama. Msimamizi wa Uchaguzi alikaa na barua ile kwa wiki mbili. Tume ingeweza kuituma barua ile moja kwa moja kwa mhusika.

Huko Singida Mjini, mgombea wa CCM aliwawekea pingamizi wagombea wa CHADEMA, AFP na CUF kwa madai kuwa hawakujaza ipasavyo fomu zao ikiwemo kusiniwa na makatibu wa wilaya wa vyama vyao na kuwa mgombea wa AFP alikuwa na wadhamini tisa

badala ya kumi. Pingamizi hili lilikubaliwa na msimamizi wa uchaguzi na hivyo kumfanya mgombea wa CCM kupita bila kupingwa. Uamuzi huu hata hivyo ulitenguliwa baadaye na Tume.

Ni vigumu kupata idadi ya mapingamizi yote yaliyowekwa na wagombea ubunge na udiwani nchi nzima lakini yalikuwepo mengi na mengi ylikubaliwa na wasimamizi wa uchaguzi. Wagombea wengi pia walikata rufaa Tume. Kwa ujumla, Tume ilipokea rufaa 56 zilizohusiana na ubunge na rufaa 124 zilizohusiana na udiwani. Kati ya hizi, Tume ilikubali rufaa nne na mbili kati yake zikihusisha watu wazito serikalini.

Uamuzi ambao ulichukua sura ya kitaifa ulikuwa ni ule wa kukubali rufaa ya mgombea wa ubunge wa CHADEMA katika jimbo la Nyamagana huko Mwanza. Mgombea wa CCM, aliyekuwa waziri wa mambo ya ndani akishughulikia masuala ya uraia, alimuwekea pingamizi mgombea wa CHADEMA kwa madai kuwa hakuwa raia. Msimamizi wa uchguzi alikualiana na pingamizi la mgombea wa CCM na hivyo kumfuta katika orodha ya wagombea mgombea wa CHADEMA na kumfanya mgombea wa CCM kutangazwa kupita bila kupingwa. Uamuzi huu ulikuja kubadilishwa na Tume kufuatia rufaa ya mgombea wa CHADEMA. Baada ya kura kupigwa mgombea wa CHADEMA aliibuka mshindi kw tofauti ya kura nyingi. Kisa hiki kiliamsha madai ya siku nyingi ya ulazima wa wagombea wanaopita bila kupingwa kupigiwa kura na wananchi. Uamuzi mwingine kama huu wa kukubali rufaa dhidi ya waziri ulifanywa na Tume kwa jimbo la Mtama ambapo mgombea wa TLP alirejeshwa baada ya kuwa amefutwa na msimamizi wa uchaguzi.

### 4.2 Mapingamizi kwa ngazi ya udiwani

Katika ngazi ya udiwani TEMCO ilishuhudia jinsi ambavyo mchanganyiko wa elimu ndogo, na weledi hafifu miongoni mwa maafisa watendaji wa kata ulivyochangia katika kuleta mkanganyiko wakati wa uteuzi. Katika baadhi ya kesi, maafisa watendaji wa kata walikuwa awakitishiwa na wanansiasa kuwa walikuwa watendaji wa serikali na hivyo wahakikishe chama twala kinashinda. Mwangalizi wa uchaguzi wa mkoa wa Kagera anahitimisha kuwa uwingi wa mapingamizi katika ngazi ya udiwani ulitokana na kiasi Fulani ujinga na kisai Fulani shinikizo kutoka kwa viongozi wa chama tawala.

## 5.0 MGOMBEA BINAFSI

Suala la mgombea binafsi limekuwa likileta mijadala mikali tangu kuanzishwa upya kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa na umechangia katika madai ya mabadiliko ya katiba. Mchezo wa kujificha unaoonekana katika suala hili unashangaza. Wale wanaotaka kuwepo kwa wagombea binafsi wanakariri vipengele vya katiba vinavyosisitiza haki na wajibu wa raia. Haki hizi ni pamoja na haki ya kupiga kura na kupigiwa kura ambayo haitakiwi kuwekewa mazonge ya vyama vya siasa. Wale wasiotaka mgombea binafsi awepo, wanadai kuwa ni vigumu kumwajibisha mgombea binafsi hasa kwa masuala ya uwajibikaji. Wanadai kuwa chama cha siasa huweka muundo wa kudhibiti wagombea na hivyo kuwafanya wawajibike zaidi kwa wananchi. Mpaka sasa kuna hukumu tatu za mahakama kuhusiana na suala la mgombea binafsi.

Mwaka 1993 Mchungaji Christopher Mtikila, Mwenyekiti wa Democratic Party (DP) alifungua kesi mahakama kuu akitaka mabadiliko katika Ibara za 39 na 67 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwani alidai vinakiuka Katiba. Uamuzi wa Mahakama, uliosomwa na Jaji Kahwa Lugakingira tarehe 16 Oktoba 1994 unachukuliwa kama “hukumu wa kihistori”. Hukumu hiyo ilikubaliana na mlalamikaji ikitilia mkazo yafuatayo:

(i) Haki za msingi siyo zawadi kutoka kwa dola, isipokuwa zinastahili kutolewa kwa mtu yeyote na zilikuwepo hata kabla ya dola na sheria. Kuwekwa kwa haki hizo kwenye katiba ni ushhidi tu wa kuzitambua na nia kwamba haki hizi zitakuwa na nguzu ya kisheria na haziwezi kuzuiwa bila sababu na dola.

(ii) Ibara ya 21(1) inampa haki kila raia kushiriki katika serikali ya nchi, ama moja kwa moja au kupitia wawakilishi waliochaguliwa kwa utashi wa wananchi. Haiingiii akilinni kwa katiba hiyohiyo tena katika Ibara ya 20(4) kulazimisha mwananchi kuwa mwananchama wa chama cha siasa ili kugombea.

(iii) Inapotokea kipengele kimoja cha katiba kinapingana na kingine kinachotoa haki ya msingi, mahakama inalazimika kutoa upendeleo kwa haki za msingi na kuacha kipengele kingine ambacho utekelezaji wake huweza kuvunja haki. Ni haki za msingi ambazo mahakama ipo kuzilinda kwa nguvu zote, na siyo vikwazo vya haki.[9]

Badala ya kukata rufaa kupinga uamuzi huu, serikali iliamua kufuata utaratibu mwingine na kuweka sheria. Ilipofika Desemba 1994 Bunge likapitisha muswada ambao ulikuwa ni mabadiliko ya 11 ya katiba ya mwaka 1994. Kipengele hiki kiliweka msisitizo kuwa ili Mtanzania agombee uchaguzi katika ngazi yoote sharti awe mwananchama wa chama cha siasa.

Suala hili liliibuka tena mwaka 2006 pale Mchungaji Mtikila alipopinga mabadiliko haya ya katiba. Jopo la majaji wanne walisikiliza kesi hii. Hukumu yao ilikuwa kwamba kuweka vizuizi kwa wananchi kugombea ilikuwa ni kinyume na katiba na uvunjifu wa haki za kidemokrasia zilizopo katika katiba (The *Citizen on Sunday*, 19 Desemba 2010). Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipinga hukumu hii akihoji nguvu ya mahakama kubadilisha katiba. Uamuzi wa Mahakama ya Rufaa ulitolewa na jopo la majaji saba tarehe 17 Juni 2010. Hukumu hii inafurahisha kwani haikugusia suala la mgombea binafsi bali ilijikita katika masuala ya utaratibu na kanuni. Mahakama ilikubaliana na hoja ya Mwanasheria Mkuu kuwa Mahakama haina uwezo wa kubadilisha vifungu vya katiba na kwamba mamlaka hayo yapo kwa Bunge pekee. Mahakama ilihitimisha hukumu yake kwa kubainisha kuwa suala la mgombea binafisi ni la kisiasa na siyo la kisheria (*The Citizen on Sunday*, 19 Desemba 2010). Mahakama ya Rufaa haikuwa kufikiria kurejea hukumu ya Jaji Lugakingira kuwa mahakama zipo kwa ajili ya kulinda haki za msingi kwa gharama yoyote na siyo kuweka vikwazo. Inaonekana mahakama sasa inajipanga siyo kulinda haki za msingi, bali hasa kuzikandamiza.

Inashangaza kuwa serikali haikufanya chochote baada ya hukumu ya mwaka 2006 na ikasubiri mpaka mwaka 2010 kukata rufaa. Ni dhahiri kuwa kwa kutoa hukumu mweiz wa Juni 2010 serilai ilikuwa inapunguza uwezekano wa wananharakati kupinga tena mahakamani. Hakika kuzuia wagobea binafsi ni kunyume cha mwenendo wa siasa za uliberali ambazo Tanzania imeanza kuzifauta mara baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi. Kwa vyovyote vile, matakwa ya kuwa mwananchama ili kugombea, ni moja ya mabaki ya mfumo wa chama kimoja. Hili ni eneo ambalo wapwnzi wa katiba mpya wana mengi ya kufanya. Inaonekana kuwa mgobea binafsi ni mwiba kwa walioko madarakani na hasa chama tawala, nah ii inoonekana kwa jinsi ambavyo suala hili limekuwa likipigwa danadana.

[9] Kwa majadala wa kisheria zaidi juu ya hukumu za mahakama juu ya mgombea binafsi, angalia *The Citizen, 18 Desemba 2010* na *TheCitizen on Sunday,* 19 Desemba 2010.

## 6.0 HEKAYA ZA KUPITA BILA KUPINGWA

Idadi ya wagombea waliopita bila kupingwa katika uchaguzi wa mwaka 2010 iliongezeka mara dufu ikilinganishwa na mwaka 2005. Wakati mwaka 2005 wagombea 8 wa CCM walipita bila kupingwa majimboni kwao, mwaka 2010 wagombea 16 walipita bila kupingwa. Mshawasha wa kupita bila kupingwa ni mkubwa na wanasiasa wajanja na wasio waaminifu watatumia mwanya huu wa kisheria kuhakikisha wanapita bila kupingwa. Baadhi wamekuwa wakipita bila kupingwa hata kwa chaguzi tatu mfululizo. Kuna sababu nyingi za kueleza kwa nini jimbo humpitisha mgombea bila upinzani. Katika baadhi ya majimbo ni wazi kuwa wananchi hawawezi kuruhusu upinzani hasa pale ambapo anayeshikilia kiti cha ubunge pia ana nyadhifa nyeti serikalini na wao wana matumaini ya kufaidika ama kwa kupata vitu au tu kwa majigambo tu ya kuwa na mtu mzito jimboni. Imekuwa kawaida kwa mawaziri wakuu kupita bila kupingwa majimboni mwao na hii ni moja ya sababu. Wakati mwingine mbunge huwa amefanya mambo mengi mazuri kwa wananchi kiasi ambacho wananchi humhakikishia ushindi na ayejitokeza kumpinga huweza kubezwa na kutengwa. Wengi wa wanaopita bila kupingwa hutaka kuonekana walifanya mambo makubwa kwa wananchi hata kama ukweli ni kinyume chake. Lakini maelezo haya hayawezi kutosheleza pale ambapo mgombea aliyejitokeza kwa mara ya kwanza anapopita bila kupingwa kama ilivyokuwa kwa jimbo la Bumbuli. Kupita bila kupingwa ni njia ya mkato ya ushindi inayomhakikishia mgombea ushindi mwororo bila kukumbana na hasira za wapiga kura na gharama zinazoendana na kampeni.

Kwa kiasi kikubwa udhaifu wa upinzani pia ulichangia katika idadi kubwa ya wagombea kupita bila kupingwa. Katika uchaguzi wa 2010 ni CCM pekee ndio waliweza kuismamzisha wagombea katika majimbo yote 239 na kata 3,337. Vyama vingine viliweka wagombea kwenye baadhi tu ya majimbo na kata. CHADEMA waliotoa ushindani mkali kwa CCM walikuwa na wagombea kwenye majimbo 182 tu (76% ya viti vyote); CUF walikuwa na wagombea 170 (71% ya majimbo) ingawa iliweka wagombea katika majimbo yote ya Zanzibar; TLP na NCCR-Mageuzi walikuwa na takriban wagombea 64 kila kimoja. Upande wa madiwani, idadi ilikuwa ya kusikitisha zaidi. Simanjiro, matahalani, CCM ilipita bila kupingwa katika kata 16 kati ya 18! Kwa ujumla wagombea 540 wa udiwani wa CCM walipita bila kupingwa (sawa na asilimia 15.3).

Rufaa mbili tata zilizohusisha mawaziri katika serikali iliyokuwa inamaliza muda wake zilitikisa anga za siasa za Tanzania. Nyamagana waziri wa mambo ya ndani ya nchi Mh. Lawrence Masha alikuwa akigombea wakati huko Mtama alikuwa ni waziri wa mambo ya nje na ushirikaiano wa kimataifa. Rufaa ya tatu ilimhusisha waziri wa afya huko Rungwe Mashariki ambapo Tume ilikubaliana na msimamizi wa uchaguzi kuwa mlalamikaji alikuwa bado kwenye huduma ya jeshi.

Nyamagana mgombea wa CCM aliweka pingamizi la uraia dhidi ya mgombea wa CHADEMA. Msimamizi wa uchaguzi alikubaliana na pingamizi na hivyo mgombea wa CCM akawa amepita bila kupingwa mpaka wakati huo. Msimamizi wa uchaguzi akakataa kumpa fomu Na 8B na 9B ili kukata raufaa. Inasemekana kuwa mmoja wa watu kutoka kambi hasimu ndani ya CCM alilipa nauli ya ndege kumwezesha mgombea wa CCM kupata fomu za rufaa makao makuu ya Tume, Dar es Salaam. Tume ilikubali rufaa na hivyo kumrudisha mgombea wa CHADEMA. Mgombea huyu alishinda kwa kupata asilimia 58 ya kura zilizopigwa dhidi ya mgombea wa CCM aliyepata asiliamia 44. Maana yake ni kuwa kama pingamizi la msimamizi wa uchaguzi lingesimama, wananchi wa Nyamagana wangekuwa na mbunge aliyejipandikiza na kujilazimisha lakini asiyetakiwa na wananchi wengi. Ikikosekana utaratibu wa kupima kukubalika kwa wagombea wanaopita bola

kupingwa, ni vigumu kusema wengine walioppita bila kupingwa wanakubalika namna gani majimboni mwao. Rufaa dhidi ya mawaziri na vigogo wengine ndani ya chama tawala huwa ngumu sana kuzifanyia kazi hasa kwa kuwa wagombea hawa huwa na mitandao mirefu nadni ya serikali na huweza kuwa na mahusiani ya karibu na mamlaka kuu. Katika hali hii mkurugenzi wa halmashauri hawezi kuwa na ubavu wa kuzuia ushawishi wa waziri kama ambavyo Nyamagana ilionyesha.

Mgombea wa TLP jimbo la Mtama naye alirudishwa baada ya kufutwa na msiamaizi wa uchaguzi kufuatia pingamizi la mgombea wa CCM, Waziri wa mambo ya nje, Mh. Bernard Membe. Mgombea huyu wa TLP alishindwa kwenye uchaguzi mkuu. Ripoti za TEMCO kutoka Mtama zinaonyesha namna gani mgombea wa CCM alipalilia njia ili kupita bila kupingwa. Kwa kuanzia, mgombea wa CUF hakurudisha fomu kufikia tarehe 19 Agosti 2010, ambayo ilikuwa siku ya mwisho ya kurudisha fomu. Siku chache baadaye alijitoa CUF na kuhamia CCM ambako alifanywa kuwa meneja wa kampeni katika jimbo la Lindi Mjini. Hii ilizusha maswali mengi sana na hatimaye wengi waliamini kuwa mgombea huyu wa CUF alihongwa na CCM. mgombea wa CUF ndiye aliyekuwa tishio kwa mgombea wa CCM. Lakini bado kulikuwa na kikwazo na mgombea wa CCM asingeweza kutangazwa amepita bila kupingwa kwani mgombea wa TLP bado alikuwepo. Ndipo mgombea wa CCM “akagundua” upungufu katika fomu za uteuzi za mgombea wa TLP. Pingamizi likawekwa kuwa baadhi ya wadhmini hawakuwamo kwenye dafatari la kudumu la wapiga kura na walighushi saini. Msimamizi wa uchaguzi akakubaliana na pingamizi na kumfuta mgombea wa TLP. Mpaka hapo, mgombea wa CCM akawa amepita bila kupingwa. TLP mara moja wakakata rufaa Tume tarehe 21 Agosti 2010. Katika rufaa yao wakakanusha kuwa wadhamini hawakuwemo kwenye dafatari la kudumu la wapiga kura na baadhi walighushi saini. Tarehe 26 Agosti 2010 Mkurugenzi wa Uchaguzi Bw. Rajab Kiravu akatangaza kuwa walipokea rufaa hiyo. Baada ya kimya cha muda mrefu bila majibu kutoka Tume, tarehe 17 Septemba mgombea wa TLP akaamua kwenda TBC1 kuelezea kilio chao. Siku iliyofuatia (Jumamosi tarehe 18 Agosti 2010) ambayo haikuwa siku ya kazi, baada ya habari kutangazwa na TBC1, msimamizi wa uchaguzi alimpa mgombea wa TLP barua kutoka Tume (Ref. No. AE.74/141/02/51 ya tarehe 04/09/2010) ikionyesha kuwa mgombea wa TLP anaruhusiwa kugombea. Kwa sababu ya ucheleweshaji huu wa makusudi, mgombea wa TLP alishindwa kufanya kampeni wala kujaza fomu muhimu za EE1 to EE11 kwani tarehe ya mwisho kufanya hivyo ilikuwa 6 Septemba 2010. Bahati nzuri karatasi za kupigia kura zilikuwa na majina ya wamgombea wa CCM na TLP.

Iringa iliongoza kwa idadi kubwa ya wagombea waliopita bila kupingwa ikilinganishwa na mikoa mingine 9 iliyokuwa na wagombea walioppita bila kupingwa. Katika majibmo matano wagombea walipita bila kupingwa ikifuatiwa na Mbeya ambayo ilikuwa na majimbo matatu na Dodoma majimbo mawili. Mikoa ya Tanga, Rukwa, Morogoro, Mara, Manyara na Kagera ilikuwa na jimbo moja moja lililopita bila kupingwa. Ripoti kutoka Iringa zinaonyesha matukio ambapo rushwa inaweza kuwa ilitumika. Madai haya kwa Isimani yaliwekwa hadharani katika mkutano wa hadhara wa CHADEMA kwani mtuhumiwa alikuwa kiongozi ndani ya CCM. Huko Ludewa kulikuwa na tukio lakushangaza ambapo msimamizi wa uchaguzi alikataa kutoa fomu kwa mgombea wa CHADEMA kwa madai kuwa mgombea mwingine kutoka CHADEMA alikwsihachukua fokkmu hizo na kwamba amtafute kwazana mtu huyo ndipo apewe fomu. Mtu anaweza akajenga taswira amabapo mtu mwenye barua ya kughushi anavyoweza kwenda kuchua fomu na watu wa Ludewa wakashindwa kumpigia kura mgombea wa CHADEMA kwa sababu pandikizi amekwenda kuchukua fomu. Kwani kuna fomu moja tu kwa kila chama? Inatia shaka kwamba Tume ya Uchaguzi inaweza kuendesha mfumo kama huu (LTO Report Iringa Region, 2010). Ripoti kutoka Mbeya

ambako majimbo matatu yalipitisha wagombea bila ushindani zinaonyesha matukio ya vitisho na manynyaso kwa wagombea wa CHADEMA. Tuhuma za namna hii pia ziliibuka huko Musoma Vijijini ambako ilidaiwa kuwa mgombea wa CHADEMA alilipwa € 1,000 (karibu shilingi milioni mbili) na mgombea wa CCM ili ajitoe katika uchaguzi (*Raia Mwema*, 25th – 31st August 2010). CHADEMA ilidai kuwa na ushahidi wa maneno ambao waliouwakilisha TAKUKURU kwa upelelezi zaidi.

## 7.0 TATHMINI YA TEMCO YA MCHAKATO WA UTEUZI

Ili kurahishisha tathmini ya mchakato wa uchaguzi, waangalizi wa uchaguzi wa TEMCO walitakiwa kufanya tathmini ya haraha ya mchakato wa uteuzi na kuituma makao makuu ta TEMCO, Dar es Salaam. Tathmini hii ilifanyika kwa michakato mingine ya uchaguzi ikiwamo kampeni na kupiga na kuhesabu kura na kuiwezesha TEMCO kufanya tathmini ya mwenendo wa cuahguzi mzima ili kubaini ni kwa kasi gani uchaguzi ulikuwa huru ha haki. Waangalizi walitakiwa kutoa alama katika michakato mitatu ya ucahguzi kama ifuatavyo:

i) 0% au alama F: kumaanisha uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) ambao ulishindwa kabisa katika menejimenti, kufuata sheria za uchaguzi, kanuni na taratibu, haki na usawa na hivyo usingeweza kufikia mwisho wa kawaida.

ii) 1 – 39% au alama E: kumaanisha uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) yenye matatizo mengi ya kimenejimenti na uvunjaji wa kanuni na sheria kiasi kwamba wadau mbalimbali wanankataa matokeo ya uchaguzi.

iii) 40 – 49% au alama D: kumaanisha mchackato wa uchaguzi ambao ulikuwa na vitendo vya vitisho, upendeleo, rushwa .

iv) 50 – 59% au alama C: kumaanisha uchaguzi ambao huruhusu ushiriki huru wa wadau (wapiga kura, wagombea, na wengineo) lakini kuna matukio mengi ya vyama vikubwa na hasa chama tawala kuvunja sheria na kanuni bila kuchukuliwa hatua. Hiyo ndio kusema uchaguzi ulikuwa huru lakini siyo wa haki.

v) 60 – 79% au alama B: kumaanisha uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) ambao kwa ujumla ni huru na haki lakini bado kuna upungufu ambayo yanaathiri baadhi ya wadau. Ni uchaguzi huru na haki "wenye shaka".

vi) 80% au zaidi au alama A: kumaanisha uchaguzi ambao ni upungufu machache tu yalijitokeza ambayo yasingeathiri mwnendo mzima wa uchaguzi. Ni uchaguzi, safi, huru na haki.

Jedwali 3.2 linaonyesha kuwa uteuzi kwenye zaidi ya nusu ya majimbo ungeweza kusemwa kuwa huru na haki "wenye shaka" katika mizania ya TEMCO. Ni majimbo asilimia 21 tu yangeweza kusema kuwa "huru na haki". Karibu asilimia 22 ya waangalizi wa TEMCO waliona kuwa kwa namna mchakato wa uteuzi ulivyokwenda, ulikuwa huru na haki lakini kulikuwa na matukio mengi ambapo wadau waliweza kushiriki kwa uhuru lakini pia chama tawala kivunja sheria bila kuchukuliwa hatua. Hiyo ndio kusema kwa ujumla, uteuzi wa wagombea unaweza kusemwa kuwa ulikuwa huru lakini siyo wa haki.

**Jedwali Na. 3.2: Tathmini ya Uteuzi iliyofanywa na Waangalizi wa Uchaguzii**

| Alama | Gredi | Masafa* | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **0** | F | 1 | 0.6 |
| **1-39** | E | 4 | 2.4 |
| **40-49** | D | 1 | 0.6 |
| **50-59** | C | 34 | 21.5 |
| **60-79** | B | 83 | 52.5 |
| **80-100** | A | 35 | 21 |
| **Zinazokosekana** | | 9 | 5.4 |
| **Jumla** | | **167** | **100** |

Chanzo: Waangalizi wa TEMCO

## 8.0 HITIMISHO

Katika sura hii tumeangalia mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama na Tume ya Tiafa ya Uchaguzi. Tumeona kuwa uteuzi wa wagombea ni mchakato pacha unaohusisha vyama na Tume kwa namba toafauti. Sheria bado inazuia mghombea binafsi na hivyo kuwafanya wote waliotaka kugombea kupata uteuizi wa vyama. Ingawa kuna vyama 18 vyenye usajili wa kudumu, nivyama sita tu ndio vilipata wabunge katika uchaguzi wa mwaka 2010: CCM, CHADEMA, CUF, NCCR-Mageuzi, TLP and UDP. Hakuna chama kingine amabacho kimewahi kupata wabunge tangu uchaguzi wa mwaka 1995.[10] Matokeo yake ni kuwa kumekuwa na walau ushindani mkali kuwania uteuzi ndani ya vyama hivi kulingana na uwezekano wa kuchaguliwa kwa tiketi ya chama husika. CCM walivutia wagombea wengi kwa sababu uwezekano wa kuchaguliwa kupitia tiketi ya CCM ni mkubwa.[11] Kimsingi vyvama vyote hudai kuwa na mifumo ya kidemokrasia ya kuteua wageombea wake. Katika uhalisia kama ambavyo ilijionyesha wakati wa uteuzi kulikuwa na upungufu mengi na kuchezewa kwa kanuni za demokrasia. Ingawa CCM iliboresha sana mfumo wake wa uteuzi, kuufanya uwe shirikishi na kidemokrasia zaidi, matendo mengi yaliyokatazwa na sheria yaliripotiwa ndani ya CCM kuliko katika vyama vingine.

Mwishowe, sheria ya wanaopita bila kupingwa kupata ushindi wa moja kwa moja kulialika vituko na hila kutoka kwa wagombea ndani ya vyama. Katika uchaguzi wa mwaka 2010 idadi ya wagombea ubunge na udiwani waliopita bila kupingwea iliongezeka mara dufu ikilinganishwa na uchaguzi wa mwaka 2005. Hii imeleta mjadala juu ya uhalali wa kidemkrasi wa mgumo huu. Maoni ya ujumla ni kuwa walau wagombea wanaopita bila kupingwa wapigiwe kura na wananchi wote kuona kama kweli wanakubalika. Hii itapunguza uwezekano wa wanansiasa wajanja kutumia hila ili kupita bila kupingwa.

[10] Baadi ya vyama hivi vya siasa hata hivyo vimekuwa vikishinda viti katika baadahi ya kata katika uchaguzi wa madiwani na uchaguzi wa serikali za mitaa.

[11]Dar es Salaam peke yake kulikuwa na wagombea 90 waliojitokeza kuomba uteuzi ndani ya CCM. Hii ni wastani wa wagombea 11kwa jimbo. Angalia TEMCO Newsletter, EEA Series No. 1, Septemba 2010.

## SURA YA NNE

## USIMAMIZI WA CHAGUZI ZA MUUNGANO 2010

### 1.0 UTANGULIZI

Sura hii inatathmini jinsi uchaguzi mkuu wa 2010 ulivyosimamiwa kwa lengo la kujiridhisha endapo chaguzi hizo zilifikisha viwango na vigezo muhimu vya uchaguzi huru na haki, na endapo chombo kilichosimamia uchaguzi huo kilijidhihirisha kuwa ni huru na endapo kanuni na taratibu zote za uchaguzi zilizingatiwa. Hivyo sura hii inajadili jinsi sheria za uchaguzi zilivyochangia katika uendeshaji wa uchaguzi na pia kutoa mapendekezo ya namna ya kuboresha usimamizi wa uchaguzi nchini Tanzania. Sehemu tano kuu zitajadiliwa katika sura hii: i) Kanuni na Sheria zilizotumika katika kuendesha uchaguzi wa 2010, ii) uteuzi wa waombea (uteuzi ndani ya vyama vya siasa na uteuzi uliofanywa na NEC), iii) Uzoefu katika usimamizi wa uchaguzi, iv) Matokeo ya Uchaguzi na v) Mambo muhimu yaliyojitokeza na mapendekezo ya namna ya kuboresha chaguzi zijazo.

### 2.0 SHERIA NA MISINGI YA KIASASI ILIYOONGOZA CHAGUZI ZA 2010

Uchaguzi ulioendeshwa vema huipatia serikali uhalali wa kutawala na hili ni sharti muhimu katika kujenga utawala bora. Hii ni kwa kuwa katika demokrasia viongozi ni lazima wapate ridhaa ya kutawala kutoka kwa wananchi wenyewe kupitia kanuni na taratibu zinazokubalika. Hivyo sheria za uchaguzi pamoja na wale wanaozisimamia ni lazima wahamasishe na siyo kuwa kikwazo cha kuwazuia wananchi kuamua juu ya uongozi wanaoutaka. Kwa mantiki hii, sheria za uchaguzi pamoja na taratibu zote za uchaguzi, ukianzia na katiba yenyewe, pamoja na sheria mbalimbali za uchaguzi hazina budi kuwawezesha wasimamizi wa uchaguzi kuendesha chaguzi huru na za haki.

Uzingatiwaji wa viwango vya haki vinavyokubalika ni muhimu sana katika uendeshaji wa uchaguzi katika mfumo wa vyama vingi vya siasa. Waangalizi wa uchaguzi wana maoni ya ujumla kwamba, "umma hupima uhalali wa uchaguzi kutokana na uadilifu halisi wa wale wanaosimamia uchaguzi, pamoja na mwonekano wa uadilifu katika mchakato wote wa uchaguzi" (IDEA,1977: 8). Hivyo, hakuna budi chaguzi zote zinazoendeshwa katika nchi yoyote ile "kuwa siyo tu za kuaminika bali pia kuonekana kuwa hivyo, ili kuongeza imani ya wananchi kwenye matokeo" (Commonwealth, 2000:5). Kinachosisitizwa hapa ni kwamba ni lazima sheria za uchaguzi pamoja na mfumo wote wa usimamiaji wa uchaguzi na taratibu zake ni lazima zionekane kuwa zinaaminika.

Ni jambo linalojadilika, lakini ni wazi pia kwamba bila kuwepo na chaguzi za kitaifa za kuaminika hakuna uwezekano wa kuunda serikali halali ya muungano. Hivyo, uhalali wa serikali ya namna hiyo unategemea uwezo wa chombo kinachosimamia uchaguzi wa kuendesha chaguzi huru na za haki. Chaguzi zinazokubalika pia zinaweza kupatikana endapo tu chombo kinachosimamia uchaguzi kinayo uadilifu wa hali ya juu. Ili jambo hili lidhihirike wazi, chombo cha kusimamia uchaguzi hakina budi kutofungamana na siasa za chama chochote kile cha siasa, yaani, ni lazima kionekane kutokuwa chombo cha kisiasa na kiwe chombo kinachoendesha shughuli zake kwa weledi mkubwa. Zaidi ya hayo, mazingira ya

kisheria nayo pia hayana budi kuhakikisha kuwa taratibu zote za uchaguzi zinazingatia uwazi wa hali ya juu utakaowawezesha wadau wote wa uchaguzi kufuatilia hatua zote muhimu za uchaguzi pasipo kujenga chembe chembe yoyote ile ya mashaka.

Hivyo, mfumo wa sheria unatakiwa kueleza bayana mchakato wote wa uchaguzi ikiwa ni pamoja na kutanabahisha madaraka, mamlaka na wajibu wa vyombo vinavyosimamia uchaguzi. Pia nia lazima mfumo wa sheria uelezee jinsi wadau wote wanavyoweza kushiriki katika mchakato mzima wa uchaguzi, k.v. kuunda majimbo ya uchaguzi na mipaka yake, kuandikisha wapiga kura, uteuzi wa wagombea, kufanya kampeni, kupiga kura na taratibu zote za kuhesabu kura na kutangaza matokeo ya uchaguzi. Mwelekeo wa nchi nyingi hasa zile ambazo ndipo zinaanza kujenga demokrasia, ni "kujenga mfumo madhubuti wa kisheria unaohakikisha uhuru na hadhi ya mchakato mzima wa uchaguzi, kujenga na mfumo usioyumba wa kusimamia uchaguzi kwa haki, na unaoshirikisha wadau wote na kuwapatia taarifa zote za mchakato wa uchaguzi ikiwa ni pamoja na vyama vya siasa, vyama vya kijamii pamoja na wapiga kura" (Wall, 2006:43). Swali muhimu la kujiuliza, ni kuwa, je kiwango gani mfumo wa sheria zinazosimamia chaguzi za muungano (Urais, Wabunge na Madiwani wa Tanzania Bara) unazingatia kanuni hizi za kimataifa?

Uchaguzi Mkuu wa 2010 uliendeshwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura 343, Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Sura 292, Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Na. 6 ya 2010, Sheria ya Vyama vya Siasa Sura 258, Sheria ya Serikali za Mitaa (Halmashauri za Wilaya) Sura 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288. Nyenzo nyingine za Kisheria zilizotumika katika Uchaguzi Mkuu wa 2010 ni pamoja na Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Uchaguzi wa Wabunge,2010 zilizotengenezwa chini ya Kifungu 124 cha Sheria za Taifa za Uchaguzi, Sura 343 na Kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali toleo Na. 279 la 13 Agosti,2010; Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani zilizotengenezwa chini ya Kifungu 125 cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani)Sura 292 kama ilivyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali toleo Na. 280 la 13 Agosti, 2010 na Maadili ya Uchaguzi kwa Ajili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2010 yaliyotiwa saini na vyama vyote vya siasa vilivyokuwa na usajili wa kudumu.

Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya 1985 na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya 1979 zilikuwa mwongozo wa kiutendaji katika jamhuri nzima. Hivyo, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi iliainisha sifa za wagombea pamoja na kubainisha taratibu za kufuata wakati wa uteuzi wa wagombea. Sheria hii pia ilielekeza namna ya kuandikisha wapiga kura, namna ya kufanya kampeni, na kuainisha pia taratibu za kupiga na kuhesabu kura na hata kutangaza matokeo ya uchaguzi. NEC kwa kushirikiana na Vyama vya Siasa pia iliandaa Maadili ya Uchaguzi kwa Ajili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2010. Maadili haya yaliaandaliwa chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985 (Sura ya 343) na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 273/2010. Maadili hayo ya Uchaguzi yalitumika kudhibiti kampeni za uchaguzi. NEC pia iliaandaa Kanuni zilizotumika katika uchaguzi kutoa mwongozo wa kisheria na kiutendaji katika maeneo ambayo Sheria ya Uchaguzi haikuyabainisha vema (Tanganyika Law Society, 2010:12).

Kama sehemu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa 2010, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Tume), ilizifanyia sheria za uchaguzi marekebisho kadhaa ili kuleta ufanisi zaidi katika kusimamia mchakato wa uchaguzi. Marekebisho hayo katika sheria za uchaguzi ni kama ifuatavyo:

i) Kufafanua maana ya Elimu ya Mpiga Kura.
ii) Kuweka bayana muda wa kuboresha DKWK kuwa awamu mbili kati ya uchaguzi mkuu mmoja na mwingine.
iii) Kuipatia Tume mamlaka ya kutangaza tarehe nyingine ya uteuzi wa wagombea endapo Mgombea au Mgombea Mwenza wa Urais atafariki.
iv) Kuandaa Maadili ya Uchaguzi yenye nguvu ya kisheria.
v) Kufuta vifungu vilivyokuwa vinawaruhusu wagombea kuwakirimia wapiga kura kwa kisingizio cha ukarimu wa kimila uliojulikana kama "takrima".
vi) Kufafanua taratibu za kuteua Wabunge Wanawake wa Viti Maalum.
vii) Kutoa fursa kwa vyama vya siasa kuweka mawakala wa vyama kwenye vituo vya kuandikishia wapiga kura wakati wa uandikishaji.
viii) Kuweka ukomo katika muda wa kuweka pingamizi za matokeo ya uchaguzi mahakamani na ukomo katika muda wa kuamua hatma ya pingamizi hizo za matokeo ya uchaguzi kwenye mahakama za kisheria.

Maandalizi ya Maadili ya Uchaguzi yenye nguvu ya kisheria yalihushisha mashauriano kati ya Vyama vya Siasa, Serikali pamoja na NEC. Ilifanyika mikutano mitatu ya mashauriano ya dhati kati ya Vyama vya Siasa, Serikali na Tume kabla ya kukamilisha maadili. Baada ya kukamilika, Maadili hayo ya Uchaguzi yalitiwa saini na vyama vyote vya siasa vilivyokuwa na usajili kamili. Kutokana na Maadili hayo ya Uchaguzi, ziliundwa kamati za mashauriano katika ngazi ya Kata, Jimbo hadi Taifa. Kamati hizo za Maadili ya Uchaguzi zilikuwa chombo muhimu sana cha kutatua migogoro iliyotokana na ukiukwaji wa maadili wakati wa kampeni za uchaguzi.

## 3.0 USIMAMIZI WA CHAGUZI

Uendeshaji wa Uchaguzi Mkuu wa 2010 ulifanyika chini ya usimamizi wa NEC iliyoundwa chini ya Ibara ya 74 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977. NEC inaundwa na wajumbe saba (7) walioteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakati wa Uchaguzi Mkuu wa 2010, NEC ilikuwa na wajumbe watatu (3) ambao ni majaji wastaafu (ikiwa ni pamoja na Mwenyekiti ambaye ni Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani), Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, na Jaji wa Mahakama ya Rufaa ya Afrika Mashariki. Wajumbe wawili (2) waliobakia ni watumishi wa umma.

Kila Mjumbe wa Tume (Kamishna) anateuliwa kwa miaka mitano, ambayo inaweza kuongezwa muda huo ukimalizika. Rais anaweza kumwondoa mjumbe yeyote endapo atashindwa kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria kutokana na kuzorota kwa afya ya mjumbe au kwa kukiuka maadili ya uongozi au kupoteza sifa ya kuwa mjumbe. Tokea kuundwa kwa NEC, hakuna mjumbe aliyewahi kuondolewa na Rais kabla ya kumaliza muda wake wa miaka mitano ya uteuzi.

## 4.0 MAJUKUMU YA NEC

Kwa mujibu wa Katiba, majukumu ya Tume in pamoja na:-

(i) Kusimamia na kuratibu Uandikishaji wa Wapiga Kura na kusimamia uendesheshaji wa Uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kusimamia na kuendesha uchaguzi wa Madiwani wa Tanzania Bara;
(ii) Kuchunguza mipaka na Kuigawa Jamhuri ya Muungano katika maeneo mbalimbali kwa ajii ya Uchaguzi wa Wabunge;
(iii) Kuto Elimu ya Mpiga Kura nchi nzima, Kuratibu na Kusimamia Asasi na Watu wanaotoa elimu hiyo;
(iv) Kuwatangaza Wabunge na Madiwani wa Viti Maalum vya Wanawake;
(v) Kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge.

Ifahamike pia kuwa Tume inatekeleza majukumu hayo ya Kikatiba bila ya kuwepo kwa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliyotungwa na Bunge mahsusi ili kufafanua na kuainisha namna Tume inavyopaswa kutekeleza wajibu wake. Kukosekana kwa sheria hiyo kumekuwa kikwazo kwa Tume kuwa na fursa ya kufungua ofisi kwenye majimbo ya uchaguzi na hili limeipunguzia Tume uwezo wa kusimamia ipasavyo na kwa ufanisi zaidi shughuli za uchaguzi majimboni.

## 5.0 UHURU WA NEC

Uhuru wa NEC unadhihirishwa na Katiba katika Ibara ya 74 (11), inayoipa uwezo wa kufanya maamuzi bila shinikizo kutoka kwa mtu yeyote yule au kutoka Serikalini, au kutoka chama chochote kile cha Siasa. Pia Katiba inawazuia Mawaziri au Naibu Waziri, Wabunge, Madiwani au Viongozi wa Vyama vya Siasa kujiunga na Tume.

Uhuru wa Tume pia unadhihirishwa kwa njia nyingine mbalimbali. Kwa mfano, Tume ndiyo inayopanga kalenda ya uchaguzi kwa kutangaza siku ya uteuzi wa wagombea, inapanga siku za kufanya kampeni na kupanga yenyewe tarehe ya uchaguzi. Ukiacha katika kuamua juu ya idadi ya majimbo ya uchaguzi ambapo Tume inalazimika kushauriana na Rais, katika maamuzi mengine yote Tume hailazimiki kutafuta ushauri kwa yeyote mwingine. Kama Tume isingelikuwa huru isingeliweza kusikiliza rufani dhidi ya uteuzi wa Mawaziri Waandamizi wa Serikali ambao awali walitangazwa kupita bila kupingwa. Lakini kwa kuzingatia sheria kama kigezo cha maamuzi yake, Tume ilipokea rufani kutoka kwa mgombea wa CHADEMA aliyeunguliwa na mgombea wa CCM ambaye alikuwa Waziri. Rufani hiyo ilikubaliwa na hivyo mgombea wa CHADEMA alirudishwa kuwa mgombea wa Jimbo la Nyamagana na hatimaye kushinda uchaguzi na kutangazwa kuwa Mbunge. Pia rufani ya mgombea wa TLP dhidi ya mgombea wa CCM ambaye naye alikuwa Waziri Mwandamizi ilikubaliwa, na hivyo waziri huyo kulazimika kuwa na mpinzani ingawaje mwanzo alionekana kuwa amepita bila kupingwa.

Uamuzi juu ya mipaka ya majimbo ya uchaguzi ni swali nyeti ambalo umakini usipotumika linaweza kuvuruga mchakato wote wa uchaguzi. Mipaka iliyotengenezwa kwa lengo la kupendelea baadhi ya vyama vya siasa na wagombea wake hufanya uchaguzi usiwe wa haki. Vyo vyote vile iwavyo, mipaka inayopendelea baadhi ya vyama vya siasa na kuvikandamiza vyama vingine na wagombea wake huadhiri na kudidimiza dhana nzima ya utawala bora, ambapo uchaguzi unatakiwa kuiboresha. Kwa kuwa ugawaji wa mipaka ya majimbo ya uchaguzi ni zoezi nyeti lenye mikingamo mingi, "baadhi ya wataalamu wamependekeza kwamba ni vema kiundwe chombo mahsusi cha kusimamia zoezi la kugawa majimbo badala ya chombo kinachosimamia uchaguzi, ili kukilinda kisiingizwe kwenye malumbano yanayoweza kuharibu kuaminika kwake" (Wall, 2006:65). Wazo la kuwa na chombo huru cha kugawa majimbo ya uchaguzi linalenga kuondoa taswira ya kuwepo upendeleo wa kisiasa kupitia zoezi la ugawaji wa majimbo ya uchaguzi.

NEC inawajibika kugawa majimbo ya uchaguzi wa Wabunge. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, NEC inatakiwa kuchunguza na kugawa mipaka ya uchaguzi angalau kila baada ya miaka kumi. Mara ya mwisho majimbo yaligawiwa mwaka 1995. Katika Uchaguzi Mkuu wa 2010, Tume ilichunguza mipaka ya majimbo na kuongeza majimbo ya uchaguzi kutoka 232 hadi 239.

Katika zoezi la ugawaji wa majimbo ya uchaguzi Tume inakabiliwa na changamoto kubwa mbili. Mosi, ni ugawaji wa majimbo ya uchaguzi Tanzania Zanzibar unaofanywa na mamlaka nyingine- Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC). Changamoto ya pili ni ugawaji wa mipaka ya Kata kwa ajili ya Uchaguzi wa Madiwani Tanzania Bara, ugawaji ambao unafanywa na mamlaka ya Serikali Kuu.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Halmashauri za Wilaya Na. 7 ya 1982 pamoja na Sheria ya Mamlaka za Halmashauri za Miji Na. 8 ya 1982, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ndiye mwenye dhamana ya kupanga mipaka ya kata. Kulingana na Kifungu cha 8 cha Sheria ya Uchaguzi ya Mamlaka za Halmashauri, (Sura 292), Waziri anapotangaza mipaka ya Kata, mipaka hiyo ndiyo itakayotumika kwa ajili ya uchaguzi katika kata husika. Ikumbukwe kwamba, Kifungu cha 7 cha Sheria hiyo kinaipatia Tume ya Uchaguzi mamlaka ya kusimamia uchaguzi wa madiwani, lakini hakuna kifungu kinachomlazimisha Waziri kutoa mapema taarifa kwa Tume ya Uchaguzi kuhusu mipaka mipya ya kata.

Waziri wa TAMISEMI anaposhindwa kutoa mapem taarifa Tume ya Uchaguzi kuhusu kugawiwa kwa mipaka mipya ya kata, huathiri uwezo wa NEC wa kusimamia uchaguzi kwa weledi na ufanisi. Hii ni kutokana na Tume kushindwa kujua idadi ya kata za uchaguzi na hivyo kushindwa kufanya maandalizi ya kutosha mapema. Mathalani, haiwezekani kabisa kuandaa kwa usahihi bajeti ya uchaguzi bila kujua kila halmashauri itakuwa na kata ngapi. Vyama vya siasa navyo huathirika kwa kuwa havitajua wapi wateue wagombea wao, hivyo zoezi la uteuzi wa wagombea nalo litakuwa na athari hasi. Vilevile, Tume haitajua mapema idadi ya kura za kuchapisha kwa kata husika na hivyo karatasi za kura hazitapatikana katika muda muafaka. Zaidi ya hayo, kwa kuwa Waziri naye ni mwanasiasa anayewajibika kwa

chama kilichompatia kazi, ni rahisi kwa chama chake kufahamu mapema juu ya mipaka na kata mpya zinazotarajiwa kugawiwa, hivyo kukipatia chama chake fursa ya kujiandaa mapema na hivyo kuweka wagombea kwenye kata zote mpya. Wagombea wa namna hiyo wanaweza kukosa ushindani wa kutosha na hivyo kuwanyima wananchi nafasi ya kuchagua viongozi wanaowataka, kwa kuwa mgombea huyo wa chama Tawala amepita bila kupingwa.

Halmashauri yoyote ya Serikali za Mitaa, iwe ni Halmashauri ya Wilaya au ya Mji, kwa kawaida hutangazwa kwamba ni jimbo la uchaguzi kwa ajili ya Uchaguzi wa Wabunge. Utata unaojitokeza ni kwamba ni Waziri wa Tamisemi ndiye mwenye dhamana ya kulitangaza eneo husika kuwa Halmashauri. Kueputa uwezekano wa kuonekana kupendelea, ni vema mipaka ya kisiasa itewekwe ndani ya mipaka ya kiutawala. Waziri anapochelewa kutangaza Halmashauri za Serikali za Mitaa mapema kabla ya Tume ya Taifa kutangaza majimbo ya uchaguzi, atakapotangaza halmashauri mpya husababisha mkanganyiko katika usimamizi wa uchaguzi.

Mikanganyiko ya namna hiyo siyo ya kufikirika tu bali ndiyo uhalisia wa mambo yalivyo. Kwa mfano, kabla ya Uchaguzi wa Halmashauri za Mitaa wa 1994 katika ngazi ya Kata, NEC haikupatiwa mapema majina na Mipaka mipya ya Kata. Majina na idadi ya kata yalipelekwa NEC baada ya mafunzo ya Wasimamizi wa Uchaguzi kufanyika. Jambo hili linamaanisha kwamba Wasimamizi wa Uchaguzi walifunzwa bila hata kuwa na uhakika wa majina na idadi ya Kata walizotakiwa kusimamia. Hivyo kwa upungufu hayo NEC yenyewe haikuwa na uhakika wa gharama halisi za vifaa vya uchaguzi pamoja na idadi kamili ya wasimamizi wasaidizi na wasimamizi wa vituo vya kupigia kura. Matokeo hasi katika usimamizi wa uchaguzi katika mazingira ya namna hiyo hayakwepeki. Ni vema sheria ikafanyiwa marekebisho kumzuia Waziri kufanya mabadiliko ya Mipaka ya Kata karibu na kipindi cha uchaguzi. Endapo itamlazimu Waziri kufanya mabadiliko ya mipaka ya Kata, ni vema sheria imtake Waziri kutoa mapema NEC, taarifa za mabadiliko ya mipaka ya kata na taarifa hizo pia zipelekwe kwa vyama vyote vya siasa pamoja umma kutangaziwa.

Katika uchaguzi mkuu wa 2010, kulikuwa na minon’gono, na baadhi ya magazeti kudai kwamba Waziri alikuwa ameunda Halmashauri mpya na hivyo kuongeza kinyemela idadi ya majimbo ya uchaguzi. Hata hivyo, taarifa hizo hazikuwa na ukweli, kwani awali NEC ilikwishatangaza kuwa katika uchaguzi mkuu wa 2010 majimbo ya uchaguzi yameongezwa kutoka 232 hadi kufikia 239, na hapakuwa na mabadiliko mengine.

Kuondoa mkanganyiko na mashaka ya upendeleo katika ugawaji wa majimbo ya uchaguzi siku zijazo, ni vema Serikali ya Tanzania ikaona umuhimu wa Kuunda Tume ya Kuchunguza Mipaka na Kugawa majimbo ya Uchaguzi. Tume hiyo iwe nje ya usimamizi wa Serikali na pia isisimamiwe na chombo kinachosimamia uchaguzi. Hili si jambo geni, kwani katika baadhi ya nchi zinazofuata tamaduni za Jumuiya ya Madola, ni kawaida kwa sheria za uchaguzi “kuunda chombo huru au tume ya kuchunguza mipaka na kugawa majimbo” (Wall, 2006:65).

Mamlaka hiyo ya kugawa majimbo ni vema isiwe ya kisiasa na pia ni muhimu ihusishe wataalam wenye uzoefu na vyama vya kijamii. Mamlaka ya kugawa majimbo ya uchaguzi pia ipewe uwezo wa kugawa mipaka ya Kiutawala ya Wilaya, Kata na hata kugawa mipaka ya kiutawala ya Vijiji. Hili likifanyika, litaondoa dhana potofu kwa washiriki wote wa uchaguzi wa Wabunge na Madiwani, kwamba ugawaji wa majimbo unakipendelea chama tawala.

## 6.0 FEDHA ZA KUGHARAMIA UCHAGUZI

Serikali ya Tanzania iliipatia Tume kwa wakati fedha zote za kuendeshea Uchaguzi Mkuu wa 2010. Bajeti ya Uchaguzi Mkuu wa 2010 iliyoidhinishwa ilikuwa Tshs. 60.5 bilioni. Tume pia ilipata misaada kutoka UNDP kutoka Mradi wa Uchaguzi (Election Support Programme (ESP). Mradi wa ESP uliiwezesha NEC kuagiza vifaa muhimu kama vile kompyuta pamoja na kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa watumishi wa Tume.

## 7.0 UBORESHAJI WA DKWK

Kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2010 NEC iliboresha DKWK mara mbili, mwaka 2007/2008 na 2009/2010. Baada ya uboreshaji wa mara ya mwisho wapiga kura walioandikishwa kwenye DKWK Tanzania Bara walifikia 19,685, 239. Wapiga Kura Zanzibar, hata wale wenye sifa za kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge wa Muungano, wanaandikishwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC). Katika Uchaguzi Mkuu wa 2010, ZEC iliandikisha wapiga kura 407,658, ambao pia waliwapigia kura viongozi wa Serikali ya Muungano kama ilivyotajwa hapo nyuma. Sheria za Uchaguzi Zanzibar zinaruhusu kuandikishwa wakazi wa Zanzibar ambo wameishi eneo husika kwa miezi isiyopungua thelasini na sita mfululizo, na si vinginevyo.

Hata hivyo, kuna wafanyakazi wa kutoka Tanzania Bara ambao hawana sifa ya ukazi, na hata wakazi wa Zanzibar ambao hawakutimiza sharti la kuishi eneo husika kwa miezi 36 mfululizo na hivyo kukosa sifa ya kuandikishwa na ZEC. NEC imepewa mamlaka ya kisheria ya kuandikisha watu wa namna hiyo. Hivyo, NEC iliandikisha wapiga kura wa Zanzibar 44,406 waliokuwa na sifa ya kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano tu. Hivyo, jumla kuu ya Wapiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifikia watu 20,137,303. DKWK (DKWK) lilichapishwa na kusambazwa kwenye majimbo yote ya Uchaguzi, na pia vyama vyote vilivyoweka wagombea vilipewa nakala ya elektroniki ya DKWK.

NEC ilipata changamoto kadhaa katika uandikishaji wa wapiga kura. Majimbo makubwa na yenye watu wengi yaligawanywa kabla ya uchaguzi kufanyika. Hivyo ulitokea mkanganyiko kwa baadhi ya wakazi ambao kata na majimbo yao yaligawanywa. TEMKO ilibaini katika uangalizi wake huko kwenye Jimbo la Morogoro Kusini kwamba baadhi ya vituo vya kujiandikishia wapiga kura vilifutwa na hivyo kupunguza pia idadi ya vituo vya kupigia kura. Hii ilisababisha "baadhi ya wapiga kura kulazimika kutembea umbali mrefu kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma, jambo ambalo liliwakatisha tamaa baadhi ya watu kushiriki kupiga kura." (TEMCO, 2010:4).

Changamoto nyingine kwa NEC ilikuwa namna ya kufuta kutoka kwenye DKWK wapiga kura waliofariki. Ndugu wengi hawakujitokeza kutoa taarifa za ndugu zao waliofariki. NEC ilijaribu kutumia viongozi wa Serikali za Vijiji lakini haikusaidia sana. Ili kufanikisha vizuri zoezi hili, siku zijazo NEC italazimika kuwa na watendaji wake wa kudumu katika ngazi ya halmashauri ili wasaidie kuboresha daftari mara kwa mara.

Baada ya Daftari la Kudumu kuchapishwa na majina kuwekwa mahali pa wazi, kasoro mbalimbali zilibainika. Baadhi ya majina ya watu waliojiandikisha hayakuonekana kwenye Daftari. Watu wengine waliripoti kasoro za kutofautiana kwa taarifa, mathalani, majina na namba kwenye kitambulisho zilikuwa tofauti na zilizoko kwenye Daftari. Mkanganyiko huu ulisabishwa na uzembe wa makarani waandikishaji. Hata, mpiga kura anayebaini kasoro za namna hiyo siku chache tu kabla ya uchaguzi ni dalili pia kwamba mtu huyu hakwenda kukagua taarifa zake wake Daftari la Awali liliporejeshwa na kukaa siku saba kwenye vituo vya uandikishaji kabla ya kuchapisha Daftari lenyewe.

Mwaka 2005 DKWK lilirejeshwa hadi kwenye ngazi ya Kata, lakini kwenye uchaguzi wa 2010 Daftari lilirejeshwa katika ngazi ya vituo vya uandikishaji (ngazi ya kijiji) ili kuwarahisisishia wapiga kura kukagua taarifa zao.Hata hivyo wapiga kura wengi hawakwenda kukagua taarifa zao, na hivyo makosa ya kukosewa majina au majina kutoonekana kabisa. Upungufu ya namna hiyo yatatoweka ikiwa NEC itakuwa na watendaji wa kudumu katika ngazi ya majimbo na endapo watendaji hao watafanya kazi ya kuboresha daftari kila wakati.

## 8.0 UBORESHAJI WA MIFUMO YA KUSIMAMIA CHAGUZI

Mwaka 2005, NEC iliunganisha Mfumo wa Kusimamia Uchaguzi (Election Management Systems) na Mfumo wa DKWK ili kuleta ufanisi katika uendeshaji wa uchaguzi. Mifumo iliyounganishwa na kuboreshwa ili kuleta ufanisi ni kama ifuatavyo:

### i) Mfumo wa Menejimenti ya Wagombea

Mfumo wa Menejimenti ya Wagombea (Candidate Management System) ulitumika kudaka taarifa za wagombea baada ya uteuzi. Taarifa zilizopatikana zilitumika katika kuaandaa karatasi ya kura za mfano. Baada ya hapo, rasimu ya karatasi za mfano za kura zilitumwa kwa njia ya elektroniki kwenda Kalamazoo Solutions wa Uingereza ambao ndio walishinda tenda ya uchapishaji wa karatasi za kura. Utengenezwaji wa karatasi za mfano wa Kura na NEC ulilenga kupunguza makosa ya kiuchapaji ya majina ya wagombea na majimbo yao ya uchaguzi. Pamoja na hatua zote hizo, bado kasoro ndogo ndogo za mkanganyiko wa majina na majimbo hasa ya kuchanganya nembo za vyama bado yalijitokeza, na hivyo kusababisha kuahirishwa kwa uchaguzi wa baadhi ya Kata na ule wa Wabunge kwenye baadhi ya majimbo ya uchaguzi.

### ii) Mfumo wa Mawasiliano ya Wapiga Kura

Mfumo wa mawasiliano ya Wapiga Kura (Voter Interaction Sytem) ulisaidia wapiga kura kukagua taarifa zao kwenye 'Database' ya NEC kwa kutuma ujumbe mfupi wa simu ya kiganjani (sms). Tume ya Mawasiliano iliipatia NEC namba rahisi ya simu ambayo wapiga kura walitakiwa kutuma ujumbe mfupi wa maandishi ili kujua kituo chao cha kupigia kura.Wapiga Kura walitakiwa kutuma Namba ya Kadi ya Mpiga Kura kwenda nambari 15455.

Kwa bahati mbaya wapiga kura wengi hawakupata fursa ya kuufahamu mfumo huu wa mawasiliano na hivyo haukuweza kuwasaidia watu wengi kwa kuwa NEC yenyewe ilichelewa kupatiwa namba hiyo. Hata hivyo, mashirika mengi ukiacha Zain hawakuwa makini sana katika matumizi ya Mfumo wa Mawasiliano ya Wapiga Kura.

### iii) Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo

Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo nao uliboreshwa ili kurahisisha utumaji wa matokeo ya uchaguzi kutoka majimboni kwenda kwenye ofisi za NEC makao makuu. Mfumo huu pia ulilenga kuongeza ufanisi katika ujumlishaji wa matokeo ya kura kutoka kwenye vituo vya kupigia kura kabla ya kuyatuma NEC. Mafunzo mahsusi yalitolewa kwa makarani wa ujumlishaji wa matokeo ya uchaguzi kutoka majimbo yote ya uchaguzi. Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo ulihusisha yafuatayo:

- Kompyuta 2 ndogo (Laptops)
- Solar Power Kit
- Mobile Internate Modem
- Skanner
- Fax machine
- Bahasha Na. 11 iliyokuwa na fomu ya kujaza matokeo

Kwa Dar es Salaam, pia zilitumika mashine za ZIPZIP ambapo baadhi ya Makarani Waongozaji walizitumia kujua mpiga kura amepangiwa kituo gani cha kupigia kura. Mashine hizo za ZIPZIP zilionyesha kuwa na manufaa jijini Dar es Salaam, hivyo kuonyesha kwamba kuna umuhimu wa kuwa nazo ili kuwasaidia wapiga kura kujua vituo vya kupigia kura hasa kwenye maeneo yenye mlundikano wa vituo vya kupigia kura.

### iv) DKWK na Mfumo wa Menejimenti ya Uchaguzi Iliyounganishwa

Kwa ujumla, mfumo wa menejimenti ya uchaguzi iliyounganishwa na DKWK (PNVR and Integrated Election Management Systems) ulifanya kazi kama ulivyokusudiwa. Hivyo, NEC iliweza kuchapisha majina ya wapiga kura ya kila kituo cha kupigia kura na kuyabandika kwenye vituo hivyo siku nane kabla ya siku ya uchaguzi kama ilivyotakiwa na sheria. Hata,

kwa bahati mbaya baadhi ya wapiga kura hawakuweza kuona majina yao kwenye orodha zilizobandikwa vituoni.

Matumizi ya mfumo huu yalilenga kupunguza uwezekano wa kughushi matokeo ya uchaguzi. Fomu zote halisi za matokeo ya vituo zilitakiwa kusomwa na scanner iliyounganishwa kwenye kompyuta. Mfumo huu haukuruhusu udanganyifu wa matokeo kwa kuwa fomu ikifutwa na kubadili tarakimu za awali, mfumo ulikataa fomu isitumike, na hivyo mfumo kuwa na kasi ndogo ya kuchambua na kujumlisha matokeo ya vituo. Kasi ndogo ilileta mtafaruku katika baadhi ya vituo vya kujumlishia kura, kwa kuwa wagombea na wafuasi wao walikosa uvumilivu wakihofia kura zao kuibiwa. Pale ambapo kulikuwa na uwezekano wa kutokea fujo, baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi walishauriana na mawakala wa vyama ili kutumia njia mbadala ya kujumlisha matokeo ya uchaguzi, kama vile 'excel spread sheet' badala ya mfumo wa menejimenti ya uchaguzi uliokuwa sahihi zaidi, ili kuharakisha matokeo. Njia hii mbadala ililazimu kuskani upya fomu za matokeo kutoka vituoni, hivyo kuzidi kuchelewesha matokeo.

Majimbo yasiyopungua 150 kati ya majimbo yote 239 ya uchaguzi yalitumia kwa ukamilifu Mfumo wa Menejimenti ya Uchaguzi. Kati ya majimbo hayo, majimbo 113 yalituma matokeo NEC moja kwa moja kutoka vituo vya kujumlishia kura. Majimbo 37 yaliyobaki yalilazimika kunakili kwanza matokeo yao kwenye fomu Na.24A kabla ya kuyatuma NEC kwa faksi.

NEC ilifanikiwa kutangaza matokeo ya awali kuhusu wagombea wa urais kama iliyvoyapata kutoka majimboni. Matokeo yalipokelewa makao makuu na kuhakikiwa kabla ya kutangazwa. Uhakiki ulifanyika kwa kulinganisha matokeo yaliyotumwa na yale yaliyokuwa kwenye fomu ya matokeo iliyosainiwa na mawakala wa vyama na msimamizi wa uchaguzi wa jimbo husika. Matokeo yaliyohakikiwa yalitangazwa moja kwa moja kwenye kituo cha kutangazia matokeo. Waandishi wa habari, mawakala wa vyama, pamoja na waangalizi wa kimataifa waliruhusiwa kuingia kwenye kituo cha kutangazia matokeo.

Matumizi ya Mfumo huu wa Menejimenti ya Uchaguzi kwa kiasi kikubwa ulifanikiwa. Ni mfumo unaoongeza uwazi katika uchaguzi kwa kuwa unabakisha kumbu kumbu zinazoweza kuhakikiwa na yeyote mwenye mashaka katika matokeo yaliyotangazwa. Mfumo hauruhusu kuiba kura, kwani hausomi fomu za matokeo zilizochezewa na matokeo yake kubadilishwa. Kasoro yake kubwa ni kasi ndogo ya kujumlisha matokeo. Kasi hii inaweza kuongezwa kwa kuuboresha mfumo wenyewe siku zijazo. Kuna umuhimu wa kutoa mafunzo zaidi yenye kuongeza weledi kwa makarani wa kujumlisha, na kutumia zaidi makarani wenye elimu ya IT.

NEC inao mpango wa kuboresha Mfumo wa Matokeo ya Uchaguzi kwa kutumia fomu maalum za matokeo (bar-coded result forms) pamoja na kutumia teknolojia ya OMR (Optical Mark Recognition), ICR (Inteligent Character Recognition) na OCR (Optica

Character Recognition) ili kuongeza kasi ya kuchambua na kujumlisha matokeo ya uchaguzi. Uboreshaji huo utaongeza kasi ya kutangaza matokeo ya uchaguzi siku zijazo.

### v) Mfumo wa Menejimenti ya Logistiki

Mfumo wa kilojistiki uliotumika mwaka 2005 pia uliboreshwa ili kuwezesha kuwa na uhakiki wa vifaa vya uchaguzi vilivyopelekwa majimboni. Lengo la mfumo huu ni kupunguza hatari za kiutendaji na kuhakisha kuwepo kwa usimamizi wa karibu zaidi wa vifaa vyote vya uchaguzi.

## 9.0 ELIMU YA MPIGA KURA

NEC inayo jukumu la kikatiba la kutoa elimu ya mpiga kura nnchi nzima na kuratibu na kusinmamia asasi na watu wanaotoa elimu ya mpiga kura. Katika uchaguzi mkuu wa 2010 Tume iliandaa Mpango Mkakati wa pamoja n Maelekezo ya namna ya kutoa elimu ya mpiga kura. Mpango Mkakati wa kutoa elimu ya mpiga kura ulitoa mwongozo wa namna ya utoaji wa elimu hiyo nchini kote,

NEC pia iliandaa vipeperushi vyenye ujumbe wa utaratibu wa kupiga kura. Pia NEC iliandaa ujumbe uliosambazwa kupitia TV na Redio za umma na za binafsi. Wasimamizi wa uchaguzi nao walipatiwa fungu la fedha kwa ajili ya kukodisha magari na vipaaza sauti kueneza elimu hiyo. NEC pia ilifuatilia mashirika ya kiraia yaliyopewa fedha na UNDP kwa ajili ya kutoa elimu ya mpiga kura kupitia mpango wa ESP (Election Support Programme).

Tume pia ilifanya kazi kwa karibu na Vyama vya Siasa, Serikali na hata vyombo vya habari katika juhudi za kujenga mahusiano mazuri. NEC ilifanya mikutano kadhaa ya mashauriano na wadau hawa. Mikutano ya mashauriano kati ya NEC na vyama vya siasa ilifanyika kitaifa na hata katika ngazi ya mkoa ikihusisha pia Zanzibar na Pemba. NEC pia ilifanya mikutano na wahariri wa vyombo vya habari pamoja na hata viongozi wa dini kama mkakati wa kutoa elimu ya mpiga kura.

Karibu na wakati wa uchaguzi NEC ilizifufua kamati mbalimbali za uchaguzi. Vyama vya Siasa, vyombo vya habari na hat asasi za kiraia zilishiriki katika mikutano ya kamati hizi. Maadili ya Uchaguzi yaliandaliwa kwa kushirikiana na vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu pamoja na Serikali. Maadili haya yalitiwa saini na Vyama vyote vya siasa, Serikali pamoja na NEC. Kamati za maadili ziliundwa katika ngazi ya Kata, Jimbo na hata Kitaifa ili kusimamia utekelezwaji wa maadili hayo. Vyama vingi vilisimamia vema utekelezaji wa maadili, na migongano ilipojitokeza kamati za maadili zilikutana kutanzua migogoro hiyo. Kwa ujumla, ni malalamiko saba na rufani mbili tu ndivyo vilivyofikishwa kwenye Kamati ya Maadili ngazi ya Taifa. Hivyo migogoro mingi katika utekelezaji wa maadili ilitanzuliwa huko huko majimboni.

## 9.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, NEC iliendesha uchaguzi wa 2010 kwa amani na utulivu. Vifaa vya uchaguzi vilipatikana na kusambazwa kwa wakati. Kasoro ndogondogo hazikukosekana, hasa upungufu wa karatasi za kura uliosababisha uchaguzi wa wabunge kuahirishwa katika majimbo saba ya uchaguzi wa wabunge.

Changamoto kubwa kwa NEC ni jinsi ya kuondoa kasoro zilizojitokeza. Kasoro kubwa ilihusisha DKWK ambapo baadhi ya majina ya wapiga kura hayakuonekana kabisa kwenye daftari la kituo lililochapishwa. Udhaifu huu unaweza kuondolewa ikiwa Tume itakuwa na watendaji wake wa kudumu katika ngazi ya jimbo watakaokuwa na mamlaka ya kuboresha daftari kila wakati.

Kasoro nyingine iliyojitokeza ni katika Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo. Mfumo huu ulikuwa sahihi zaidi kuliko mifumo mingine lakini ulikuwa na kasoro kubwa ya kuwa mpya kwa watumiaji wengi na pia kukosa kasi ya kutoa matokeo. Ipo haja kubwa ya kuongeza ufahamu wa matumizi na kasi ya kujumlisha matokeo ya Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo. NEC inatakiwa kutumia muda wa kutosha kuelimisha wadau wote juu ya usahihi wa mfumo huu wa Menejimenti ya Matokeo. Ni vema hasa vyama vya siasa vikapata elimu ya kutosha kuhusu ubora na umuhimu wa Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo kusudi wauelewe na kuukubali.

# SURA YA TANO

# MWENENDO WA KAMPENI

## 1.0 UTANGULIZI

Sura hii inaongelea kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa Tanzania wa mwaka 2010. Inaelezea na kutathmini mwenendo wa kampeni kwa kuzingatia mabadiliko yanayotokea duniani kuhusiana na mambo ya kisiasa, pamoja na kanuni na maadili yaliyosimamia uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 nchini Tanzania. Sura hii imegawanywa mahsusi katika sehemu kuu kumi. Sehemu ya pili inatoa muktadha wa mjadala kwa kuzingatia mabadiliko yanayotokea mara kwa mara katika miundo ya chaguzi duniani, ikihusisha taswira ya pana ya kidunia na tabia za kampeni za uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2010. Sehemu ya tatu hadi ya sita zinahusu kanuni za uchaguzi na maadili yaliyosimamia kampeni hizo, mitindo na mbinu, masuala na ajenda muhimu zilizozungumziwa kwenye kampeni na usimamiaji ya usalama wakati wa kampeni. Sehemu tatu nyingine zinazofuata zinazungumzia masuala ya gharama za kampeni, faida ambazo serikali iliyoko madarakani ilizipata wakati wa kampeni, na migogoro au matatizo makubwa yaliyojitokeza katika kipindi hiki cha mchakato wa uchaguzi. Sehemu ya mwisho inaongelea tathmini ya jumla kama ilivyotolewa na Mpango wa Usimamizi wa Uchaguzi Tanzania, TEMCO, na inatoa mapendekezo kwa ajili ya siku za usoni.

## 2.0 MUKTADHA NA MAJUMUISHO

Katika lugha ya kawaida, kampeni za uchaguzi ni sehemu tu ya dhana pana ya kampeni za kisiasa. Katika kukubaliana na wachangiaji wengine juu ya dhana hii, mwanazuoni wa Sayansi ya Siasa Richard Nadeau amefafanua kwamba wakati wa kampeni za uchaguzi vyama vya siasa hushindana kuwajulisha wapiga kura kuhusu viongozi wao, masuala muhimu, na misimamo yao kuhusiana na masuala muhimu yaliyopo kwa kipindi husika. Kutokana na vigezo hivyo, mwanazuoni huyo anafafanua kampeni za uchaguzi kuwa ni "aina mahsusi ya kampeni ya taarifa" yenye makusudi ya kuwataarifu wapiga kura husika juu ya masuala muhimu yaliyo mbele yao hasa yale yanayowahusu wale walio kwenye madaraka ya kisiasa (Nadeau na wenzake, 2001:1). Lengo mahsusi la kampeni za uchaguzi huwa ni kuwawezesha wapigakura kufanya maamuzi mazuri wakati wa kupiga kura; maamuzi ambayo msingi wake ni taarifa walizopata kabla na wakati wa kampeni. Hata hivyo watafiti wameonyesha mashaka juu ya mtazamo huu wa kijuujuu. Kwa mfano Zaller (1989) ameonyesha kwamba mbali na kuwezesha utoaji wa taarifa, kampeni za uchaguzi zinasababisha mkabala au ukinzani wa taarifa unaotokana na kampeni za vyama vinavyopingana. Hivyo baadhi ya watu wamekuwa wakijiuliza kama kampeni za uchaguzi zina manufaa yoyote au la. Itoshe tu kusema kwamba hili ni suala pana, na ndiyo maana watafiti bado wanalifanyia uchunguzi.

Sehemu mojawapo ya ugumu uliopo kuhusu manufaa ya kampeni za uchaguzi ni ukweli kwamba mazoea, namna na mbinu zinazotumika katika shughuli hii zimekwa zikibadilika mara kwa mara. Mwanazuoni wa Sayansi ya Siasa Norris (2004:2-3) ameyahusisha mabadiliko haya kwa suala zima la utandawazi, ambalo linajumuisha mabadiliko katika taasisi za kichama, vyombo vya habari na mienendo ya wapiga kura. Akifuatilia mchakato

huu kuanzia mwishoni mwa karne ya 19, na kwa kuzingatia mabadiliko yaliyoletwa na utandawazi, Norris anabainisha awamu tatu za mabadiliko ya kampeni za uchaguzi katika nchi za Magharibi, ambazo ameziita mkabla-usasa (pre-modern), usasa (modern), na mbada-usasa (post-modern).

Akikubaliana na wachangiaji wengine kwenye mjadala huo, Norris (2004:2-5) anazielezea kampeni za kipindi cha mkabla-usasa (karne ya 19 hadi miaka ya 1950) kuwa "zimejengwa juu ya msingi ya mawasiliano baina ya watu" kwa kutumia njia kama mikutano, kutembelea nyumba hadi nyumba na mikutano ya vyama, zikiwa zimepangwa kwenye msingi wa vipindi vifupi vya ushririki wa viongozi wa vyama katika ngazi husika na mazoea ya kutofuata ratiba maalumu. Noris ameonyesha namna ambavyo tabia muhimu za kampeni katika awamu ya usasa (kwa makadirio kipindi cha kuanzia miaka ya 1950 mpaka 1980) zinavyotofautiana kwa kiasi kikubwa na zile za awamu ya mkabla-usasa, akisistiza kwamba kampeni katika kipindi kilichotangulia zilitegemea zaidi  mbinu zilizoandaliwa kutoka ngazi ya kitaifa na kwa kutumia mawasiliano ya kitaalamu na washauri wa matangazo ya kibiashara, tofauti na hali ilivyokuwa katika awamu iliyofuatia, ambapo jukumu kubwa  lilibebwa na maafisa wa vyama wa mahalia husika na wanaojitolea.

Kwa mujibu wa Norris, kuanza kwa awamu ya kampeni za uchaguzi ya mbada-usasa (yaani kuanzia miaka ya 1980 hadi sasa) kwa kiasi fulani kulijidhihirisha katika mabadiliko ya matumizi ya matangazo katoka ngazi ya kitaifa kuelekea kwenye matumizi makubwa zaidi ya "mazingira ya habari ambayo ni mapana zaidi, yaliyogawanyika, na yenye kubadilika haraka mno" (uk. 6) ambayo yanahusisha matumizi ya vituo vya TV vya satelaiti na kebo, mijadala redioni, intaneti na matumizi ya kura za maoni. Mazingira haya mapya ya habari kwa kiasi fulani yalifufua mawasiliano ya karibu baina ya wapiga kura na vyama, na kwa hiyo kwa namna fulani kuashiria 'kurudi kwenye mfumo ya mawasiliano ambao Ulitumika zaidi katika kipindi cha mkabla-usasa' (uk.7). Shanjari na maendeleo haya, kampeni za uchaguzi katika nchi za Magharibi katika siku za karibuni zimeshuhudia kurejea kwa nguvu za kampeni zinazofanywa na vyama katika maeneo mahususi. Hali hii kwa kiasi fulani imedhoofisha umuhimu wa mikakati ya kampeni inayobuniwa na kusimamiwa katika ngazi ya taifa, ambayo huambatana na matumizi ya matangazo ya kulipiwa na ushauri wa masuala ya masoko, mikakati mambo ambayo iliibuka na kupata umaarufu katika miaka ya 1980.

Ingawa mwenendo huu wa mabadiliko ya kihistoria katika mikakati ya kampeni za chaguzi katika nchi za magharibi hauwezi kutumiwa kuelezea mambo yanayojiri katika kampeni kote duniani, bado unaweza kutumika kuelewa baadhi ya mambo yaliyojitokeza katika kampeni za uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2010. Hii ni kutokana na ukweli usiopingika kwamba hata katika mifumo ya mpito kama uliopo Tanzania hivi sasa, nyendo za chaguzi huathiriwa na muktadha mpana zaidi wa kilimwengu, ambao kwa kiasi fulani unadhihirishwa na tabia zilizoelezwa hapo juu. Kwa hiyo haishangazi kwamba, pamoja na vyama shindani vilivyoshiriki katika uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2010 kutofautiana katika mikabala na mbinu zao za kampeni, mingi ya mikakati waliyotumia ilizingatia misingi ya zile awamu tatu za mabadiliko ya kampeni katika nchi za magharibi. Zikiwa zimefanyika katika muongo wa kwanza wa karne ya 21, kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 Tanzania zilionyesha dalili za vyama kutaka kuwafikia wapiga kura kwa kupitia majukwaa ya kitaifa kama vile vituo vya televisheni, redio, magazeti, n,k., zote hizi zikiendana na mwelekeao wa

kampeni za chaguzi wakati wa enzi ya usasa katika nchi za magharibi. Hata hivyo, kampeni za mwaka 2010 zilielemea zaidi kwenye kutumia fursa zinazotokana na matumizi ya teknolojia mpya ya habari na mawasiliano na njia nyingine kwa nia ya kuwezesha mawasiliano ya karibu zaidi kati ya wanasiasa na wapiga kura. Kwa kufanya hivyo, kwa kiasi Fulani kampeni hizi zilishabihiana na nyendo za kampeni za kimagharibi katika kipindi cha mbada-usasa.

Hata hivyo ni lazima tusisitize kwamba vyama shindani katika uchaguzi wa mwaka 2010 nchini Tanzania vilitofautiana kwa kiasi kikubwa katika mitindo na mbinu mbalimbali walizotumia, na kwamba tofauti hizi zilichangiwa, angalau kwa kiasi Fulani, na uwingi wa raslimali ambazo chama husika ilikuwa nazo. Kwa hiyo, vyama vilivyokuwa na rasilmali kidogo vilitegemea moja kwa moja kampeni za mitaani na majumbani. Hizo zilikuwa na gharama nafuu, hasa kwa kuwa zilifanywa zaidi na watu wa kujitolea kwa msingi wa ukereketwa kwa chama husika. Kwa upande mwingine, vyama vyenye uwezo zaidi vilifanikiwa kuchanganya mitindo ya kampeni iliyotumika katika nchi za Magharibi wakati wa enzi za mkabla-usasa na usasa. Sehemu ya 4 ya sura hii inafafanua mitindo hiyo kwa kutumia mifano halisi.

## 3.0 TARATIBU NA MAADILI YA KAMPENI

Kampeni za uchaguzi wa mwaka 2010 wa Tanzania zilifanyika kwa kufuata miongozo ya na Kanuni za Uchaguzi (Chaguzi za Raisi na Wabunge) (2010:18-20), zilizoundwa chini ya Kifungu cha 124 cha Sheria ya Chaguzi za Taifa (1985) Sura ya 343, na Maadili ya Chaguzi za 2010, ambayo yamebainishwa chini ya sheria hiyo hiyo ya Uchaguzi. Miongozo na taratibu hizi zinaelezea mambo yanayokubalika na yasiyokubalika, ambayo viongozi wa vyama, wafuasi na wagombea walitakiwa kuyazingatia ili mwenendo wa kampeni za uchaguzi uwe wa haki na huru. Kwa kuwa orodha ni ndefu na wakati mwingine inajirudia, haitakuwa vizuri kuziorodhesha zote hapa. Badala yake tunajitahidi kuonyesha baadhi ya mambo au kanuni muhimu ambazo zilitumika katika kutunga au kubaini taratibu na maadili haya.

Moja ya mambo yaliyozingatiwa katika kubainisha taratibu husika ni uwekaji wa ratibu za kampeni ili kuepusha migongano na usumbufu kwa wananchi. Katika ratiba hiyo, kampeni rasmi kwa ajili ya nafasi za uraisi na ubunge zilitakiwa zianze mara moja baada ya kuteuliwa kwa wagombea na kusitishwa siku moja kabla ya siku ya inayotangulia siku yenyewe ya uchaguzi; kwamba kampeni ziongozwe na mpango ulioratibiwa na kukubaliwa kwa pamoja baina ya wahusika wote na mamlaka rasmi zinazohusika; na kwamba shughuli za siku kwa siku za kampeni zifanywe ndani ya muda kati ya saa 2 asubuhi na saa 12 jioni.

Jambo jingine muhimu ni kanuni inayohusu uwepo wa amani na utulivu katika kipindi cha kampeni. Kanuni na taratibu zinazolenga suala hili zililenga umuhimu wa kufanya kampeni kwa namna ambayo haitasababisha uvunjifu wa amani na uhasama katika jamii. Pia Taratibu na Maadili ya Kampeni zina vipengele ambavyo vinavitaka vyama, wafuasi na wagombea kutoingilia kwa namna yoyote ile mikutano ya kampeni ya vyama vingine; ukosoaji holela wa vyama vingine au wagombea wake na badala yake ukosoaji huo uishie kwenye masuala

ya kisera tu; kuzingatia taratibu na miongozo yote ya Tume ya Uchaguzi ya Taifa; kutotumia lugha au picha zenye lengo la kukashifu; na kutobeba silaha yoyote wakati wa mikutano ya kampeni.

Kanuni ya tatu ambayo ilitumika kuelezea taratibu na mwenendo inahusiana na maadili ili kuboresha heshima ya uchaguzi na uwajibikaji kwa wananchi. Sanjari na hilo, kauli mahsusi kwenye taratibu na maadili ya uchaguzi zinatoa wajibu mbalimbali kwa vyama vya siasa na wagombea wake. Zinajumuisha, pamoja na mambo mengine, masharti kadhaa yakiwemo wagombea kutopokea au kutotoa zawadi ili kupata kura au kuwashawishi wagombea kujiondoa katika kinyanga'anyiro; kukodi magari au chombo chochote cha usafiri ili kuwapeleka wapiga kura kwenye vituo vya kupigia kura, kubandika matangazo kwenye magari au nyumba binafsi za watu bila ridhaa ya wahusika; na kuchafua jina la mpinzani kwa kutumia vyombo vya habari kwa uonevu. Badala yake vyama na wagombea wanapewa wajibu wa kijamii kuhakikisha kwamba chaguzi zinakuwa huru na za haki, kwa mfano kwa kukemea hadharani vurugu, vitisho, kukataa kila aina ya ubaguzi (wa kijinsia, ukabila, udini na rangi) na kwa kutoa taarifa sahihi kwa umma kuhusu mchakato wa uchaguzi. Ni kwa kiwango gani taratibu na maadili haya yalizingatiwa wakati wa kampeni? Swali hili linajibiwa katika maelezo yafuatayo juu ya matukio makuu na mienendo iliyoshuhudiwa katika Uchaguzi mkuu (wa Muungano) wa mwaka 2010.

# 4.0 MLOLONGO, TARATIBU NA MBINU ZA KAMPENI

## 4.1 Mlolongo

Kampeni za Uchaguzi Mkuu (wa Muungano) wa Tanzania wa mwaka 2010 zilianza rasmi katika wiki ya tatu ya Mwezi Agosti. Katika wiki hiyo na zile zilizofuata baadhi ya vyama shindani, hasa Chama cha Mapinduzi, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Chama cha Wananchi (CUF), vilifanya mikutano ili kuzindua rasmi kampeni zao. CCM ilikuwa ya kwanza kufanya hivyo hapo tarehe 21 Agosti katika viwanja vya Jangwani (Dar es Salaam), kikifuatiwa na CUF Kidongo Chekundu (Dar es Salaam) hapo Agosti 27 na CHADEMA tarehe 28 Agosti, pia Jangwani. Vyama vingine vilizindua kampeni zao baadae kidogo na vingine havikufanya uzinduzi rasmi wa aina hiyo.

Kwa ujumla kampeni za vyama vyote zilianza kwa kasi ndogo katika nchi nzima, lakini vyama vikubwa zaidi, hasa CCM, CHADEMA na CUF na kwa kiasi kidogo NCCR Mageuzi na TLP, viliongeza kasi ya kampeni zao kuanzia wiki ya tatu na kuendelea. Hata hivyo kwa upande wa vyama vingine, uhaba wa fedha ulimaanisha kwamba kampeni ilibidi zitawanywe ili ziweze kufikia mwishoni mwa muda uliotolewa na hivyo kupata manufaa makubwa kwa gharama ndogo. Kampeni zilimalizika tarehe 29 Oktoba, siku moja kabla ya uchaguzi, kama sheria ilivyotamka. Ni vizuri kueleza hapa kwamba sharti la kumaliza kampeni katika siku hiyo iliyoamriwa ilizingatiwa kikmilifu na vyama vyote.

## 4.2 Namna na Mbinu za Kampeni

Awali ya yote, kila chama kilichoshiriki kiliunda timu za kampeni, na hizi pia zilitengeneza namna na mbinu kwa ajili ya kampeni katika ngazi za jimbo na kata. Kwa vyama vikubwa

kama vile CCM, CUF na CHADEMA, timu hizo ziliundwa na wajumbe hadi 16, na pengine zaidi, wakati kwa vyama vidogo wajumbe walikuwa wachache hadi kiasi cha watu watano (Ripoti za Majimbo za TEMCO). Viongozi wakuu wa vyama katika ngazi husika, pamoja na wagombea ubunge na udiwani ndiyo waliokuwa mihimili ya timu hizo. Kampeni kwa ngazi ya kitaifa zilipangwa na kutekelezwa chini ya uongozi wa kitaifa ya vyama husika, na kila chama maarufu kilikuwa na mtu maalum aliyesimamia au aliyengoza kampeni.

Mitindo au namna za ufanyaji kampeni zilitofautiana baina ya chama na chama, na pia zilitegemea uwezo wa kifedha wa chama husika. **Mikutano ya hadhara** ndiyo ulikuwa mtindo uliotumika zaidi katika kampeni. Mtindo huu ulitumiwa zaidi na vyama vikubwa na baadhi ya vidogo, hasa katika kampeni za Urais na Ubunge. Kama ilivyotanabahishwa hapo juu, vingi kati ya vyama vidogo vilitumia mtindo huu kwa kiasi kidogo sana kutokana na gharama kuwa kubwa, na baadhi ya hivyo kama vile DP, APPT, SAU na DEMOKRASIA MAKINI havikulitumia kabisa jukwaa hili.

Mtindo wa pili ulioongoza kwa umaarufu ulikuwa ni ule wa **kupita nyumba hadi nyumba**, ambao ilihusisha makundi ya wafanyakampeni au wajumbe wa timu za kampeni kutembelea nyumba moja moja ili wagombea wao waweze kuungwa mkono. Katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Arusha njia hii ilikuwa maarufu kwa jina la BMW, ikiwa ni ufupisho wa maneno, Boma, Mzee, Watoto. Lengo lilikuwa kukutana na mkuu wa kaya, mkewe au mumewe na wategemezi wake wengine wenye umri wa kutosha kupiga kura. Njia hii ya nyumba-kwa-nyumba ilikuwa na umaarufu mkubwa sana katika baadhi ya maeneo kiasi cha kwamba ilipewa majina ambayo kwa kiasi fulani yalitia chumvi kile kilichokuwa kikitendeka hasa. Katika majimbo ya Moshi mjini na Muheza watu walikuwa wanaiita mbinu ya kampeni ya *mtu kwa mtu, kitanda kwa kitanda* na *shuka kwa shuka,* yote hayo yakiashiria umuhimu wa kutumia mahusiano ya karibu baina ya watu kwa manufaa ya kisiasa. Njia hii ilikuwa na umaarufu sawa kwa sawa kwa vyama vidogo na vikubwa.

Msisitizo wa matumizi ya mawasiliano binafsi baina ya mtu na mtu unafanana na maelezo ya Norris juu ya kampeni za kipindi cha mkabla-usasa katika nhi za Magharibi, ingawaje kulikuwa na utofauti mkubwa wa kimuktadha. Inaoneka vyama viliamua kutumia mbinu hii kunatoka na sababu nyingi. Mojawapo inaweza kuwa ni ile tabia ya baadhi ya watu kutojihusisha na mambo ya kisiasa na hatimaye kutoshiriki kwenye mikutano ya kampeni. Hivyo wapiga kampeni waliamua kuwafuata makwao au katika sehemu zao za kazi. Inaoneka pia kwamba kuwatembelea wapiga kura kwa jinsi hii kulitoa mwanya wa matumizi ya rushwa, na kwamba huenda baadhi ya vyama vilitumia fursa hiyo ili kuwahonga wapiga kura. Vilevile inawezekana wapiga kampeni walitaka kuwafikia watu ambao hushindwa kuhudhria mikutano ya hadhara kutokana na kukwepa gharama za usafiri, chakula na nyinginezo.

Njia nyingine ambayo inafanana na hiyo ya kupita nyumba kwa nyumba au mtu kwa mtu ni ile ambayo waangalizi wameiita **kampeni-tembea** (mobile campaigns). Hizi zilihusisha makundi madogo madogo hasa ya vijana waliotembea sehemu tofauti wakiwa wamebeba alama za vyama vyao (bendera, matangazo, picha za wagombea, .) na kufanya kampeni kwa

jitihada za hali ya juu kwa ajili ya wagombea wao wa Uraisi, Ubunge na Udiwani. Njia hii ilitumika zaidi katika majiji na miji mikubwa, na ilitumiwa zaidi na vyama vya CUF, CHADEMA na CCM.

Pia njia nyingine iliyoenea sana ni matumizi ya **Teknolojia ya Mawasiliano** (TEKNOHAMA), hususani simu za mkononi kwa ajili ya utumaji wa ujumbe mfupi wa maneno ; au pia kwa kuwaita wajengahoja muhimu katika jamii (kama walimu na wafanya biashara) ; matumizi ya mtandao (intaneti) kama hasa nyenzo kama vile vile mabaraza ya majadiliano (kwa mfano Baraza la wana-JAMII), facebook na U-Tube ; TV na vituo vya redio kwa mfano kwa kuendesha mijadala ; na kwa kutumia vyombo vya uchapishaji, vikiwa ni pamoja na magazeti (kama vile Mtanzania, Tanzania Daima, Uhuru na An-Nuur). Ingawaje kwa kiasi Fulani kila chama shindani kilitumia vyombo na njia hizi, vyama vya CHADEMA, CCM na CUF ndivyo vilivyokwa vinara katika matumizi ya njia na teknolojia hizi.

**Mijadala ya wazi** radioni na kwenye luninga ilikuwa pia ni njia muhimu iliyotumika mara kwa mara. Mara nyingi mijadala hii iliandaliwa na mashirika fulani ambayo yako mijini kwa kulipia muda kwenye luninga na Redio na kuwaalika wazungumzaji kutoka vyama kushiriki. Mifano ni mijadala iliyoandaliwa Jijini Mbeya na Mbalizi ilioandaliwa na shirika la *Foundation for Civil Society* kwa ushirikiano na *MBENGONET* hapo mwezi Oktoba 2010. Waongeaji wakuu walikuwa ni wagombea ubunge wa majimbo wakiwakilisha vyama vya CHADEMA, CUF na DP. CCM haikushiriki kufuatia katazo lililotolewa na mamlaka za juu za chama hicho. Mijadala hiyo ilihudhuriwa na washiriki wapatao 400 hadi 500 kutoka katika majimbo hayo mawili, wengi wao wakiwa wanaume. Yalirushwa hewani moja kwa moja na kituo cha redio cha *Highlands FM Radio Generation* (Ripoti ya TEMCO ya Mkoa, Mbeya). Baadhi ya maeneo ambako mabaraza ya aina hiyo pia yaliandaliwa ni Dar es Salaam, Meru, Musoma na Mwanza (Ripoti za TEMCO za Mikoa).

Njia nyingine ambazo pia kwa kiasi fulani zinahusiana na mijadala katika vyombo vya habari ni matangazo kwenye luninga, redio na katika magazeti na machapisho mengine. Tofauti na na mijadala ya wazi, matangazo kwenye vyombo vya habari yaliandaliwa kitaalamu yakiwalenga wapiga kura katika ngazi pana ya kitaifa.

Matumizi haya ya mijadala na matangazo kwa kutumia vyombo vya habari kwa kiasi fulani yana mwelekeo wa aina ya kampeni katika nchi za Magharibi wakati wa enzi ambayo Norris (2004) amekitanabaisha kama kipindi cha 'usasa' (mwishoni mwa miaka ya 1950 hadi ya miaka ya 1980). Hili limedhihirika hasa katika kupunguza msisitizo wa kuwaendea watu mmoja mmoja katika mazingira yao halisia, na badala yake kutumia utaalamu na teknolojia ya mawasiliano. Mwelekeo mwingine ambao unashabihiana sana mtindo wa kampeni katika enzi ya usasa ya karne ya 20 ni mijadala na matangazo kwa kutumia vyombo vya habari ikiratibiwa katika ngazi ya taifa. Njia hizi zilitegemea zaidi luninga kama nyenzo kuu, na zilitumia utaalamu wenye gharama kubwa katika kuandaa matangazo. Mwelekeo huu ulikinzana kabisa na njia zilizotumika katika nchi za Magharibi wakati wa kipindi cha mbada usasa, ambazo zilijikita zaidi kwenye upenzi kwa chama husika na kujitolea katika kuendesha

kampeni. (Norris, 2004: 1-3). Kuchelewa kuanza kwa matumizi ya mtindo wa kampeni zinazotumia teknolojia za kisasa nchini Tanzania hakushangazi kwa sababu mawasiliano ya kielektroniki na taaluma ya matangazo kama njia ya kujinadi ndiyo kwanza yameanza kuchukua nafasi muhimu nchini.

Hakuna utafiti rasmi uliokwishafanywa kubaini njia au mtindo wa kampeni ulio bora zaidi kati hii ilizotajwa. Lakini inaeleweka kwamba kila chama kilichotumia mtindo Fulani kiliona kuwa mtindo huo una tija katika kampeni zake. Hata hivyo inaonekana kwamba wakati vyama vikubwa vilitumia njia mbalimbali kati ya zilizokuwepo, vile vidogo vilitumia njia chache tu ambazo waliziona kuwa na manufaa zaidi kwao, kama vile kutembelea nyumba hadi nyumba. Hii inaashiria kwamba kanuni ya msigni iliyotumiwa na vyama vingi katika kuchagua mitindo ya kukampeni ni ile ya kuhakikisha kwamba tija kubwa inapatikana kutotokana na rasilmali zilizokuwepo.

## 4.3 Mbinu za Kampeni

Vyama vilitumia mbinu na stadi mbalimbali kwa lengo la msingi la kuvutia watu wengi zaidi na kuzipa nguvu kampeni zao. Mbinu moja ambayo ilitumika zaidi ni kubeba watu na kuwapeleka kwenye sehemu za mikutano, kitu ambacho kilifanywa zaidi na CCM ingawaje CUF na vyama vingine viliitumia pia ingawaje kwa kiwango kidogo. CHADEMA hawakutumia mbinu hii, labda kutokana na mafanikio yao katika kushawishi watu kwa namna nyinginezo.

Wagombea uraisi wa CCM na CHADEMA walitumia helikopta hasa kwa lengo la kuwafikia wananchi wengi katika kipindi kifupi, lakini pia vyombo hivyo vyenyewe vilikuwa ni vivutio kwa wapiga kura watarajiwa. Twaweza kusema kwamba tatizo la mbinu hii ni gharama kubwa za kukodi chombo chenyewe, suala ambalo pia linaleta swali kwamba ni kwa namna gani pesa zinazotumika katika katika miradi kama hii zilipatikana katika nchi maskini kama Tanzania, na pia ni jinsi gani gharama hizi zitarudishwa, hasa tukizingatia kwamba pesa hizi yawezekana zilikopwa. Swali jingine ambalo halijapata jibu ni kama gharama zilizotumika katika matumizi ya helikopta zinastahiki ukilinganisha na kinachopatikana kutokana na kampeni au la. Kwa maneno mengine, tunajiuliza kama matokeo ya uchaguzi yangeweza kuwa tofauti sana na yale yaliyopatikana kama pasingekuwepo na matumizi haya ya helikopta. Tatizo linguine lililo dhahiri katika utumiaji wa helikopta ni kutokuwepo kwa fursa kwa wagombea kukutana na watu vijijini na wilayani ambako helokpta hizo zilipita juu kwa juu. Kwa hakika usafiri wa barabara ungeweza kutoa fursa kwa watu kusogea kandokando ya barabara na hivyo kuonana na pengine kuongea kwa kifupi na wagombea husika. Ni wazi kwamba maswali haya yanaweza tu kujibiwa vizuri baada ya kufanynika kwa utafiti wa kutosha. Hata hivyo, mwisho wa yote matokea ya uchaguzi yasingetokana tu na mbinu zilizotumika katika mawasiliano na manufaa yake, bali hasa muktadha mzima wa hali halisi ya kisiasa, kijamii na kiuchumi ambamo uchaguzi ilifanyika.

Mbinu nyingine iliyokuwa maarufu sana ni matumizi ya **sanaa** kama vile michezo ya kuigiza, vichekesho, ushairi na maonyesho ya ngoma. Mameneja wa kampeni walivipa kazi vikundi vya sanaa kufanya maonyesho wakati wa mikutano. Kazi yao muhimu ilikuwa ni

kuita watu na kuwatumbuiza wakati wakisubiri mzungumzaji mkuu wa siku hiyo afike. Mara nyingi vikundi hivyo vilitumiwa kufikisha ujumbe muhimu wa kampeni wa chama husika. Vyama vya CCM, CHADEMA na CUF vilikuwa mstari wa mbele katika kutumia mbinu hii, ingawa vyama vingine navy vilifanya hivyo kwa kiasi fulani. Uwezo wa kifedha ndio sababu kubwa iliyovifanya baadhi ya vyama vitumie vikundi vya wasanii kwa kiasi kikubwa na vingine kufanya hivyo kwa kiasi kidogo. Vyama vyenye uwezo mkubwa kifedha vilikodi vikundi maarufu vya wasanii wakati vyama vyenye uwezo mdogo vilikodi kwa gharama ndogo vikundi visvyo maarufu sana katika medani ya usanii.

Ingawa kampeni chafu zilikiwa zimepigwa marufuku kwa mujibu wa Kanuni za Maadili zinazosimamia shughuli za kampeni, mara kwa mara kampeni za aina hii zilitumika kama mbinu. Wagombea walitoa habari nusu nusu ama za kupotosha kuhusu wasifu wa mtu au vitendo vya wapinzani wao. Pia walitia chumvi au kusema uongo kuhusu hali halisi za kiuchumi na kijami katika kata, jimbo au nchi kwa ujumla hususani kwenye kampeni za kiti cha uraisi. Vyama vyote maarufu, yaani CCM, CUF na CHADEMA vilitumia mbinu hii ingawa kwa viwango tofauti.

Mifano ya kampeni chafu ni pamoja na ujumbe uliotumwa kwenye mtandao wa *Wanajamii* mwezi Oktoba ukionyesha kuwa malori mawili yakiwa yamebeba karatazi za kupigia kura yalikamatwa mjini Tunduma, Mkoani Mbeya. Mwanachama husika wa matandao huo alidai kwamba aliziona karatasi za kupigia kura ambazo tayari zilikuwa zimewekewa alama “V” kwenye nafasi ya mgombea wa kiti cha urais kwa tikiti ya CCM. Lakini madai hayo hayakuthibitishwa na askari wa Jeshi la Polisi wa mjini Tunduma ambao kweli walikama lori lililoshukiwa na kulipekua mbele ya viongozi wa vyama vya upinzani kwa ushahidi (Ripoti ya Tume ya Uangalizi wa Uchaguzi Mkuu Tunduma). Katika tukio linalofanana na hilo, Katibu wa CCM Wilaya ya Moshi Mjini alidai kwamba aliliona bango la CHADEMA likitengenezwa lenye ujumbe usemao kwamba mara tu baada ya kushinda uchaguzi CHADEMA ingewaondoa watu wote ambao siyo Wachaga kutoka Manispaa ya Moshi (Ripoti ya Tume ya Uangalizi wa Uchaguzi Mkuu Moshi Mjini). Lakini bango hilo halikuonekana sehemu yeyote kipindi chote cha kampeni. Inawezekana kwamba kampeni za aina hii ziliwasadia wagombea au vyama husika, lakini zingeweza kuleta madhara makubwa kwa taifa. Kwa mfano, zingeweza kuchochea chuki na kutoaminiana kati ya chama kimoja na kingine au mgombea mmoja na mwingine; zingeweza pia kusababisha kushamiri kwa siasa za uongo zinazokiuka maadili, na pia kuwa njia ya kuwatisha wananchi kwa maslahi binafsi.

Njia nyingine ni ile ya kufanya mikutano ya kampeni wakati mmoja kwenye maeneo yaliyo karibu na sehemu ambayo chama pinzani kilikiuwa kinaendesha mkutano wake wa kampeni. Kampeni za aina hii zilijulikana kwa jina la *operation usafi* na zilifanywa sana na CCM kwa lengo la kufifisha mahudhurio katika mikutano ya vyama pinzani. Ili wasivunje kanuni za kampeni na Kanuni za Maadili waandaaji walihakikisha kwamba kuna umbali wa kutosha kati ya eneo lao la mkutano na lile la wa mkutanao wa chama pinzani. Ni vizuri kufanya utafiti siku za usoni kuona jinsi gani mbinu hii ilifanikiwa.

## 5.0 MASUALA NA AJENDA ZA KAMPENI

Mikutano ya kampeni iliendeshwa zaidi kimazoea. Wagombea walizungumzia mambo waliyoona yanagusa maisha ya wapiga kura. Mambo yaliyozungumzwa sana yalihusu umuhimu wa kuimarisha uchumi wa nchi, masuala ya kijamii na kisiasa na Katiba ya nchi. Kwa sababu zinazofahamika, wagombea uraisi walizungumzia masuala ya kitaifa na kimataifa wakati wagombea ubunge na udiwani wazingumzia mambo yanayohusu maeneo husika. (Ripoti za TEMCO kutoka Majimboni, 2010). Mara nyingi masuala ya kitaifa na kimataifa yaliingiliana, na kwa hiyo wagombea wa kitaifa, hasa wa vyama pinzani, walitumia changamoto zilizopo mahali husika kuelezea matatizo ya kitaifa na umuhimu wa kubadili utawala.

Wakati wa uzinduzi wa kampeni vyama vilianisha mambo ambayo vingeshughulikia kama vingepewa ridhaa ya kuongoza nchi. Hotuba zilizotolewa na wagombea uraisi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na wasemaji wengine zilianisha mambo ambayo wangeyapa kipaumbele na utekelezaji wake endapo wangeshinda uchaguzi. CCM ilihaidi kuendelea kutekeleza sera zake kwa nguvu zaidi, kasi zaidi na ari zaidi ili kuboresha hali ya kisiasa, kijamii na kiuchumi nchini. Iliahaidi kuimarisha uchumi wa nchi kwa kuboresha kilimo na kukifanya cha kisasa, kuboresha na kuongeza miundombinu (barabara, reli, usafiri wa anga na wa maji, .), kuongeza idadi ya shule, huduma za afya, maji na huduma zingine za jamii, kusomesha walimu wengi zaidi, kujenga maabara mashuleni, kuweka vifaa kwenye maabara hizo, kuboresha vituo vya afya na kuzipandisha hadhi baadhi ya hospitali kuwa hospitali za rufaa. Pia, mara kwa mara CCM ilizungumzia nia na uwezekano wake wa kuimarisha amani na utulivu nchini.

Vyama vya upinzani viliahidi kutekeleza sera mbadala kwa kutumia mbinu tofauti. Vyama vya CHADEMA na CUF, kwa mfano, viliahidi kutoa elimu ya msingi na sekondari bure, kutoa huduma ya afya bure kwa wananchi wote, kubadili muundo wa muungano ili kuwa na serikali tatu, yaani serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, serikali ya Zanzibar na serikali ya Tanganyika; na kuimarisha vita dhidi ya rushwa kwenye sekta ya umma nchini. Msisitizo uliwekwa pia kwenye umuhimu wa kuimarisha usimamizi wa uvunaji wa mali asili (CHADEMA, CUF), matumizi mazuri ya fedha za umma ili kumnufaisha mwananchi wa kawaida (CUF, CHADEMA, NCCR-Mageuzi) na kuboresha makazi ya watu kwa kuondoa kodi ya vifaa vya ujenzi kama saruji na bati (CHADEMA). Karibu vyama vyote vilizungumzia kushamiri kwa rushwa nchini na jinsi ya kupamabana na janga hili la kijamii. Ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma CHADEMA na CUF walidhamiria kuunda serikali ndogo ya kitaifa na kusimamia kwa karibu matumizi ya serikali (Ripoti ya Tume ya TEMCO, 2010). Pia, vyama vya CHADEMA, CUF na NCCR-Mageuzi vilisisitiza kwamba kuandika katiba mpya ni moja ya vipaumbele vyao kama wangeshinda uchaguzi. Kwa upande wao, CHADEMA waliahidi kuanza mchakato huo ndani ya siku 100 za mwanzo za utawala wake (Daily News, 30$^{th}$ August, 2010).

Ni muhimu kusisitiza mambo kadhaa yatokanayo na yaliyotajwa hapo juu. Kwanza kabisa, wakati wa kupiga kampeni vyama vilifanya rejea kwenye ilani zao za uchaguzi. Kwa sababu wananchi hawakufahamu yaliyomo kwenye ilani hizo viongozi wa vyama waliona ni vyema kutumia fursa hiyo kufafanua ilani za vayma vyao japo kwa juu juu tu. Lakini inafahamika kwamba vyama pia vilizungumzia mambo ambayo hayakuwepo kwenye ilani zao. Kwa

mfano, walielezea masuala yanayogusa maisha ya watu moja kwa moja na kueleza jinsi watakavyoyashughulikia wakishinda uchaguzi.

Pili, vyama vya upinzani vilikosoa baadhi ya shughuli za kimaendeleo zilizofanywa na serikali iliyokuwa madarakani. Shughuli hizo ni kama ujenzi wa shule za kata. Vyama hivyo vilisema kwamba shule za kata ni miongoni mwa matatizo yanayoikabili sekta ya elimu, wakidai kwamba shule hizo zilikuwa na miundombinu duni na walimu wachache. Vyama vilisisitiza kwamba upanuzi ungefanyika hatua kwa hatua kwa kuzingatia rasilimali zilizopo. Vyama hivyo pia viliikosoa serikali kwa kufanya upanuzi wa huduma zingine za jamii kwa kutumia rasilimali chache, hatua ambayo iliathiri ubora wa huduma hizo.

Tatu, vyombo vya habari vilichambua ajenda za baadhi ya vyama vya siasa kwenye vipindi vyao vilivyohusu uchaguzi. Utafiti uliofanywa na Synovate (Tanzania) kipindi chote cha uchaguzi ulionyesha kwamba mambo matano yaliyozungumzwa sana na vyombo vya habari kipindi cha kampeni za uchaguzi (Ripoti za Synovate Namba 3 na 17, 2010). Masuala ambayo yalizungumzwa kipindi chote cha kampeni ni pamoja na rushwa, elimu, afya, amani na kilimo. Kiwango cha kujitokeza kwa masuala haya katika kampeni kilibadilika kulingana na wakati ingawa yote yalizungumzwa kipindi chote cha kampeni. Kwenye tathmini linganifu iliyofanywa mwishoni mwa mwezi Ogasti, 2010 suala la amani lilitawala vyombo vya habari kwa 28%, rushwa 21%, elemu 12% na afya 6%. Kwenye tathmini nyingine ya mwisho wa mwezi Septemba, 2010 elimu ilipata 21%, afya 19%, amani 18%, kilimo 16% na rushwa 10%. Masuala mengine hayakupewa uzito sana ingawa yalizungumzwa pia.

Viongozi wa dini walizungumzia umuhimu wa kudumisha amani nchini (Maoni ya Mhariri, The Citizen, 23rd August, 2010). Jeshi la Polisi na wananchi pia walizungumzia suala hilo (Maoni ya Mhariri, The Citizen, 18th August, 2010). Vilevile vyama vilivyozungumzia sana rushwa. Vyama vya UDP, CCM, CUF, CHADEMA na NCCR-Mageuzi vilizungumzia rushwa katika muktadha wa ilani zao za uchaguzi, wakitaja hatua ambazo wangezichukua dhidi ya tatizo hili sugu mara tu baada ya kushika dola. CHADEMA iliahidi kuwashughulikia haraka watu wote wanaojihusisha la rushwa kubwa. Lakini CCM iliendelea kusisitiza kwamba rushwa ni tatizo lililoshamiri, na kwamba mkakati uliokuwa ukuchukuliwa na chama hicho wa kulishughulikia tatizo hili kwa taratibu na kutumia vyombo vya sheria ni sahihi. (The Guardian, 24th August; Ripoti ya TEMCO, 2010).

Nne, masuala mengine kama haki na hatma ya makundi maalumu kama walemavu, watoto na akina mama hayakuzungumzwa sana. Utafiti wa Synovate wa mwezi Septemba ulionyesha kwamba vyombo vya habari vilizungumzia masuala kama haya kwa 6% tu. Pia, kampeni hazikuzungumzia sana changamoto kubwa za kitaifa kama kushamiri kwa vitendo vya uhalifu na utendaji mbovu wa sekta za uchumi kama reli, usafiri wa anga na utendaji unaotia maudhi wa bandari ya Dar es Salaam. Lakini cha kusikitisha zaidi ni kitendo cha kutozungumzia kabisa masuala muhimu ya kimataifa kama Umoja wa Afrika Mashariki, utunzaji wa mazingira na nafasi ya Tanzania kwenye mfumo wa uchumi wa kimataifa. Ijapokuwa hakuna utafiti uliofanywa ili kuona ni kwa nini mambo haya hayakuzungumzwa, tunafikiri kwamba wagombea walijikita kwenye matatizo mahususi ambayo Watanzania

wengi wanaendelea kukabiliana nayo moja kwa moja, kama vile umaskini, ukosefu wa ajira, ubovu wa huduma za kijamii na rushwa katika sehemu za huduma muhimu. Kwa hali hiyo, pengine vilisoma alama za nyakati na kugundua kwamba kuzungumzia mambo ambayo yako mbali na wananchi yasingeleta tija katika uchaguzi wa 2010.

Ilielezwa hapo awali kwamba kwa kiasi kikubwa kampeni zilizungumzia sana mambo yaliyohusu maeneo husika badala ya masuala ya kitaifa. Lakini kutokana na uwingi na ukubwa wa mambo hayo, ni vigumu kuanisha muktadha wa kila jambo kwenye ripoti hii. Lakini tunaweza kutoa mifano michache. Jijini Dar es Salaam vyama vya CCM, CHADEMA na NCCR-Mageuzi viliahidi kutatua tatizo la foleni za magari kwa kuboresha barabara zinazounganisha barabara kuu na kujenga barabara za kupishana juu kwa juu (CCM) na kupunguza idadi ya magari yanoyingia katikati ya jiji kwa kuweka magesho nje kidogo ya mji ili kuhidhia magari ya watu waingiao mjini na kuwapa watu hao fursa ya kutumia usafiri wa jumla (publc transport) kwenda na kurudi kutoka mjini (NCCR-Mageuzi). Kwenye Jimbo la Mpanda CHADEMA iliahidi kutatua tatizo la makazi duni kwa kuondoa kodi ya vifaa vya ujenzi ili wananchi wamudu (Ripoti ya TEMCO, Mpanda, 2010). Mkoani Mwanza, mgombea uraisi wa CCM aliahidi kutatua tatizo la Chama Cha Ushirika Cha Nyanza kwa kusaidia kulipa deni lake la shilingi bilioni 5 na kununua meli kubwa ya abiria kwa ajiri ya safari za miji ya Mwanza na Bukoba kupitia Ziwa Viktoria (Taarifa za Magazeti, 2010). Baadhi ya ahadi hizi zilizua malumbano tuliyoyaeleza awali.

Kwenye Jimbo la Unguja Magharibi, wagombea ubunge wa bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walizungumzia mambo kama usafiri duni wa maji, ukosefu wa ajira, ukosefu wa makampuni ya kutoa mikopo na bei ndogo za mazao ya wakulima (Ripoti ya TEMCO, Unguja Magharibi, 2010). Mgombea ubunge wa Jimbo la Ubungo kwa tiketi ya CHADEMA aliyaunganisha masuala yake ya kampeni na kuyapa jina AMUA, yaani AJIRA, MAJI, UWAJIBIKAJI, AFYA (Ripoti ya TEMCO, Ubungo, 2010). Kama ilivyoonyeshwa awali siyo rahisi kuelezea kwa undani kila suala lililojitotokeza wakati wa kampeni hizii.

## 6.0 MASUALA YA KIUSALAMA

Kwa ujumla wananchi wengi waliridhishwa na kazi nzuri iliyofanywa na Jesi la Polisi na vyombo vingine vya usalama. Mara nyingi askari wa Jeshi la Polisi walikuwepo sehemu ambazo walipaswa kuwepo kama kwenye mikutano ya kampeni na waliwasindikiza wagombea waliohitaji kusindikizwa. Wananchi wa Zanzibar, hususani katika Jimbo la Unguja Kusini, waliridhishwa na huduma ya Jeshi la Polisi na kulipongeza waziwazi, hususani kwa kitendo cha kupiga simu kila siku kuulizia mahali na saa ya mkutano wa kampeni, kuulizia kama mkutano utakuwepo na kwa kutoingilia ama kuwatisha wananchi wakati wa kampeni (Ripoti ya TEMCO, Unguja Kusini, 2010).

Lakini kulikuwa na upungufu mengi ya kiuasalama kipindi cha kampeni. Kwenye baadhi ya maeneo wananchi walililaumu Jeshi la Polisi kwa kutuma askari wachache ama kwa kutofika kabisa kwenye mikutano (Ripoti ya Tume ya Uangalizi wa Uchaguzi Mkuu ya Mikoa ya Morogoro na Tabora). Ilifahamika baadaye kuwa Jeshi la Polisi lilituma askari wake eneo fulani kulingana na ufahamu wake kuhusu eneo hilo. Lakini kuwepo kwa askari wachache au

kutokuwepo kabisa kulisababisha kuwepo kwa vurugu kwenye kampeni kama ilivyokwisha elezwa, na kuvifanya vyama vya siasa kuwa na askari wao wenyewe kama “Green Guards” (CCM) na “Read Guards” (CHADEMA) (Ripoti ya Mratibu wa TEMCO, Mkoa wa Morogoro, 2010). Kama ilivyoelezwa awali kwenywe sura hii, matumizi ya askari hawa wa vyama kilikuwa chanzo cha migongano wakati wa kampeni.

Baadhi ya wananchi walililaumu Jeshi la Polisi kwa kukipendelea Chama Cha Mapinduzi katika kushughulikia uvunjaji wa sheria za uchaguzi na Kanuni za Maadili. Mfano mzuri ni kukamatwa kwa mgombea ubunge wa Jimbo la Maswa Magharibi kwa tiketi ya CHADEMA Bw. John Shibuda, ambaye alikamatwa tarehe 21 Oktoba, 2010 kufuatia vurugu zilizotokea karibu na eneo alilokuwa anafanya mkutano siku hiyo (The Citizen, 22nd October, 2010; Ripoti ya TEMCO, Maswa Magharibi). Tukio hili lilisababisha kifo cha mtu mmoja ambaye alitambulika kuwa mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM). Mtuhumiwa Shibuda aliachiwa huru siku chache baadaye kukosekana ushahidi unaonyesha ushiriki wake katika tukio hilo. Jeshi la Polisi lilitoa taarifa tofauti inayohusiana na kampeni hizo hizo katika tukio lingine la kusikitisha. Katika taarifa hiyo ilielezwa kwamba mgombea ubunge wa Jimbo la Maswa Magharibi kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) alimjeruhi OCD wa Wilaya ya Maswa. Lakini mgombea huyo hakukamatwa hadi ilipofika tarehe 24 Oktoba, 2010, baada ya zaidi ya siku mbili kupita tangu tukio litokee (The Citizen, 25th October, 2010; Ripoti ya TEMCO, Maswa Magharibi, 2011). Siku iliyofuata mtuhumiwa aliachiwa huru kwa dhamana, na tangu hapo hakuna taarifa yeyote iliyotolewa. Ripoti ya kama hizi zinazoonyesha udhaifu katika kusimamia usalama na haki wakati wa kampeni pia zimetolewa na Waangalizi wa TEMCO katika maeneo mengine kadhaa.

## 7.0 GHARAMA ZA KAMPENI

Mwanzoni, vyama vya siasa vilipata fedha kutoka serikalini za kugharamia shughuli za uchaguzi kulingana idadi ya wabunge na madiwani iliyokuwa nao. Kwa hiyo, CCM ilipata bilioni 2.3 za kiTanzania, CHADEMA shilingi milioni 750, CUF shilingi milioni 150, NCCR-Mageuzi shilingi milioni 1.2 na APPT-Maendeleo shilingi 100, 000.

Pia, kabla kampeni hazijaanza rasmi, vyama viliendesha shughuli mbalimbali za kuchangisha fedha kwa njia tofauti tofauti, kwa mfano tafrija za uchangishaji fedha na njia ya mtandao au simu. CCM iliandaa chakula cha jioni ili kuchangisha fedha katika mahoteli kadhaa makubwa jijini Dar es Salaam na kwenye Ukumbi wa Mikutano wa ‘Mlimani City’ jiji Dar es Salaam. Kwenye chakula cha jioni ambacho kiliandaliwa New Africa Hotel siku ya tarehe 19 Septemba, 2010, CCM ilipata fedha tasilimu shilingi bilioni 6.5 na ahadi nyingi. Katika hafla zingine mbili chama hicho kilifanikiwa kupata bilioni 7.5 (Uhuru, 21 Septemba, 2010). Awali Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kilianzisha mitandao kadhaa ya kuchangisha fedha. Kwa mfano, kilianzisha mtandao uliojulikana kama Marafiki wa Dkt. Slaa (FOS). Lengo la mtandao huo lilikuwa kuchangisha fedha ili kumwenzesha mgombea uraisi kwa tiketi ya CHADEMA. Chama cha Wananchi (CUF) kilifanya mambo kama hayo hayo, ikiwa ni pamoja na kuanzisha mtandao wa kuchangisha fedha kwa ajili ya shughuli za kampeni. Baadhi ya wagombea ubunge pia walianzisha tovuti zao binafsi ambazo zilitumika kwenye kuchangisha fedha za kampeni (Taarifa za magazeti mbalimbali).

Hapo awali serikali iliweka kiwango cha shilingi bilioni tano kama kiwango cha juu zaidi cha kugharamia kampeni za uchaguzi, lakini baadaye kiasi hicho kiliongezezwa hadi kufikia shilingi bilioni 50. Hatua hiyo lifuatia makubaliano ya Chama Cha Mapinduzi na vyama vingine vya siasa (*The EastAfrican*, 1st November, 2010).

Ingawa ilikuwa dhahiri kuwa kwa kutumia mbinu na njia mbalimbali baadhi ya vyama vilikusanya fedha nyingi, hakuna hata chama kimoja kilichotaja kiasi cha fedha kilichokusanya au kuifahamisha jamii kuhusu vyanzo vyao vya fedha. Kampeni zilipopamba moto, ilidhihirika ni vyama vipi vilikuwa vimekusanya kiasi kikubwa cha fedha na vipi vilikusanya kiasi kidogo. Tofauti hii ilionekana zaidi katika siku za mwisho za kampeni, kipindi ambacho baadhi ya vyama vilisitisha shughuli za kampeni kwa sababu ya bajeti finyu.

Kipindi chote cha kampeni, ilioneka waziwazi kuwa CCM ilikuwa na fedha nyingi za kufanyia kampeni. Kiliweka picha kubwakubwa na nyingi za wagombea nchi nzima, kilikodi helikopta tatu, kilitumia magari mengi ya gharama kubwa kwenye shughuli za kampeni za uraisi, kilisafirisha watu wengi kwenda kwenye maeneo ya mikutano ya wagombea uraisi na ubunge na kugawa nguo za chama zenye picha za wagombea kwa watu wengi Tanzania Bara na Visiwani. CUF na CHADEMA vilichukua nafasi ya pili katika hili, na vilikuwa karibu sawa. CUF ilisambaza fulana, kofia na khanga Tanzania Bara na Visiwani lakini kwa kiwango kidogo ukilinganisha na kile cha CCM. CHADEMA ilikodi helikopta moja tu kwa ajiri ya kampeni za uraisi na magari machache ukilinganisha na yale ya CCM. Pia hakikupeleka watu kwenye mikutano kwa usafiri wake, na hakikugawa nguo kwa wananchi. Kama CCM ilivyofanya, CUF na CHADEMA mara kwa mara vilikodi vikundi vya wasanii kwa ajili ya kuburudisha kwenye kampeni. NCCR-Mageuzi na TLP vilionekana kufanya vizuri kwenye baadhi ya majimbo, ingawa kwa ujumla vilikuwa nyuma ya vyama vikuu tulivyotajwa tayari. Vyama vingine vilikuwa na hali mbaya kifedha, hali ambayo ilijidhihirika pale ambapo vyama hivyo vilishindwa kufanya uzinduzi rasmi wa kampeni zao au pale walipolazimika kufanya mikutano ya hadhaa michache tu, au kutofanya kabisa mikutano hiyo kutokana na kukosa fedha za kugharimia.

## 8.0 FAIDA ZA KUWA MGOMBEA/CHAMA KILICHOPO MADARAKANI

Ijapokuwa inafahamika kuwa ni vigumu kuondoa faida za kuwa mgombea anayetetea kiti chake katika nchi zenye demokrasia ya kutosha, ni wazi kwamba faida hizo zilitumika vibaya katika uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2010 katika ngazi zote. Hii ilidhihirika pale baadhi ya vyombo vya serikali vilipotumiwa na wagombea kwa kiwango kinachozidi kile kinachokubalika kisheria. Kuna ushahidi unaonyesha kuwa baadhi ya wakuu wa wilaya waliwapigia kampeni wagombea wa CCM au walitumia fedha za serikali kugharamia kampeni hizo (Ripoti za TEMCO, Majimbo ya Serengeti, Mbulu, Hanang na Mbinga Mashariki). Mara kwa mara CCM ilitumia rasilimali za kitaifa au za mahali husika, kama vile magari ya Halmashauri za Wilaya kusafirisha watu kuelekea na kutoka maeneo ya kampeni.

Wagombea waliokuwa wanatetea nafasi zao wangeweza kutumia nafasi zao na ushawishi walioujenga walipokuwa madarakani. Ushawishi huo ungeweza kutumika kujenga picha nzuri ya mgombea na kutafuta fedha kwa ajili ya kugharamia kampeni za mgombea husika.

Lakini kwa sehemu kubwa kwenye uchaguzi wa mwaka 2010 ilikuwa vigumu kwa wagombea watetezi wa viti kupata huo unafuu. Hii ilitokana na sababu mbalimbali, ikiwemo rekodi mbaya ya kiutendaji ya mgombea mhusika na sababu zingine zinazoambatana na mazingira mapya ya siasa.

Faida zitokanazo na hali ya kuwa mtetezi wa kiti alichakalia zilimnufaisha zaidi mgombea wa uraisi kwa tiketi ya CCM. Hali hii ilitokana na stahili alizopewa kisheria na rasilimali zilizopo kweye ofisi ya Raisi nchi nzima. Ijapokuwa hatuna data, pesa zilizotumiwa na viongozi wa serikali walioshiriki kwenye kampeni na shughuli zingine zinazohusiana na kampeni ya Rais ni nyingi sana. Cha ziada ni kwamba mengi ya matumizi haya ya fedha hayakuwa na uhalali wa kutosha.

Pia, wagombea wa chama tawala walifaidika kutokana na upendeleo wa kisirisiri au wa wazi waliopewa na viongozi wa serikalii, kwa mfamo katika suala la kufuata kanuni za kampeni. Kuna mifano mingi ambayo inaweza kutolea kuhusiana na suala hili, lakini mfano mzuri ni ule ulioripotiwa kwenye magazeti kuhusiana na maamuzi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Huyo aliongeza muda wa kufanya kampeni hadi kufikia saa moja kamili usiku toka muda uliopangwa awali wa saa kumi na mbili kamili jioni. Msajili alichukuwa hatua hiyo baada ya vyama vya upinzani kulalamika kuwa mara nyingi mgombea uraisi kwa tiketi ya CCM alizidisha muda wa kampeni. Hatua hii iliyochukuliwa na Msajili wa Vyama vya Siasa ilikosolewa hadharani na Mwenyekiti wa NEC, Jaji Mstaafu Lewis Makame, akisema kuwa ni Kamati ya Maadili ya Uchaguzi pekee ndiyo ina mamlaka juu ya masuala ya ratiba za kampeni. Hatimaye Msariji wa Vyama vya Siasa alikiri kuwa alifanya kosa kuongeza muda wa kampeni (The Citizen, 23rd September, 2010).

Faida hizi za kuwa mgombea alioko madarakani zilienda sambamba na adha za kutokuwa mgombea alioko madarakani. Wagombea ambao hawakuwa madarakani walifanya kampeni zao bila kunufaika na faida yeyote iliyoorodheshwa hapo juu. Mara kwa mara walikuwa wahanga wa unyanyasaji wa vyombo vya usalama vya serikali hususani kwenye suala la uvunjaji wa kanuni za uchaguzi, kama machafuko yaliyotokea mwezi Oktoba katika Jimbo la Maswa Magharibi. Iliripotiwa kuwa viongozi wa serikali walivinyima ruhusa vyama vya upinzani kufanya kampeni kwenye maeneo mazuri, kama vile kwenye viwanja vya mpira kwa maelezo kuwa vilikuwa mali ya CCM tangu enzi za mfumo wa chama kimoja (Ripoti ya TEMCO, Iringa Mjini, 2011). Kwenye baadhi ya maeneo nchini CCM na viongozi wa serikali waliwaita wagombea wa vyama vya upinzani wafanya fujo na tishio kwa amani na utulivu wa nchi (Ripoti Mbalimbali za TEMC, Uchaguzi Mkuu 2010).

## 9.0 MATATIZO NA MIGONGANO

### 9.1 Malumbano ya Awali Kati ya Vyama Shindani

Ingawa kwa ujumla mwanzoni shughuli za kampeni ziliendeshwa kwa utulivu na amani, kulikuwa na malumbano kati ya chama kimoja na kingine na malalamiko yalitolewa zaidi na CHADEMA na CCM katika hatua hii. Kwa mfano, TBC1, ambacho kilikuwai chombo cha habari pekee ambacho kilirusha matangazo ya uzinduzi wa kampeni uliofanywa na

CHADEMA kwenye viwanya vya Jangwani tarehe 28 Ogasti, 2010, ghafla TBC1 ilisitisha kutangaza tukio hilo. TBC1 ilitoa tamko kuwa ilisitisha matangazo hayo kwa kile ilichokiita matumizi ya lugha ya chuki na matusi yaliyofanywa na viongozi wa CHADEMA katika mkutano huo, ambayo ni kinyume na Kanuni ya Maadili iliyokubaliwa na kusainiwa na vyama vyote vilivyoshiriki kwenye kinyang'anyiro hicho. Viongozi wa CHADEMA waliijibu kauli hiyo wakisema kuwa hatua hiyo ilikuwa na nia ya kukitenga chama chao na kukipendelea chama tawala, yaani CCM. Baada ya majibizano ya muda fulani, vyama vyote viwili viliacha kulizungumzia suala hilo.

Viongozi wa CHADEMA pia walitoa malalamiko mwanzoni mwa shughuli za kampeni dhidi ya kauli za mgombea uraisi kwa tiketi ya CCM. Kwa mfano, Katibu Mkuu wa Muda wa CHADEMA, Ndg. John Mnyika, alipeleka lalamiko la kimaandishi kwa Msajiri wa Vyama vya Siasa nchini akidai kuwa ahadi za Ndg. Kikwete kupandisha mishahara, serikali kuchukua deni la Chama cha Ushirika Nyanza na ahadi ya kununua meli kubwa ya kusafirisha abiria kati ya Miji ya Mwanza na Bukoba kupitia Ziwa Viktoria ni kitendo cha kutafuta kuungwa mkono na wapiga kura kwa kutumia fedha za serikali. Aliomba mgombea huyo wa CCM aondolewe kwenye kinyang'anyiro hicho. Lakini Meneja wa Kampeni wa CCM, Ndg. Abdurahaman Kinana, alisitiza kuwa mgombea wao alikuwa anafafanua ilani ya uchaguzi ya CCM na hakuna kanuni yeyote iliyovunjwa kwa sababu ahadi hizo zisingetekelezwa kabla ya kipindi cha uchaguzi kuisha. Uamuzi uliotolewa na Msajiri wa Vyama vya Siasa nchini siku chache baadaye ulitupilia mbali madai ya CHADEMA, ukisema kuwa maelezo yaliyotolewa na mgombea uraisi wa CCM hayakuvunja kanuni yeyote ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Suala hili lilitokomea bila kujitokeza tena kipindi chote cha kampeni.

Katika kipindi hicho CHADEMA pia ilimtuhumu mke wa Mgombea Kikwete wa CCM kuwa alikuwa anakifanyia CCM kampeni kwa kutumia fedha za walipa kodi. Kwa mara ya kwanza tuhuma hizi zilitolewa na Mkurugenzi wa Kampeni wa CHADEMA, Bi. Suzan Kiwanga, na baadaye kurudiwa na viongozi wa juu wa chama, wakitaja gharama za usafiri za mke wa Mgombea Kikwete na gharama zingine zifananazo na hizo. Kwa mara nyingine tena, Meneja wa Kampeni wa CCM alisema kuwa walitumia fedha za CCM kugharamia kampeni alizofanya mke wa Rais Kikwete, ikiwa ni pamoja na kumkodia helikopta. Hata hivyo, CHADEMA ilisisitiza kuwa ingelipeleka suala hilo mahakamani, ingawa haikufanya hivyo.

Malalamiko mengine, ambayo pia yalitolewa na CHADEMA yalihusu CCM kutumia mabango ambayo yalionyesha shughuli ambazo mgombea wake alizifanya akiwa mkuu wa nchi. Ilidaiwa kuwa mabango hayo ni mali ya serikali na vyama vingine visingeweza kuitumia, na kwa hiyo CCM iache kutumia mabango hayo kwenye kampeni zake. CCM ilisema kwamba mabango hayo yalikuwa yameidhinishwa na NEC (NEC). Lakini, siku chache baadaye CCM iliyaondoa badhi ya mabango hayo.

Wakati malumbano kuhusu mabango yakiendelea, Meneja wa Kampeni wa CCM alisema kwamba moja ya mabango ya CHADEMA lilimwonyesha mgombea wake wa uraisi kuwa tayari ni wakati yeye alikuwa mgombea tu. Alisema kuwa bango hilo lilivunja sheria na

kuishawishi NEC kuchukua hatua kali dhidi ya matumizi ya mabango ya aina hiyo. Mwanasheria wa CHADEMA, Ndg. Tundu Lissu, alisema hakuna sheria inayopinga mgombea uraisi kujitambulisha kama raisi. Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Jaji Mstaafu Lewis Makame, alisema kwamba Tume yake haikuliona bango lolote lililomwonyesha mgombea uraisi kama raisi. Baada ya muda suala hilo nalo lilififia na kutokomea.

### 9.2 Upungufu na Changamoto

Japokuwa tangu mwanzo hadi mwisho kampeni ziliendeshwa kwa utulivu na msisimko mkubwa, upungufu na changamoto nyingi ziliripotiwa na Waangalizi wa TEMCO na magazeti mbalimbali. Upungufu ya aina hii yalijitokeza pia katika chaguzi zilizopita kama ilivyoelezwa awali. Baadhi ya upungufu hayo yanafafanuliwa hapa chini.

### a) Kushamiri kwa Vurugu

Waangalizi wote wa Muda Mrefu wa TEMCO wamesisitiza kuwa kwa ujumla kampeni ziliendeshwa kwa amani na utulivu. Lakini pia wameonyesha matukio mengi ya vurugu zilizojitokeza kipindi cha kampeni mijini na vijijini. Matukio hayo ni kama mapambano ya moja kwa moja kati ya wafuasi wa vyama vya upinzani, na wakati mwingine vurugu hizo kusababisha matatizo makubwa kwa wananchi. Matukio ya aina hii yalitokea sehemu kadhaa za nchi, zikiwemo Maswa Magharibi (Shinyanga), Mpanda, (Rukwa), Musoma, Arusha, Morogoro, Dar es Salaam na Dodoma. Hii ni mifano michache tu.

Kwenye baadhi ya maeneo, matukio ya aina hii yalitokea kwenye mikutano ya kampeni. Kwa mfano, wafuasi wawili wa CCM wakiwa wamevaa nguo za chama chao walivamiwa Mpanda Mjini na wafuasi wa CHADEMA baada ya kupita au kujichanganya sehemu ambayo CHADEMA walikuwa wanafanya kampeni. Mmoja wa wahanga hao alilazwa hospitalini. Suala hapa ni uchokozi wa wafuasi wa CCM na kukosa uvumilivu kwa wafuasi wa CHADEMA. Tukio la kikatili zaidi lilitokea katika Jimbo la Maswa Magharibi, tarehe 21 Oktoba, 2010, baada ya wafuasi wa CCM na CHADEMA kupambana kwenye eneo ambalo CHADEMA walikuwa wanafanya mkutano. Katika tukio hilo mtu mmoja aliuwawa na wengine wengi kujeruhiwa vibaya (The Guardian, 23$^{rd}$ October, 2010). Tukio linguine lililotokea Arusha mjini, ambapo kulitokea mapambano tarehe 7 Oktoba, 2010, kati ya wafuasi wa CHADEMA na wa CCM kwenye eneo la soko. Iliripotiwa kwamba mapambano hayo yalianza baada ya CHADEMA kujaribu kupandisha bendera yao na kufungua ofisi karibu na ngome ya CCM. Baadaye, Jeshi la Polisi liliwatia nguvuni watu sita, mmoja wao akiwa mgombea udiwani wa Kata ya Kaloleni kupitia CHADEMA.

Vivyo hivyo, ripoti kutoka Musoma zilionyesha mlolongo wa vurugu. Moja ya matukio hayo lilitokea tarehe 11 Oktoba, 2010, na lilihusisha matumizi ya panga na kujeruhi vibaya watu watatu ambao walilazwa hospitalini. Inadaiwa kwamba tukio hilo lilitokea tarehe 12 Oktoba, 2010, na lilifanywa na wafuasi wa CCM. Vilevile Jeshi la Polisi liliwakamata wafuasi sita wa CHADEMA Arusha mjini ambao walisemekana kujihusisha na vurugu zilizotokea eneo la Kaloleni na kujeruhi wafuasi sita wa CCM. Iliripotiwa kwamba mapambano hayo yalianza

baada ya wafuasi hao kukutana njiani wakielekea nyumbani kwao baada ya kuhudhuria kampeni za vyama vyao.

Ingawa ripoti nyingi zinaonyesha misuguano kati ya CCM na CHADEMA, vurugu zingine zilihusisha wafuasi wa CUF na vyama vingine vya upinzani. Tukio moja lilitokea Igagula (Mkoani Tabora) kati ya wafuasi wa CUF na CCM tarehe 10 Oktoba, 2010. Inadaiwa kuwa vurugu hizo zilisababishwa na uvamizi wa mkutano wa kampeni wa CCM uliofanywa na kundi la wafuasi wa CUF. Jijini Dar es Salaam, tarehe 9 Oktoba, 2010, mgombea ubunge wa Jimbo la Kawe kwa tiketi ya NCCR-Mageuzi, Ndg. James Mbatia, alilamika kuwa mara kwa mara alishambuliwa kwa mawe na watu wasiojulikana, matukio ambayo yalisabisha kujeruhiwa kwa kwa baadhi ya watu kwenye msafara wake. Matukio mengine yaliyohusisha vyama vingine yalitokea kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Mifano hii yote inaonyesha matukio ambayo yalihatarisha uwezekano wa kampeni hizo kumalizika kwa amani. Msimamo wa wananchi kuhusu suala la amani ulielezwa kwenye taarifa mbalimbali za Synovate zilizotajwa hapo awali. Magazeti na vyombo vingine vya habari viliweka msistizo juu ya umuhimu wa kudumisha amani nchini. Kwa upande moja twaweza kusema kwmba vyombo vya habari viliona kuwa amani ni jambo muhimu na la kimsingi. Pia inawezekana kwamba hali hii iliashiria hofu na wasiwasi waliokuwa nao wananchi wenye ufahamu mkubwa kuhusu umuhimu wa amani katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu.

### b) Kampeni Chafu

Pia ripoti za TEMCO na taarifa za magazeti zilionyesha kuwepo kwa kampeni chafu amabazo zilifanywa katika ngazi zote, yaani katika ngazi ya udiwani, ubunge na uraisi. Kama ilivyoonyeshwa awali, kampeni chafu zilikuwa moja ya upungufu ya kampeni za uchaguzi wa mwaka 2010. Zilichukua sura mbalimbali na zilifanywa kwa njia mabalimbali. Kwa mafano, katika mwezi Septemba 2010 wagombea wa CCM wakifanya kampeni maeneo mbalimbali walizungumzia masuala binafsi na ya kifamilia ya mgombea uraisi kwa tiketi ya CHADEMA, vikitaja kutengana kwake na mke wake wa zamani na kesi yake kuhusu uhusiano wake wa kimapenzi na mwanamke aliyedaiwa ni mke wa mtu. Pia ujumbe wa simu ya mkononi ulisambazwa na mtu asiyefahamika kuhusu kesi hii ili kuchafua jina la mgombea huyo.

Pia, mgombea ubunge kupitia CHADEMA wa Jimbo la Morogoro Kusini alisema kuwa mgombea ubunge kwa tiketi ya CCM ni mla rusha, mtu asiye na maadili na aliyekuwa na virusi vya Ukimwi. Wakati huohuo, katika Majimbo ya Ulanga na Mvemoro (Mkoani Morogoro) wanakampeni wa CHADEMA walibeba mabango ambayo yaliituhumu serikali ya CCM kuwa ilifuja kila kitu, pamoja na *uji wa wagonjwa*. Hali kadhalika kampeni za CCM zilizofanyika Jimbo la Morogoro Kusini zilimwelezea mgombea ubunge kwa tiketi ya CHADEMA kama mtu mkorofi na mlevi. Pia mgombea ubunge wa Jimbo la Igalula Mkoani Tabora kwa tiketi ya CCM aliripotiwa kuwaambia wananchi kuwa kama wakichagua chama cha upinzani wataiingiza nchi kwenye vita kama ile ya Idd Amin ya miaka ya sabini. Nako Mkoani Mtwara mgombea ubunge kupitia CUF alimwita mpinzani wake wa CCM kuwa ni mtu asiye raia kamili wa Tanzania, mtu anayetoka kwenye familia Kihindi - watu wabinafsi, wezi na wasio waaminifu. Wakati mwingine kampeni chafu zilifanywa kupitia magazeti. Humo baadhi ya vyama viliandika au kuchapisha zenye jumbe za kukashifu vyama pinzani, au walitumia katuni za kiuchochezi.

Kampeni chafu zina matatizo ya aina mbili. Kwa upande mmoja zinawanyima wananchi fursa ya kutumia muda wa kampeni kujadili au kusikiliza mambo ya msingi yanayohusu njia na jinsi ya kuboresha maisha yao. Kwa upande mwingine zilileta mgawanyiko miongoni mwa wananchi na vyama vinavyoshindana, hali ambayo inaweza kujenga utamaduni wa chuki na malumbano baina ya watu na vyama.

**c) Vitendo vya Rushwa**

Ingawa Sheria ya Gharama za Uchaguzi Namba 6 ya mwaka 2010 ilianzishwa, na ingawa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilisambaza makachero wake nchi nzima kuzuia rushwa kipindi cha kampeni, waangalizi wengi wa TEMCO wameeleza kuwa kulikuwa na kashfa nying kuhusu vitendo vya rushwa katika kipindi hicho. Baadhi ya kasha zilihusu ununuaji wa kadi za wapiga kura, kuwapa fedha wapiga kura, au kuwapa fedha wagombea wa vyama pinzani ili wajiondoe kwenye kinyanganyiro, . Kashfa zingini zilihusu dalili za rushwa iliyojificha katika vitendo vya takhrima. Kwa mfano, katika tukio fulani chakula kiliuzwa kwa bei ya chini kwenye eneo la kampeni. Tuhuma hizi za rushwa ziliwahusisha zaidi viongozi wa CCM na wagombea wake.

Viongozi wa upinzani walilalamika wakati fulani kuwa Jeshi la Polisi na TAKUKURU walishughulikia tuhuma za rushwa kwa kusita, kwa taratibu mno na kwa upendeleo. Mfano mzuri ni tukio lilojir Arusha mjini tarehe 4 Oktoba, 2010, ambapo wagombea ubunge na udiwani kwa tiketi ya CHADEMA walifanya maandamano kuelekea ofisi ya TAKUKURU ya Manispaa. Waandamanaji hao waliituhumu TAKUKURU kwa kutochukua hatua dhidi ya wanachama wa CCM ambao ilisemekana walifanya vitendo vya rushwa ambavyo wao CHADEMA walisema walivishuhudia na kuviripoti (Mwananchi, 4 Oktoba, 2010). Lakini pia iliripotiwa kwenye magazeti kuwa Jeshi la Polisi liliwatia nguvuni watu wengi na kesi nyingi za rushwa zilikuwa zinaendelea mahakani. Vitendo vya rushwa vinaelezwa kwa kina kwenye moja ya sura za ripoti hii.

**d) Changamoto Zingine za Msingi**

Matukio mengine ya uvunjani taratibu yaliyojitokeza kipindi cha kampeni ni haya yafuatayo:

i) Kutoheshimu ratiba za kampeni kulikofanywa na baadhi ya vyama vya siasa na wagombea wake: Baadhi ya wagombea walichelewa kufika kwenye maeneo ya kampeni au wengine hawakutokea kabisa. Kwa upande mmoja hali hii ilisababishwa na ukosefu wa fedha, au ilikuwa mbinu ya vyama husika. Kuchelewa au kutofika kwa wagombea kulileta adha kwa wananchi ambao mara nyingi walisubiri juani kwa muda mrefu sana.

ii) Kukosekana kwa askari wa Jeshi la Polisi waliovaa sare katika maeneo ya kampeni, hali ambayo inadaiwa kuchangia ongezeko la vitendo vya vurugu, lilikuwa tatizo pia. Kukosekana huko kwa askari wa Jeshi la Polisi kulivifanya vyama kutumia askari wao wenyewe kulinda usalama kwenye mikutano. CCM ndio chama ambacho kilikuwa na idadi kubwa ya askari wa aina hii, na kupelekea vyama vya upinzani kueleza wasiwasi wao juu ya kitendo cha CCM kuendelea kuandaa askari wake waliojulikana kwa jina la 'Green Gurds', wakihofu kuwa askari hao wangeweza kuwa chanzo cha vurugu.

iii) Uwakilishi mdogo wa wanawake ulionekana katika maeneo mengi ikiwa ni pamoja na Dar es Salaam. Lakini iliripotiwa kwamba mara kwa mara kwenye vikao vya CCM idadi ya wanawake ilikuwa karibu sawa na ile ya wanaume, na katika baadhi ya

maeneo wanawake walikuwa wengi zaidi ya wanaume. Ingekuwa vizuri kufahamu kama hali hii ilijitokeza nchi nzima na kama kulikuwa na tofauti kubwa kati ya CCM na vyama vya upinzani katika hilo.

iv) Pia imeripotiwa kuwa wagombea walitumia lugha zao za asili hususani maeneo ya vijijini, hasa kwenye mikoa ya Mara, Kagera, Shinyanga, Mwanza, Manyara, Mtwara, Tabora na Morogoro. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa ingawa kufanya hivi ni kwenda kinyume na kanuni za uchaguzi, yaelekea kwamba hakuna mtu aliyetumia lugha hizo kwa nia mbaya. Ilionekana kuwa katika maeneo yote wazungumzaji walitumia lugha zao za asili ili kuboresha tu mawasiliano na wapiga kura.

v) Ilidaiwa kuwa baadhi ya wagombea walitumia majukwaa ya Mwenge wa Uhuru, ambao ulikimbizwa kipindi hicho hicho cha kampeni za uchaguzi, kufanyia kampeni zao. Mara kadhaa vyama vya upinzani vilitoa malalamiko yao dhidi ya matumizi mabaya ya majukwaa hayo.

vi) Baadhi ya vyama vilifanya kampeni hafifu au havikujitokeza ipasavyo katika kipindi cha kampeni. Jambo hili limelalamikiwa na baadhi ya watu, wakiwemo waandishi wa habari. Katika kuonyesha kutoridhika huko gazeti moja (The Citizen, 30th August, 2010) lilichapisha makala ndefu kuhusu hali hii. Kitu cha msingi kilichoelezwa kwenye makala hiyo ni haki ya vyama hivyo kupewa fedha na serikali kwa ajili ya shughuli za uchaguzi na halafu visionekane hadharani.

## 10.0 TATHMINI YA JUMLA

### 10.1 Tathmini

Wiki moja kabla ya kuhitimisha kipindi cha kampeni TEMCO iliwapatia Waangalizi wake wa muda mrefu dodoso ili kutafiti uendeshaji wa uchaguzi katika maeneo yao, wakifuatia mchakato mzima kuanzia kwenye uteuzi wa wagombea, kampeni, upigaji na uhesabuji kura na utangazaji wa matokeo. Waangalizi hao walipaswa kutoa alama kwa hatua zote tatu za uchaguzi kulingana na hali ilivyokuwa kwa kipindi chote walipokuwa kwenye maeneo yao. Mwongozo wa utoaji alama ulikuwa hivi:

(a) Asilimia sifuri (0%) au alama **F** ilimaanisha uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) ambayo haikufanya vizuri kabisa katika kipengele cha usimamizi, uvunjaji wa sheria ya uchaguzi au maadili na usawa; na kwa hiyo kusababisha uchaguzi kumalizika katika hali isiyo ya kawaida.

(b) Asilimia 1-39 au alama **E** ilimaanisha uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) yenye matatizo mengi sana ya kiutawala na mikanganyiko kiasi kwamba wadau wakuu (wapigakura, wagombea, vyama) wanakataa au wanaweza kukataa matokeo.

(c) Asilimia 40-49 au alama **D** ikimaanisha kwamba mchakato wa uchaguzi umekuwa na vitendo vya vurugu, vitisho, upendeleo, rushwa .

(d) Asilimia 50 – 59 au alama **C** - ikimaanisha kwamba uchaguzi umeruhusu ushiriki wa wazi wa wadau (wapiga kura, wagombea, vyama, .), lakini kumekuwa na matukio mengi ya vyama vikubwa (au hasa chama tawala) kukiuka taratibu bila hofu ya kuadhibiwa. Hii ina maana kwamba uchaguzi umekuwa wa haki lakini si huru.

(e) Asilimia 60 – 79 au alama B – ikimaanisha uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) kwa ujumla umekuwa ni huru na wa haki, lakini bado umekuwa na upungufu ambayo yanawanyima fursa baadhi ya wadau (wapiga kura, wagombea, vyama, .).

(f) Asilimia 80 au alama A – ikimaanisha uchaguzi umekuwa na upungufu machache sana na ambayo hayaathiri matokeo ya jumla. Uchaguzi wa namna hii unachukuliwa kuwa uchaguzi safi ulio huru na wa haki.

Wasimamizi wa majimbo walijaza na kurudisha dodoso hizi kwenye makao makuu ya TEMCO hapo tarehe 25 Oktoba, ambapo wataalamu wa takwimu walikusanya na kuchambua matokeo ya majimbo 167 kati ya 173 waliyosimamia. Kuhusiana na KAMPENI kama hatua ya uchaguzi, uchambuzi unaonyesha kwamba:

(a) Jimbo moja (0.6%) lilipata alama **E**, ikimaanisha kwamba kulikuwa na matatizo mengi ya kiutawala na mikanganyiko wakati wa kampeni kiasi kwamba wadau wakuu (wapigakura, wagombea, vyama) wangeweza kuyakataa matokeo.

(b) Jimbo moja (0.6%) lilipata alama **D** ikiwa na maana kwamba kampeni zilijaa vurugu, vitisho, upendeleo, rushwa n.k.

(c) Majimbo ishirini na mbili (22) (sawa na 13.2%) yalipata alama **C**, ikiwa na maana kwamba kampeni ziliruhusu ushiriki huru wa wadau (wapigakura, wagombea, vyama, n.k.) lakini kulikuwa na matukio mengi ya vyama vikubwa (au chama tawala) kukiuka taratibu bila kuwa na hofu ya kuadhibiwa. Hii ni sawa na kusema kampeni zilikuwa huru lakini si za haki.

(d) Majimbo mia moja na sita (106) (sawa na asilimia 63.5) yalipata alama **B**, ikiwa na maana kwamba kampeni zilikuwa huru na za haki, lakini hata hivyo zilikuwa na upungufu ambayo yaliwanyima fursa baadhi ya wadau (wapiga kura, wagombea, vyama n.k.) kwahiyo 'zilifaulu' kuwa kampeni huru na za haki lakini zenye upungufu.

(e) Majimbo thelathini na saba (37) (sawa na asilimia 22.2) yalipata alama A, ikiwa na maana kwamba kampeni zilikuwa na upungufu machache tu ambayo hayakuathiri matokeo ya jumla. Kwahiyo ulikuwa ni uchaguzi safi ulio huru na wa haki.

## 11. HITIMISHO

Ukichukulia kampeni zote kwa kipindi chote cha kampeni, tathmini hii ya waangalizi wa TEMCO inakubaliana kwa karibu sana na mtazamo wa haraka na taarifa za vyomo vya magazeti. Ingawaje kulikuwa na upungufu makubwa na changamoto katika majimbo na maeneo mengi, picha ya jumla ni kuwepo kwa amani na haki. Kutokana na uzoefu mbaya wa siku za nyuma huko Zanzibar, hali ya amani ilionekana zaidi katika upande huu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kiasi cha kwamba kuelekea mwishoni mwa kipindi cha kampeni Jeshi la Police liliwapongeza waziwazi wananchi wa Visiwani kwa uwepo wa amani na utulivu.

## SURA YA SITA

## VYOMBO VYA HABARI KATIKA MCHAKATO WA UCHAGUZI

### 1.0 UTANGULIZI

UCHAGUZI ulio huru na wa haki ni moja ya nguzo kuu katika mfumo wa demokrasia ya uwakilishi wa vyama vingi.Kwa upande mwingine msingi mkuu wa demokrasia ya vyama vingi ni mawasiliano kwa njia ya vyombo vya habari.

Vyombo vya habari katika jamii ya kidemokrasia ni nyenzo muhimu katika kukuza na kudumisha utamaduni wa siasa za ushindani ikizingatiwa kuwa jamii ya kisasa ni yenye watu wengi zaidi wenye mawazo na mitazamo tofauti kuhusu kila kitu ikiwepo misimamo ya kisiasa.

Pamoja na kutambua kuwa vyombo vya habari humilikiwa na kuendeshwa na watu wenye itikadi, malengo na mwelekeo tofauti wa kisiasa, kiuchumi na kijamii bado kuna majukumu ya msingi kwa vyombo hivyo ambayo hupimwa kama yanazingatiwa.

Hali kadhalika, pamoja na tofauti za kisera na malengo ya kuanzishwa kwa vyombo vya habari, kuna wajibu na maadili ya kitaaluma ambayo kila chombo cha habari na kila mtendaji (mwanahabari) anapaswa kuyazingatia. Haya ni pamoja na:

i. Kuhabarisha na kuelimisha umma;
ii. Kutoa tafsiri ya hali halisi (hii inahusu kuipatia jamii maana pana ya ukweli kuhusu tukio kulingana na mazingira yao ya kisiasa);
iii. Kuwa uwanja wa maoni wa kutolea dukuduku kuhusu jambo lo lote katika jamii;
iv. Kuwahamasisha wananchi kushiriki katika siasa na hasa wapiga kura; na
v. Kuwajenga kifikra wagombea na vyama shiriki kwenye mchakato wa uchaguzi wa kisiasa.

Katika sura hii, tunachambua nafasi na utendaji wa vyombo vya habari katika mchakato wa uchaguzi wa mwaka 2010. Katika kufanya hivyo, tunachambua nafasi ya vyombo vya habari vya umma na vyombo vya habari binafsi. Sura hii pia inajielekeza katika kuchambua uhuru wa kujieleza na kupata habari kutoka vyanzio mbalimbali, weledi katika kupeleleza na kuibua uozo wa kisiasa, weledi na udhaifu wa vyombo vya habari na wanahabari wenyewe pamoja na uzingatiaji wa maadili ya kitaaluma.

### 2.0 WAJIBU WA VYOMBO VYA HABARI KATIKA MCHAKATO WA UCHAGUZI

Kwa kiasi kikubwa, demokrasia ya ushindani wa kisiasa imesimikwa katika majadiliano na mawasiliano. Vyombo vya habari ni nyenzo muhimu sana katika mawasiliano na majadaliano haya.

Jinsi wigo wa demokrasia unavyozidi kupanuka kwa ukubwa na maingiliano, uwanja wa mawasiliano na mijadala kuhusu masuala ya umma unazidi kudhibitiwa na vyombo vya habari-redio, televisheni, magazeti, majarida, vitabu na hata takwimu na habari nyingine kutokana na teknolojia ya kisasa ya mawasiliano kupitia kumpyuta na hata simu za mkononi.

Vyombo vya habari katika jamii ya kidemokrasia vina majukumu mengi sana yanayoingiliana lakini yanayoeleweka wazi. Orodha hii inahusu majukumu ya vyombo vya habari wakati wa mchakato wa uchaguzi:

### 2.1 Kukusanya, kuchambua na kusambaza habari

Ni wajibu vya vyombo vya habari kukusanya, kuchambua na kusambaza habari za matukio mbalimbali ili kuwawezesha wananchi kuwa na uelewa wa kile kinachoendelea katika mazingira yao na hata nje. Ili wananchi waweze kufanya uamuzi wenye busara na wenye tija, wanahitaji habari ambazo ni sahihi, za wakati huo na ambazo hazikupindwa. Na kwa sababu watu wanayo mawazo yanayotofautiana, huhitaji pia kupata maoni tofauti katika masuala mbalimbali. Hii ndiyo sababu ya kuhimiza miliki ya vyombo vya habari kuwa mikononi mwa wamiliki tofauti, wenye mitazamo inayokinzana na pia wenye itikadi tofauti kama ilivyo jamii yenyewe.

### 2.2 Upashaji Habari na Elimu kwa Umma

Ni wajibu wa vyombo vya habari kutoa habari na kuelimisha umma kuhusu uchaguzi. Elimu inayotakiwa hapa ni ya aina mbili. Kwanza ni elimu ya mpiga kura, na pili ni elimu ya uraia.

Wakati elimu ya mpiga kura ni zoezi la muda mfupi linalohusiana na uchaguzi tu, elimu ya uraia ni zoezi la muda mrefu linaloendelea hata nje ya kipindi cha uchaguzi.

Elimu ya uraia ni zoeli la kudumu lenye lengo la kumjengea raia uelewa mpana wa siasa na nafasi yake katika siasa. Kupitia elimu ya urai mwananchi wa kawaida anajengewa uwezo na kuchukua nafasi yake kama raia mwenye haki na wajibu.

Kwa upande mwingine elimu ya mpiga kura, inajikita zaidi katika kuelimisha raia mambo yote yanayohusu mchakato uchaguzi hatua kwa hatua vikiwemo umuhumu wa kujiandikisha kama mpiga kura, sheria, kanuni na taratibu mbalimbali za uchaguzi, nafasi ya vyama vya siasa, uteuzi wa wagombea, sifa za wagombea, kampeni na sheria zote zinazotawala mwenendo wa kampeni, upigaji kura na taratibu zake, makosa yanayopaswa kuepukwa wakati wa upigaji kura, haki wa wagombea na wapiga kura, wajabu wa mamlaka zinazohusika usimamizi wa uchaguzi, muda wa kupiga na kura na kadhalika.

Elimu ya mpiga kura inalenga katika kuhamasisha raia wenye sifa na nia ya kuwa viongozi wa kisiasa kujitokeza na kuchukua fomu za kugombea kupitia vyama vyao, ilihali kwa upande mwingine, ikihamasisha wapiga kura kujiandikisha na kisha kwenda kupiga kura.

Wakati ni jambo la kufurahisha kwamba vyombo vya habari vilifanya kazi kubwa sana katika utoaji wa elimu ya mpiga kura, vyombo hivyo havikufanikiwa katika elimu ya uraia, kazi ambayo ni ya muda wote.

### 2.3 Kuwapa nafasi watu kutoa maoni yao kuhusu mwenendo wa uchaguzi

Demokrasia haiwezi kukamilika na hasa katika mchakato wa uchaguzi pasipo kuwepo na nyenzo za kuwawezesha wananchi kutoa maoni. Ni ili maoni hayo yaweze kuwafikia watu wengi bila kujali tofauti na mitazamo yao ya kisiasa, vyombo vya habari vinatarajiwa kuwa

daraja la kusambaza maoni hayo. Uhuru wa kutoa maoni pamoja na uhuru wa vyombo vya habari unatambuliwa na kuanishwa katika sheria za kimataifa na ndani ya katiba kwa minajili hiyo.

Tathmini ya vyombo vya habari wakati wa mchakato wa uchaguzi wa mwaka 2010, unaonyesha kuwepo kwa utitiri wa maoni kwa njia mbalimbali zikiwemo barua kwa mhariri, sms, simu kwenye vituo vya redio na televisheni, mijadala katika vipindi vya redio na televisheni, n.k. Faida ya kuwepo kwa vyombo vingi vyenye mitazamo tofauti ndiko kulikowezesha kusambazwa kwa maoni tofauti yenye mitazamo tofauti. Faida yake ni kwamba barua au simu ya maoni inayokataliwa kupokelwa katika kituo fulani cha redio/televisheni au gazeti inapokelewa kwa mikono mwili katika kituo cha redio/televisheni au gazeti lingine.

## 2.4 Kuonyesha Dira /Kuongoza Umma

Kama vikitaka, vyombo vya habari vinaweza kuwa na wajibu mkubwa katika kuonyesha dira au njia kwa taifa. Kupitia njia ya maoni na upembuzi yakinifu, vyombo vya habari vinaweza kuendesha kampeni kwa ajili ya sera fulani au hata kudai mabadiliko katika sera ambayo vinadhani lazima yafanyike kwa manufaa ya umma. Pia vyombo vya habari vinaweza kutumika kama uwanja kwa ajili ya taasisi mbalimbali na watu binafsi kueleza maoni yao kupitia barua za wasomaji na makala nyingine zenye mawazo tofauti. Kwa kuchagua ni masuala gani yatangazwe au kuwekwa kando, vyombo vya habari vinakuwa vinafanya kazi ya kuongoza umma kwani maamuzi ya namna hii hatimaye huwashawishi watu kutambua yapi ni masuala ya muhimu zaidi katika jamii. Vita dhidi ya *ufisadi* kwa mfano, ni ajenda ambayo kwa kiasi kikubwa imeshikiliwa bango na vyombo vya habari kiasi kwamba imekuwa ni ajenda ya kitaifa ambayo isingeweza kupuuzwa na wanasiasa hasa katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu.

## 2.5 Kuchunguza mwenendo wa serikali na viongozi wa kisiasa

Ni wajibu wa vyombo vya habari kuchunguza mwenendo wa serikali, viongozi wa kisiasa na taasisi nyingine zenye nguvu katika jamii. Kwa kushikilia msimamo wa kuwa huru na kufuata haki, hata kama kuna matatizo katika utekelezaji wa dhana hizo, vyombo vya habari vinaweza kutoboa ukweli kuhusu madai ya serikali na hivyo kuwafanya viongozi na watumishi wa umma kuwajibikia kwa vitendo vyao.

Jambo lingine na la msingi katika uchunguzi wakati wa mchakato wa uchaguzi ni kuona kuwa vyama vya siasa na wagombea wake bila kusahau watendeaji wakuu katika mchakato huo wanaendesha shughuli za uchaguzi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zote zinazoongoza mchakato huo. Kwa kutambua kuwa hofu ya kushindwa uchaguzi huwafanya baadhi ya wagombea na wapambe wao au hata watendaji wasio na maadili kujiingiza katika kutoa rushwa, kupinda sheria na kanuni za uchaguzi, vyombo vya habari vinakuwa na wajibu wa ziada kuchunguza mienendo ya watendaji au wagombea wote pamoja na washirika wao kuona kuwa wanazingatia sheria zilizopo pasipo upendeleo. Kama hiyo haitoshi, baadhi ya wanasiasa wasio kuwa waaminifu hudanganya elimu yao na umri wao, mali zao na madeni ili mradi kujifanya wanazo sifa zote za kuwa wagombea huku wakifukia uchafu mbele ya macho ya umma. Ni wajibu wa vyombo vua habari kufuatilia haya yote, kuyafichua na kuyaanika hadharani.

Kuna suala la maadili kwa wanasiasa na viongozi wote kwa ujumla wao. Ni jukumu la vyombo vya habari kuona kuwa vinawajibika kufuatilia haya yote na kuyafichua.

Pamoja na hatua kubwa iliyopigwa hadi sasa bado vyombo vya habari vinatakiwa kuongeza juhudi katika kufichua uozo katika nyanja ya siasa na hasa katika mchakato wa uchaguzi. Katika mchakato wa uchaguzi wa 2010 madai yaufisadi miongoni mwa wagombea na wapambe wao yalisikika kila kona na kila mahali. Lakini kwa kushindwa kwa vyombo vya habari kutekeleza wajibu wake, habari hizi ziliishia kuwa ni majungu tu.

**2.6 Kuwasilisha mambo ya msingi wakati wa kampeni**

Wakati wa kampeni, vyombo vya habari vinawajibika kutoa fursa kwa vyama na wagombea wao ili waweze kunadi sera zao ili kupata kuungwa mkono na hivyo kupigiwa kura. Kwa upande mwingine, kupitia vyombo vya habari wapiga kura wanatarajiwa kuweza kupima uwezo wa wagombea wapya na wale waliokuwa madarakani na hivyo kuweza kufanya uamuzi wa busara wakati wa kupiga kura. Kuwa na habari sahihi za wagombea kunawasadia wapiga kura kuepuka mtengo wa kupiga kura kwa kufuata ahadi tu na badala yake wanapiga kura kwa kuzingatia utendaji wa mgombea hasa yule anayetetea kiti chake. Kusudio la jumla hapa, ni kwamba katika demokrasia serikali za kuchaguliwa, vyama vyake na wagombea wake sharti waendelee kuwepo madarakani kwa kutokana na utendaji wao na siyo ahadi wala kitu kingine cho chote.

Takwimu zilizokusanya na Shirika la Synovate Tanzania (rejea ripoti nambari 3 na 17) zinaonyesha kuwa wakati wa mwenendo mzima za kampeni ajenda na sera za vyama ziliweza kuanishwa kwenye vyombo vya habari. Kwa mujibu wa takwimu za Synovate mambo makuu matano ndiyo yaliyopewa uzito mkubwa na vyombo vya habari wakati wa kampeni za uchaguzi wa 2010. Haya yalihusu rushwa (*ufisadi*), elimu, afya, amani na kilimo. Ikumbukwe tu kuwa katika kuandikwa, uzito wa kila suala ulibadilika kutoka mwezi hadi mwezi kadri mwenendo wa kampeni ulivyokuwa ukipamba moto.

**2.7 Kuwakilisha wagombea na watendaji wengine wakati wa kampeni**

Vyombo vya habari vinapaswa kutumika kama uwanja wa majadilio kwa pande zote zinazoshirika katika kinyang’anyiro cha madaraka ya kisiasa nia ikiwa ni kuwawezesha wapiga kura kuwaelewa kinagaubaga wagombea pamoja na sera wanazozisimamia. Kuna njia nyingi zinazotumiwa na wagombea kupitia vyombo vya habari: matangazo, mahojiano, mabango, picha za matangazo, majarida, vipeperushi na kufuatia ujio wa teknolojia mpya njia nyingine zimeongezeka mathalani sms, blogs na internet.

**2.8 Kuwaunganisha Viongozi (wagombea) na wananchi (wapiga kura)**

Katika kipindi chote cha mchakato wa uchaguzi, vyombo vya habari vilitumiwa kwa mapana na marefu katika kuwanadi wagombea. Njia mbalimbali zilitumika katika kuwasilisha ujumbe. Teknolojia ya kisasa hasa matumizi ya sms ilitumika kwa mara ya kwanza kwa kiwango kikubwa. Njia zilizozoeleka nazo hazikiachwa nyuma ikiwa ni pamoja na mikutano ya hadhara, mahojiano katika redio na televisheni, makala katika magazeti, vipindi maalum kama vile *Jimbo kwa Jimb*o (TBC) pia vilibuniwa na kutumika vizuri sana. Wagombea mbali mbali kutoka vyama vilivyoshiriki katika uchaguzi walipata fursa kufanya kampeni kupitia vyombo vya habari. Isisitizwe tu kwamba vyama ambavyo vilisimamisha wagombea urais

vilikuwa na fursa zaidi ya kutumia vyombo vya habari. Hali kadhalika, vyama na wagombea wenye uwezo mkubwa wa kifedha pia walikuwa na fursa zaidi ya kupenyeza sera zao kupitia vyombo vya habari kwenda kwa wapiga kura kwa kulipia vipindi kwa njia ya matangazo.

## 3.0 VYOMBO VYA HABARI VILIVYOTANGAZA MCHAKATO WA UCHAGUZI WA 2010

Jinsi vyombo vya habari vilivyotangaza mchakato wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 ni kielelezo tosha cha jinsi jamii ya watanzania ilivyo na watu wengi, wenye mitazamo na fikra tofauti wanapo kutanishwa kwenye ushindani wa soko la siasa. Wakati vyombo vya habari vya serikali viliendelea naa utamaduni wao wa kuungano mkono chama tawala na wagombea wake, vyombo vya habari vya binafsi viligawanyika na hata kwenda nje ya utamaduni uliozoeleka wa vyombo vya habari wa demokrasia ya nchi za magharibi.

Kitu kimoja kilicho wazi ni kwamba vyombo vyote vya habari vya serikali na vile vya binafsi bado vimeendelea kurubuniwa na pande zinazoshindana (hasa vyama vya siasa na wagombea wake) au bado vinakubali kurubuniwa ili kushiriki kuwayumbisha wapiga kura. Kwa maneno mengine, ingawaje nchi imeshamiri utitiri wa vyombo vya habari, bado vimekosa uhuru na weledi wa kuweza kutimiza wajibu wake ipasavyo. Ni kweli kwamba wanahabari wanaweza kabisa wakawa wanawania kufikia kiwango cha juu katika uandishi wao, lakini habari zote huchujwa kufuata matakwa na hisia za watu wenye nguvu katika jamii na wenye kumiliki taasisi hizo. Kwa lugha nyingine, ni kwamba ile dhana kwamba vyombo vya habari vinakuwa huru zaidi vikiwa mikononi mwa watu binafsi kuliko serikali ni dhana potofu kwa vile si kweli kwamba wanaowekeza kwenye vyombo vya habari wanafanya hivyokwa minajili ya kupanua wigo wa demokrasia na kulinda haki za binadamu, wanafanya hivyo kwa maslahi yao binafsi ambayo wakati mwingine huenda kinyume kabisa na demokrasia na pengine hata haki za binadamu.

Ukaribu wa vyombo vya serikali na vile vya binafsi, na hasa vile vilivyoko mikononi mwa makada wa CCM ulijidhihirisha waziwazi wakati wa uchaguzi pale baadhi yao vilipogeuzwa mwiba mkali kwa wapinzania hususani mgombea urais kupitia CHADEMA Dk. Willibroad Slaa.

Magazeti yaliyoibuka wakati wa kipindi cha mchakato wa uchaguzi yalijidhirisha kwa nini yameibuka wakati huo. Tahariri na makala zilizojaa chumvi na kejeli, kashfa na hata matusi zilisheheni kwenye kurasa za magazeti ilhali makala elekezi, zenye kuibua mijadala kuhusu masuala ya kijamii pamoja na upembuzi yakinifu zilikuwa haba. Na kama hiyo haitoshi, baadhi ya wahariri na wanahabari wa waandamizi walitumbukia kwenye mtego wa kupepenea kwa wakubwa labda kwa kupewa vijisenti au ahadi za ukuu wa wilaya baada ya uchaguzi, wakajisahau hadi kufika hatua ya kuvalishwa majoho ya CCM yaliyobandikwa tangazo la '***Kikwete Press 2010'*** , ilihali wakijua huo ni ukiukaji wa maadili ya kitaaluma.

Wakati mgombea urais wa CCM Jakaya Kikwete alipodondoka jukwaani pale Jangwani tarehe 21 Agosti 2010 siyo kwamba televisheni zilizuia kuonyesha kinachoendelea lakini hata kesho yake habari hivyo haikuguswa kwenye vyombo vya habari vya umma na maswahiba wake. Badala ya vyombo hivyo kujadili hali ya afya ya mkuu wa nchi, habari ambayo ni ya manufaa kwa umma, vyombo vya habari viligeukiwa kwenye mambo yasiyo ya msingi wakati huo kama vile *Kilimo kwanza.*

Kwa sababu ya kutokuwa na uhakika wa nini cha kufanya, siku CHADEMA ilipozindua kampeni yake kwenye uwanja huo huo wa Jangwani tarehe 28 Agosti 2010, Shirika la

Utangazaji (TBC) lilisimamisha kwa muda matanganzo kwa madai kwamba wazungumzaji walikuwa wakitoa matusi.

Kuna magazeti ambayo yaliweza kuchapishwa na kusambazwa bure pale yalipokuwa na habari zenye kashfa dhidi ya upinzani na hasa hasa Dk.Slaa. Moja ya habari iliyochapishwa kwenye gazeti la *Mwananchi* ya tarehe 14 Septemba 2010 ilihusu kusambazwa bure kwa nakala za gazeti la *Changamoto* kwenye mikoa ya Mwanza na Arusha huku likinadi habari yenye kumkashifu Dr .Slaa. Kwamba *Changamoto* lingeweza kuchapisha na kusambaza nakala bure huku likikabiliwa na faini ya shilingi 1.5 bilioni iliyotolewa na mahakama kuu kwa kumkashifu moja wa wafanyabiashara jijini Dar es Salaam ni jambo lenye maswali mengi kuliko majibu.

Kama kipindi cha uchaguzi ni kipimo cha kupima umadhubuti wa vyombo vya habari katika kupanua na kudumisha demokrasia, ni dhahiri uchaguzi wa 2010 umedhirisha jambo moja, kwamba vyombo vya habari bado vina njia ndefu.

Sababu moja kubwa ni aina yamiliki ya vyombo vya habari, kwani takwimu zilizopo zaonyesha kuwa, mbali ya vyombo vya serikali vyombo binafsi vilivyo vingi vinamilikiwa na makada wa CCM wakiwemo wabunge na mawaziri (***angalia Jedwali Nambari 2).*** Na kana kwamba hiyo haitoshi, wahariri na wanahabari wengine 'walinunuliwa' na wanasiasa-wafanyabiashara ili kufanikisha malengo yao kibiashara au siasa. Kwa kufanya hivyo, taaluma ya habari ikawekwa rehani.

Kwa upande mwingine, kuna wahariri na wanahabari wakereketwa ambao wamepewa madaraka ndani ya vyama vya siasa kama makatibu wenezi, maafisa habari au washauri na kuna wale ambao wamegombea nafasi za uongozi kwenye vyama au jumuiya zake na hivyo kushikilia majukumu yanayokinzana. Hivyo, haikushangaza pale kwa mara nyingine tena walipoibuka wandishi mamluki (mercenary journalists) ambao kazi yao ni kuandika na kutangaza lo lote kwa malipo, na mno zaidi pale wanapolipwa kwa 'kumuua mtu kisiasa'.

Kitu kingine kilichojitokeza waziwazi wakati wa mchakato wa uchaguzi wa 2010, ni kupuuzwa kwa habari za majimbo ya vijijini na wagombea wake na vyombo vya habari viwe vya umma au binafsi. TBC ambayo ilifanya kazi kubwa sana katika uchaguzi uliopita iliandaa vipindi vya *Jimbo kwa Jimbo* ambapo wagombea ubunge kutoka vyama mbalimbali waliweza kunadi sera zao na kuulizwa maswali na wapiga kura kwa mafaniko makabwa. Hata hivyo, si majimbo yote 239 yaliyofikiwa na kipindi hicho kizuri. Magazeti na vyombo vingine viliweza kuandika na kutangaza habari za kampeni katika majimbo ya uchaguzi ya vijijini pale tu wagombea urais walipofika huko na habari ziliwahusu wao na siyo wananchi au wagombea wa ngazi za ubunge au udiwani. Mathalani katika jimbo la Mtwara mjini kwa mujibu wa taarifa za TEMCO, kulikuwa na habari mbili tu katika kipindi chote cha kampeni. Habari ya kwanza ilikuwa kwenye gazeti la *Mwananchi* la tarehe 15 Oktoba 2010 likiwa ni kichwa cha habari ' *Mgombea wa CUF aahidi kumfilisi mwenzake wa CCM*'. Habari ya pili ilikuwa kwenye *The Citizen* wakati mgombea urais wa CCM alipofanya kampeni liyodumu dakika 36 tu hapo 18 October 2010.

Nafasi udiwani ndiyi ngazi ambayo ilipuuzwa kabisa na vyombo vyote vya habari. Hii ni habari mbaya ikizingatiwa kuwa maamuzi yanayofanywa na madiwani yanagusa moja kwa moja maisha ya watu kwa kila siku. Cha ajabu ni kwamba hata redio za kijamii ambazo zimeanza kuzagaa hata kwenye majimbo ya uchaguzi nazo ziliona fahari kutangaza habari uchaguzi wa wabunge na rais kuliko zile za madiwani. Katika jimbo la Mtwara mjini

mathalani, licha ya kuwepo vituo vine vya redio: Pride, Peace, Safari na Maria bado vituo hivyo vilikuwa kimya muda wote wa kampeni vikipendelea kuwatumbuiza watu kwa muziki wa kileo.

## 4.0 UTANGAZAJI WA VYOMBO VYA SERIKALI

Vyombo vya habari vya serikali ni vile vinavyomilikiwa na serikali moja kwa moja kama vile Televisheni ya Zanzibar (TVZ), Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ) na magazeti ya *Nchi Yetu* na *Zanzibari Leo* pamoja na vituo vya redio na televisheni vinavyomilikiwa na Halmashauri za Wilaya mathalani Sibuga FM au Ulanga FM. Vyombo vingine vinavyomilikiwa na serikali ni vile vinavyoendeshwa na mashirika ya umma kama vile TBC, *Daily News, Sunday News, Habari Leo* na Mlimani Redio. Idara ya Habari ni chombo pia cha serikali ikichapisha gazeti la *Nchi Yetu* na kusambaza habari za serikali kupitia *Maelezo.*

Sera ya vyombo hivi vyote ni kuiunga mkono serikali pamoja na chama tawala. Msimamo huu hata hivyo, unakinzana na Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya 2010 ambayo katika Ibara ya 28 (1) inasema kwamba '*Mgombea wa nafasi ya urais atakuwa na haki ya kutumia vyombo vya utangazaji vya Serikali wakati wa kampeni kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Uchaguzi (**angalia cap.343**'*

Hali kadhalika, Ibara ya 28(2) inafafanua zaidi kwamba '*Vyombo vya habari vya Serikali vitakusanya na kusambaza habari za uchaguzi pasipo upendeleo na kwamba habari hizo hazitapindishwa dhidi ya mgombea'.*

Na kama hiyo haitoshi, maadili ya kitaaluma nayo yanakataza upendeleo wa aina yote wakati wa uchaguzi kwa vyombo vyote vya habari. Msumari wa mwisho ni mwongozo wa kimataifa kwa vyombo vya habari vya Serikali /Umma ambayo unatoa maelekezo 17 yafuatayo wakati wa uchaguzi:

i. Vyombo vya habari havina budi kuufahamisha umma kuhusu vyama vya siasa, wagombea, sera zao, utaratibu wa kupiga kura na mambo yote yanayohusu mchakato wa uchaguzi;
ii. Vyombo vya habari havina budi kutokuegemea upande au kufanya upendeleo wo wote dhidi ya chama cha siasa au mgombea katika kuandika na kutangaza habari za uchaguzi;
iii. Habari, mahojiano au vipindi vya habari lazima visibague au kupendelea chama au mgombea ye yote;
iv. Kigezo kinachotumika katika kuamua habari au kipindi lazima kiwe wazi pasipo shaka yo yote;
v. Mgombea yo yote au chama anapolalamikia kukashifiwa au kuumizwa na chombo cha habari lazima apewe haki ya kusikilizwa, kusahihisha au kufuta kile kilichokuwa kimeandikwa /tangazwa dhidi yake kwa haraka kadri inavyowekana;
vi. Katika kuandika/kutangaza habari, vyombo vya Serikali vyapaswa kuwa mfano katika kuhakikisha kuwa habari ni sahihi, zilizosimama kati na bila upendeleo;
vii. Kanuni ya kuweka habari katika mizania inahitaji vyama au wagombea kupewa uzito wa habari zoa kulingana umuhimu wao katika uchaguzi na vile wanavyoungwa mkono;
viii. Kwa kuzingatia uwezekano wa tahariri kuchanganywa na habari za matukio, inahimizwa kwamba vyombo vya habari vya Serikali kutotanganza maoni kabisa.

Iwapo chombo cha habari cha Serikali kitatangaza maoni, kinalazimika pia kutangaza maoni ya vyama vikuu vya upande wa upinzani. Kama ni mhariri anatangaza/anaandika maoni yake inabidi ifafanuliwe na kuliweko hilo wazi, na kwa hakika inapendekezwa kwamba maoni hayo yasiandikwe au kutangazwa kabisa;

ix. Habari zenye utata zinazotokana na mikutano na wanahabari au taarifa za kiserikali zinazotolewa na mawaziri (nje ya shughuli za kiserikali)au wabunge hazina budi kujibiwa na upande wa pili unaohusishwa. Kanuni hii ipewe uzito mkubwa hasa pale yule anayetoa taarifa hiyo atakuwa pia ni mgombea;

x. Vyombo vya habari vya Serikali vinawajibika kutoa fursa sawa na bila ubaguzi wala upendeleo kwa vyama vya siasa na wagombea wote;

xi. Muda unaotengwa kwa ajili ya vyama au wagombea uwe wa kutosha kuweza kuwasilisha ujumbe kuhusu msimamo, sera au kile ambacho chama au mgombea anakisimamia;

xii. Muda wo wote uliotengwa kwa ajili ya mgombea au chama kwa malipo, basi uwe sawa kwa muda utakaotengwa kwa ajili ya wagombea zote au vyama vingine vyote. Hali kadhalika, kama chama au mgombea anatakiwa kulipia muda wa ziada wa matangazo, basi wagombea wengine au vyama nao wapangiwe muda huo huo kwa gharama zile zile kwa usawa;

xiii. Vyombo vya habari viandae vipindi ambavyo vitawawezesha wanahabari, wadadisi na wataalamu wengine kupata fursa ya kuuliza na kuwachambua kwa maswali wagombea au vyama na pia kuwawezesha wagombea kulumbana wao kwao katika mdahalo;

xiv. Vyombo vya Serikali vinawajibika kutoa elimu ya mpiga kura labda kama serikali yenyewe imejitwisha jukumu la kufanya kazi hiyo kwa kiwango cha kuwafikia wapiga kura wengi zaidi;

xv. Mpango wa elimu ya mpiga kura hauna budi kuwa sahihi usio na upendeleo na wenye kuwaelimisha kinagaubaga wapiga kura jinsi ya kujiandikisha, siri ya kura, umuhimu wa kupiga kura, majukumu ya wasimamizi wa uchaguzi, umuhimu wa vyeo vinavyogombaniwa kwa maisha yao ya kila siku na kadhalika;

xvi. Vyombo vya habari vya Serikali vinawajibika kutangaza vipindi kwa lengo la kuwafikia watu wengi kwa kadri inavyowekana. Matangazo haya hayana budi kuwafikia hata jamii/makabila ya wa watu wa pembezoni ikibidi kuandaa vipindi maalum kwa ajili yao na kwa kutumia lugha za jamii hizo;

xvii. Ikiwa vyombo vya Serikali vitachapisha matokeo ya kura za maoni au mwenendo wa uchaguzi, ni lazima kutoa taarifa hizo kwa umakini na uangalifu mkubwa na kwa kutoa vidokezo vyote vitakavyowasaidia wapiga kura kuelewa kwa mapana na marefu maana ya kura kama hizo.

Kama maelekezo haya yakitumiwa kama vigezo vya kupima utendaji wa vyombo vya habari vya Serikali nchini Tanzania katika uchaguzi wa 2010, ni dhahiri kuwa haviwezi kufaulu mtihani. Vyombo vya Serikali hasa vya utangazaji vilifanya vizuri sana katika utoaji wa elimu ya mpiga kura. Hata, hivyo, vikatatizika lilipokuja suala la vyama vya siasa na hususani wagombea hasa urais.

Tathmini iliyofanywa na Syunovate Tanzania, shirika huru lililokuwa limetwishwa jukumu la kufuatilia mwenendo wa vyombo vya habari na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), lilitoa matokeo yanayoanika ukweli kuhusu vyombo hivi. Mosi ni jinsi CCM ilivyopendelewa katika kuandikwa na kutangazwa na vyombo vyote katika kipindi chote cha mchakato wa kampeni (***rejea jedwali nambari 1 chini).***

**Jedwali Na. 6.1. Jinsi vyombo vya habari vilivyoandika/kutangaza habari za vyama mwezi Oktoba 2010**.

| S/N | Jina la Chama | Magazeti (%) | Radio (%) | TV (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | CCM | 49 | 48 | 41 |
| 2 | CHADEMA | 26 | 27 | 29 |
| 3 | CUF | 17 | 16 | 16 |
| 4 | NCCR-Mageuzi | 3 | 6 | 6 |
| 5 | TLP | 3 | 2 | 5 |
| 5 | APPT-Maendeleo | 2 | 1 | 3 |
| | **Jumla** | **100** | **100** | **100** |

***Angalizo: Takwimu hizi ni kwa vyombo vyote vya habari vya serik*ali *nabinafsi***

Kilichoibuliwa na tathmini ya Synovate Tanzania ni kwamba hata baada ya takriban miongo miwili tangu kuingia kwa utamaduni wa demokrasia ya vyama vingi , vyombo vya habari bado vimeshindwa kujivua joho la aina ya uandishi uliokuwa umeshamiri enzi za utawala msonge wa chama kimoja. Utamaduni wa kuwaingiza wanahabari na vyombo vya habari katika mfumo wa utawala ambao uliwageuza kuwa sehemu ya watumishi wa serikali kwa kila kitu bado haujabadilika miongoni mwa baadhi ya wanahabari. Na hii inajidhirisha zaidi miongoni mwa wanahabari katika vyombo vya habari vya serikali wanaoshindwa kwenda na wakati. Kufanya kazi kwa unafiki na matarajio ya kupendelewa na hasa kuambulia cheo cha kisiasa bado unawasonga na kuwakwaza kufanya kazi kitaaluma na kwa weledi.

Mfano mzuri ni tahariri iliyoandikwa katika gazeti la *Daily News* hapo 24 Septemba 2010. Tahariri hiyo iliyoandikwa katika ukurasa wa mbele (kwa kawaidia tahariri za *Daily News* huwa ukurasa wan ne) ilisema:

*“Dr. Slaa will not be the fifth president of Tanzania. The CHADEMA candidate has a lot of issues to settle, beginning at family level, from where he will need to practice leadership upwards. He will indeed garner some votes in October, just like Augustine Mrema in 1995, but that will be it, and the media behind the former priest can quote us on that”.*

Hali kadhalika, wanahabari wanaofanya kazi kwenye vyombo vya serikali bado wmejenga dhana kwamba wao ni watumishi au sehemu ya serikali na siyo wanataaluma inayopaswa kujitegemea. Ushihidi wa hili ni tahariri nyingine ya *Daily News* ya tarehe 31 Oktoba 2010 yenye kichwa cha habari: “*Vote for CCM, vote for unity.”*

Kama ilivyo kwa watumishi wengine serikalini, wahariri katika vyombo vya habari vya serikali bado wanateuliwa na Rais. Kwa mantiki hiyo wanatarajiwa kuonyesha utiifu wao

kwa mteule wao kama inavyojidhihirisha katika mifano hiyo miwili ya gazeti la serikali la *Daily News.*

Kitu kingine kinachohusiana na uandishi wa upande moja ni kuwepo kwa mtandao uliojengwa kumzunguka Rais Kikwete mwaka 2005 ambapo wahariri na wanahabari kadhaa kutoka vyombo vya serikali na binafsi walijikuta wamenaswa kwenye mtandao au ulimbo wa kupiga debe na kusahau wajibu wao kwa matarajio ya vyeo vya kisiasa baaada ya uchaguzi. Hii ndiyo sababu licha ya sheria kuwa wazi kuhusu wajibu wa vyombo vya serikali bado inakiukwa kama ilivyojidhirisha katika gazeti la serikali la *Daily News.*

## 5.0 UTENDAJI WA VYOMBO VYA HABARI VYA BINAFSI

Miliki ya vyombo vya habari vya binafsi inaweza kugawanywa katika mafungo manne kama ifuatavyo:

i. Miliki binafsi kwa ajili ya biashara (mfano wa IPP, Mwananchi, New Habari, Global Publications, Business Times n.k.);
ii. Miliki binafsi isiyo ya faida (mfano wa redio SAU ya Chuo Kikuu cha St Augustine iliyoko Mwanza)
iii. Miliki binafsi mahsusi ( mfano wa redio Tumaini ya Kanisa Katoliki, redio Quran ya Bakwata na Agape Televisheni ambazo ni mahsusi kueneza neon la Mungu);
iv. Mmiliki ya Umma/Jamii Huru (mfano wa redio Orkonorei iliyoko katika kijiji cha Terrat huko Simanjiro).

Ni vema kufafanua hapa tofauti ya vyombo binafsi na vyombo huru. Neno huru kwa mujibu wa Shirikisho la Wanahabari Duniani (IFJ), linahusu kutokinzwa na mbinyo wa kiserikali, kisiasa, kiuchumi au nyenzo nyingine katika kukusanya, kuchambua na kusambaza habari. Ni dhahiri, kwa maana hii ya IFJ, ni vyombo vichache sana vinaweza kutiwa vyombo huru hapa Tanzania labda redio Orkonorei inayomilikiwa na jamii badala ya kampuni au mtu inafsi, dini au chama cha siasa.

Hii ina maana kuwa , hata kama vyombo ni vya binafsi bado inabidi kuangalia kama wamiliki wake wanaegemea au wana ukaribu na chama kipi cha siasa , na vile vile kuangalia kama hakuna kuingilia katika utendaji wa kila siku wa vyombo hivyo. Kitu kinachojitokeza zaidi hapa Tanzania ni kuwemo kwa wingi kwa wanasiasa na wafanyabishara katika miliki ya vyombo vya habari.

Ukiacha vyombo vya habari vichache kama gazeti la *Raia Mwema* linalomilikiwa na wanahabari wenyewe, karibu vyombo vingine vyote vinamilikiwa na na wafanyabiashara waliovaa ngozi za kisiasa. Lakini mno zaidi ni uwepo wa makada wengi wa Chama cha Mapinduzi kila mahali (angalia jedwali nambari 6. 2)

**Jedwali Na. 6.2 Miliki ya Vyombo vya Habari**

| Na | Jina la Chombo | Mmiliki | Uanachama |
|---|---|---|---|
| 1 | Abood TV/Redio | Aziz Abood (MB) | CCM |
| 2 | Redio Tabora | Ismail Aden Rage (MB) | CCM |
| 3 | Redio Kasibante | Khamis Kagasheki (MB) | CCM |
| 4 | New Habari 2006 | Rostam Aziz (MB) | CCM |
| 5 | Zenj Redio FM | Mohamed Seif Khatib(MB) | CCM |
| 6 | Moshi Redio FM | Philemon Ndesamburo(MB) | CHADEMA |
| 7 | Taifa Tanzania | Nizar Karamagi (ex-MB) | CCM |
| 8 | StarTV/RFA | Antony Diallo (ex-MB) | CCM |
| 9 | IPP | Regionald Mengi | CCM |
| 10 | BTL | Hayati Ricjhard Nyaulawa (ex-MB) | CCM |
| 11 | Tanzania Daima | Freeman Mbowe | CHADEMA |
| 12 | African Media | Rostam Aziz | CCM |

Kushamiri kwa makada wa CCM wanaomiliki vyombo vya habari kunaua hata ile dhana ya kuwepo kwa vyombo maridhawa na sawia katika ulingo wa siasa. Katika jamii ambayo nguvu ya vyombo vya habari ni kubwa mno na katika mazingira ambayo huwezi kutenganisha nguvu ya kisiasa na kiuchumi kwa vile inamilikiwa na wale wale, ni ndoto za alinachi kufikiria kuwa kunaweza kukawapo na uhuru wa vyombo vya habari. Ni hii inadhihirishwa na jinsi vyombo vya habari vilivyoandika na kusambaza habari za uzushi dhidi ya Dk. Slaa aliyekuwa mgombea wa CHADEMA.

Takwimu kutoka Synovate Tanzania zaonyesha mathalani kwamba, kati ya sentimeta za mraba 246,691 zilizotumika na magazeti kwa aliji ya uchaguzi, sentimeta za mraba 4,318 zilitumiwa kuandika vibaya dhidi ya CHADEMA ukilinganisha na sentimeta za mraba 4,099 zilizotumika kuiandika vibaya dhidi ya CCM.

Kitu kingine kilichojitokeza ni matumizi mabaya wahariri na wanahabari na wamiliki wa vyombo vya habari. Msukumo wa kuwalazimisha kuandika kile ambacho wasingekifanya kwa utashi wao na matakwa ya kitaaluma ulikuwa ni mkubwa mno kiasi cha kushindwa kufuata maadili. Mfano mojawapo ni huu.

Tarehe 10 Septemba 2010 gezeti la *Taifa Tanzania* liliandika katika ukurasa wake wa mbele habari iliyosomeka”

*Dk. Slaa asichaguliwe*

- *anawadhalilisha wanawake*
- *itakuwaje awa rais bila wabunge*

Hii ni moja ya maoni yalijitokeza kwenye kurasa za mbele katika magazeti ambazo hutengwa kwa ajili ya habari za matukio na mhariri ye yote mweledi hawezi kufanya kosa kama hilo pasipokuwapo shinikizo kutoka kwa mwenye mali au ushabiki wa kisiasa. Mbali ya shinikizo, tatizo jingine hapa ni ushabiki na tamaa kwa baadhi ya wahariri na wanahabari ya kuwa tayari kuandika/kutangaza cho chote kwa malipo /ufisadi. Ndani ya vyombo vya habari vya binafsi kuliibuka kile kinachoweza kuitwa wandishi mamluki ambao wako tayari kuandika na kutangaza lo lote bila kujali matokea baadaye kwa malipo. Kuzukwa kwa wandishi mamluki kumepelekea kuwageuza wanahabari wapiganaji katika vita vya kisiasa na kibiashara visivyo vyao kwa gharama kubwa ya taaluma yao ambayo imezidi kupoteza mwelekeo.

Uchaguzi wa 2010 ulishuhudia mgawanyiko mkubwa wa wanahabari katika makundi hasimu tofauti huku kila kundi likidai kuwakilisha maslahi ya jamii. Kugawanyika kwa wanahabri, hata hivyo, ni kielekezo tosha cha mgawanyiko wa jamii nzima kutokana na mgangano wa kimaslahi na ukosefu wa maadili ya kitaifa kielelezo kikubwa kikiwa ni *ufisadi.*

## 6.0 UHURU WA KUJIELEZA WAKATI WA MCHAKATO WA UCHAGUZI

Umuhimu wa uhuru wa kujieleza na ule wa vyombo vya habari katika mchakato wa siasa, umefafanuliwa kinaga ubaga katika Ibara ya 7.8 ya Tamko la Copenhagen la mwaka 2002 ambalo linasema kusiwepo na pingamizi lo lote au ubaguzi katika matumizi ya vyombo vya habari iwe kwa chama, kikundi au mtu binafsi. Tamko hilo linasisitiza haja ya vyama au wagombea wote kupewa nafasi sawa katika vyombo vya habari ili wapiga kura waweze kuwa na uelewa mpana kuhusu sera, mipango na kile ambacho wagombea wanakisimamia kwa minajili ya kufanya uamuzi wa busara katika kupiga kura.

Vile vile tamko hilo linaelekeza kuwa upatikanaji wa nafasi kwenye vyombo vya habari uwe ni wa wakati wote ni siyo tu wakati wa kampeni kuelekea uchaguzi kama ilivyo nchini Tanzania.

Tathmini ya matumizi ya vyombo vya habari katika mchakato wa uchaguzi wa 2010 inabainisha bayana kuwa kulikuwa na kuyumba au ukiukaji wa viwango vinavyokubalika katika kutangaza habari za vyama na wagombea na sababu zake zinajulikana.

Wakati CHADEMA kilipozindua kampeni zake pale Jangwani mnamo Augost 28, 2010 TBC ilisitisha kwa muda matangazo yake kwa kile kilichodaiwa matumizi ya lugha ya ‘matusi’ na baadhi ya wazungumzaji.

Gazeti la *Mwananchi* nalo lilijikuta likiwa matatani ya Msajili wa magezi pale iliporipotiwa na gazeti dada la *The Citizen* kwamba *Mwananch*i lilikuwa linakabiliwa hatari ya kufungiwa kwa kuandika habari za kuidhalilisha serikali.

Msajili katika barua yake tarehe 10 Oktoba 2010 yenye kichwa kisemacho *Karipio kali kwa kuandika habari zenye mwelekeo wa kudhalilisha,* na ambayo ilikuwa ni ya pili ndani ya kipindi cha mwezi moja, alionya kuwa serikali isingesita kuliufungia kama gazeti hilo lingeendelea kuandika habari za kudhalilisha. Cha ajabu ni kwamba serikali haikutoa mfano wa wa habari au kichwa cha habari au hata toleo ambalo lilikuwa na habari za kudhalilisha

serikali. Na kama hiyo haitoshi, bado barua haikuonyesha kipengele cha sheria iliyokuwa imekiukwa na gazeti la *Mwananchi* katika uandishi wake.

Kwa vyo vyote vile , tafsiri ya barua za aina hii ni kufinya uhuru wa habari na wa kujieleza wakati uchaguzi. Ni aina fulani ya vitisho kwa vyombo vya habari na madhara yake huwa ni pamoja na kujengwa kwa woga miongoni mwa wanahabari unaoambatana na kuchuja habari bila hata kuulizwa.

Ni jambo la kushangaza kwamba Serikali iliamua kuliandama gazeti la *Mwananchi* ambalo limejipambanua kwa kutokufumbia macho ukiukwaji wa maadili miongoni mwa wahariri na wanahabari wake. Itakumbukwa kuwa mwaka 2005 liliweza kumfukuza kazi mhariri wake mtendaji baada ya kukiuka maadili kuhusiana na mwenendo wa uchaguzi. Ni jambo la kushangaza zaid kwamba Serikali ililiandama *Mwananchi* lakini ikayafumbia macho magazeti mengine ambayo yaliandika habari za uchochezi wa waziwazi kwa mujibu wa sheria ya Magazeti ya 1976 na ile ya Usalama wa Taifa ya 1977. Mifano iko mingi:

" *CHADEMA kuteka vituo vya redio: Kumtangaza Dk. Slaa kuwa Rais"* (***Sauti Huru***).

Kulikuwa pia na habari za kufitinisha dini pasipo sababu:

"*Maaskofu na Slaa wao watatuleta Rwanda"* ***(An Nuur***)

Itakumbukwa vile vile kuwa ni makampuni yanayomiliki *Mwananchi/Citizen* na *Raia Mwema* ndiyo pekee yaliyokwepa mtego kwa kukataa tangazo la biashara kutoka Chama cha Mapinduzi lenye thamani ya milioni 8/= lililotolewa kwa mazageti karibu yote kwa masharti kwamba liwekwe ukurasa wa mbele na katika rangi za CCM. Gazeti jingine ambalo halikupewa tangazo hilo, lilikuwa ni *Mwanahalisi* kwa vile msimamo wake unajulikana na kila mtu.

Shirika lisilo la kiserikali la Policy Forum nalo lilionja joto la jiwe pale TBC ilipovunja mkataba wa matangazo kwa kupitia televisheni na redio kwa madai kuwa matangazo hayo kuhusiana na rasimali madini yalikuwa yanakiuka maadili ya utangazaji kama yalivyokuwa yamewekwa na uongozi wake.

Ukizingatia ukweli kwamba matangazo hayo yalikuwa yamekubaliwa awali na kwa vile yalikuwa yanahusu maeneo nyeti wakati huo wa kampeni, ni dhahiri TBC ilishinikizwa kufanya uamuzi wa kuvunja mkataba, na kwa kufanya hivyo ni dhahiri, ilikuwa ni kubinya uhuru wa kujieleza kama inavyotamkwa katika tamko la Copenhagen la 2002.

Mifano yote hii inadhirisha wazi kwamba suala la uhuru wa kujieleza bado lina safari ndefu.

## 7.0 KUCHUNGUZA NA KUIBUA MAOVU

Ni wajibu wa vyombo vya habari kuchunguza, kuibua na kuweka hadharani maovu ndani ya serikali, taasisi za serikali na watendaji wake. Lakini mwanahabari anayefuatilia mwenendo wa uchaguzi hawezi kukwepa kuchunguza matumizi ya fedha katika mchakato wa uchaguzi.

Nani amekusanya fedha ngani na kwa ajili ya uchaguzi? Hakuna mwanahabari ambaye anafuatilia mchakato wa uchaguzi anayeweza kuacha kunusa kuhusu suala la fedha. Fedha hukusanywa kugharamia kila kitu kuanzia matangazo hadi sare, usafiri, vikundi vya kwaya na chakula na malazi. Hii ni gharama kubwa hivyo ni vizuri kujua ni nani anajitwishwa mzigo huu mkubwa na kwa faida gani. Kwa kufuatilia fedha zinavyokusanywa na kutumiwa,

mwandishi anaweza hata kubaini mwelekeo wa baada ya uchaguzi kwa wale waliofanikisha ushindi.

Na kupitishwa kwa Sheria ya Gharama za Uchaguzi Nambari 6, 2010, inayowataka wagombea kutangaza gharama za uchaguzi, kazi ya ziadi iliongezeka kwa wanahabari. Ni jamba la kufadhaisha kuwa hakuna cha kuripoti kuhusu vyombo vya habari vilivyojihusisha na habari za gharama za matumizi ya uchaguzi.

Wanasiasa pia wanajulikana kwa sifa ya kudanganya au kutoa taarifa zisizosahihi kuhusu elimu, umri, afya, na hata mali zao, achilia mbali rekodi ya utendaji wao, matumizi ya mabaya ya madaraka yao na sasa ufisadi. Hili ni eneo jingine ambalo wanahabari wanapaswa kuchungunza na kuibua. Kwa bahati mbaya hakuna kitu cha kuwasifia katika eneo hili pia. Mbali ya ukosefu wa maarifa na stadi za kufanya kupeleleza, tatizo kubwa linaloikumba sekta ya habari na wanahabari wenyewe kama ilivyokwisha kuelezwa huko nyuma, ni mgongano wa maslahi, rushwa, woga, dhamira ya kutenda pamoja na ubutu wa kitaaluma kwawanahabari wengi.

## 8.0 UWEZO NA UDHAIFU WA VYOMBO VYA HABARI NCHINI TANZANIA

Mwandishi mahiri katika maendelo ya jamii aitwaye Marshall (1964) amebanisha katika kitabu chake kiitwacho *Class, Citizenship and Development* kwamba raia mtimilifu ni yule anayepata habari zilizokamilika za kumwezesha kupata picha kubwa ya hali halisi ya jamii inayomzunguka na ambazo zinamwezesha kufaidi haki zake za kijamii.

Kadhalika, kwa mujibu wa Marshall, raia mtimilifu anapaswa kupata habari za mijadala katika ulingo wa kisiasa na apewe nafasi ya kuchagia mamuzi mbalimbali yanayofikiwa kupitia majadiliano hayo na kwa njia ya uwakilishi.

Mwisho, raia mtimilifu anapaswa kujengewa uwezo wa kuweza kutambua hali yake halisi ya kisiasa kulingana na mazingira yake pamoja na kuwa na uzoefu katika mfumo wa mawasiliano. Swali hapa ni kwa kiasi gani vyombo vya habri vya Tanzania vimefanikiwa kuwawezesha wananchi kupitia habari vinavyozikusanya na kusambaza kuwa na weledi wa kisiasa kama anavyopendekeza Marshall ili kupata haki zao za kiraia na kutimiza wajibu wao wa kijamii. Jambo kubwa linalojitokeza hapa, ni kushindwa kwa vyombo vya habari kuwafikisha habari zake kwa watu wote. Pale ambapo sehemu kuwa ya raia wanapokuwa hawafikiwi na vyombo vya habari, maana yake ni kwamba wanakosa ufahamu ambao ungewawezesha kushirika katika siasa katika mazingira yao na hata katika mchakato wa uchaguzi.

Kwa maana hiyo moja ya udhaifu wa vyombo vya habari nchini Tanzania, ni kutowafikia watu wengi zaidi hasa huko vijijini ambako asilimia 70 ya watanzania wanaishi.

Udhaifu mwingine uko katika maeneo yafuatayo:

i. Mlundikano wa vyombo vya habari pamoja na wanahabari wenyewe kwenye maeneo/majimbo cha uchaguzi ya mijini;
ii. Kuendelea kutumia vigezo vya kizamani katika kuchagua habari. Hii ndiyo inayopelekea kushamiri kwa habari za vituko/uzushi kuliko habari za mambo endelevu yanayowahusu watu katika mazingira yao ya kila siku;

iii. Uchumi duni (uchumi imara hukuza matangazo ya biashara kama chanzo muhimu mapato, kinyume chake vyombo vya habari vinajikuta vinaegemea kwenye uandishi nyenyekevu)
iv. Ukwasi kwa walaji wa vyombo vya habari (watazamaji, wasomaji na wasikilizaji) unaowafanya washindwe kununua mazao ya wanahabari. Mfano halisi ni idadi ndogo ya nakala za magazeti yanayosomwa Tanzania ukilinganisha na Kenya;
v. Ubovu wa miundo mbinu unakwamisha kufikishwa kwa haraka kwa magazeti hadi vijijini na umeme unaokwamisha kusambaa kwa huduma ya matangazo ya televesheni. Hadi sasa ni asilimia 10 ya watanzania wanafikiwa na TV sababu kubwa ikiwa umeme.
vi. Udhaifu wa kitaaluma (wakati idadi ya vyombo vya habari imepanuka weledi wa watendaji wake umeporomoka)
vii. Kushamiri kwa uchujaji wa habari wa kujitakia, sababu kubwa ikiwa ni ushabiki wa kisiasa, woga, sheria kandamizi na rushwa
viii. Mafunzo duni kwa baadhi ya wanahabari na muono wao mbele ya jamii
ix. Ukosefu wa sera iliyowazi kuhusu nafasi ya vyombo vya habari vya umma/serikali katika mazingira ya sasa ya siasa za ushindani
x. Bado sekta ya habari haijaweza kujidhihirisha kwma kweli mi mhimili wa nne katika jamii (kwani bado inayumbishwa na mihimili mingine hasa ule wa dola)
xi. Kuendelea kuwepo kwa sheria kandamizi zinazokinzana na mfumo wa soko huria katika ulingo wa siasa
xii. Ukosefu wa uhuru wa kitaaluma wa wanahabari (editorial independence)
xiii. Kutozingatia maadili ya kitaaluma miongoni mwa wanahabari
xiv. Ukosefu wa mabaraza (Consumer's Councils )ya kutetea haki za walaji wa vyombo vya habari

Ukizingatia mazingira ya kisiasa, kisheria na kijamii ambamo vyombo vya habari vinafanya kazi, ni dhahiri vyombo vya habari vimeonyesha ukomavu na kuwa na mabadiliko endelevu ukilinganisha na mwaka wa uchaguzi wa 2005. Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) linastahili kupongezwa kwa namna ya pekee yake kwa jinsi lilivyoweza kufanya mageuzi makubwa katika mfumo wake wa utangazaji wa mwenendo wa uchaguzi na kuendesha utangazaji wake kwa weledi wa hali ya juu kabisa kwenye uchaguzi wa 2010.

Maeneo ambayo vyombo vya habari vimekuwa na mageuzi makubwa kwa ujumla wao ni kama ifuatavyo:

i. Kuongezeka kwa idadi (sasa kuna vituo vya redio 62, televisheni 28, magazeti ya kila siku 19 na kila wiki zaidi ya 41) hasa ya vituo vya redio hadi mikoani. Nchi zingine kuongezeka kwa vituo vya redio huenda sambamba na uanzishwaji wa magazeti ya vijijini
ii. Kuongezeka wa idadi ya wanahabari kwani angalau karibu katika kila jimbo la uchaguzi kuna wanahabari
iii. Kuongezeka kwa hamu ya kufuatilia, kuandika na kusambaza habari za mchakato wa uchaguzi (rejea ongezeko la habari na vipindi wakati wa uchaguzi)

## 9.0 UZINGATIAJI WA MAADILI YA KITAALUMA

Uandishi wa habari kama ilivyo kwa taaluma nyingine unaongozwa na maadili ambayo ni ndicho kigezo muhimu katika kupima weledi wa watendaji wake. Shirikisho la Wanahabari Duniani (IFJ) limepitisha maadili yafuatayo kwa wanahabari:

i. Kuzingatia ukweli na haki ya umma kujua ukweli wakati wote, ni wajibu wa kwanza wa mwanahabari
ii. Katika kutekeleza wajibu huu, wanahabari wakati wote atalinda na kutetea misingi ya uhuru wa kukusanya, kuandika na kusambaza habari katika misingi ya haki ya kukosoa na kutoa maoni
iii. Kusambaza habari zile tu ambazo mwanahabari anao uhakika kuwa ni za kweli na anajua chanzo chake
iv. Mwanahabari hatafumbia macho au kupindisha ukweli
v. Mwanahabari atatumia njia rasmi/zinazokubalika katika kupata habari, picha na taarifa nyingine
vi. Mwanahabari atafanya kila jitihadi kusahihisha habari ambayo imebainika kuwa si sahihi, potofu na yenye madhara
vii. Mwanahabari atalinda siri ya chanzo cha habari ambayo amepewa kwa kuaminiwa kwa usiri
viii. Mwanahabari atakuwa na tahadhari kuhusu hatari ya ubaguzi kuendelezwa katika vyombo vya habari, na kwamba atafanya kila linalowezekana kuepusha mwendelezo wa ubaguzi wa rangi, jinsia, lugha, dini, siasa na maoni ya mitizamo mingine ya kijamii
ix. Mwanahabari atachukulia kuwa ni ukiukwaji mkubwa kimaadili haya yafuatayo:
   - wizi wa kitaaluma
   - kupindisha ukweli kwa maksudi
   - Kashfa,tuhuma zisizo na ukweli
   - Kupokea rushwa ya aina yo yote ile kwa lengo la kuacha kuchapisha au kuchapisha
x. Atahakikisha kwamba kulingana na sheria za nchi anakoishi na kufanya kazi weledi wa taaluma yake ndicho kigezo muhimu cha utendaji wake wa kazi na siyo maelekezo ya serikali au nguvu nyingine nje ya taaluma yake.

Tathmini ya utendaji wa wanahabari wakati wa mchakato wa uchaguzi wa 2010 imeng'amua ukiukwaji wa maadili kama yalivyoorodeshwa hapo juu. Orodha ya ukiukwa ni ndefu, lakini baadhi ya maeneo ni kama ifuatavyo:

i. Upendeleo wa kisiasa
ii. Kupuuzia/kuzikalia baadhi ya habari kwa maksudi
iii. Kucheza na footage kwenye televisheni ili kupotosha kilichotokea kwenye tukio hasa wingi/uchache wa wat au hata kutumia footage ya tukio moja kuwakilisha jingine (Chanel 10 ilionyesha mara nyingi footage za Unguja kuhusu matukio ya Pemba)
iv. Kushindwa kusahihisha makosa/kuomba radhi
v. Rushwa (pamoja na kupokea bahasha/mshiko)
vi. Uandishi wa kujichuja kutokana na woga na hofu
vii. Kushindwa kutoa nafasi kwa mtuhumiwa kusilizwa/kusahihisha makosa
viii. Kuandika na kutangaza pasipo kusikiliza upande wa pili tena kwa maksudi kabisa
ix. Uongo(deception) kutokana na rushwa au ushabiki
*x.* Kuchochea udini, ubaguzi na ukabila (mathalani, *Maaskofu na Slaa wao wataleta Rwanda (**An Nuur)***
*xi.* Kukiuka sheria mathalani, *CHADEMA kuteka kituo cha redio: kumtangaza Slaa rais **(Sauti Huru)***-rejea sheria ya *Magazeti ya 1976* na ya *Usalama wa taifa ya 1977.*

xii. Kushindwa kutenganisha habari za matukio na maoni binafsi mathalani *Dk. Slaa asichaguliwe, anawadhalilisha wanawake, atakuwaje rais bila wabunge (**Taifa Tanzania)***

xiii. Kukosa umakini kwenye masuala ya jinsia na kudhalilisha wanawake (mathalani Rose Kamili na Josephine Mshumbushi waliandikwa kwenye magazeti kwa nia ya kuwadhalilisha.

xiv.

**9.1 Sababu ya Ukiukwaji wa Maadili kwenye habari za Uchaguzi**

- Udhaifu wa kitaaluma
- Ushabikiwa kisiasa
- Rushwa na vitisho
- Mgongano wa maslahi
- Umaskini wa kipato
- Ukosefu wa dira ya kitaifa
- Udhaifu wa asasi za kiraia katika kulinda uhuru wa habari na kuwatetea wanahabari
- Ukosefu wa Press Councils kwa ajili ya kutetea wananchi dhidi ya vuombo vya habari (press intrusion)

**10.0 HITIMISHO**

Mchango wa vyombo vya habari katika mchakato wa uchaguzi ni wa msingi sana. Vyombo vya habari katika jamii ya kidemokrasia vina majukumu yanayoingiliana lakini yanayoeleweka wazi. Moja ni kutoa habari na kuelimisha. Ili watu waweze kutoa maamuzi ya busara kuhusu sera za umma, wanahitaji habari ambazo ni sahihi, za wakati huo na ambazo hazikupindwa. Na kwa sababu mawazo hutofautiana, watu pia huhitaji kupata maoni tofauti katika masuala mbalimbali na hasa linapokuja suala la uchaguzi wa vyama vingi vya siasa.

Vyombo vya habari pia hutumika kama uwanja wa kuelezea maoni kwa asasi mbalimbali za kiraia kuhusu mchakato wa uchaguzi. Hali kadhalika, vyombo vya habari vinawajibika kuongoza umma kwa kuonyesha vipaumbele vya kitaifa. Vyombo hivi pia vina wajibu wa kuchanguza mwenendo wa serikali na taasisi nyingine zenye nguvu katika jamii ili ziweze kutenda haki na kuwajibika. Kwa minajili hiyo, vyombo vya habari vyapaswa kupewa uhuru wa kutosha kufanya kazi zake. Kwa upande mwingine vyombo hivi vyapaswa kuendeshwa na wanahabari wenye weledi na wanaozingitia maadili ya taaluma yao.

Pamoja mafanikio yaliyoonyeshwa wakati wa mchakato wa uchaguzi wa 2010, bado kuna udhaifu mwingi katika utendaji kutokana na sababu mbalimbali ambazo zimeorodheshwa katika makala hii. Changamoto hapa ni kutoa uhuru zaidi lakini papo hapo kuboresha weledi wa watendaji na kupambana na ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma.

# SURA YA SABA

# USHIRIKI WA WANAWAKE KATIKA UCHAGUZI

## 1.0 UTANGULIZI

Sura hii inahusu ushiriki wa wanawake katika uchaguzi mkuu wa mwaka Kwanza nyenzo za kuimarisha ushiriki wa wanawake katika michakato ya kisiasa, ikiwemo uchaguzi inaainishwa. Pili, ushiriki wa wanawake katika mchakato wa uchaguzi kama wagombea na ushiriki wao katika uandikishaji wa wapiga kura, kampeni na program za elimu ya mpiga kura nazo zinafanyiwa tathmini. Tatu, tunapima mchango wa wadau mbalimbali katika kuboresha ushiriki wa wananwake katika mchakato wa uchaguzi.

## 2.0 NYENZO ZA KITAIFA NA KIMATAIFA

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imedhamiria kwamba wanawake wanafurahia haki zao za kisiasa. Dhamira hii imo katika nyenzo nyingi za kitaifa na kimataifa.

Kwa ngazi ya kitaifa haki ya wanawake kupiga kura imeelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977, Sheria ya mamlaka serikali ya mtaa (Wilaya) ya mwaka 1982, na Sheria ya mamlaka serikali ya mtaa (Mji) ya mwaka 1982, Sheria ya gharama za uchaguzi ya mwaka 2010, na sheria ya vyama vya siasa. Kwa mfano Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania inatoa haki sawa mbele ya sheria bila ubaguzi. Ibara ya 18 inatoa uhuru wa kuongea na Ibara ya 20 inatoa uhuru ya kushirikiana.

Kwa ngazi ya kimataifa, Tanzania imeridhia mikataba mingi ya kimataifa ikiwemo CEDAW (Convention on the Elimination of All Forms of Decrimination Against Women) ya mwaka 1979; Tamko na Jukwaa la Harakati la Beijing, 1995 (Beijing Declaration and Platform for Action, 1995); Protokali ya AU ya Hati ya Haki za Binadamu, 2003; Tamko la Umoja wa Mataifa la Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake; na Tamko la SADC la Jinsia na Maendeleo. Mathalani, Ibara ya 7 ya CEDAW inaeleza kwamba nchi wanachama zinatakiwa kuchukua hatua maalum kuhakisha wanatokomeza aina zote za ubaguzi zinazozuia wanawake kushiriki sawa katika siasa na uongozi wa taifa. Nchi wanachama wanatakiwa kuhakisha wanawake wanapiga kura, wanapigiwa kura katika vyombo vya utawala ikiwemo kutunga na kutekeleza sera. Tanzania inatakiwa kuhakikisha kwamba inatekeleza maazimio haya.

## 3.0 USHIRIKI WA WANAWAKE KAMA WAPIGA KURA

Wanawake Tanzania walipewa haki ya kupiga kura mwaka 1959 na mwaka huo sheria iliwapa wanawake nafasi ya kushiriki kama wagombea (TAWLA, 2010). Tangu uchaguzi wa vyama vingi wa mwaka 1995 kumekuwa na ongezeko la wanawake wanaojiandikisha kupiga kura. Kwa mfano, katika uchaguzi wa mwaka 2005 wanawake walikuwa asimia 51 ya wote waliojiandikisha kupiga kura. Hata hivyo idadi yao ilipungua kidogo katika uchaguzi wa mwaka 2010 kama Jedwali Na. 7.1 hapa chini linavyoonyesha.

**Jedwali Na. 7.1: Walioandikishwa kwa Mchanganuo wa Jinsia**

| Jinsia | 2004-2005 | UBORESHAJI WA DKWK | |
|---|---|---|---|
| | | **2008-2009** | **2009-2010** |
| **Wanaume** | 7,747,371 (49%) | 1,290,594 (62) | 2,206,660 (57%) |
| **Wanawake** | 8,184,377 (51%) | 782,946 (38%) | 1,644,239 (43%) |
| **Jumla** | **15,931,748 (100%)** | **2,073,540 (100%)** | **3,850,899 (100%)** |

Chanzo: *Election Support Project* (ESP, 2010)

## 4.0 USHIRIKI YA WANAWAKE KAMA WAGOMBEA

Katika uchaguzi wa mwaka 2010 wanawake 750 waliteuliwa na NEC kugombea nyadhifa katika ngazi mbalimbali. Kati ya hawa, wanawake 191 waliteuliwa kwa nafasi za ubunge na 559 kwa nafasi za udiwani (kama inavyoonywesha katika Jedwali Na. 7.2). idadi ya wagombea wanawake katika uchaguzi wa mwaka 2010 iliongezeka ikilinganishwa na wagombea 606 mwaka 2005. Kati ya wagombea 8,854 walioteuliwa na Tume kugombea nyadhifa mbalimbali, ni asilimia 6.8 tu ndio walikuwa wananwake ikilinganishwa na asilimia 8.6 mwaka 2010. Hii inaweza kuwa ilichangiwa na juhudi za kuimarisha usawa wa jinsi zilizofaywa na wadau mbalimbali wakiwemo serikali, Azaki, wadau wa maendeleo na vyombo vya habari.

**Jedwali Na. 7.2 Idadi ya Wagombea kwa Chama na Jinsia**

| Chama | Wagombea Urais | | Wagombea Ubunge | | | Wagombea Udiwani | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Me | Ke | Me | Ke | JUMLA | Me | Ke | JUMLA |
| AFP | - | - | 11 | 4 | 15 | 9 | 2 | 11 |
| APPT-MAENDELEO | 1 | - | 9 | 7 | 16 | 19 | 8 | 27 |
| CCM | 1 | - | 215 | 24 | 239 | 3,102 | 223 | 3,325 |
| CHADEMA | 1 | - | 154 | 25 | 179 | 1,786 | 78 | 1,864 |
| CHAUSTA | - | - | 8 | 5 | 13 | 17 | 6 | 23 |
| CUF | 1 | - | 168 | 14 | 182 | 1,510 | 65 | 1,575 |
| DP | - | - | 24 | 11 | 35 | 33 | 8 | 41 |
| JAHAZI ASILIA | - | - | 15 | 6 | 21 | 14 | 12 | 26 |
| MAKINI | - | - | 12 | 5 | 17 | 8 | 5 | 13 |
| NCCR-MAGEUZI | 7 | - | 52 | 15 | 67 | 251 | 29 | 280 |
| NLD | - | - | 15 | 8 | 23 | 26 | 11 | 37 |
| NRA | - | - | 13 | 6 | 19 | 26 | 17 | 43 |
| SAU | - | - | 26 | 6 | 32 | 81 | 16 | 97 |
| TADEA | - | - | 20 | 12 | 32 | 11 | 4 | 15 |
| TLP | 1 | - | 36 | 6 | 42 | 258 | 27 | 285 |
| UDP | - | - | 31 | 14 | 45 | 167 | 21 | 188 |
| UMD | - | - | 13 | 10 | 23 | 25 | 17 | 42 |
| UPDP | 1 | - | 23 | 13 | 36 | 22 | 10 | 32 |
| **JUMLA** | **7** | **-** | **845** | **191** | **1,036** | **7,365** | **559** | **7,924** |

**Source:** NEC, 2010

## 5.0 UTEUZI WA VITI MAALUM KATIKA VYAMA

Wanawake pia walipata fursa ya kushindana miongoni mwao katika nafasi za viti maalum ndani ya vyama vyao. Vyama vilitumia mbinu tofauti kuteua wanawake kugombea nafasi za viti maalum. Baadhi vilitumia mbinu za kidemokrasai na vingine vilitumia mbinu zisizo za kidemokrasia. Kwa kulinganisha, CCM walikuwa na mfumo unaoeleweka uliokuwa wa ushindani, wa wazi, shirikishi na ulioheshimu sheria. Uteuzi wa wanawake kugombea nafasi za viti maalum ndani ya CHADDEMA na CUF uligubikwa na ukiukwaji wa sheria, shutuma na majibizano. Shutuma za rushwa ziliripotiwa ndani ya CCM na CHADEMA. CUF na vyama vingine vidogo havikuweka wazi utaratibu wao wa uteuzi. Ni muhimu kugusia kuwa idadi ya viti maalum vya wanawake bungeni imeongezeka kutoka 75 mwaka 2005 mpaka 102 mwaka 2010 kufuatia mabadiliko ya katiba ambayo yalipandisha uwiano wa viti amaalum kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 40 ya viti vyote vya majimbo.

Ndani ya CCM utaratibu ulikuwa wa wazi, na kura za maoni zilipigwa na wanachama wote. Kila mwanamke aliyetimiza umri wa miaka 21 alikruhusiwa kuchukua fomu za uteuzi na kulipia ada ya uteuzi ya Shilingi 100,000. Upande wa uchaguzi wa madiwani viti maalum, wagombea walipigiwa kura katika kata na majina yao kuthibitishwa na vikao vya wilaya. Hata hivyo kulikuwa na malalamiko katika baadhi ya majimbo. Mathalani huko Sikonge kulikuwa na tuhuma kuwa uteuzi uligubikwa na rushwa na upendeleo.

Katibu wa wilaya wa CCM alieleza kwamba katika jimbo la Kawe mchakato wa uteuzi kwa ajili ya viti maalumu vya uchaguzi wa wabunge ulishughulikiwa na makao makuu ila viti maalumu vya udiwani ulishughulikiwa na CCM UWT ndani ya jimbo na majina yaliwasilishwa NEC (Temeke LTO Report 2010). CCM waliteua wanawake kupitia UWT kwa ngazi ya wilaya kupitia mkutano mkuu na kura za maoni. Chama tayari kilikuwa na wagombea udiwani wa viti maalum (Ripoti ya Mwangalizi wa TEMCO, 2010).

Uteuzi ya viti maalumu vya wanawake CHADEMA ulifanywa na BAWACHA (Baraza la Wanawake Chadema), (Ripoti ya Mwangalizi wa TEMCO wa Temeke, 2010). Wanachama walipiga kura kwa ajili ya mgombea moja kati ya wanawake wote walioomba kuteuliwa (Ripoti ya Mwangalizi wa TEMCO wa Kawe, 2010). Kwenye jimbo la uchaguzi la Iringa orodha ya viti maalum ya CHADEMA ilikuwa siri kwa sababu ya madai ya rushwa (Iringa TEMCO LTO Report, 2010). Katika jimbo la Njombe wanawake hawakujitokeza kuomba viti maalumu vya udiwani, kwa hiyo vyama kama CHADEMA vilitumia mfumo ya uteuzi kutoka ngazi za juu (Njombe TEMCO LTO Report 2010)

CUF ilikuwa na utaratibu ufuatao kwa ajili ya uteuzi wa viti maalumu; wanachama (wanawake) walichukua fomu kugombea uchaguzi wa wabunge ndani ya chama. Wanachama walikuwa na jukumu la kupiga kura na hatimaye walimchagua mgombea mmoja. Utaratibu huo pia ulitumika kupata wagombea wa viti maalumu ndani ya chama. Kwa ajili ya viti maalumu, wanachama waliwajibika kwa mchakato mzima (Temeke TEMCO LTO ripoti 2010). CUF walikuwa na mkutano mkuu pia kwa ngazi ya kata na walipiga kura kwa wagombea na aliyepata kura zaidi ndio alichaguliwa (Kawe TEMCO LTO ripoti, 2010). Hata hivyo kulikuwa na matukio machache ya ukikwaji wa taratibu wakati wa uteuzi wa wanawake kugombea nyadhifa mbalimbali. Upande wa vyama vidogo, hakukuwa na utaratibu wa wazi uliojulikana na watu wote.

Baadhi ya wagombea wa nyadhifa mbalimbali kupitia viti maalum hawakuridhishwa na mchakato wa uteuzi ndani ya vyama vyao na waliamua kuhamia vyama vingine. Mathalani, katika jimbo la uchaguzi la Mufindi, mmoja wa wagombea wa viti maalum kupitia NCCR-Mageuzi alihamia CHADEAM (Iringa TEMCO LTO ripoti 2010).

## 6.0 USHIRIKI WA WANAWAKE KATIKA KAMPENI

Wanawake walishiriki katika kampeni kwa namna tofauti kulingana na uzito wa nafasi yenyewe, na kama mhusika alikuwa mgombea au la. Wanawake walishiriki kama wagombea, wanachama wa vyama vya siasa, watoaji wa elimu ya mpiga kura na kama wahudhuriaji wa mikutano ya hadhara.

Baadhi ya washiriki wagombea waliamua kujifanyia kampeni kwa kutumia mbinu mbalimbali. Mathalani katika Manispaa ya Ilala, Naomi Kaihula wa CHADEMA aligombea ubunge. Ingawa hakushinda uchaguzi, baadaye aliteuliwa kupitia viti maalum. Wagombea

wengine wanawake kama Jennifsta Mhagama wa CCM alitetea kiti chake. Baadhi ya wanawake walipania kuwaunga mkono wagombea wanawake hata baada ya uchaguzi.

Isitoshe, Mke wa Rais, Slma Kikwete aliifanyia CCM kampeni hasa mgombea urais. Mbinu hii ya kampeni ilihpingwa na vyama vingine kama mgombea urais wa CHADEMA aliyedai kuwa Mke wa rais alikuwa akitumia rasilimali za taifa kupigia kampeni chama. Tuhuma hizi zilijbiwa na meneja wa kampeni za urais za CCM. Mgombea urais wa CHDEMA pia alipigiwa kampeni na wanawake, mathalani mwenza wake wa zamani Rose Kamili na mwenza wa sasa, Josephine Mushumbushi. Mke wa mgombea mwenza wa urais kwa tiketi ya CCM pia alionekana akifanya kampeni katika mkutano wa kampeni huko Ludewa.

Wanawake waliwahimiza wenzao kugombea kama alivyofanya mgombea ubunge katika jimbo la Ukerewe, Bi Getrude Mongela. Ndani ya BAWACHA, wagombea wanawake walikuwa wakihimizwa kugombea pamoja na wanaume. Viongozi wa jumuiya za wanawake pia walifanya jitihada kubwa kuhakikisha vyama vyao vinashinda. Kwa ujumla wanawake walichangamsha sana na kutia hamasa katika mikutano ya kampeni.

## 7.0 ELIMU YA KURA KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE

Elimu ya mpiga kura kwa vikundi vya wanawake ilitolewa na asasasi mbalimbali. Tume ya Uchaguzi ilijitahidi kutoa elimu kwa wapiga kura wanawake kupitia mfulizlizo wa semina na makongamano na vikundi vya akina mama. Wanawake nchi nzima kutoka vyama tofauti walialikwa kushiriki katika mihadhara hii. Asasi za kiraia zinazopigania haki za wanawake pia zilishiriki mihadhara hii.

Mashirika ya kimataifa kama UNDP kupitia Mradi wake wa Kusaidia Uchaguzi (ESP) walishiriki kikamilifu katika kutoa elimu ya mpiga kura kwa vikundi vya wanawake. Msaada wa kiufundi na kifedha ulitolewa na UNDP kwa mashirika kama vile UNIFEM. UNDP ilitoa fedha kwa asasi kadhaa za kiraia ili zitoe elimu ya uraia na upigaji kura nchini kote.UNIFEM ilitoa mafunzo kwa wanawake wanaogombea bila kujali itikadi ya chama ili kuongeza uelewa wa wanawake kuhusu masuala ya elimu ya uraia na upigaji kura. Sehemu ya mafunzo ilihusu sheria ya uchaguzi. Pia kupitia UNDP, jumla ya watangazaji 125 wa redio za jamii walipata mafunzo na seti 1,500 za redio zilitolewa kwa vikundi mbalimbali wakiwemo wafugaji wanaohamahama (ESP, 2010).

Nafasi ya asasi za kiraia katika suala la uchaguzi kuhusiana na wanawake ilijumuisha ushawishi na utetezi wa watu wanyonge kushiriki katika uchaguzi, kuelimisha umma ili kuongeza ushiriki, kuhamasisha usawa na uelewa wa masuala ya haki, kuboresha utekelezaji wa MDG 3 na kuhamasisha masuala ya uwazi na utawala bora kwa upande wa serikali katika kutimiza ahadi kwa wananchi, na elimu ya uraia na upigaji kura.

Mtandao ya wanawake na mashirika ya wanawake pia walishiriki katika kuelimisha umma kuhusu elimu ya uraia na utawala bora. Kwa msaada wa UNIFEM, TAWLA walifundisha wanawake 350 kuhusu nafasi yao katika uchaguzi katika mkoa saba ikiwemo Zanzibar. Mashirika ya wanawake kama TGNP, TAMWA, TAWLA na mashirika mengine ya kiraia kama LHRC, Haki Elimu walisaidiwa na wafadhili/washirika wa maendeleo kutoa elimu ya uraia na upigaji kura kwa umma. TAMWA na Haki Elimu walitumia vyombo vya habari kuelimisha umma kuhusu uchaguzi wa mwaka 2010. TAMWA walitengeneza matangazo kwenye TV kuonyesha sifa za kiongozi bora na kuwaonyesha wanawake kuwa wao pia ni viongozi mahiri.

## 8.0 UUNGAJI MKONO WAGOMBEA WANAWAKE

Maandalizi na uhamasishaji ya wagombea wanawake yalifanywa na waadau wengi wakiwemo NEC, vyama vya siasa, UNDP/ESP, UNIFEM, TCD, asasi za kiraia kama TAWLA, TGNP, TAMWA na LHRC.

Vyama vya siasa waliandaa wagombea wao wanawake kwa kuwaharifu kuhusu fursa za kushikiri katika uchaguzi kama wagombea na wapiga kura. Hii ilishuhudiwa hasa katika vyama vya CHADEMA na CCM .Vyama vingine kama CUF, NCCR MAGUEZI na TLP walijitahidi kuandaa wagombea wao kwa kiasi fulani. Kwa baadhi ya vyama kama SAU, TADEA, UMD na JAHAZI ilionekana hawakufanya maandalizi na uhamasihaji wa kutosha kwa wagombea wao. Katika vyama hasa vyenye jumuiya za wanawake, wagombea wanawake walipewa nafasi ya kushindana na wanaume katika uteuzi na pia walikuwa na nafasi ya kugombea viti maalumu vya ubunge na udiwani. Kwa CCM wagombea wa viti maalum vya wanawake ambao walishindwa kwenye ngazi ya ubunge walipewa nafasi katika viti maalum vya udiwani.Wanawake katika vyama ambavyo vilifanya mikutano ya hadhara walisaidiwa na ofisi za matawi ya chama na timu za kampeni kuandaa kampeni. Vyama pia walisaidia wagombea wao wote wakiwamo wanawake kwa kuweka wakala wa chama katika vituo vya kupigia kura. Kwa asilimia kubwa, CCM, CHADEMA na wakati mwingine NCCR MAGEUZI na CUF ndo walikuwa na mawakala wa chama.

Kwa upande wa NEC maandalizi ya wagombea wanawake na wagombea kwa ujumla yalijumuisha kutoa taarifa kuhusu mchakato wa uchaguzi, kuendesha warsha na semina kwa wanawake na mitandao ya wanawake.NEC iliandaa na kusambaza machapisho kuhusu mchakato ya uchaguzi kuwezesha wagombea wote kushiriki katika uchaguzi bila kupata matatizo. Vitini vya NEC vilikuwa; Madili ya uchaguzi, Sheria ya gharama ya uchaguzi na sheria nyingine na utaratibu ya siku ya uchaguzi.

UNDP/ESP walisaidia katika shughuli kadhaa za uchaguzi zilizohuasiana na wanawake na uchaguzi mkuu wa mwaka 2010. Msaada huu ulikuwa kwa njia ya kutoa msaada ya kitaalumu, kujenga uwezo kupitia semina na warsha. UNIFEM ilitoa mafunzo kwa wanawake wagombea kuhusu namna ya kuongea mbele ya umma, sheria ya uchaguzi na namna ya kupata rasilimali fedha.UNIFEM pia waligawa vifaa kama vitini vya kufundisha, fulana, khanga na redio. Vifaa kama redio viliwezesha vikundi vya wanawake kupata taarifa kuhusu uchaguzi kupitia vyombo vya habari. Fulana na khanga pia zilitumika kupeleka ujumbe kwamba wanawake wanaweza kuwa viongozi bora.

Asasi za kiraia kama TAWLA na TGNP walielimisha umma na wanawake wenzao kuhusu nafasi ya mwanamke katika uchaguzi kwa msaada wa UNIFEM. TGNP walitumia nafasi vyema kwa kufundisha viongozi katika jamii wakati TAWLA walifundisha vikundi vya wanawake, asasi za kiraia na mtandao wa wanawake kuhusu nafasi ya mwanamke katika uchaguzi. TAWLA iliandaa chapisho la mafunzo kuhusu nafasi ya wanawake katika uchaguzi na yaliyokuwemo ndani ya chapisho hilo ni; maana ya asasi ya kiraia,nafasi ya asasi ya kiraia kuwezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika uchaguzi, wanawake na uchaguzi, changamoto na namna ya kukabiliana nazo, wanawake wanaweza, na haki ya wanawake kushiriki katika uchaguzi.TGNP pia waliandaa chapisho kwa ajili ya kufundisha viongozi katika jamii kwa kuzingatia nafasi ya wanawake na masuala ya kijinsia.

Asasi nyingine za kiraia pia zilishiriki kikamilifu katika kuandaa na kuhamasisha wanawake wagombea kwa njia mbali mbali. TAMWA na HakiElimu walitumia vyombo ya habari kama TV na redio kutangaza sifa za kiongozi na wagombea wazuri ikiwemo wanawake. Vipindi vya umma vya TAMWA na HakiElimu kwenye vyombo vya habari vilitetea haki ya wanawake kama viongozi na wagombea. Mtandao kama FEMACT waliamua kuwa na ilani ya kijinsia ya 2010 kudai masuala kadhaa kama haki ya wanawake kushiriki kama wagombea na kuwezeshwa na serikali na vyama vya siasa.

Kituo cha demokrasia Tanzania ( TCD) walishiriki kwa kuendesha warsha kwa ajili ya vyama vya siasa na baadhi ya washiriki walikuwa wanawake wagombea.TCD pia ilishirikiana na asasi za kiraia kama TAWLA kuendesha vipindi kwenye redio kuhusu masuala ya uchaguzi, nafasi ya wanawake na vyama vya siasa. Vipindi vyao vya warsha viliwezesha vyama vya siasa kuwa na mjadala ya uwazi kuhusu ushiriki wa wanawake katika mchakato ya uchaguzi.

## 9.0 MATOKEO YA UCHAGUZI KWA WANAWAKE: WASHINDI NA WALIOSHINDWA

Kwa ujumla wanawake 21 walichaguliwa kuwa wabunge moja kwa moja majimboni kati yao watatu walipita bila kupingwa katika majimbo ya Njombe Kusini, Muleba Kusini, na Ulanga Mshariki. Wabunge hawa ni Mh. Anne Makinda, Mh. Prof. Anna Tibaijuka na Mh. Celina Kombani. Pia, wanawake 102 waliingia bungeni kupitia viti maalum. Rais pia aliteua mbunge mmoja mwanamke kwa mujibu wa mamlaka aliyonayo. Baraza la Wawakilishi Zanzibar liliteua wanawake wawili kuwa wabunge. Pamoja na ongezeko la wanawake walioingia bungeni kupitia majimboni kuongezeka, wao ni asilimia 9 tu ya wabunge wote wa kuchaguliwa. Kwa sasa bunge la Jamhueri lina jumla ya wabunge 350 kati yao 126 (asimia 36) ni wanawake.

**Jedwali Na 7.3: Idadi ya Wanawake katika Bunge**

| Chama | Idadi ya Viti | wanawake | Viti maalum | Jumla ya viti maalum |
|---|---|---|---|---|
| CCM | 186 | 19 | 67 | 86 |
| CHADEMA | 23 | 2 | 25 | 27 |
| CUF | 24 | - | 10 | 10 |
| NCCR-M | 4 | - | 0 | - |
| TLP | 1 | - | 0 | - |
| UDP | 1 | - | 0 | - |
| **Jumla** | **239** | **21** | **102** | **123** |

Chanzo: NEC, 2010

Pamoja na jitihada zote za wanawake kushiriki katika uchaguzi kuna changamoto ambazo walikutana nazo katika ushiriki wao. Wanawake kama wagombea na wapiga kura walioshiriki katika mchakato wa uchaguzi walikutana na changamoto za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kulikuwa na matukio ya ubaguzi ya kijinsia, ukakili ya kijinsia na vitendo hasi wakati wa uchaguzi. Mwanamke mgombea Kigamboni aliambiwa kwamba hawezi kuwa kongozi kwa sababu amezaa watoto na wanaume tofauti (Kigamboni TEMCO LTO ripoti 2010). Kiwango kidogo cha elimu ya wanawake ukilinganisha na wanaume ilikuwa changamoto (TAWLA  2010). Baadhi ya wanaume waliwakataza wake zao kushiriki katika siasa kwa sababu tu ya hisia za kimapokezi (TAWLA  2010).

Kulikuwa na vikwazo vingine ambavyo vimekuwa vikijitokeza katika chaguzi zilizopita na vilijitokeza katika ucvhaguzi wa mwaka 2010. Baadhi ya vikwazo hivi ilikuwa ni pamoja na wanawake wagombea kukosa idadi ya kutosha ya waungaji mkono, kukosa uungwaji mkono wa vyombo vya habari, kukosa mafunzo ya uongozi, mifumo ya uchaguzi na taratibu ambazo hazizingatii jinsia. (TAWLA, 2010). Vyama vya siasa walikosa mkakati ya kuhakikisha wanawake wanashinda (TAWLA, 2010).  Muonekano hasi wa wanawake hutokea pale ambapo kampeni za uchaguzi hujikita katika kuangalia mambo binafzi badala ya kuangalia misingi ya chama. Hii ilijionyesha wakati wa kampeni za urais kupitia CHADEMA ambapo vyombo vya habari vilijikita katika masuala binafsi ya mgombea urais pale ambapo Roser Kamili na Josephine Mushumbushi walipokuwa wakiripotiwa kwa mtazamo hasi kwa sababu ya uhusiano wao na mgombea urais wa CHADEMA wakati jamii na waandishi wa habari hawafanyi hivyo kwa wanaume.

Mambo tuliyojifunza katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 ni kwamba wanawake wanaweza kushiriki kikamilifu wakijihamasisha wenyewe na wakiwa na mazingira mazuri ndani ya vyama.

Elimu ya uraia na elimu ya mpiga kura inajumuisha kueleza kwa kina nafasi ya wanawake na haki yao kushiriki katika uchaguzi ili kubadilisha maoni katika baadhi ya sehemu ambazo mfume dume umekithiri. Mchakato ya elimu ya uraia na elimu ya mpiga kura vinatakiwa

kufanyika kwa muendelezo na siyo wakati  wa uchaguzi tu na hii itasababisha watu wengi sana katika jamii kujua haki ya wanawake kushiriki katika uchaguzi.

## 10.0 HITIMISHO

Kwa ujumla ushiriki wa wanawake katika uchaguzi wa mwaka 2010 ulikuwa mzuri katika mchakato mzima wa uchaguzi na hasa kama wapiga kura na washriki wa mikutano ya hadhara. Idadi ya wabunge wanawake imeongeza kiasi kikubwa kupitia mpango wa viti maalum. Hii inaweza kuwa imechangiwa na juhudi za wadau mbalimbali wakiwemo serikali, azaki, vyombo vya habari na washirika wa maendeleo. Hata hiyo, ikilinganishwa na wanaume, wanwake wachache sana walijiotokeza kama wagombea katika nyadhifa zote za kuchaguliwa.

## SURA YA NANE

## KUPIGA KURA, KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO

### 1.0 UTANGULIZI

Tarehe 31 Oktoba 2010 Watanzania walipiga kura katika uchaguzi mkuu wa nne baada ya kuanzishwa tena mfumo wa vyama vingi nchini mwaka 1992. Chaguzi tatu zilizotangulia zilifanyika 1995, 2000 na 2005. Siku ya kupiga kura ni siku ya mavuno inayowasisimua wadau wote: vyama, wagombea, wapiga kura, wakereketwa na wengineo. Vyama vyote 18 vilivyosajiliwa vilishiriki katika uchaguzi huu kwa viwango vinavyolingana na uwezo wao.

Tanzania Bara ilikuwa na chaguzi tatu zilizofanyika pamoja: uchaguzi wa rais wa muungano; uchaguzi wa wabunge, na uchaguzi wa madiwani. Wapiga kura wa Zanzibar wao walikabiliwa na chaguzi tano zilizofanyika kwa pamoja: uchaguzi wa rais wa muungano; uchaguzi wa rais wa Zanzibar; uchaguzi wa wabunge; uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, na uchaguzi wa madiwani. Walisimama wagombea urais saba: Peter Mziray Kuga wa APPT, Jakaya Mrisho Kikwete wa CCM, Dkt. Willibrod Peter Slaa wa CHADEMA, Prof. Ibrahim Haruna Lipumba wa CUF, Hashimu Rungwe wa NCCR-Mageuzi, Mutamwega Mugahywa wa TLP, na Yahmi Dovutwa Dovutwa wa UPDP.

Kwa sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa vifaa vya kupigia kura, uchaguzi haukuweza kufanyika katika majimbo kadhaa tarehe 31 oktoba 2010; haya yalipangiwa kufanya uchaguzi tarehe 14 novemba 2010. Hali kadhalika, uchaguzi katika kata 23 ulisogezwa hadi tarehe 28 Novemba 2010. Sura hii inahusu chaguzi za ngazi ya muungano, yaani uchaguzi wa Rais wa Muungano na wa Wabunge ambazo zilifanyika Bara na Visiwani, na uchaguzi wa madiwani wa Bara. Chaguzi za Rais wa Zanzibar, Wawakilishi na madiwani wa Zanzibar zimeandikwa katika ripoti maalum ya Zanzibar. Kuhusu chaguzi hizi za ngazi ya Muungano na Bara mwezi Septemba 2010 TEMCO iliweka waangalizi wa muda mrefu katika majimbo 223 kati ya majimbo 239 (93.3%), 173 wakiwa Bara na 50 Visiwani. Kisha TEMCO ikaweka waangalizi wa muda mfupi 7,367 kuangalia michakato ya upigaji kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo, 6,667 wakiwa Bara na 700 Visiwani.

Kwa sababu mbalimbali, waangalizi 120 wa muda mfupi waliokwisha pata mafunzo hawakuweza kuhudhuria katika vituo vyao vya kupigia na kuhesabu kura siku ya uchaguzi. Kwa hiyo TEMCO ikaviangalia vituo 7,247 kati ya 7,367 vilivyotarajiwa (98.37%). Jumla ya vituo vyote nchini vilikuwa 53,023, vituo 51,732 vikiwa Bara na 1,291 Visiwani. Kwa hiyo vituo 7,247 vilivyoangaliwa na TEMCO ni sawa na asilimia 13.67 ya vituo vyote nchini, ambavyo ni toshelevu.

Katika sehemu ya pili inayofuatia utangulizi huu, tutauzungumzia mchakato wa upigaji kura. Hii itafuatiwa na sehemu ya tatu itakayozungumzia michakato ya kuhesabu kura, kujumlisha kura na kutangaza matokeo. Matokeo yatahusu yale ya kura za urais, za ubunge na udiwani Tanzania Bara.

## 2.0 MCHAKATO WA KUPIGA KURA

### 2.1 Ufunguzi na Mazingira ya Vituo

Vituo vilitakiwa kufunguliwa rasmi saa moja asubuhi na kufungwa saa kumi jioni, yaani kulikuwepo jumla ya saa tisa za shughuli za kupiga kura. Kwa kuwa watu wapatao milioni 20 waliandikishwa nchi nzima na vilikuwepo vituo 53,023, kwa wastani kila kituo kingeshughulikia watu 377 katika muda huo wa saa tisa, au wapiga kura 42 kwa saa. Kama wangeshiriki wapiga kura wote waliojiandikisha, ingekuwa ni kazi kubwa tukizingatia vitu mbalimbali vinavyochelewesha upigaji kura katika chaguzi za Tanzania. Lakini kama tutakavyoona baadaye, mwitikio wa wapga kura ulikuwa wa chini kuwahi kushuhudiwa katika historia ya uchaguzi Tanzania.

Asilimia 96 ya vituo vilivyoangaliwa vilifunguliwa katika muda wake na asilimia 4 vilichelewa. Sababu za kuchelewa kufunguliwa ni pamoja na ucheleweshaji wa vifaa vya kupigia kura, maafisa wa uchaguzi kuchelewesha maandalizi, matukio yasiyotarajiwa kama mvua, kuhamishia kituo mahali pengine, n.k.

Kati ya vituo 260 vilivyochelewa kufunguliwa, 57 vilikabiliana na hasira ya wapiga kura, baadhi yao wakiamua kurudi nyumbani bila kupiga kura ili kuendelea na shughuli zao za kawaida, na wengine wakidai kwamba muda wa kufunga kituo uongezwe kulipizia muda uliopotea. Katika vituo 11 vyenye madai hayo muda uliongezwa kama wapiga kura walivyodai.

Sheria ya uchaguzi inataka eneo lote linalokizunguka kituo cha kupigia/kuhesabia kura liwe shwari, bila kuwepo watu wanaopiga kampeni au kubembeleza kura kwa namna yoyote, na bila kuwa na kitu chochote kinachowaogofya wapiga kura. Ubembelezaji kura ulionekana katika vituo 443 (asilimia 6.4) tu, ikilinganishwa na vituo 6,459 (asilimia 93.6) ambamo sheria ilizingatiwa. Katika asilimia 5.2 ya vituo, vitambulishi vya vyama kama fulana (T-shirt), bendera, picha za wagombea na kanga za vyama vilionekana. Vitu hivi navyo vimekatazwa na sheria kwa sababu vimekusudiwa kuwashawishi wapiga kura.

Vitu vinavyoogofya wapiga kura vilionekana katika vituo 165 tu (asilimia 2.3). Mifano ya vitu hivyo ni uwepo mkubwa wa askari (polisi, jeshi na wengineo), na fujo zilizotokana na mashabiki wa vyama. Fujo hizi hazikuwa nyingi katika uchaguzi huu, zilionekana zaidi katika sehemu zenye ushindani mkali, hasa kati ya CCM na CHADEMA Tanzania Bara . Sehemu hizo ni pamoja na majimbo mengi ya Mikoa ya Dar es salaam, Shinyanga, Arusha na Kigoma, na katika majimbo mengi ya mjini, kwa mfano, Moshi Mjini, Kigoma Mjini, na majimbo ya Nyamagana na Ilemela katika Jiji la Mwanza. Fujo zilizoweza kufanya uchaguzi usitishwe kwa muda zilionekana katika asilimia 6 tu ya vituo vilivyoangaliwa na TEMCO; na ni katika asilimia moja tu kulikokuwepo matukio yaliyoogofya kiasi cha kuwafanya baadhi ya wapiga kura kuondoka kituoni kabla ya kupiga kura zao.

## 2.2 Utoshelevu wa Watumishi na Vifaa Vituoni

Sheria ya uchaguzi inaagiza kwamba orodha ya wapiga kura ibandikwe vituoni wiki moja kabla ya siku ya uchaguzi. Katika vituo vingi vilivyoangaliwa na TEMCO orodha ya wapiga kura ilibandikwa jumamosi tarehe 23 Oktoba 2010. Kwa mara ya kwanza, Zanzibar nayo ilifanya hivyo, ambavyo huko nyuma haikuwa na kipengele hicho cha sheria. Kwa hiyo wapiga kura walikuwa na wiki nzima ya kukagua orodha ya vituo vyao kuona kama majina yao yalikuwepo bila hitilafu, na kuchukua hatua zinazopasa kuhakikisha hitilafu zinaondolewa kabla ya siku ya uchaguzi. Karibu robo tatu nzima (74.8%) za orodha zilizobandikwa vituoni hazikuwa na hitilafu. Katika vituo vilivyobaki, asililimia 24.8 vilikuwa na orodha yenye hitilafu, na asilimia 0.4 (vituo 28) havikubandika orodha kabisa.

Kwa hiyo matatizo yalionekana katika asilimia 25.2 ya vituo vilivyoangaliwa na TEMCO ambavyo baadhi yao havikubandika orodha vituoni kwa mujibu wa sheria (0.4%) na vile vilivyobandika orodha zenye hitilafu (24.8%). Matatizo yaliyojitokeza ni pamoja na yafuatayo:

- Katika asilimia 8.1 ya vituo vilivyoangaliwa, baadhi ya wapiga kura hawakuyakuta majina yao katika orodha.
- Katika asilimia 0.1 ya vituo (vituo vinne), orodha zilizokutwa kituoni zilikuwa za vituo vingine.
- Katika asilimia 3 ya vituo, baadhi ya majina ya wapiga kura yalikosewa au yalikuwa tofauti na yaliyo kwenye kadi ya mpiga kura; na
- Katika asilimia 5.1 ya vituo kulikuwako matatizo mengine ya kumtambua mpiga kura ambayo yalichukua muda wa maafisa wa uchaguzi kuyashughulikia.

Tatizo la kubandika orodha zenye hitilafu vituoni si geni katika chaguzi za Tanzania; limejitokeza katika chaguzi kuu zote zilizotangulia chini ya mfumo wa vyama vingi (1995 ,2000 na 2005). Kuendelea kwa tatizo hili wakati ambapo tume zetu mbili zinapewa fedha na teknolojia ya kutosha kuliondoa kumezua mjadala, hasa miongoni mwa vyama vya upinzani, kwamba inawezekana kukawa na mbinu za kisiasa katika matatizo haya yanayoonekana kama ni ya kimenejimenti. Matatizo ya namna hii yamepelekea wapinzani kulalamika kwamba NEC ina upendeleo, malalamiko yaliyovumishwa zaidi katika uchaguzi mkuu wa 2010 kuliko katika chaguzi za huko nyuma.

Waangalizi wa TEMCO walielekezwa kutathmini utoshelevu wa vifaa vya kupigia kura katika vituo vyao. Katika asilimia 85 ya vituo karatasi za kupigia kura zilikuwepo za kutosha na hazikuwa na hitilafu yoyote. Katika asilimia 15 ya vituo, karatasi hizo ama hazikutosha au zilikuwa na hitilafu mbalimbali. Hitilafu zilikuwa pamoja na zifuatazo: picha za wagombea zlizofifia,picha zisizo na majina ya wagombea; picha zenye majina yaliyofifia ,na picha zenye majina yaliyokosewa au majina ya watu wengine. Vifaa vingine vilikosekana vituoni au vilipungua au kuwa na hitilafu kama ifutavyo:

- Muhuri wa kituo — asilimia 0.6 ya vituo
- Wino — asilimia 0.6 ya vituo
- Fomu aina mbalimbali — asilimia 7.7 ya vituo
- Vifaa vinginevyo — asilimia 7.3 ya vituo

Kuhusu watumishi wa vituo, kila kituo kilikuwa na maafisa wanne: afisa msimamizi wa kituo, wasaidizi wa upigaji kura wawili, na karani wa kuwaongoza wapiga kura. Hawa walipewa mafunzo siku mbili au tatu kabla ya siku ya kupiga kura. Hawa walitosheleza katika vituo ambavyo vilikuwa na orodha ya wapiga kura isiyo na hitilafu na ambako hapakuwa na wapiga kura wengi waliohitaji msaada maalum (k.m. walemavu, wasioweza kusoma, n.k.); lakini walipelea katika vituo ambavyo watu wengi walihitaji msaada.

## 2.3 Fursa ya Wananchi Kupiga Kura

Vitu vinavyoweza kumpunguzia mwananchi fursa ya kupiga kura ni pamoja na vifuatavyo: umbali wa vituo, menejimenti mbovu ya orodha ya wapiga kura, na ushirikiano mdogo wa maafisa wa uchaguzi katika kutatua matatizo ya wapiga kura. Taarifa za wangalizi wa TEMCO hazisemi umbali wa kituo ulikuwa tatizo kubwa la kuweza kuwazuia watu wasiende kupiga kura. Kama tulivyoona, menejimenti mbovu ya orodha ya wapiga kura ilionekana katika robo nzima ya vituo vlivyoangaliwa, na hii ingeweza kuwanyima fursa ya kupiga kura baadhi ya hao ambao majina yao hayakuonekana katika orodha, na pia kuwapunguzia wananchi imani katika mfumo wetu wa uchaguzi. Je, maafisa wa uchaguzi walitoa ushirikiano kiasi gani ili kuwawezesha watu kupiga kura?

Kundi la kwanza la watu waliohitaji msaada maalum ni lile la watu wenye ulemavu, wagonjwa, wazee, wasioweza kusoma, n.k. Watu hawa walisaidiwa bila kuwepo malalamiko?

- Katika asilimia 88.2 ya vituo vilivyoangaliwa na TEMCO, watu kama hao walisaidiwa bila kuwa na malalamiko yo yote.
- Katika asilimia 11.05 ya vituo, watu kama hao walisaidiwa, lakini bado kulikuwapo malalamiko.
- Katika asilimia pungufu ya moja (vituo 6 tu ) watu kama hao hawakusaidiwa kabisa.

Malalamiko yalikuwa ya aina tatu. Lalamiko la kwanza lilitolewa na baadhi ya wenye ulemavu na wasioweza kusoma na kuandika ambao walidai kwamba wale waliowasaidia hawakuwachagua kwa ridhaa yao. Pili, walilalamika kwamba waliowasaidia kupiga kura waliwashawishi au kuwaongoza kumpigia mgombea asiye chaguo lao. Tatu, baadhi ya wapiga kura waliokuwa katika foleni (katika maeneo yenye watu wengi wanaohitaji kusaidiwa) walilalamika kwamba kusaidia na kuwapa kipaumbele wasiojiweza kuliwachelewesha kupiga kura. Malalamiko haya yanahitaji ufafanuzi. Kwanza, wengi wa wale waliolalamika kuwa kuwasaidia wenye ulemavu na wasioweza kusoma kulipindisha chaguo la yule aliyesaidiwa walikuwa mawakala wa vyama ambao waliwaonea wivu wale waliopata nafasi hiyo. Kwa hiyo malalamiko hayo hayana uzito sana. Pili, hao wapiga kura waliolalamikia msaasa uliotolewa kwa waliohitaji walikuwa wachache kulinganisha na waliolifurahia. Wengi walizingatia agizo la NEC/ZEC kwamba wasiojiweza, wazee, wajawazito, na watu waliowabeba watoto wadogo wapewe kipaumbele katika kupiga kura.

Kundi jingine lililohitaji kusikilizwa na kusaidiwa ni lile la watu waliopoteza kadi zao za kujitambulisha kama mpiga kura na wale ambao kadi zao zilikuwa zimeharibika. Watu hao

walijaribu kujieleza kadri walivyoweza ili waruhusiwe kupiga kura. Watu wenye tatizo hili walionekana katika asilimia 18.1 ya vituo vilivyoangaliwa na TEMCO. Katika asilimia 4.4 ya vituo hivyo, watu hao wote waliruhusiwa kupiga kura; katika asilimia 2 ya vituo baadhi yao waliruhusiwa kupiga kura; na katika asilimia 11.7 ya vituo hivyo watu kama hao wote walinyimwa fursa ya kupiga kura. Haieleweki sawasawa kiasi cha mamlaka aliyo nayo msimamizi wa kituo katika maamuzi ya mambo kama haya, lakini inatakiwa mawakala wa vyama wawe makini ili asiyatumie mamlaka yake vibaya.

Matukio yanayousitisha upigaji kura yanaweza pia kumvuruga mpiga kura. Katika asilimia 2.8 ya vituo, mchakato wa uchaguzi ulisitishwa kwa muda wa saa moja hadi tisa. Sababu za kusitishwa huko zilikuwa pamoja na fujo za wakereketwa wa vyama katika vituo au maeneo yanayopakana na vituo, upungufu wa vifaa vya kupigia kura,mvua za ghafla,na matukio mengineyo. Hakuna sababu za kisiasa zilizohusishwa na usitishwaji wa kupiga kura.

## 3.0 MCHAKATO WA KUHESABU KURA

Kuhesabu kura ni wajibu wa msimamizi wa kituo na wasaidizi wake watatu, huku watu walioruhusiwa kisheria kuwa kituoni (ikiwa ni pamoja na mawakala wa vyama na wagombea) wakiufuatilia mchakato huo kwa makini. Malalamiko ya kuwepo watu wasioruhusiwa kisheria yalisikika kwenye asilimia 2 tu ya vituo 7,247 vilivyoangaliwa na TEMCO. Sheria inataka kura zihesabiwe palepale kura zilipopigiwa, labda ziwepo sababu nzuri za kuhamia mahali pengine.

Katika asilimia 95.5 ya vituo vilivyoangaliwa, kura zilihesabiwa palepale zilipopigiwa; na asilimia 4.5 vilipaswa kuhama. Vituo vipya vilikuwa mahali panapokubalika kisheria: majengo ya shule, ofisi za serikali, vituo vya jamii, vituo vya polisi, n.k. Nyumba za watu binafsi, ofisi za vyama vya siasa na nyumba za ibada haziruhusiwi kuwa vituo vya kupigia au kuhesabia kura. Sababu mbili kuu za kuhamisha vituo zilikuwa usalama na mwanga kwa sababu sehemu ya muda wa kuhesabu kura ilikuwa usiku. Kote vituo vilikohama mawakala wa vyama waliruhusiwa kulifuata kwa karibu gari lililobeba masanduku ya kura kuhakikisha usalama wa masanduku hayo.

Kuhesabu kura kunaweza kurudiwa pale wagombea wamelingana katika idadi ya kura walizopata, au kura zimekaribiana sana, au mgombea mwenye shaka anapoomba kura zihesabiwe upya. Marudio ya kuhesabu yalionekana katika asilimia 10.5 ya vituo vya kuhesabu kura vilivyoangaliwa; asilimia 3.4 vikirudia mara moja, asilimia 5 mara mbili na asilimia 1.4 vikirudia mara tatu. Karibu theluthi moja ya marudio yalitokana na maombi ya wagombea waliokuwa na kura zilizokaribiana sana. Katika matukio mengi ya marudio ya kuhesabu kura, matokeo hayakutofautiana kiasi cha kuleta mabadiliko katika ushindi. Hali hii inaonyesha kwamba wizi wa kura katika vituo vya kuhesabia kura ama ulikuwa mdogo sana au haukuwepo kabisa. Ushahidi wa jambo hili ni uwepo wa malalamiko machache sana (ya mawakala wa vyama na wagombea) kuhusu kuhesabu kura katika vituo vya kuhesabia kura. Kuhesabu kura kulipokamilika, mawakala wote wa vyama walichukuwa nakala zao za matokeo ya vituo vyao wakaenda kungojea ujumlishwaji wa kura na utangazaji wa matokeo ngazi ya kata (kwa wagombea udiwani), ngazi ya jimbo (kwa wagombea ubunge), na hatimaye ngazi ya taifa (kwa wagombea urais).

Ujumlishaji wa kura ulikuwa jambo lililowakera sana wapiga kura katika uchaguzi wa 2010. Ujumlishaji wa kura na utangazaji wa matokeo ya madiwani ngazi ya kata ulifanywa na Msimamizi wa Uchaguzi Msaidizi kwa kuzingatia Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya 1979. Kwa upande mwingine, ujumlishaji na utangazaji wa matokeo ya wabunge ulifanywa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa kuzingatia Sheria ya Uchaguzi ya 1985. Matokeo ya kura za urais yalitangazwa na NEC jimbo baada ya jimbo kabla ya kuyajumlisha kupata matokeo ngazi ya taifa.

Vituo hivi vya kujumlishia kura vilikuwa kipimo cha uvumilivu wa wapiga kura. Wapiga kura wengi, hasa wakereketwa wa vyama, walikesha usiku kucha wakisubiri masanduku ya kura yawasili katika vituo vya kujumlisha kura. Masanduku yaliwasili kwa vipindi mbalimbali ikitegemea wepesi wa kuhesabu kura katika vituo vya kuhesabia kura.

Masanduku yalipowasili kazi ya kujumlisha katika ngazi husika ilianza kwa kutumia technolojia mpya inayoitwa "Results Management System" (RMS) ambayo ilicheleweshа ujumlishaji na utangazaji wa matokeo hata yakawepo madai kwamba ucheleweshaji ulitokana na "uchakachuaji" wa matokeo. Kwa bahati mbaya, NEC ilikuwa haijawaeleza wananchi kwamba safari hii mfumo mpya wa kujumlisha matokeo ungetumika na kwamba ungechelewesha utangazaji wa matokeo. Mwangalizi wa jimbo la Mbeya Vijijini anaeleza jinsi wapiga kura walivyoupokea ucheleweshaji huu:

> "Japo kuhesabu kura katika vituo vya kuhesabia kura kulifanyika bila matatizo yo yote, kujumlisha kura katika ngazi ya kata kulianza kuleta maneno. Vituo vya kutoa matokeo ngazi ya kata na jimbo vilichelewesha ujumlishaji wa kura. Kutokana na hali hii, matokeo ngazi ya jimbo yalitangazwa tarehe 2 Novemba 2010 baada ya mapambano makali kati ya polisi na wakereketwa wa CHADEMA walioongozwa na mgombea wao wa ubunge."

Mratibu wa TEMCO wa Mkoa wa Mara naye alizizungumzia shaka na dukuduku za wapiga kura kama ifuatavyo:

> "Kulikuwepo mtindo wa watu kukusanyika katika vikundi vidogodogo maeneo yaliyo karibu na vituo vya kupigia kura, na baadaye wakajikusanya vituo vya kujumlisha kura vya kata na jimbo. Ilionekana kama kwamba walikuwa na agenda iliyoratibiwa…. Hali hii ilijitokeza mahali pengi katika Mkoa wa Mara. Na watu hawa walipoulizwa walikuwa wanafanya nini walisema walikuwa wakizichunga kura zao zisiibiwe."

Katika vituo vingi vya kupigia na kuhesabia kura, kadhalika katika vituo vya kujumlisha kura (kwenye kata na jimbo) watu walionekana kutokuwaamini watumishi wa serikali na vyombo vyake: maafisa wa uchaguzi, polisi na maafisa wa TAKUKURU. Kwa nini? Kuhusu polisi na maafisa wa TAKUKURU, watu waliohojiwa walidai kwamba walikuwa wamepeleka taarifa za uvunjifu wa kanuni kwa polisi na maafisa wa TAKUKURU bila kuona matokeo yake. Walisema taarifa walizopeleka zilihusu vitu kama rushwa, karatasi feki za kupigia kura, ukusanyaji (au "ununuzi") wa kadi za wapiga kura, n.k. Baadhi ya wapiga kura walidai kwamba maafisa hawa wa dola walishirikiana na wahalifu waliokiuka taratibu za uchaguzi.

Kwa sababu vituo vya kujumlishia kura (ngazi zote) havikuwaruhusu wananchi wenye dukuduku kushuhudia, hofu ya wizi wa kura iliongezeka. Walioruhusiwa kuingia katika chumba cha kujumlishia kura ni mgombea au wakala wake mmoja tu. Watu wengine wote walitakiwa kuwa sehemu ya kutangazia matokeo. Usiri huu unaonekana vizuri katika barua ya msimamizi wa uchaguzi aliyowaandikia wagombea ubunge wa jimbo lake la Serengeti siku moja kabla ya uchaguzi. Barua ilionya ifuatavyo: "Hutakubaliwa kuingia na watu wakorofi katika chumba cha kujumlishia kura au sehemu ya kutangazia matokeo" ( Barua Ref. No. SDC/ E.20/2A. Vol IV/144 ya 3.10.2010).

Sheria inawataka wapiga kura kuondoka kituoni mara tu baada ya kumaliza kupiga kura. Katika vituo vingi, wakereketwa wa vyama waliohofia wizi wa kura waliamua kubaki maeneo yaliyo jirani na kituo ili kuwadadisi watu wote wanaingia na kutoka kituoni. Uamuzi huu ulileta mapambano ya wakereketwa na polisi waliotaka kuwaondosha kwa nguvu.

Ucheleweshaji wa kuhesabu kura katika sehemu nyingi ambao ulipelekea ucheleweshaji wa kutangaza matokeo ya ubunge na udiwani uliongeza mapambano kati ya wakereketwa wa vyama waliodai matokeo yatangazwe haraka na polisi. Maelezo ya NEC kwamba ucheleweshaji wa matokeo ulitokana na ukosefu wa utaalamu wa kuitumia teknolojia mpya ya kujumuisha kura hayakusadikiwa na wapiga kura kwa sababu haikuelezwa hivyo mapema.

Wapiga kura waliamini kwamba ucheleweshaji wa matokeo ulitokana na **mbinu za kisiasa** na siyo **tatizo la kiufundi**. Kwa bahati mbaya, kura zilihesabiwa au kujumuishwa sehemu ambazo hazikuwa na mwanga wa kutosha, jambo ambalo liliongeza hofu ya wizi wa kura.

## 4.0 KUTANGAZA MATOKEO

Tofauti kubwa ya uchaguzi wa 2010 na chaguzi za 2000 na 2005 ni kwamba matokeo ya uchaguzi wa 2010 yana urari mzuri zaidi kutokana na vyama vya upinzani kuwa na mafanikio makubwa zaidi. Mwaka 2005 mgombea urais wa CCM (Jakaya Kikwete) alijizolea asilimia 80.3 ya kura zote halali, lakini katika uchaguzi wa 2010 kura zake zikupungua hadi asilimia 61. 16. Tena, kuhusu ubunge, katika uchaguzi wa 2005 vyama vya upinzani vilipata ushindi katika majimbo 26, na 7 tu yakiwa ya Bara, lakini katika uchaguzi wa 2010 vyama hivyo vilijipatia ushindi katika majimbo 51, na 31 kati yake yakiwa ya Tanzania Bara.

Katika matokeo ya urais, kura zote zilizopingwa ni 8,626,213 kati ya watu 20,137,303 walioandikishwa Bara na Visiwani. Kwa hiyo kiwango cha upigaji kura kilikuwa asilimia 42.8. Kura zilizoharibika zilikuwa 227,605 (asilimia 2.6), zikiacha kura halali 8,398,608 (au asilimia 97.4). Mgawanyo wa kura hizo kwa wale wagombea saba wa urais umeonyeshwa katika Jedwali 1 ambayo inampa ushindi Jakaya M. Kikwete wa CCM aliyepata asilimia 61.16 ya kura zote, akifuatiwa na Dkt. Willibrod Slaa wa CHADEMA aliyepata asilimia 26.34 na, katika nafasi ya tatu, Profesa Ibrahim Lipumba wa CUF aliyepata asilimia 8.08 ya kura. Wagombea wanne waliobaki waligawana asilimia 1.78 ya kura halali zilizobaki.

**Jedwali Na. 8.1: Mgawanyo wa Kura za Uchaguzi wa Rais Katika Uchaguzi Mkuu wa 2010**

| SN | Jina | Chama | Idadi ya Kura | asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Jakaya Mrisho Kikwete | CCM | 5,275,899 | 61.16 |
| 2. | Dkt. Willibrod Slaa | CHADEMA | 2,271,885 | 26.34 |
| 3. | Prof. Ibrahim H. Lipumba | CUF | 697,014 | 8.08 |
| 4. | Peter Mziray Kuga | APPT | 96,932 | 1.12 |
| 5. | Hashim Rungwe | NCCR-M | 26,321 | 0.3 |
| 6. | Mutamwega Mgaya | TLP | 17,434 | 0.20 |
| 7 | Yahmi Dovutwa Dovutwa | UPDP | 13,123 | 015 |

Chanzo: NEC, 2010

Karibu asilimia 95 ya kura halali za uchaguzi wa wabunge (7,681,196) ilizolewa na vyama vitatu tu: CCM (asilimia 60.04), CHADEMA (asilimia 24.8) na CUF (asilimia 9.8). Asilimia 5 iliyobaki viligawana vyama vingine 15 vilivyoshiriki uchaguzi wa wabunge. Kati ya vyama 18 vilivyoshiriki uchaguzi wa 2010, ni sita tu viliweza kushinda viti vya Bunge. Vyama hivyo ni CCM (Viti vya majimbo 186), CHADEMA (viti 23), CUF (viti 24), NCCR – Mageuzi (viti 4), TLP (kiti kimoja), na UDP (kiti kimoja). Kuhusu mgawanyo wa viti vya majimbo kijinsia, viti 218 vilichukuliwa na wanaume (asilimia 91.2) na 21 vilichukuliwa na wanawake (asilimia 8.8), ikionyesha wazi kwamba bado kuna mwendo mkubwa kabla ya wanawake kuweza kushindana na wanaume kwa usawa majimboni.

**Jedwali Na. 8.2: Mgawanyo wa Kura za Wabunge, 2010**

| Na. | Chama | Kura halali | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1. | AFP | 3,917 | 0.05 |
| 2. | APPT | 5,731 | 0.07 |
| 3. | CCM | 4,641,436 | 60.4 |
| 4. | CHADEMA | 1,904,540 | 24.8 |
| 5. | CHAUSTA | 2,653 | 0.03 |
| 6. | CUF | 752,617 | 9.8 |
| 7. | DEMOKRASIA MAKINI | 2,202 | 00.3 |
| 8. | DP | 6,389 | 0.08 |
| 9. | JAHAZI ASILIA | 3,777 | 0.05 |
| 10. | NCCR-MAGEUZI | 193,797 | 2.5 |
| 11. | NLD | 14,387 | 0.19 |
| 12. | NRA | 1,179 | 0.02 |
| 13. | SAU | 3,670 | 0.05 |
| 14. | TADEA | 2,284 | 0.03 |
| 15. | TLP | 52,608 | 0.68 |
| 16. | UDP | 85,395 | 1.11 |
| 17. | UMD | 1,102 | 0.01 |
| 18. | UPDP | 3,512 | 0.05 |
| | **TOTAL** | **7,681,196** | **100** |

Chanzo: NEC, 2010

Katika uchaguzi wa madiwani CCM ilishinda viti 2786 (83.4%), CHADEMA 323 (11.6%), CUF 119 (4.3%), NCCR-Mageuzi 25 (0.9%), TLP 21 (0.8%), UDP 24 (0.9%) na vyama vingine 41 (1.5%).

## 5.0 MWITIKIO WA WAPIGA KURA

Mwitikio wa wapiga kura uilikuwa mdogo sana katika vituo vilivyoangaliwa na TEMCO. Jambo hili liliwashangaza waangalizi kwa sababu watu walikuwa wameonyesha msisimko wa hali ya juu sana katika kampeni za uchaguzi ambazo walihudhuria kwa wingi. Nukuu chache za waangalizi zitaonyesha mshangao wao.

**Mwangalizi wa Jimbo la Kilindi:**

> "Kulikuwepo viwango vidogo vya upigaji kura, chini ya asilimia 40 katika vituo vyote. Sijui kitu kilichosababisha hali hii. Kuna haja ya kulifanyia jambo hili utafiti ili tuweze kuwa na ushiriki mkubwa zaidi katika chaguzi zijazo."

**Mwangalizi wa Jimbo la Korogwe Vijijini:**

> "Jambo kubwa lililojitokeza katika uchaguzi huu ni kwamba wapiga kura pungufu ya nusu ya waliojiandikisha ndio walioshiriki. Kuna haja ya kujua nini kilisababisha hali hii."

**Mwangalizi wa Jimbo la Mbeya Vijijini:**

> "Siku ya upigaji kura, watumishi na vifaa vya kupigia kura vilitimia, na upigaji kura ulikamilika mapema kuliko ilivyotarajiwa kwa sababu ya ushiriki mdogo. Katika vituo vingi, chini ya nusu ya wapiga kura walioandikishwa walijitokeza kupiga kura. Inashangaza kwamba kulikuwepo wakereketwa wa vyama wengi nje ya vituo kuliko waliokuwa ndani wakipiga kura. Haikueleweka nini kiliwanyima hao wakereketwa kuingia ndani na kupiga kura."

Waangalizi wa TEMCO walidadisi sababu za viwango vya upigani kura kuwa chini hivyo. Sababu nyingi walizotoa wapiga kura zinaweza kujumuishwa katika mafungu matano. Kwanza, ile kanuni kwamba kila mtu atapiga kura katika kituo alichojiandikisha inawanyima wahamahamaji fursa ya kupiga kura. Kwa mfano, katika sehemu za wafugaji, wapiga kura walioandikishwa wanaweza kuwa mbali na vituo vyao siku ya uchaguzi wakitafuta malisho ya wanyama wao, na hawaruhusiwi kupiga kura katika vituo vilivyo karibu na pale walipo. Kuna watu wengine wengi pia wanaojikuta wako mbali na vituo vyao siku ya uchaguzi kwa sababu mbalimbali.

Kanuni ya kumtaka mtu apigie kura pale alipojiandikisha inaweza kutumiwa kisiasa pia kuwanyang'anya wakereketwa wa vyama vya upinzani haki ya kupiga kura. Kwa mfano, katika uchaguzi wa 2010 serikali ilitoa amri kwamba vyuo vikuu visifunguliwe hadi uchaguzi upite. Inaelekea amri hii ilikusudiwa kuupunguzia upinzani kura kwa sababu wanafunzi wengi wa vyuo vikuu walikuwa wakereketwa wa vyama vya upinzani na walikuwa wamejiandikisha katika vituo vilivyokuwa vyuoni mwao.

Sababu ya pili ya kutokupiga kura ilikuwa upotevu au uharibifu wa kadi ya mpiga kura. Watu wengi wanatembea na kadi hizi mifukoni wakizitumia kama kitambulisho katika shughuli nyingi. Kwa hiyo zinaweza kupotea au kuharibika haraka.

Sababu ya tatu ya kutokupiga kura ilitokana na watu kutokuyakuta majina yao katika orodha au regista ya wapiga kura iliyobandikwa kituoni. Wale ambao hawakupata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa maafisa wa uchaguzi walijiondokea na kurudi nyumban bila kupiga kura.

Sababu ya nne iliyotolewa na wapiga kura ni kukosekana elimu ya uraia na ya wapiga kura inayotosheleza. Ni kweli kwamba Tume zetu za uchaguzi zilijitahidi kutoa elimu ya wapiga kura zikisaidiwa pia na vyama vya wananchi na vyombo vinginevyo. Lakini nchi ya Tanzania ni kubwa sana (hasa Bara) na si rahisi kuwafikishia watu wote elimu hiyo. Kwa hiyo baadhi ya watu hawajaelewa umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi kama mpiga kura. Kwa mfano, mtu mmoja mwenye kadi yake ya mpiga kura alikiri mbele ya mwangalizi wa jimbo la Segerea kwamba hakupiga kura. Alipoulizwa kwa nini hakufanya hivyo, alijibu haraka kwamba alitaka "kumwadhibu" Rais Jakaya Kikwete kwa kutotimiza ahadi zake alizotoa katika uchaguzi wa 2005. Alisema hakuweza kupata kazi japo Rais Kikwete aliahidi kuzalisha ajira milioni moja katika kipindi cha kwanza. Alipoulizwa angemwadhibuje Rais kwa kususia kupiga kura na kwamba haoni angefanya jambo la maana zaidi kumpigia kura mmoja wa wapinzani wa Rais Kikwete, alikiri mara moja kwamba alifanya makosa!

Sababu ya tano inahusu ununuzi wa kadi za wapiga kura ili kupunguza kura za wapinzani. Hili si jambo jipya, lakini inasemekana lilifanyika kwa kiwango cha juu zaidi katika uchaguzi wa 2010. Huko nyuma utaratibu ulikuwa kununua na kuziharibu kadi hizo; lakini kwa sababu sasa kadi hizo zinatumika kama kitambulisho kwenye shughuli nyingi zisizohusiana na uchaguzi, utaratibu unaokubalika ni kuzichukua na kuziweka kadi hizo hadi uchaguzi upite ndipo zirudushwe kwa wenyewe. Wale wanaokubali kuzitoa kadi zao wanalipwa kiasi wanachokubaliana na wale wanaozichukua.

## 6.0 MALALAMIKO BAADA YA KUPIGA KURA

Wapiga kura wanaruhusiwa kutoa malalamiko yao kabla ya kuondoka kituoni baada ya kupiga kura. Malalamiko yalisikika katika asilimia 12 ya vituo vilivyoangaliwa. Hata hivyo, ni katika asilimia 4 ya vituo hivyo tu ndipo wapiga kura waliolalamika waliyaandika malalamiko yao katika fomu maalum ya malalamiko ya wapiga kura. Malalamiko hayo yalihusu mambo yafuatayo:

i) Kuchelewa kufunguliwa vituo vya kupigia kura
ii) Upungufu wa vifaa vya kupigia kura
iii) Kuwepo kwa askari polisi au askari wengine wengi mno kituoni au katika eneo linalokizunguka kituo.
iv) Kutoruhusiwa kupiga kura, .

Wapiga kura wengi wa Tanzania hawapendi kutoa malalamiko yao kwa maandishi, labda kwa kuhofia kuitwa mahakamani kama shahidi katika kesi za malalamiko ya uchaguzi. Kwa mfano, katika asilimia 6 ya vituo vilivyoangaliwa na TEMCO, kulikuwepo wapiga kura waliojiunga na foleni kabla ya muda wa kupiga kura kwisha (saa 10) lakini wakakataliwa kupiga kura muda ulipofika. Tendo hili lilikiuka sheria, lakini wapiga kura husika waliondoka vituoni wakilalamika bila kujaza fomu rasmi za malalamiko ya wapiga kura. Tatizo hili linaweza pia kutokana na upungufu ya elimu ya uraia na ya wapiga kura.

Waangalizi wa TEMCO waliripoti jumla ya vituo 109 (au asilimia 1.5 ya vituo vilivyoangaliwa) ambapo watu waliojiunga na foleni baada ya muda rasmi kwisha (saa 10) waliruhusiwa kupiga kura. Wapiga kura wangeweza kujaza fomu za malalamiko kuhusu jambo hili, lakini hawakufanya hivyo. Kwa upande mwingine, katika vituo 404 vilivyoangaliwa (asilimia 5.9) mawakala wa vyama na wagombea walijaza fomu za malalamiko wakiyalalamikia mambo mbalimbali. Sehemu hii ndogo ya mawakala na wagombea waliolalamika ni ushahidi kwamba upigaji kura ulifanyika kwa uhuru, haki na amani katika vituo vingi.

## 7.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, mchakato wa kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo ulifanyika kwa mujibu wa sheria na taratibu za uchaguzi. Hata hivyo, kulikuwa na matukio ya upindishaji wa sheria katika kupeleka vifaa vya kupigia kura, kuhesabu kura na kuchelewesha matokeo ya uchaguzi. Mwitikio wa wapiga kura ulikuwa wa chini kwa kiasi cha kushtusha ikilinganishwa na chaguzi zilizopita hasa kutokana na wapiga kura kuchoka, vikwazo vya kisheria kuhusiana na vituo vya kupigia kura, upotevu wa kadi za kupigia kura, matatizo ya DKWK na pengine kuuza na kununua kadi.

## SURA YA TISA

## UCHAGUZI MKUU TANZANIA 2010: KWA KIASI GANI ULIKUWA HURU NA WA HAKI?

### 1.0 UTANGULIZI

Mwaka 2010 Tanzania ilifanya uchaguzi mkuu wa nne chini ya mfuno wa vyama vingi ulioanzishwa mwaka 1992 baada ya nchi kuwa na utawala wa chama kimoja kwa kipindi kinachokaribia miaka thelathini. Kamati ya Kuangalia Uchaguzi Tanzania (KKCT/TEMCO) ambayo iliangalia na kuandika ripoti juu ya chaguzi tatu za kwanza (1995, 2000 na 2005), ilichukua tena jukumu la kuangalia uchaguzi mkuu wa 2010 ngazi za muungano, bara na visiwani Zanzibar. Bara kulikuwepo chaguzi za aina tatu: uchaguzi wa rais wa muungano; uchaguzi wa wabunge, na uchaguzi wa madiwani. Kwa upande wa Zanzibar, chaguzi tano zilifanyika sawia: uchaguzi wa rais wa muungano; uchaguzi wa rais wa Zanzibar; uchaguzi wa wabunge; uchaguzi wa Baraza la Wawakilishi, na uchaguzi wa madiwani.

Sura hii inahusu chaguzi za ngazi ya muungano, yaani uchaguzi wa rais wa muungano na wa wabunge. Zanzibar itakuwa na ripoti yake itakayokuwa na sura inayopima kiasi cha uhuru na haki ya chaguzi zake. KKCT/TEMCO iliweka waangalizi wa muda mrefu katika majimbo ya uchaguzi 223 kati ya jumla ya majimbo 239 (asilimia 93.3) mwezi Septemba 2010. Kisha ikaweka waangalizi wa muda mfupi 7,363 kuaangalia upigaji kura tarehe 31 Oktoba 2010. Lengo la sura hii ni kufanya tathmini ya viwango vya uhuru na haki vilivyoonekana katika michakato mikuu ya uchaguzi kwa kutumia taarifa za hawa waangalizi. Tutaizungumzia michakato minne mikuu ya uchaguzi kama ifuatavyo: (i) mchakato wa kuandikisha wapiga kura; (ii) mchakato wa kuteua wagombea; (iii) mchakato wa kupiga kampeni, na (iv) mchakato wa kupiga kura, kuhesabu kura, na kutangaza matokeo.

Kwa madhumuni mahususi ya sura hii, waangalizi waliombwa kufanya tathmini ya michakato hiyo (hususan mitatu ya mwisho) kabla ya kuondoka katika majimbo au vituo vyao. Walitakiwa kutoa gredi au "maksi" kwa michakato mitatu (uteuzi wa wagombea, kampeni, na upigaji, kuhesabu hadi kutangaza matokeo ya kura) kama ifuatavyo:

i. 0% au herufi F: kuwa na maana kwamba mchakato huo au hatua hiyo ya uchaguzi imeshindwa kabisa kufikia viwango vinavyotakiwa vya menejimenti, uzingatiaji wa sheria, uhuru na haki; na kutokana na hili inakuwa vigumu hata kufanya tathmini.
ii. 1-39% au herufi E: kuwa na maana kwamba mchakato au hatua ya uchaguzi inayohusika ina matatizo mengi ya menejimenti na kutozingatia taratibu hata wadau wengi (vyama, wagombea, wapiga kura) wanayakataa yaliyofanyika katika hatua hiyo au hata kujitoa katika uchaguzi kwa upande wa vyama na wagombea wao.
iii. 40-49% au herufi D: kuwa na maana kwamba uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) una fujo, vurugu, vitisho, upendeleo (husasan wa chama tawala), rushwa, na matatizo mengine.
iv. 50-59% au herufi C: kuwa na maana kwamba uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) unaruhusu ushiriki wa wadau (vyama, wagombea, wapiga kura), lakini bado kuna ukiukwaji wa sheria na kanuni unaofanywa na vyama vikubwa au chama tawala

bila kuadhibiwa. Hii ina maana kwamba uchaguzi (au hatua husika ya uchaguzi) ni huru lakini si wa haki.

v. 60-79% au herufi B hadi B+: kuwa na maana kwamba uchaguzi (au hatua husika ya uchaguzi) ni huru na wa haki kwa jumla; lakini bado kuna upungufu ambayo yanaathiri sudi za baadhi ya wadau (wapiga kura, wagombea, vyama , ). Hii ina maana kwamba uchaguzi (au hatua husika ya uchaguzi ) ni huru na wa haki ila kuna "walakini".

vi. 80% au zaidi, au herufi A: kuwa na maana kwamba yameonekana upungufu machache na ambayo hayawezi kuathiri matokeo ya uchaguzi kwa kiwango cha kutambulikana. Ni uchaguzi (au hatua ya uchaguzi ) ulio huru na wa haki.

Hatua zote tatu za uchaguzi zilipewa gredi kwa kufuata utaratibu huu kabla ya kutafuta gredi ya wastani kwa ajili ya mchakato nzima wa uchaguzi. Hata hivyo, gredi ya mwisho ilizingatia pia upungufu ya mfumo wa uchaguzi na utawala tulio nao ambao unaleta dosari nyingi katika kuendesha uchaguzi ulio huru na wa haki.

## 2.0 MASUALA YATOKANAYO NA UANDIKISHAJI WAPIGA KURA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (TTU/NEC) na Tume ya Zanzibar ya Uchaguzi (TZU/ZEC) zilikuwa na vipindi viwili vya kuandikisha wapiga kura ili kuliboresha Jadala la Kudumu la Wapiga Kura. Kutoandikishwa kwa baadhi ya wapiga kura kulitokana zaidi na upungufu ya elimu ya rai na ya wapiga kura kuliko kukosekana kwa fursa za kujiandikisha.

Kiwango cha uandikishaji cha watu 19.6 millioni kilichotolewa na TTU/NEC kilikosolewa na vyama vya upinzani (hasa CHADEMA). Vyama hivi vilisema idadi hiyo ilikuwa kubwa kuliko matarajio, na huenda zilikuwepo njama za kisiasa za kupiga chuku. TTU/NEC ilisema kwamba kiwango hicho kinatokana na makadirio ya 2003 yaliyoonyesha kuwa Tanzania ilikuwa na watu 44 millioni. Kujitokeza kwa wapiga kura katika vituo vingi vilivyoangaliwa na TEMCO kulikuwa chini kuliko viwango vilivyokadiriwa, mahali pengine vikiwa chini kwa asilimia 50 au zaidi. Wastani wa kujitokeza kupiga kura nchi nzima ulikuwa asilimia 42, kiwango cha chini kuliko vyote vilivyopata kufikiwa katika uchaguzi mkuu Tanzania.

Waangalizi wengi wa TEMCO walirudi kutoka mikoani na nadharia kwamba wapo watu wengi ambao hawakupiga kura kutokana na kuzitoa kadi zao kwa mawakala wa chama tawala waliagizwa kuzikusanya kutoka kwa mashabiki wa vyama vya upinzani kwa kuwalipa kifuta machozi kidogo. Kadi hizo zingerudishwa kwa wenyewe baada ya uchaguzi kwa sababu zina matumizi mengine,kwa mfano, zinatumika kama vitambulisho katika shughuli mbalimbali.

Yapo mambo mengine mawili yanayoleta wasiwasi katika uandikishaji wa wapiga kura Tanzania Bara. Mfumo unaotumika hauna vidhibiti vya kutosha dhidi ya uandikishwaji wa watu wa umri mdogo au wageni sehemu za mpakani. Upungufu huu unaweza kutumiwa (hasa kwa shinikizo la chama tawala) kujinufaisha kisiasa. Wakati wa mfumo wa chama kimoja, viongozi wa nyumba kumi kumi (mabalozi,kama walivyoitwa siku hizo) waliweza kudhibiti hali hii kwa kiwango kikubwa. Lakini sasa udhibiti wa "mabalozi" wa vyama vya

siasa umepungua kwa sababu kila chama kingependa wanachama wake wajiandikishe hata kama hawana umri wa kutosha au ni wageni. Kazi wanayofanya masheha huko Zanzibar kudhibiti uandikishwaji wa wageni, wasio wakaazi na wasio na umri wa kutosha ingeweza kuwa kielezo cha kuigwa Bara, lakini imeonekana katika chaguzi zilizopita kwamba masheha, kutokana na masharti ya ajira zao, wanakipendelea chama tawala. Kuna haja ya kuendelea kutafuta utatuzi wa jambo hili.

## 3.0 MASUALA YATOKANAYO NA UTEUZI WA WAGOMBEA

### 3.1 Njia mbalimbali za Kuteua Wagombea

Uteuzi wa wagombea una hatua mbili: uteuzi ndani ya vyama na uteuzi rasmi unaofanywa na Tume ya Uchaguzi (NEC). Kama ilivyokuwa katika chaguzi zilizotangulia, uteuzi ndani ya vyama ulikuwa wa aina tatu: (i) mfumo wenye ushiriki mpana wa wanachama, (ii) mfumo wenye ushiriki wa kiasi na (iii) mfumo usioshirikisha wanachama.

Katika uchaguzi wa 2010, mfumo wa uteuzi ndani ya CCM uliboreshwa sana kidemokrasia kwa kuruhusu wanachama wote kuwapigia kura za maoni wale walioomba kuteuliwa. Mfumo huu ulikuwa na ushiriki mpana sana, na kutokana na uwazi wake, Tume ya kuzuia na kupigana na Rushwa (TAKUKURU) ikaweza kunasa na kuwahoji baadhi ya wale walioshukiwa kutoa rushwa ili wateuliwe. Hata hivyo, juhudi za TAKUKURU zilipoa moto baada ya uteuzi ndani ya CCM.

Mfumo wa uteuzi wenye ushiriki wa kiasi unawatumia wajumbe (siyo wanachama wote) wanaowapigia kura za maoni wagombea wa chama husika kabla ya vikao vya juu kufanya uteuzi: mfumo huu unatumiwa na vyama vilivyojiimarisha, hususan CUF, CHADEMA na NCCR-Mageuzi. Kura za maoni kwa CCM na vyama hivi zinakisaidia chama kuteua wagombea ambao wana nafasi kubwa ya kushinda, kwa hiyo mara nyingi wale wenye kura nyingi ndio wanaoteuliwa, lakini hutokea pia wenye kura chacha wakateuliwa na wenye nyingi wakaachwa kwa sababu mbalimbali.

Mfumo wa tatu ni ule usiowashirikisha wanachama katika uteuzi; viongozi wa juu wanafanya uteuzi wenyewe kama wapendavyo. Huu si mfumo mzuri kidemokrasia, nao unatumiwa na vyama vyote ambavyo havijaimarika. Katika baadhi ya vyama hivi mwanachama ye yote mwenye fedha za kutosha kufanya kampeni anaweza kusimama kwa sababu vyama hivi havina rasilimali nyingi kuweza kusimamisha wagombea rasmi. Kwa hiyo migogoro ya uteuzi ni michache katika vyama hivi kuliko katika vyama imara kama CCM, CUF na CHADEMA ambavyo vina wagombea wengi wenye uwezo mkubwa wa kifedha. Migogoro ya uteuzi iliyozuka CCM ilipelekea wagombea kadhaa waliokosa uteuzi kukihama chama hicho na kukimbilia vyama vya upinzani (husasan CHADEMA) ambamo waliweza kuteuliwa na baadhi yao kushinda katika uchaguzi.

Uteuzi rasmi uliofanywa na NEC haukuleta utata wala migogoro mingi. Wagombea wawili wa urais walinyimwa kugombea kwa kushindwa kutimiza masharti ya uteuzi. Suala kongwe

la wagombea kupita bila kupingwa lilijitokeza tena katika uchaguzi huu. Wagombea wa CCM wa udiwani wapatao 500 na 16 wa ubunge walipita bila kupingwa. Uzoefu wa chaguzi zilizopita (toka siku za mfumo wa chama kimoja) unaonyesha kwamba baadhi kubwa ya wale waliochaguliwa bila kupingwa walitumia njia haramu (ufisadi) kufikia hali hiyo. Pendekezo lililotolewa katika chaguzi zote zilizopita lilikuwa kwamba kila mgombea aliyekosa mpinzani apigiwe kura ya Ndiyo/Hapana ili kuona kama wapiga kura wa jimbo lake wanampenda. Tungependa kulirejeza tena pendekezo hili.

### 3.2 Waangalizi Walivyotathmini Uteuzi

Tathmini ya uteuzi iliyofanywa na waangalizi wa TEMCO katika majimbo 167 (kati ya 223 yaliyoangaliwa) ilitoa matokeo yafuatayo:

i) 0% au gredi F: jimbo moja (0.6%)
ii) 1-39% au gredi E: majimbo 3 (1.8%)
iii) 40-49% au gredi D: jimbo moja (0.6%)
iv) 50-59% au gredi C: majimbo 31 (18.6%)
v) 60-79% au gredi B- B+ : majimbo 68 (40.7%)
vi) 80% au zaidi, au gredi A: majimbo 31 (18.6%)
Jumla = majimbo 167 yaliyotathminiwa kati ya 223 yaliyoangaliwa (75%).

Uchambuzi wa majimbo 167 yaliyotathminiwa unaonyesha kwamba mchakato wa uteuzi (ndani ya vyama mbalimbali) katika asilimia 18.6 ya majimbo ni "huru lakini si wa haki" kwa kupata gredi ya C. Katika asilimia 40.7 ya majimbo mchakato wa uteuzi ulipewe gredi B/B+, yaani ni mchakato ulio huru na wa haki, ila kuna "walakini," na katika asilimia 18.6 mchakato wa uteuzi ulipewa gredi A au cheti kisafi cha uteuzi ulio huru na wa haki.

## 4.0 MASUALA YATOKANAYO NA KAMPENI

### 4.1 Upande Chanya

Tukikitazama kipindi chote cha siku 70 za kampeni rasmi tunaona dhahiri kwamba kilikuwa kipindi cha amani zaidi kuliko migogoro na machafuko. Hili ni jambo la kufurahia kwani amani hupatikana kwa nadra pale watu wanaposhindania nafasi zenye mamlaka ya kisiasa . Kwa hiyo inapasa kuwapa heko wadau wafuatao:

i) Wapiga kura waliohudhuria mikutano ya kampeni kwa wingi lakini bado wakamudu kuzidhibiti hisia zao
ii) Vyama vya siasa ambavyo vilijitahidi sana kuudhibiti umori wa wakereketwa wao
iii) Wagombea waliojitahidi kupunguza jazba na kampeni hasi dhidi ya wapinzani wao.
iv) Watendaji wa Tume zetu mbili, NEC na ZEC, ambao walijibidisha kuhakikisha kwamba ratiba iliyokubaliwa kwa ajili ya mikutano ya kampeni inafuatwa kwa kiwango kikubwa
v) Jeshi la Polisi lililotunza amani na usalama katika mikutano ya kampeni, husasan ile ya kampeni za wagombea urais ambayo ilifurika watu kwa maelfu.
vi) Vyombo vya habari ambavyo viliwaeleza watu mambo mengi kuhusu uchaguzi, ikiwa ni pamoja na yale yaliyomo katika ilani za vyama mbalimbali na yale yanayosemwa na wagombea katika mikutano ya kampeni. Vyombo vya habari vilijitahidi kuliko vilivyofanya katika chaguzi zilizopita kuzingatia maadili ya kazi yao na yale

yaliyowekwa na Tume za Uchaguzi , NEC na ZEC, hasa katika kuhakikisha kwamba vyama na wagombea viliripotiwa kwa usawa.

Yapo mambo mengi chanya yanayoweza kutajwa kuhusu kampeni za uchaguzi wa mwaka huu. Lakini ni muhimu pia kuyaangalia mambo hasi yaliyojitokeza.

## 4.2 Upande Hasi

Mambo mengi hasi waliyoyaona waangalizi wa TEMCO katika kampeni za uchaguzi huu hayakuwa mapya, lakini yalijitokeza kwa nguvu na uwazi kuliko ilivyokuwa katika chaguzi zilizotangulia. Mambo haya tumeyagawa katika mafungu manne kama ifuatavyo:

i. **Matumizi mabaya ya Madaraka**

Rais aliye madarakani pamoja na Mawaziri wake wanapotaka kuchaguliwa tena huwaendea wananchi kuwaomba kura wakiwa na vyeo vyao. Hali hii inawapa fursa na nafuu nyingi ambazo wagombea wa kawaida hawawezi kuzipata. Rais anayetetea kiti chake ndiye mwenye fursa nyingi sana, baadhi yake zikiwa za lazima, kwa mfano, ulinzi mzito. Hii ni sawa. Lakini tatizo lililojitokeza katika chaguzi zote chini ya mfumo, wa vyama vingi ni kwamba fursa hizi za kuwa madarakani hutumiwa kupita kiasi. Kwa mfano, waangalizi wa TEMCO waliona yafuatayo katika uchaguzi mkuu wa 2010:

a) Wakuu wa mikoa na wilaya walitumia rasilimali nyingi za serikali (watumishi, magari, .) kufanikisha kampeni za mgombea urais wa CCM. Mfumo wetu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa umejengwa kisiasa kukifaidi chama kilicho madarakani. Wakuu wa mikoa na wilaya pamoja na makatibu wao, na mkurugenzi mtendaji wa wilaya wanateuliwa na Rais kwa kuzingatia ushabiki wao wa chama kilicho madarakani. Hawa wanajua kabisa kwamba chama kilicho madarakani kikishindwa katika uchaguzi watazipoteza kazi zao.
b) Mara kadhaa mgombea urais aliyeko madarakani alifanya mikutano ya kampeni nyakati ambazo muda rasmi wa kampeni ulikuwa umekwisha, yaani baada ya saa 12 jioni. Kwa sababu hakukemewa na NEC, wagombea wengine wa urais waliiga mfano huo (hasa yule wa CHADEMA).
c) Mara kadhaa mgombea urais aliyeko madarakani alifanya maamuzi kama Rais katika Mikutano ya kampeni, na hata kutangaza mabadiliko ya uamuzi uliokwishafanywa na Serikali huko nyuma kwa madhumuni ya kuwashawishi wananchi kumpigia kura. Hii ilikiuka maadili ya uchaguzi. Kuahidi watu utakachowafanyia ikiwa watakuchagua tena ni sawa; lakini kutumia madaraka uliyo nayo kufanya au kuondoa maamuzi yaliyokwisha fanywa katika mikutano ya kampeni si sahihi, maana wagombea wengine hawana fursa ya kufanya hivyo.

ii. **Kampeni za Gharama Kubwa**

Huu ulikuwa uchaguzi wa kwanza chini ya sheria ya kudhibiti matumizi katika uchaguzi. Nia ya sheria hii ilikuwa kupunguza matumizi ya fedha katika uchaguzi lakini, kinyume chake, kampeni za uchaguzi huu zilikuwa za gharama kubwa hata kuliko za chaguzi zilizopita. Kampeni za vyama vikubwa, na hasa za chama tawala (CCM), zilipambwa na vifaa (magari, t-shirt, vikundi vya muziki na maonyesho, .)

ambavyo mtu aliyeviona hatakosa kusema kuwa huu ulikuwa uchaguzi ghali sana. Kwa sababu vyama vikubwa vilitumia "fedha kubwa", kampeni zilionekana kama ushindani kati ya watu wasiolingana. Kampeni za vyama vidogo vyenye "fedha ndogo" hazikuonekana kuwa ni kampeni zikilinganishwa na hizo za vyama vikubwa.

### iii. Matendo ya Vurugu

Matendo mengi ya vurugu yalitokana na ushindani mkali hasa kati ya CCM na CUF. Kwa mfano:

a) Waangalizi wa TEMCO mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kilimanjaro, Mbeya na Mara walileta taarifa za kutupiana matusi yaliyofuatiwa na mapigano kati ya watu walioshukiwa kuwa mashabiki wa CCM na CHADEMA. Kadhalika, vifo vitokanavyo na kipigo viliripotiwa Maswa, Dodoma na Dar es salaam.
b) Mwangalizi wa TEMCO katika wilaya ya Hai alicharurwa na kada wa CCM kwa kumshutumu kuwa jasusi wa CHADEMA. Kadhalika, mwangalizi wa jimbo la Kinondoni alitishiwa na mtu aliyejitambulisha kama afisa usalama wa CUF alipohudhuria mkutano wa kampeni wa chama hicho, akaambiwa yeye ni mkereketwa na CCM.

Matukio mengi ya vurugu na migongano kati ya wafuasi wa vyama yaliweza kudhibitiwa na Polisi wakishirikiana na viongozi wa vyama husika.

### iv. Ukiukwaji wa Sheria na Maadili ya Uchanguzi

Kulikuwepo matukio kadhaa ya ukiukwaji wa sheria na maadili ya uchaguzi. Ifuatayo ni mifano michache:

a) Kutokuzingatia ratiba ya kampeni na viwanja vilivyotengwa kwa ajili ya kampeni za vyama mbalimbali.
b) Baadhi ya mikutano ya kampeni kupitiliza muda rasmi (saa 12 jioni). Kama tulivyoona, waliozidi sana katika ukiukwaji wa muda wa kampeni ni wagombea urais wa CCM na CHADEMA.
c) Kuharibu au kurarua vifaa vya kampeni (picha za wagombea, bendera za vyama, matangazo yaliyobadikwa ukutani na kwingineko, .)
d) Kuhutubia mikutano ya kampeni kwa kuchanganya lugha rasmi ya kampeni (Kiswahili) na lugha za kikabila (lahaja za kienyeji). Tabia hii ilijitokeza sana katika mikoa ya Mwanza, Kagera, Ruvuma, Shinyanga na Tabora.
e) Kupiga kampeni chanya (wagombea kuumbuana majina), tabia ambayo iliripotiwa katika majimbo ya Ilala, Temeke, Bukoba Mjini, Nyamagana, Moshi Mjini, Vunjo, Hai, Tunduma, Arusha Mjini, Busanda na Maswa Mashariki. Tabia hii ilijitokeza zaidi katika kampeni za wabunge na madiwani, na kwa kiasi kidogo katika kampeni za urais.

## 4.3 Waangalizi walivyotathmini Kampeni

Tathmini ya kampeni iliyofanywa na waangalizi wa TEMCO katika majimbo 167 (kati ya 223 yaliyoangaliwa) ilitoa matokeo yafuatayo:

a) 0% au gredi F: hakuna jimbo lililopewa gredi hii.
b) 1 – 39% au gredi E: jimbo 1 (0.6%)
c) 40 – 49% au gredi D: Jimbo 1 (0.6%)
d) 50 – 59% au gredi C: majimbo 21 (12.6%)
e) 60 – 79% au gredi B – B+: majimbo 87 (52.1%)
f) 80% au zaidi au gredi A: majimbo 25 (15.0%)
Jumla = majimbo 167 yaliyofanyiwa tathmini kati ya 223 yaliyoangaliwa ( 75%)

Uchambuzi huo hapo juu unaonyesha kwamba kampeni za asilimia 12.6 ya majimbo ya uchanguzi zilitathminiwa kama ni "huru lakini si za haki"; kampeni za asilimia 52 ya majimbo zilitathminiwa kama "huru na za haki, ila kuna walakini"; na kampeni za asilimia 15 ya majimbo zilipewa cheti cha "kampeni safi zilizo huru na za haki".

## 5.0 KUPIGA KURA, KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO

### 5.1 Upigaji Kura

Mahali pote ambapo vifaa vya kupigia kura vilikuwepo vya kutosha, na watu waliyakuta majina yao katika orodha ya wapiga kura iliyobandikwa katika kituo cha kupigia kura, au wasiokuta majina yao wakaweza kutambuliwa vinginevyo na kuruhusiwa kupiga kura, upigaji kura uliendelea kwa amani mpaka mwisho. Kwa upande mwingine, malalamiko na matendo ya vurugu yalijitokeza katika vituo ambavyo havikuwa na vifaa vya kutosha au watu hawakuyakuta majina yao katika orodha ya wapiga kura. Matatizo haya mawili si mapya; yamejitokeza katika kila uchanguzi mkuu na kuwakera watu ilisivyo lazima; hata kuwafanya wapoteza haki yao ya kupiga kura. NEC ilipaswa kuhairisha uchaguzi katika majimbo na kata kadhaa kwa sababu ya kukosekana kwa vifaa vya kutosha vya kupigia kura. Kuna haja ya NEC kuwa makini zaidi ili haya matatizo ya kimenejimenti yasichukue sura ya "uchakachuaji" wa matokeo, jambo ambalo limelalamikiwa na vyama vya upinzani katika chaguzi zote nne chini ya mfumo wa vyama vingi. Katika chaguzi za nyuma, NEC na ZEC zilidaiwa kupeleka vifaa vichache katika majimbo yaliyo ngome ya vyama vya upinzani.

Kwa upande chanya, katika baadhi ya majimbo wapiga kura walionekana kuwa na motisha kubwa wa kwenda katika vituo vyao vya kupigia kura. Foleni za wapiga kura zilionekana kuanzia saa kumi na mbili na nusu (asubuhi). Vituo vingi vilifunguliwa katika muda uliotakiwa na vilikuwa na usalama na vifaa vya kuanzia kazi. Watu wenye ulemavu, wazee, wajawazito na wagonjwa walipewa kipaumbele katika kupiga kura.

Wakati upigaji kura ukiendelea kwa amani katika sehemu nyingi, yalijitokeza matukio yaliyoutia doa uchaguzi katika baadhi ya mikoa. Ifuatayo ni mifano michache:

- Katika mkoa wa Dar es Salaam (majimbo ya Ubungo na Segerea) waangalizi wa TEMCO walitoa taarifa ya watu walioonekana wakiwa na malundo ya karatasi za kupigia kura. Baadhi ya wapiga kura waliokuwa macho walitoa taarifa polisi na watu hao wakatiwa mbaroni, lakini haijulikani ni nini kilitokea baada ya hapo. Kilicho wazi ni kwamba hakuna mashtaka yaliyofunguliwa dhidi yao hadi sasa.
- Kulikuwako na taarifa kama hiyo pia kutoka Mbeya ambapo wapiga kura makini waliweza kuzigundua karatasi za kupigia kura za uchaguzi wa wabunge na urais zilizofichwa katika nyumba ya msimamizi wa kituo cha kupigia kura. Waangalizi

hawakuweza kujua kilichomfika msimamizi huyo wala karatasi zilikopelekwa baada yake kubambwa na polisi kutokana na taarifa waliyoipata kwa wapiga kura.

- Katika maeneo kadhaa (k.m. Dar es Salaam na Moshi) waliripotiwa watu waliokamatwa na askari kwa kukutwa na kadi nyingi za wapiga kura. Hii ina maana kwamba wenye kadi hizo hawakuweza kupiga kura na kuifanya idadi ya watu waliojitokeza kupiga kura katika vituo vingi kuwa ndogo kuliko makadirio. Tutalirejea tena suala hili

### 5.2 Waangalizi Walivyotathmini Upigaji Kura, Kuhesabu Kura na Kutangaza Matokeo

Waangalizi wa TEMCO wa vituo vya kura walifanya tathmini ya vituo 7,109 kati 7,247 vilivyoangaliwa Tanzania. Matokeo ya tathmini zao yalikuwa kama ifuatavyo:

- 0% au gredi F: kituo kimoja kilipewa gredi hii (0.01%)
- 1-39% au gredi E: vituo 22 (0.31%)
- 40-49% au gredi D: vituo 89 (1.25%)
- 50-59% au gredi C: vituo 138 (1.94%)
- 60-79% au gredi B/B+: vituo 2,130(30%)
- 80% au zaidi, au gredi A: vituo 4,729% (66.52%)
  Jumla vituo 7,109 vilivyotathminiwa kati ya vituo 7,247 vilivyoangaliwa (98.1%)

Uchambuzi huu unaonyesha kwamba shughuli za kupiga kura, kuhesabu kura hadi kutangaza matokeo katika asilimia zipatazo 2 za vituo zilitathminiwa kama “huru lakini si za haki”; katika asilimia 30 zilitathminiwa kama “huru na za haki, ila kuna walakini” na asilimia kubwa ya 66.52 ilipewa cheti safi cha shughuli zilizofanyika kwa uhuru na haki.

Jedwali Na. 9.1 limeweka pamoja matokeo ya tathmini hizo tatu (uteuzi, kampeni na shughuli za upigaji kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo). Kama inavyoonekana katika jedwali, majimbo mengi yalipata gredi ya B/B+ katika uteuzi wa wagombea (52.5%) na kampeni (63.5%) ; ambapo vituo vingi zaidi viliweza kupata gredi A (66.5% ya vituo vilivyotathminiwa). Katika vituo vingi upigaji na kuhesabu kura vilifanyika kwa amani. Matatizo yalianza matokeo yalipochelewa kutangazwa katika ngazi ya kata ( kwa wagombea udiwani), ngazi ya jimbo ( kwa wagombea ubunge), na ngazi ya taifa ( kwa wagombea urais).

## 6.0 TAMKO LA TEMCO KUHUSU UCHAGUZI WA 2010

Ili kurahisisha tathmini ya uchaguzi wa mwaka 2010, TEMCO iliandaa nyenzo za kusaidia kuweka alama za ubora kwenye michakato yote muhimu ya uchaguzi. Jedwali Na. 9.1 ni muhtasari wa tathmini ya hatua tatu muhimu za uchaguzi: uteuzi wa wagombea, mwenendo wa kampeni na shughuli zinazoendana na siku ya upigaji kura (kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo). Tathmini hii ikichukuliwa pamoja na maelezo yakinifu ndani ya ripoti hii yaliiwezesha TEMCO kufikia hitimisho kuhusiana na uchaguzi wa 2010.

**Jedwali Na. 9. 1: Tathmini ya Ujumla ya Uchaguzi wa 2010**

| Gredi | Uteuzi wa Wagombea (%) | Kampeni (%) | Upigaji Kura, (%) |
|---|---|---|---|
| A | 22.2 | 22.2 | 66.5 |
| B/B+ | 52.5 | 63.5 | 30.0 |
| C | 21.5 | 13.2 | 1.9 |
| D | 0.6 | 0.6 | 1.2 |
| E | 2.5 | 0.6 | 0.3 |
| F | 0.6 | 0.0 | 0.1 |
| **Jumla** | **100** | **100** | **100** |

Kama inavyojidhihirisha katika Jedwali Na. 9.1, asilimia 37 ya Waangalizi wa Uchaguzi wa TEMCO walitoa alama **A** kwa mchakato mzima wa uchaguzi wakati asilimia 48 waliota alama ya **B/B+.** Hii inaendana na maelezo ya kina yaliyomo katika ripoti hii. Kwa hiyo TEMCO inatoa tamko kuwa uchaguzi wa mwaka 2010 Tanzania ulikuwa **Huru na wa Haki wenye Walakini**. Hii ni kusema kuwa uchaguzi kwa ujumla uliendeshwa kwa uhuru na haki lakini kulikuwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria na kanuni ambao uliwaathiri vibaya baadhi ya washiriki wa uchaguzi.

## 7.0 MAPENDEKEZO

Kutokana na yale yaliyosemwa katika sura mbalimbali za ripoti hii, tunapenda kutoa mapendekezo kwa wadau mbalimbali wa uchaguzi Tanzania.

### 7.1 Tume za Uchaguzi (NEC na ZEC)

(i) Uboreshaji wa DKWK ufanywe mara kwa mara kuliko ilivyo sasa. Mfumo wa sasa wa uandikishaji wa wapiga kura inabidi uboreshwe kwa kufanya yafuatayo:

a) Kufungua ofisi katika mikoa, wilaya na kata
b) Kuanzisha utaratibu wa wapiga kura kujiandikisha na kurekebisha taarifa zao kupitia mtandao
c) Kuanzisha vituo vya kuhamishika vya kuandikisha wapiga kura
d) Wakala wa Usajili, Udhamini na Ufilisi (RITA) iboreshwe ili iweze kutoa habari za uhakika za wapiga kura wanaofariki.

(ii) Elimu ya uraia na elimu ya mpige kura itolewe wakati wote na iwe endelevu. Kuna haja ya kuwa na mkakati wa kitaifa wa elimu ya uraia.

(iii) Elimu ya uraia na elimu ya mpiga kura itolewe muda wote hasa kwa wanawake vijijini ili kuwaongezea hamasa ya kushiriki katika uchaguzi.

(iv) Kuna haja ya kuziendeleza redio za jamii katika kutoa elimu ya uraia hasa maeneo ya vijijini

(v) Muda wa kampeni uongezwe ili kuwawezesha wagombea na vyama vya siasa kuwafikia wapiga kura wengi zaidi

(vi) Kuna umuhimu wa kufanya utafiti ili kubaini mwitikio hafifu wa wapiga kura katika uchaguzi wa mwaka 2010

(vii) Mchakato wa kupiga kura na kuhesabu kura ufanywe kwa haraka na ufanisi

## 7.2 Serikali

(i) Sheria za uchaguzi hazina budi kupitiwa upya ili kuruhusu wagombea binafsi katika uchaguzi katika ngazi mbalimbali

(ii) Sheria inayotoa mamalaka ya uteuzi wa makamishna katika mchakato wa uchaguzi haina budi kuangaliwa upya ili kuongeza uwazi, uhuru na kuongeza imani ya jamii

(iii) Kuna haja ya kupitia upya sheria ya uchaguzi ili kuruhusu matokeo ya urais kupingwa mahakamani

(iv) Wagombea wanaopita bila kupingwa hawana budi kupigiwa kura walau ya Ndiyo/Hapana ili kuimarisha demokrasia

(v) Mamlaka kubwa ya rais katika kuteua watendaji wa muhimu ammbao huhusika sana katika uchaguzi kama vile Mkurugenzi wa Uchaguzi, Mkuu wa Jeshi la Polisi, majaji, wakuu wa vyombo vya habari vya dola, wasimamzi wa uchaguzi, na wengineo iangaliwe upya ili kuimarisha imani ya jamii katika vyombo vya dola

(vi) Kuna umuhimu wa kufuatilia kwa ukaribu na kuzuia matumizi ya rasilimali za umma wakati wa kampeni ili kuhakikisha chama tawala hakijinufaishi

(vii) Serikali haina budi kuendelea kuweka mazingira mazuri kuwatia moyo wananwake kushiriki katika vyombo vya maamuzi ikiwemo halmashauri, bunge na baraza la wawakilishi

(viii) Kuwe na mipaka inayoeleweka katika majukumu ya utekelezaji wa sheria ya gharama za uchaguzi na sheria nyingine za uchaguzi. Wajibu wa vyama vya siasa, TAKUKURU, Polisi, Tume ya Uchaguzi, na Msajili wa Vyama vya Siasa yaelezwe bayana.

(ix) Kuna haja ya kuongeza uelewa wa jamii kuhusu sheria ya gharama za uchaguzi.

## 7.3 Vyama vya Siasa

(i) Viongozi wa vyama, wanachama na wagombea yabidi waheshimu maadili yanaoongoza kampeni

(ii) Vyama vya siasa na wagombea waache kutumia lugha ya kashfa na kejeli, kuchochea vurugu na kuvunja sheria, taratibu na miongozo ya uchaguzi

(iii) Mchakato wa uteuzi wa wagombea wa viti maalum uwe wazi na shirikishi zaidi

(iv) Vyama vya siasa vitengeneze mbinu za uhakika za kuhakikisha wanawake wanashiriki kama wagombea na wapiga kura

(v) Kuna haja ya vyama vya siasa kuimarisha uwezo wao wa oganaizesheni na uhamasishaji ili kuwafikia wapiga ura wengi zaidi hasa vijijini

(vi) Vyama vya siasa viongeze uwezo wao wa kuandaa ilani za uchaguzi ambazo zinaelezea itikadi, masuala muhimu na sera za maendeleo

(vii) Vyama vya siasa na wagombea waepukane na rushwa na vitendo vinavyohusiana na rushwa wakati wa uchaguzi

(viii) Vyama vya siasa havina budi kuimarisha uwezo wao wa menejimenti ya pesa ili kurahisisha utekelezaji wa sheria ya gharama za uchaguzi

(ix) Kwa kadri inavyowezekana, vyama vya siasa na wagombea wajitahidi kuheshimu utawala wa sheria.

### 7.4 Vyombo vya Habari

(i) Vyombo vya habari vya umma havina budi kutoa muda sawa kwa vyama vyote vya siasa bila upendeleo

(ii) Uhuru wa wahariri hauna budi kuheshimiwa na wamiliki wa vyombo vya habari ili kupunguza muingilianao usiokuwa wa lazima

(iii) Vyombo vya habari vichukue jukumu la awali katika kutoa elimu ya uraia

(iv) maadili ya vyombo vya habari lazima yaheshimiwe na vyombo vya habari

(v) Kuna haja ya kupigania kupitishwa kwa sheria ya uhru wa habari (FIA) ambayo itatoa uhuru zaidi kwa waandishi wa habari na jamii kupitia nyaraka za serikali

(vi) Kuna haja ya kuongeza weledi kwa waandishi wa habari kwa kuanzisha kozi mahsusi za kutoa taarifa za uchaguzi.

**REJEA**


Barkan, J. "Elections in Agrarian Societies," Journal of Democracy, Vol. 6, No. 4 October, 1995 pp 106-116

Baxter, J. "Techniques for Effective Election Management" in United Nations, Elections: Perspectives on Establishing Democratic Practices: United Nations, New York, 1997

Benjamin Highton "Voter Registration and Turnout in the United States", Perspectives on Politics, September, Vol. 2, No. 3. September, 2004 pp 507-515

Commonwealth Secretariat, "Report of the Commonwealth Observer Group Tanzania General Elections", 31 October, 2010

Commonwealth Secretariat, Commonwealth Workshop on Democracy and Small States, Valetta, Malta, 10-12 May 2000

Daily News, September 24, 2010

Denis Kadima and Susan Booysen Compendium of Elections in Southern Africa 1989-2009: 20 Years of Multiparty Democracy, Johannesburg: EISA, 2010

Diamond, L. "Elections without Democracy: Thinking About Hybrid Regimes." Journal of Democracy, Vol. 13, No. 2, 2002 pp 21-35

EISA "Tanzania Presidential, National Assembly and Local Government Elections" EISA Election Observer Mission Report, No. 20, 14 December, 2006

EISA and ECF, "Principles for Election Management, Monitoring and Observation in the SADC Region." Electoral Hand Book No. 13: 4

Election Expenses Act No. 6 of 2010

Elklit J. & Svensson, P. "The Rise of Election Monitoring: What Makes Elections Free and Fair?" Journal of Democracy, Vol. 8, No. 3, 1997 pp 32-45

FEMACT Election Manifesto "Ilani ya Wapiga Kura, 2010"

Gloppen, S. and Rakner, L.; "Accountability Through Tax Reform? Reflections from Sub-Saharan Africa." IDS Bulletin Vol. 33 No. 3, 2002

Government Notice No. 279. 2010. The Elections (Presidential and Parliamentary Elections) Regulations, 2010. Made Under Section 124 of the National Elections Act CAP 343, United Republic of Tanzania

Graber A. Doris, Media Power in Politics, Macmillan India Ltd, New Delhi, 1990

Grant Masterson "Tanzania and Zanzibar" in Denis Kadima and Susan Booysen (eds) Compendium of Elections in Southern Africa 1989-2009: 20 Years of Multiparty Democracy, EISA, Johannesburg, 2009

Habari Leo, 31st July 2010

Hyden, G., “Governance and the Study of Politics”, in Goran Hyden and Michael Bratton (ed), Governance and Politics in Africa. Boulder, Colorado; Lynne Rienner Publishers, 1992

IDEA, Ethical and Professional Observation of Elections. International IDEA Code of Conduct Series 2, 1977

IFJ, Election Reporting Handbook, Brussels, 1993

Kilimwiko Lawrence, Media Power and Politics in Tanzania: Critical Analysis of Media Trends and Practice, Association of Journalists and Media Workers, Dar es Salaam , 2009

Majira Newspaper, 6th October, 2010

Marias, C., “A Study of Voting Behavior in the 1992 Namibian Regional and Local Government Elections.” University of Namibia, October 1993

Marshal, T.H. Class, Citizenship and Social Development, London, 1964

Mørck, A.B. (2006) “The United Republic of Tanzania: Presidential and Parliamentary Elections”, December 2005

Mtanzania, 19th July, 2010

Mwananchi Newspaper, 4th October, 2010

Mwananchi September 18, 2010

Mwananchi, 18th July, 2010

Mwananchi, 19th August, 2010

Mwananchi, October 13, 2010

Mwananchi, October 15, 2010

Mwananchi, September 4, 2010

Nadeu, Richard et. al., “Election Campaigns as Information Campaigns: Who Learns What and Does It Matter”. Political Communication, Vol. 25, 2008 pp. 229-248

NEC The Report of the National Electoral Commission on the 2000 Presidential, Parliamentary and Councillor’s Elections, Dar es Salaam, 2001

NEC The Report of The National Electoral Commission on the 2005 Presidential, Parliamentary and Councillors Elections, Dar es Salaam, 2006

Nipashe 13th August 2010

Norris, Pippa, 2004. "The Evolution of Election Campaigns: Eroding Political Engagement?" www.pippanorris.com, retrieved 24th December, 2010

Nyerere, J., "Our Leadership and The Destiny of Tanzania". African Publishing Group, Harare, 1995

Raia Mwema 25th – 31st August 2010

Raia Mwema 2nd - 8th June 2010

Shayo, R. 2005, "Women Participation in Party Politics During the Multiparty Era, The Case of Tanzania." EISA Occasional Paper Number 34, July 2005

Sheria ya Taifa ya Uchaguzi (Sura 343), Dar es Salaam, 30 June 2010

Synovate Tanzania Media Election Coverage, Reports Nos. 3 &17 2010

Taifa Tanzania September 10, 2010

Tanzania Daima, 18th August 2010

TAWLA Manual on Elections 2010

TEMCO Constituency Report, Kinondoni 2010

TEMCO Constituency Report, Korogwe 2010

TEMCO Constituency Report, Lindi 2010

TEMCO Constituency Report, Njombe, 2010

TEMCO Constituency Report, Nzega, 2010

TEMCO Constituency Report, Singida 2010

TEMCO Constituency Report, Vunjo 2010

TEMCO LTO Report, Dar es Salaam Region, 2010

TEMCO LTO Report, Iringa Region, 2010

TEMCO LTO Report, Kigoma Region, 2010

TEMCO LTO Report, Manyara Region 2010

TEMCO LTO Report, Tanga Region 2010

TEMCO LTO Report, Temeke 2010

TEMCO Report on the CCM Presidential Nomination Process for the 2010 General Elections, July 9-11, 2010

TEMCO "An Interim Report on Performance of Tanzania's 2010 General Elections in Tanzania", 2010a
TEMCO "Report on the Civic United Front Intraparty Nomination Process for the 2010 General elections in Zanzibar" (2010b)

TEMCO Constituency Reports 2010

TEMCO Data Set, 2010

TEMCO Report on the 2000 General Election in Tanzania, TEMCO Dar es Salaam, 2001

TEMCO Report on the 2005 General Election in Tanzania, TEMCO, Dar es Salaam, 2006

TEMCO Mtwara Report, 2010

TEMCO Newsletter EEA Series No. 1 September, 2010

TEMCO Regional Report, Dar es Salaam, 2010

TEMCO, Newsletter, Second Issue on Tanzania 2010 General Elections, Issue NO.2, 30th October, 2010

TGNP Manual on Elections, 2010

The Citizen 18th December, 2010

The Citizen, 18th August, 2010, 23rd August, 2010, 30th August, 2010, 23rd September, 2010, 22nd October, 2010, 25th October, 2010

The Citizen on Sunday, 19th December 2010

The Citizen, 16th August 2010

The Citizen, 17th September 2010

The Citizen, October 15, 2010

The Daily News, 30th August, 2010

The Guardian (Tanzania), 24th August, 2010; 23rd October, 2010

The Guardian, 12th August 2010

The Tanganyika Law Society Observer Mission to the 31st October, 2010 General Election in the United Republic of Tanzania, Final Report.Dar es Salaam, 28th November, 2010

NEC, Maadili ya Uchaguzi kwa Ajili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2010 ( Chini ya Kifungu cha124A cha Sheria ya Uchaguzi Na.1 ya mwaka 1985 – Sura ya 343)

Tume ya Taifa ya Uchaguzi.2010. Maadili ya Uchaguzi kwa Ajili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2010, Made under Section 124A of the Elections Act No. 1 of 1985

UNIFEM Manual on Elections, 2010

URT 2010 The National (Presidential and Parliamentary Elections) Regulations, 2010

Wall, A. et al., "Electoral Management Design: The International IDEA Handbook." IDEA, 2006:43

Zaller, J. 1989. "Bringing Converse Back In: Modelling Information Flow in Political Campaigns", in Political Analysis, Vol. 1, No.1 pp. 181-234

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO NA. 1: ORODHA YA ASASI WANACHAMA WA TEMCO

1. Action for Development Forward (ADF)
2. Action for Justice in Society (AJISO)
3. African International Group of Political Risk Analysis (PORIS)
4. Agency for Co-operation and Research in Development (ACORD)
5. Agenda Participation 2000
6. Amani the Foundation of Life (AFL)
7. Amka Kazinga
8. Association of Women for Democracy
9. Association of Journalists and Media Workers (AJM)
10. Association of Non-Governmental Organizations of Zanzibar (ANGOZA)
11. Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA)
12. B'villea Community Services
13. Campaign for Good Governance (CGG)
14. Centre for Civil Society and Strategic Studies (CCSSS)
15. Centre for Informal Sector Promotion (CISF)
16. Chama Cha Saidia Jamii-Kilombero (CHASAJAKI)
17. Chama cha Wafugaji Muheza (CHAWAMU)
18. Chama Cha Walemavu Tanzania - Kigoma
19. Chama cha Walimu Tanzania (CWT)
20. Chama cha Wastaafu na Wazee Lindi (CHAWALI)
21. Chama Cha Wastaafu Wilaya ya Kisarawe (CHAWAKI)
22. Chambani Development Society (CHADESO)
23. CHAWAKATA
24. Children in Need Outreach (CINO)
25. Christian Council of Tanzania (CCT)

26. Christian Professionals of Tanzania (CPT)
27. Civic Education Teachers' Association (CETA)
28. Coast Region NGOs Network (CORNNET)
29. Community Development for All (CODEFA)
30. Community Services Tanzania - COSETA
31. Dar es Salaam Business School, Mzumbe University
32. Department of Fine and Performing Arts (DFA – University of Dar es Salaam)
33. Department of Political Science and Public Administration, University of Dar es Salaam
34. Development and Relief Foundation (DRF)
35. Development of Sustainable Community Based Activities (DESCOBA)
36. District Organization for Aids Control and Orphans Right (DOACO)
37. ENVIRONATURE
38. Environment Conservation for Social Development
39. Environmental Protection and Humanitarian Agency (EPHA)
40. Forum for African Women Educationalists (FAWE)
41. Guluka Kwalala Youth Environment Group
42. Hakielimu
43. Institute for Development Studies (IDS), University of Dar es Salaam
44. Jamoja Trust
45. Jikomboe Integral Development Association (JIDA)
46. Jumuiya ya Sanaa ya Elimu ya Ukimwi na Mazingira (JSEUMA)
47. Jumuiya ya Wahitimu wa Chuo cha Demokrasia Zanzibar (JUWADEZA)
48. Kagera Development and Credit Revolving Fund (KADETFU)
49. Kagera Youth Empowerment Network
50. Kanyigo Aids Prevention Foundation
51. Kashai Development Initiative Organization (KADEI)
52. Kibaha Network of Civil Society Organizations (KNCSO)

53. Kidike Environmental Conservation Club

54. Kigoma Paralegal Aid Centre (KIPACE)

55. Kigoma Women Development Group

56. Kikundi Cha Wanawake Kilimanjaro Kupambana na Ukimwi (KIWAKKUKI)

57. Kilimanjaro Women Information Exechange and Consultancy Organization (KWIECO)

58. Kinga za Haki za Binadamu/Haki Za Raia (DHR)

59. Kinondoni Youth Parents Counseling Centre (KNYPC)

60. Kiziba Development Initiatives

61. Kongwa Alliance Development Trust (KADET)

62. Lindi Support Agency for Welfare (Lisawe)

63. Lindi Women's Paralegal Aid Centre

64. Lisawe on Poverty Alleviation

65. Liwale Farmer's Association (LIFA)

66. Lumemo Farmers Club

67. Makambako Environmental Community Society

68. Mapambano Centre for Children Rights

69. Matumaini Women and Care of Children

70. Mara Youth NGO

71. Mbeya Older Persons Care (MOPEC)

72. Mbeya Paralegal Unit (MBEPAU)

73. Mbeya Women Organization for Preventing HIV/Aids

74. Mbeya Youth Development Organization

75. Mbinga Development and Environment Action (MBIDEA)

76. Micheweni Islamic Development Environmental Conservation and Aids Control (MIDEC

77. MIICO

78. Millennium Aids Herbalist Programme (MAHP)

79. Mkoani Poverty Eradication Society (MPESO)

80. Moses Foundation Tanzania (MFT)
81. Mowers Planters and Cleaners (MOPLAC)
82. Mshikamano and Advancement Women Organization (MAWO)
83. Mtwara Region NGOs Network (MRENGO)
84. Muheza District Paralegal Centre
85. Multiple Education Centre (MEC)
86. Muungano wa Vijana Tanzania (MUVITA)
87. MUVIKA
88. National Youth Information Centre (NICE)
89. Ndela Kituo cha Maendeleo ya Vijana Kigoma
90. NGO Network for Dodoma Region (NGONDEDO)
91. Nyengedi Environment Development and Diseases Control
92. Oak Tree Tanzania
93. Pamoja Aids and Environmental Foundation
94. Patronage in Environmental Management and Health Care Warriors (PEMWA)
95. Peace House Foundation Ltd.
96. Pemba Awareness for Land Use and Environment Society (PALESO)
97. Pemba Environmental Gender and Advocacy Organization
98. Pemba Investment and Youth Development Organization (PIYDO)
99. Pemba Press Club
100. Pemba Rapid Development Organization (PRADO)
101. People's Organization Transparency Agency (POTA)
102. Research and Education for Democracy In Tanzania (REDET)
103. Ruangwa Non-Governmental Organization Network (RUANGONET)
104. Ruangwa Organization of Poverty Alleviation
105. Rural and Urban Development Initiatives (RUDIT)
106. Rural Initiatives and Relief Agency

107. Ruvuma Network of Organizations Working With HIV/Aids (RUNOWA)

108. Sanganigwa Children's Home

109. Self-Help Development Community (SEDECO)

110. SHIKWAUKI

111. Shinyanga Civil Society Organization (SHINGONET)

112. Society for Rural Development Initiatives (SRDI)

113. Songea Network of Non Governmental Organization (SONNGO)

114. Taaluma Women Group (TWG)

115. Taasisi ya Nyumba ya Haki (House of Justice)

116. Tanzania Action for Coastal Education Advocacy

117. Tanzania Episcopal Conference (TEC)

118. Tanzania Home Economics Association (TAHEA)

119. Tanzania Journalists Association (TAJA)

120. Tanzania Media and Youth Development Association (TAMEADA)

121. Tanzania Muslim Professional Association (TAMPRO)

122. Tanzania Organization for Permaculture Promoters (TOPP)

123. Tanzania Private Sector Foundation (TPSF)

124. Tanzania Women for Self Initiatives

125. Tanzania Women Graduate Federation (TWGF)

126. Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA)

127. Tanzania Young Farmers Club (TAYFAC)

128. Tanzania Youth Team for Campaign Against Aids (TAYOTA)

129. Tanzania Youth Vision Association (TYVA)

130. TCCIA Kigoma

131. The Institute of Peace and Conflict Studies (IPCS)

132. Tumaini Trust Fund

133. Uelekeo Tz (UTZ)

134. Umoja wa Maendeleo Kaskazi Mtende Unguja (UMAKAMU)
135. Umoja wa Wawezeshaji Kioo Kigoma
136. Vitongoji Environmental Conservation on Association (VECA)
137. Wamata Head Office
138. Wazee Wastaafu Kigoma (WAWAKI)
139. Wete Environmental Conservation Club (WECOC)
140. White Orange Youth (WOY)
141. Women and Community Development (MUDUGU-WACOD)
142. Women in Law and Development in Africa (WILDAF)
143. Women Initiatives of Tabora
144. Youth Against Poverty Trust Fund (YAP)
145. Youth Development Society
146. Youth Environment Rescue Organization Tanzania (YEROTAN)
147. Youth Service Volunteers Society
148. ZAM Foundation
149. Zanzibar Association of the Disabled
150. Zanzibar Female Lawyers Association (ZAFELA)
151. Zanzibar Legal Services Centre (ZLSC)
152. Zanzibar National Association of the Blind (ZANAB)

KIAMBATISHO NA. 2

# TANZANIA ELECTION MONITORING COMMITTEE (TEMCO)

**P. O. BOX 35039. DAR ES SALAAM.TANZANIA**

Telephone: +255 22 2410131
+255 22 2410207

Fax: +255 22 2410084

TEMCO

Email: temco@udsm.ac.tz

Website: http://www.temco.udsm.ac.tz

## AN INTERIM REPORT ON PERFORMANCE OF TANZANIA'S 2010 GENERAL ELECTIONS IN TANZANIA

### 1. INTRODUCTION

In 2010 Tanzania held its fourth general election under the multiparty system which was reintroduced in the country in 1992 after nearly 30 years of one-party rule. The Tanzania Election Monitoring Committee (TEMCO) which observed and wrote reports on the first, second and third general elections in 1995, 2000 and 2005 respectively, undertook to do the same again in the 2010 general election, covering both Mainland and Zanzibar. The Mainland has three types of elections: Presidential election for the Union Presidency, Parliamentary election for the Union Parliament, and Civic election for the local government councils. In contrast, Zanzibar held five elections simultaneously: Union Presidential election, Zanzibar Presidential election, Union Parliamentary election, Zanzibar House of Representatives election and Civic election for the local government councils.

This interim report relates to the union elections. A separate report has been written for the Zanzibar elections. TEMCO fielded long-term observers to cover 223 out of 239 constituencies (93.3%) in Tanzania in September 2010. These were joined by 7,363 short-term observers (STOs) to observe or "watch' the polls on the election day, 31st October, 2010. The purpose of the interim report is to give an overview of the trends of the electoral process leaving details to the full report to be written when the detailed field reports have been analysed. We shall have a word on each of the four main steps of the electoral process, namely: (i) registration of voters; (ii) nomination of candidates; (iii) campaigns, and (iv) election-day activities: voting, vote counting and declaration of results.

For the purpose of this interim statement, the LTOs and STOs were required to make rapid assessments of the nomination, campaigns and election-day activities (up to declaration of some results) and wire them to TEMCO headquarters in Dar es Salaam. These rapid assessments provide the trend of the three electoral processes and enable us

to predict the extent to which the total electoral process can be considered 'free and fair'. They were asked to score each of the three electoral steps as follows:

i) 0% or letter grade F: to mean an election (or electoral step) which has failed totally in terms of management, compliance with electoral rules, code of conduct and fairness; and therefore it does not come to normal finality.

ii) 1 – 39% or letter grade E: to mean an election (or electoral step) with so many managerial problems and irregularities that most major stakeholders (voters, candidates, parties) reject or are likely to reject the final results.

iii) 40 – 49% or letter grade D: to mean that the election process has acts of violence, intimidation, favouritism, corruption, etc.

iv) 50 – 59% or letter grade C: to mean the election permits free participation of stakeholders (voters, candidates, parties, others), but there are many instances where bigger parties (or especially the ruling party) break the rules with impunity. That is to say, the election is free but not fair.

v) 60 – 79% or letter grade B: to mean an election (or electoral step) which is generally free and fair, but still has short-comings which work against fortunes of some stakeholders (voters, candidates, parties, etc.). It is a 'qualified' free and fair election (or electoral step).

vi) 80% or more or letter grade A: to mean an election with only a few short-comings which do not affect the overall results. It is a clean free and fair election.

## 2. REGISTRATION OF VOTERS VERSUS VOTER TURNOUT

The National Electoral Commission (NEC) and the Zanzibar Electoral Commission (ZEC) organized two rounds of voter registration so as to up-date the Permanent Voters' Register. Non-registration of some eligible voters would be more a result of inadequate voter and civic education than the lack of effort by NEC and ZEC.

NEC registration figures for the 2010 elections stand at 19.6 million, a figure which has been questioned by opposition parties (especially CHADEMA). They claim that the figure is unrealistically high for an estimated population of 40million and that there may be political motive for exaggerating the figure. The NEC explanation is that the figure is based on the 2003 population estimate of 44million. Voter turnout in many voting stations observed by TEMCO in Tanzania were lower than the estimated figure, in some places by 50 per cent or less. If this happens to be the pattern, explanations will have to be found to clear the cloud.

There are two other points of controversy regarding voter registration on Mainland Tanzania. The existing system does not have adequate controls for underage and foreigner registration, especially in border regions. During the one-party system the ten-cell leaders provided some controls, but these controls no longer exist under the multiparty system because each party may want their own supporters to be registered whether underage or foreigner. The Zanzibar Sheha could provide a model for the Mainland, but experience has shown that Sheha's role can be abused to serve the interests of the party in power. Some thinking is required in this area.

## 3. NOMINATION OF CANDIDATES

Nomination of candidates has two stages: nomination within each participating party and the official nomination by NEC. The 2010 elections continued to show three models of intra-party nominations, namely: (i) fully participatory model, (ii) partially participatory model, and (iii) hand-picking model.

So far the fully participatory model has been used by CCM and CUF. The model was democratized further during the 2010 elections to allow all party members to vote for party members who seek party nomination for council and parliamentary candidacy. The preferential votes of party members are considered at party sittings at district, regional and national levels, with the possibility of making changes at each level. The model proved so transparent that it was possible for the Prevention and Combating of Corruption Bureau (PCCB) to track corrupt practices by several CCM aspirants on the mainland. However, the PCCB initiative was toned down for reasons which are still unclear.

The partially participatory model is based on delegates (not all members) who give preferential votes for the candidates before higher organs make final choice. This model is used by the better established parties in the opposition camp, especially CHADEMA and NCCR.

The hand-picking model is the least democratic and is used by most of the remaining 'small' or less established parties. It is really a top-down model, with the decision of who stands for what position being made by top party leaders. In practice, any member who wants and can finance his/her own campaigns can stand for a position in these parties because they have relatively few resources to support 'official' party candidates; and therefore there are fewer conflicts than in the larger parties. Conflicts were more pronounced in the larger parties, especially in the nominations of CCM. These conflicts led to several defections to opposition parties (especially to CHADEMA) by those who failed to secure nomination in CCM.

The official nomination of candidates by NEC did not raise many problems. Two presidential aspirants were dropped due to their failure to fulfill nomination conditions. The issue of unopposed candidates was back on the table during this election. Up to 500 CCM council and 16 parliamentary candidates were elected unopposed. Past experience (including the experience of the one-party system) show that at least some of those declared elected unopposed may have used corrupt means to achieve this status. Past recommendations have been that all those who have no opposers should be subjected to a Yes/No vote to see if the voters actually approve them. We should again repeat this recommendation. Observers' Assessment of Nomination in 135 constituencies out of the 223 observed by TEMCO in Tanzania provides the following scores:

- 0% or grade F: 1 constituency (0.7%)
- 1 – 39% or grade E: 3 constituencies (2.2%)

- 40 – 49% or grade D: 1 constituency (0.7%)
- 50 – 59% or grade C: 31 constituencies (23.0%)
- 60 – 79% or grade B: 68 constituencies (50.4%)
- 80% or above, or grade A: 31 constituencies (23.0%)

**Total = 135 constituencies**

Analysis of the 135 constituencies suggest that, if this pattern persists in all the constituencies, the nomination process of 23% of the constituencies will be judged "free but not fair"; in 50.4% of the constituencies the nomination process will receive a 'qualified free and fair' certification; and in another 23% of the constituencies, nomination will receive a 'clean free and fair' certification. These figures are expected to change slightly when assessments of all the 223 constituencies observed by TEMCO in Tanzania are analysed.

## 4. ELECTION CAMPAIGNS

### 4.1 Positive Side

Taking the entire campaign period of 70 days, it will be seen that it was typified more by peace than by conflict. This is significant and cannot be taken for granted where people are competing for political power. Credit must be given to the major stakeholders:

- The voters who attended campaign meetings massively and yet were able to control their emotions.
- Political parties which struggled hard to curb the enthusiasm of their supporters.
- Candidates who observed reasonable limits of negative campaigning against opponents.
- NEC and ZEC personnel in the field who tried hard to enforce campaign timetables.
- Security personnel (police) who kept order in campaign meetings, especially big public rallies, of presidential candidates.
- Media people who informed the public about the contents of party manifestos and campaign themes covered by candidates of different parties. Clearly the media (print and electronic) tried more than in previous elections to adhere to their own (and NEC's and ZEC's) code of conduct, especially in giving equal consideration to all parties and their candidates.

There are a lot more positive things that could be said about campaigns in this year's election. But it is equally important to look at some of the negative aspects as well.

### 4.2 Negative Side

Most of the negative things picked by TEMCO observers are not new; they however seem to have acquired bigger magnitude in this election. These will be classified into several categories:

**(i) Overstretched use of advantages of incumbency:**

Minister-candidates and presidential candidates seeking re-election do have certain advantages of incumbency by the sheer fact that they are in power even as they market

themselves to voters. Presidential candidates in power, in particular, attract state resources which he/she cannot be denied (e.g. security). This is fine. The problem has in all elections under the multiparty system been that this advantage has been overstretched or overexploited. During 2010 elections, for example, the following have been observed by TEMCO field observers:

- Regional and District Commissioners have placed state resources (vehicles etc) in campaign processions of the presidential candidate defending his position.
- In several places the presidential candidate in power addressed public meetings outside the legal campaign time (beyond 6.00pm), a practice which was then imitated by other presidential candidates (especially that of CHADEMA).
- There were several cases of making a decision or reversing a government decision previously made in campaign meetings – which violates the code of ethics, etc. Promises for what one will do for the people if returned to power are fine; but using current position to make or unmake a decision to gain votes is improper; for other candidates cannot do the same.

**(ii) Over-decorated campaigns**

This was the first election under the new law on election expenses whose original purpose was to limit the use of big money in elections. Ironically, the campaign materials for the bigger parties, especially the ruling CCM, are clearly more elaborate and expensive in this than in previous elections. Even a casual observer of these campaign materials will not fail to conclude that this was a very expensive election and that some parties and candidates have spent fortunes. Because of the use of big money by big parties, the campaigns became a competition among unequals. The less resourced parties did not seem to be campaigning at all when compared with giants.

**(iii) Violent actions**

Most violent actions on the Mainland related to the stiff competition, especially between CCM and CHADEMA and in a fewer cases CCM and CUF. For example:

- TEMCO observers in Dar es Salaam, Mwanza, Kilimanjaro, Mbeya and Mara regions reported several incidents of provocative language sometimes followed by physical confrontations between people believed to be members or supporters of CCM and CHADEMA. There were deaths reported in Maswa, Dodoma and Dar es Salaam.
- The TEMCO observer in Hai District received a veiled threat from a CCM cadre who charged him with being a CHADEMA supporter. Similarly, the Kinondoni constituency observer was intimidated at a CUF campaign rally by an individual who identified himself as a security officer of the party, charging him with being a CCM supporter.

In some of the cases of inter-party violence the police and party leaders were able to keep the situation under control.

**(iv) Breaking Rules and Code of Ethics**

There were cases spread here and there of breaking election rules and the code of ethics. The following are examples:

- Non-adherence to the campaign timetable (and allocated venue for campaign meetings) which in some cases caused clashes.
- Some campaign rallies being extended beyond the official ending time (6.00pm). As we have noted, the main perpetrators were CCM and CHADEMA.
- Mutilation of campaign materials (photographs, flags, posters, etc) observed in a number of constituencies.
- Addressing campaign meetings while mixing the official language (Kiswahili) with local languages (vernacular). This was dominant in Mwanza, Kagera, Ruvuma, Shinyanga and Tabora regions.
- Incidences of negative campaigning (demeaning opponent's character) were noted particularly in Ilala, Bukoba urban, Nyamagana, Moshi, Vunjo, Hai, Tunduma, Arusha Urban, Busanda, Temeke and Maswa East Constituencies. These related mainly to council and parliamentary candidates; but presidential candidates were not immune to this either.

### 4.3 Observers' Assessment of Campaigns

Observer's assessment of the campaigns in 135 out of the 223 constituencies observed by TEMCO Tanzania give the following scores:

- 0% or grade F: No constituency had this grade
- 1 – 39% or grade E: 1 constituency (0.7%)
- 40 – 49% or grade D: 1 constituency (0.7%)
- 50 – 59% or grade C: 21 constituencies (15.6%)
- 60 – 79% or grade B: 87 constituencies (64.4%)
- 80% and above, or grade A: 25 constituencies (18.5%)
  **Total = 135 constituencies**

The trend suggested by this analysis is that the campaigns of 15.6% of the constituencies will be assessed as 'free but not fair'; in 64.4% of the constituencies the campaigns will receive a 'qualified free and fair' certification, while in 18.5% of the constituencies the campaigns will receive a 'clean free and fair' certification. As in the case of nomination, these figures are expected to change slightly when all assessments of 223 constituency campaigns have been analysed.

## 5. ELECTION-DAY ACTIVITES: VOTING, VOTE COUNTING AND DECLARATION OF RESULTS

### 5.0 Voting

In all places where voting materials had been supplied in adequate amount and voters were able to find their names on the list of voters posted at the polling station, or they were otherwise identified and allowed to vote, voting continued peacefully to the end. On the other hand, problems, complaints and desperate actions by voters typified all

voting stations with inadequate supply of voting materials and where voters could not find their names on the list of voters.

These two are old problems which have continued to recur in every election, causing unnecessary inconveniency to voters or denying some the opportunity to cast their votes. NEC has had to postpone elections in several constituencies and wards because of non-availability of adequate voting materials. More care is needed to ensure that these managerial hitches are not interpreted as political strategies for rigging elections, and such interpretation has already been voiced by some stakeholders.

On the positive side, in most constituencies voters were reported to have high motivation to vote, forming queues at voting stations as early as 6.30am. Most stations opened on time and had adequate security and materials to commence voting. People with disability, elderly people, pregnant women and the sick were in all cases observed given priority.

As voting was continuing peacefully, some ugly episodes were reported in several places, for example:

- In Dar es Salaam (Ubungo and Segerea constituencies) there were reports of people seen with voting papers. It is still unclear as to what happened after their arrest by the police following reports by voters. There was a similar report from Mbeya where alert voters discovered a person with voting papers for parliamentary and presidential elections in the house of a presiding officer. It is still unclear what happened to the presiding officer after the voters had taken initiative to get him arrested by the police.
- In several places (including Dar es Salaam and Moshi) people were arrested for carrying several voters' cards. This may partly account for the observed discrepancy between estimated voters and people actually turning up to vote in a polling station.

### 5.1 Vote Counting and Declaration of Results

Problems and violent actions started at this stage. Law demands that people should vacate the polling station as soon as they completed voting. In many places party fans, already suspecting that there may be fake voting papers which could be used to rig elections, were determined to remain within the vicinity of the polling station to monitor all suspicious activities. This led to violent confrontation with the police who tried to evacuate them forcibly.

Delay in counting the votes which led to delays in declaring the results of council and parliamentary elections fired the confrontation between the police and party fans who demanded declaration of results. Explanation by NEC personnel that delays were due to the lack of mastery of the new computerized counting system could not be accepted by anxious voters partly because it came late.

The voters attributed delays to **politics** rather than **technics**. Unfortunately, it so happens that counting of votes took place in venues with poor lighting, further raising suspicions of vote rigging. Enough attention was not paid to the problem of lighting in many places, which is probably managerial slippage.

### 5.2 Observers' Assessment of the Polling Day Activities

Poll observers' on-the-spot assessment of the process of voting, vote counting and declaration of results in 4,332 out of 7,363 polling stations observed by TEMCO in Tanzania gives the following scores:

- 0% or grade F: No polling station had this grade
- 1 – 39% or grade E: No polling station had this grade
- 40 – 49% or grade D: 7 polling stations (0.16%)
- 50 – 59% or grade C: 54 polling stations (1.25%)
- 60 – 79% or grade B: 1,313 polling station (30.31%)
- 80% or above, or grade A: 2,958 polling stations (68.28%)
  **Total = 4,332 polling stations**

The trend suggested by this analysis is that the voting activities of less than 2% polling stations will be considered as 'free but not fair'; and voting activities of 30.31% polling stations will receive a 'qualified free and fair' certification, while voting activities of 68.28% polling stations will receive a 'clean free and fair' certification, high proportion indeed. As in the case of the nomination and campaign figures, these figures are expected to change slightly when data for the full package of 7,363 polling stations have been analysed. At that point it will be possible to make an assessment of the entire election.

## 6. ACKNOWLEDGEMENTS

TEMCO would like to acknowledge the contribution of the following who have made this interim statement possible:

- Financial support from the Election Support Project (ESP, 2010) managed by the UNDP and all missions/embassies contributing towards that Project, namely: Canada, Denmark, The European Commission, Finland, the Netherlands, Norway, Sweden, Switzerland and the United Kingdom.
- The National Electoral Commission (NEC) and the Zanzibar Electoral Commission (ZEC) for accreditation of TEMCO observers and provision of much needed documents; also for the cooperation shown the TEMCO observers by NEC and ZEC personnel in the field, namely NEC Regional Coordinators, Returning Officers, and Presiding Officers and their assistants.
- TEMCO member organizations which have extended unshakable cooperation to the Executive Committee and Secretariat of TEMCO.
- TEMCO Regional Coordinators, Constituency Poll Observers who worked around the clock to supply the data needed by the Secretariat.

- The Media for cooperation shown in the field.
- Other observer groups from within and outside the country who interacted with TEMCO observers for mutual benefit.

## KIAMBATISHO NA. 3: ORODHA YA WAANGALIZI WA TEMCO

| MKOA | MRATIBU WA MKOA | NA. | MAJIMBO | WAANGALIZI WA MAJIMBO |
|---|---|---|---|---|
| ARUSHA | Mr. Mohamed Riyami | 1 | Arumeru Mashariki | Ms. Furaha Comoro |
| | | 2 | Arumeru Magharibi | Ms. Zired Abdulkarim Musanifu |
| | | 3 | Karatu | Mr. Robert Muna |
| | | 4 | Monduli | Mr. Elias Bingasila Joel |
| | | 5 | Longido | Mr. Daudi Richard Kweba |
| | | 6 | Ngorongoro | Ms. Tedy Mbuya |
| | | 7 | Arusha Mjini | Mr. Mohamed Riyami |
| | | | | |
| DAR ES SALAAM | Ms. Annmarie Mavenjina Nkelame | 8 | Ilala | Ms. Annemarie Mavenjina |
| | | 9 | Segerea | Ms. Felister Mushi |
| | | 10 | Ukonga | Ms. Shani Adam |
| | | 11 | Kawe | Ms. Josephine Besha |
| | | 12 | Ubungo | Dk. Bernadetta Killian |
| | | 13 | Kinondoni | Prof. Yunus Rubanza |
| | | 14 | Temeke | Mr. Lupa Ramadhani |
| | | 15 | Kigamboni | Mr. John Jingu |
| | | | | |
| DODOMA | Mr. Hurbert M. Lubyama | 16 | Dodoma Mjini | Mr. Hurbert M. Lubyama |
| | | 17 | Mtera | Ms. Salama Mbarouk Khatib |
| | | 18 | Bahi | Ms. Pheby Ambwene Mwaseba |
| | | 19 | Mpwawa | |
| | | 20 | Chilonwa | Mr. Kevin Oswin Haule |
| | | 21 | Kibakwe | Mr. Hamis Kihongoa |
| | | 22 | Kondoa Kaskazini | Ms. Leonida Paul Tenga |
| | | 23 | Kondoa Kusini | Mr. Ludger Kasumuni |
| | | 24 | Kongwa | |

| MKOA | MRATIBU WA MKOA | NA. | MAJIMBO | WAANGALIZI WA MAJIMBO |
|---|---|---|---|---|
| IRINGA | Prof. Amos Mhina | 25 | Iringa Mjini | Prof. Amos Mhina |
| | | 26 | Isimani | |
| | | 27 | Kalenga | |
| | | 28 | Kilolo | Mr. Renatus Mkinga |
| | | 29 | Mufindi Kaskazini | Ms. Mariam Njama |
| | | 30 | Mufindi Kusini | |
| | | 31 | Ludewa | |
| | | 32 | Makete | Ms. Seraphine Bernad Nsana |
| | | 33 | Njombe Kaskazini | Ms. Maria Duncan Mwakasege |
| | | 34 | Njombe Kusini | |
| | | 35 | Njombe Magharibi | Ms. Marietta Kaijage |
| | | | | |
| KAGERA | Mr. Baumba Chogero | 36 | Bukoba Mjini | Mr. Jesper Katomero |
| | | 37 | Bukoba Vijijini | Mr. Baumba Chogero |
| | | 38 | Chato | Ms. Salome Nungu |
| | | 39 | Biharamulo | Mr. Hilary Tesha |
| | | 40 | Ngara | Ms. Janeveva Emanuel |
| | | 41 | Karagwe | Mr. Oddo Hekela Egino |
| | | 42 | Muleba Kaskazini | Ms. Neema Mukandala |
| | | 43 | Muleba Kusini | |
| | | 44 | Nkenge | Ms. Martha Mushi |
| | | 45 | Kyerwa | Ms. Eva Azaria Nkonya |

| MKOA | MRATIBU WA MKOA | NA. | MAJIMBO | WAANGALIZI WA MAJIMBO |
|---|---|---|---|---|
| KIGOMA | Mr. Ramadhani Kingi | 46 | Kigoma Mjini | Mr. Ramadhani Kingi |
| | | 47 | Kigoma Kusini | Mr. Humphrey Nyandindi |
| | | 48 | Manyovu | Mr. Illuminatus J. Mkoka |
| | | 49 | Kigoma Kaskazini | Mr. Parestico Pastory |
| | | 50 | Muhambwe | Mr. Salum Mkubwa |
| | | 51 | Buyungu | Mr. Johaness Bigirwamungu |
| | | 52 | Kasulu Mjini | Mr. Martin Kihunrwa |
| | | 53 | Kasulu Vijijini | Rev. Canon Raphael Haule |
| | | | | |
| KILIMANJARO | Prof. Daudi Mukangara | | | |
| | | 54 | Moshi Mjini | Prof. Daudi Mukangara |
| | | 55 | Vunjo | Ms. Rashida Shariff |
| | | 56 | Same Magharibi | Mr. Hussein B. Kinguyu |
| | | 57 | Same Mashariki | Mr. Paul Chilewa |
| | | 58 | Rombo | Mr. Hulka K. Omari |
| | | 59 | Mwanga | Mr. Juma Wambura |
| | | 60 | Hai | Ms. Matrona Kabyemela |
| | | 61 | Siha | Mr. Adam Maziku |
| | | 62 | Moshi Vijijini | Dk. Patrick Masanja |

| MKOA | MRATIBU WA MKOA | NA. | MAJIMBO | WAANGALIZI WA MAJIMBO |
|---|---|---|---|---|
| LINDI | Dk. Rebecca Sima | 63 | Lindi Mjini | Dk. Rebecca Sima |
| | | 64 | Mchinga | Ms. Fatma Kange |
| | | 65 | Mtama | Mr. Paschal Itangaja |
| | | 66 | Nachingwea | Mr. Allan P. Mkopoka |
| | | 67 | Liwale | Mr. Sixbert John Khamsini |
| | | 68 | Ruangwa | Mr. Juma Ismail Malundila |
| | | 69 | Kilwa Kusini | Mr. Ibrahim Samwel Materego |
| | | 70 | Kilwa Kaskazini | Mr. Mohamed Kombo Khamis |
| | | | | |
| MANYARA | Mr. Leons Kimaryo | 71 | Babati Vijijini | Mr. Angelus Mapunda |
| | | 72 | Mbulu | Mr. Esperatus Mukyanuzi |
| | | 73 | Simanjiro | |
| | | 74 | Hanang' | Mr. Bihaga Edward Saimon |
| | | 75 | Kiteto | Ms Neusta Justinian |
| | | 76 | Babati Mjini | Mr. Leons Kimaryo |
| | | | | |
| MARA | Mr. Audax Kweyamba | 77 | Musoma Mjini | Mr. Audax Kweyamba |
| | | 78 | Musoma Vijijni | |
| | | 79 | Serengeti | Mr. Kampambe Francis Davis |
| | | 80 | Rorya | Ms. Rebeca. S. Mahege |
| | | 81 | Tarime | Mr. Charles Irigo |
| | | 82 | Mwibara | Mr. Harrison Justo Isaiah Lyombe |
| | | 83 | Bunda | Mr. Nathanael Mwandete |

| MKOA | MRATIBU WA MKOA | NA. | MAJIMBO | WAANGALIZI WA MAJIMBO |
|---|---|---|---|---|
| MBEYA | Mr. Joseph Paul Ibreck | 84 | Mbeya Mjini | Ms. Consolata Raphael |
| | | 85 | Mbeya Vijijini | Mr. Joseph Paul Ibreck |
| | | 86 | Mbozi Mashariki | Mr. Pius Libaba |
| | | 87 | Mbozi Magharibi | Mr. Emmanuel Kipole |
| | | 88 | Ileje | Ms. Sesilia Muloki |
| | | 89 | Songwe | Unopposed candidate |
| | | 90 | Kyela | Ms. Nyanzobe Hemed |
| | | 91 | Mbarali | Mr. Richard Kappia |
| | | 92 | Rungwe Magharibi | |
| | | 93 | Rungwe Mashariki | |
| | | 94 | Lupa | Mr. Wilfred Wilbard Kahumuza |
| | | | | |
| MOROGORO | Dk. Ambrose Kessy | 95 | Morogoro Mjini | Dk. Ambrose Kessy |
| | | 96 | Morogoro Mashariki | Ms. Gladness Besha |
| | | 97 | Morogoro Kusini | Ms. Dorothy John Kaloli |
| | | 98 | Kilosa | Ms. Tumaini Gwatalile |
| | | 99 | Gairo | Ms. Egidia Evans |
| | | 100 | Mvomero | Ms. Jacqueline Mchapwaya |
| | | 101 | Ulanga Magharibi | Mr. Deodatus Zephrine |
| | | 102 | Ulanga Mashariki | |
| | | 103 | Kilombero | Mr. Elijah Kondi |
| | | 104 | Mikumi | Ms. Asinani Ramadhani |

| MKOA | MRATIBU WA MKOA | NA. | MAJIMBO | WAANGALIZI WA MAJIMBO |
|---|---|---|---|---|
| MTWARA | Mr. Lawrence Kilimwiko | 105 | Mtwara Mjini | Mr. Lawrence Kilimwiko |
| | | 106 | Mtwara Vijijini | Ms. Cecilia Rugimbana Kokwenda |
| | | 107 | Masasi | Mr. Dicky Bantu Unga |
| | | 108 | Nanyumbu | Mr. Jesmart Nderingo |
| | | 109 | Tandahimba | Mr. John Kihamba |
| | | 110 | Newala | Ms. Bernadetha Franco Khamsini |
| | | 111 | Lulindi | Ms. Bridgeth Rogath |
| | | | | |
| MWANZA | Prof. Frederick Kaijage | 112 | Ilemela | Mr. Felix Mwombeki Mulengeki |
| | | 113 | Nyamagana | Prof. Frederick Kaijage |
| | | 114 | Busega | Ms Kellen Sylvester Mngoya |
| | | 115 | Geita | Ms. Radegunda P. Mchau |
| | | 116 | Nyang'hwale | Mr. Kelvin Munisi |
| | | 117 | Misungwi | Dk. Charles Saanane |
| | | 118 | Ukerewe | Ms. Agnes N. Lema |
| | | 119 | Sengerema | Ms. Amina Mnenge Mlawa |
| | | 120 | Kwimba | Mr. Raashid Hamad Abdalla |
| | | 121 | Sumve | Ms. Anita Masaki |
| | | 122 | Busanda | Ms. Angelina Murangila |
| | | 123 | Buchosa | Mr. David Magoda |
| | | 124 | Magu | Ms. Perpetua Mashelle |

| MKOA | MRATIBU WA MKOA | NA. | MAJIMBO | WAANGALIZI WA MAJIMBO |
|---|---|---|---|---|
| PWANI | Prof. Ernest Mallya | 125 | Kibaha Mjini | Prof. Ernest Mallya |
| | | 126 | Kibaha Vijijini | Ms. Adrophina Salvatory |
| | | 127 | Bagamoyo | Prof. Kapepwa Tambila |
| | | 128 | Chalinze | Ms. Theresia John Gama |
| | | 129 | Rufiji | Mr. Maximillian Buhatwa |
| | | 130 | Kibiti | Ms. Edwardina Byamungu |
| | | 131 | Mkuranga | Ms. Anna Keneth Mgalla |
| | | 132 | Mafia | Mr. Elias M. Mtaki |
| | | 133 | Kisarawe | Ms. Leyla Zuberi |
| | | | | |
| RUKWA | Mr. Christonsia Reginald | 134 | Sumbawanga Mjini | Mr. Christonsia Reginald |
| | | 135 | Kwela | Ms. Winifrida France |
| | | 136 | Kalambo | Ms. Pamela Kijazi |
| | | 137 | Mpanda Kati | Dk. Jasson Kalugendo |
| | | 138 | Nkasi Kusini | Ms. Maundi Keneth Mwasomola |
| | | 139 | Nkasi Kaskazini | Mr. Christopher Joseph Kiiza |
| | | 140 | Katavi | |
| | | 141 | Mpanda Vijijini | Mr. Muharram Omar Moh’d |
| | | | | |
| RUVUMA | Dk. Hubert Makoye | 142 | Songea Mjini | Dk. Hubert Makoye |
| | | 143 | Peramiho | Mr. Respicius Damian |
| | | 144 | Mbinga Mashariki | Mr. Anthony Kija |
| | | 145 | Mbinga Magharibi | Mr. Benedict Kisaka |
| | | 146 | Tunduru Kaskazini | Ms. Elizabeth Bitegera |
| | | 147 | Tunduru Kusini | Ms. Aurelia R. Kimaro |
| | | 148 | Namtumbo | Ms. Ritha Kimaro |

| MKOA | MRATIBU WA MKOA | NA. | MAJIMBO | WAANGALIZI WA MAJIMBO |
|---|---|---|---|---|
| SHINYANGA | Mr. Dezideri Tibesigwa | 149 | Shinyanga Mjini | Mr. Dezideri Tibesigwa |
| | | 150 | Solwa | Mr. Kevin Rugaimukamu |
| | | 151 | Bariadi Mashariki | Ms. Christina Mbilinyi |
| | | 152 | Bariadi Magharibi | Mr. Stephen. J. Kilasi |
| | | 153 | Meatu | Mr. Claudius Damian Ngindo |
| | | 154 | Maswa Mashariki | Mr. Frank J. Mateng'e |
| | | 155 | Maswa Magharibi | Mr. Ayoub Abwor |
| | | 156 | Kishapu | Mr. Emanuel Elia |
| | | 157 | Kisesa | Mr. Shedrack Mbogoye |
| | | 158 | Bukombe | Ms. Joyce Mwacha |
| | | 159 | Kahama | Ms. Sophia Ndjike |
| | | 160 | Msalala | Mr. Deodatus Shayo |
| | | 161 | Mbogwe | Ms. Hedwiga Pastory Mvungi |
| | | | | |
| SINGIDA | Prof. Issa Musoke | 162 | Singida Mjini | Prof. Issa Musoke |
| | | 163 | Singida Kaskazini | Ms. Joanita Mochiwa |
| | | 164 | Iramba Magharibi | Mr. Khamis Issa Ali |
| | | 165 | Manyoni Magharibi | Ms. Jocelyne Emmanuel Mkilima |
| | | 166 | Manyoni Mashariki | Mr. Benson Msemwa |
| | | 167 | Iramba Mashariki | Ms. Bernadetha Choma |
| | | 168 | Singida Magharibi | Dk. Frowin Nyoni |
| | | 169 | Singida Mashariki | Mr. Muhidin Shangwe |

| MKOA | MRATIBU WA MKOA | NA. | MAJIMBO | WAANGALIZI WA MAJIMBO |
|---|---|---|---|---|
| TABORA | Prof. Max Mmuya | 170 | Tabora Kaskazini | Mr. Henry Hebron Mwasongwe |
| | | 171 | Igalula | Mr. Anthony Mlelwa |
| | | 172 | Nzega | Dk. Abunuwasi Mwami |
| | | 173 | Bukene | Dk. Boniface Eliamini Mgonja |
| | | 174 | Urambo Mashariki | Ms. Neema Nkalang'ango |
| | | 175 | Sikonge | Mr. Albert Chalamila |
| | | 176 | Igunga | Mr. Gozbert Kamugisha |
| | | 177 | Urambo Magharibi | Mr. Francis Kwangu |
| | | 178 | Tabora | Prof. Max Mmuya |
| | | | | |
| TANGA | Dk. Alban Hokororo | 179 | Muheza | Mr. Mathew Agripinus Senga |
| | | 180 | Bumbuli | |
| | | 181 | Pangani | Mr. Jonia Bwakea |
| | | 182 | Kilindi | Mr. Anold Philemon |
| | | 183 | Korogwe Vijijini | Mr. Jacob Salasu |
| | | 184 | Handeni | Ms. Immaculate Dominic |
| | | 185 | Tanga | Dk. Alban Hokororo |
| | | 186 | Mkinga | Mr. David Jeremia |
| | | 187 | Lushoto | Mr. Yulli Jeremia |
| | | 188 | Korogwe Mjini | Mr. Renatus Thadeo Rweshabula |
| | | 189 | Mlalo | Ms Getruda J. Likango |